

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 3 Mei, 2017

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO (K.n.y. MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA MAENDELEO YA JAMII):

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. GODWIN O. MOLLEL - MSEMaji MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, swali la kwanza ni la 130 ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Zainab Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Peter Serukamba.

Na. 130

Kufanya Vibaya kwa Shule za Sekondari za Umma Nchini

MHE. PETER J. SERUKAMBA (K.n.y. MHE. ZAINAB A. KATIMBA) aliuliza:-

Shule za Sekondari za Umma zimeendelea kufanya vibaya katika mitihani ya kidato cha nne na sita, ambapo kwa mwaka 2015 katika matokeo ya kidato cha nne watahiniwa waliopata daraja la nne ni 240,996 sawa na asilimia 67.91 na waliopata daraja la sifuri ni 113,489 sawa na asilimia 32.09:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi katika kuboresha mazingira ya kujifunzia katika Shule za Umma za

Sekondari nchini ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu ya majengo ya madarasa, mabweni na maabara?

(b) Je, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuifuta kazi Bodi ya Menejimenti ya Mamlaka ya Elimu Tanzania na kuiunda upya kutokana na kushindwa kusimamia ubora wa elimu nchini ambayo ni moja ya jukumu lake?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifufua zilizokuwa shule za vipaji maalum za Ilboru, Kilakala, Mzumbe na Kibaha zilizowahi kufanya vizuri miaka ya 1990?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II) Serikali imekamilisha uboreshaji wa Shule za Sekondari 792 kwa kukarabati miundombinu na kuweka samani; shule 264 ziliboreshwa katika awamu ya kwanza kwa gharama ya shilingi bilioni 56; na shule 540 katika awamu ya pili kwa gharama ya shilingi bilioni 67.8 na zote zimekamilika. Ukamilishaji wa ujenzi wa shule hizo, umesaidia katika kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia katika Shule za Sekondari za Serikali.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ubora wa elimu linajumuisha mambo mengi ambayo yanahusisha kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia jambo ambalo linatekelezwa kupitia mipango na bajeti kila mwaka. Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) inasimamia udhibiti wa ubora wa elimu ikishirikiana na taasisi nyingine zinazotekeleza Sera ya Elimu Tanzania. Kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali kuboresha elimu nchini, hatuoni sababu ya kuvunja

Bodi hiyo, badala yake tutaendelea kuiwezesha kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi kwa kushirikiana na taasisi nyingine.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ukarabati wa shule kongwe zote 89 nchini zikiwemo Ilboru, Kilakala, Mzumbe na Kibaha. Mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali ilitoa shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya shule kongwe na shilingi bilioni 3.5 zilitolewa na kutumika kukarabati shule saba za ufundi za Iyunga, Moshi, Mtwara, Musoma, Bwiru *Boys* na Ifunda. Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) itakarabati shule kongwe 11 zikiwemo za vipaji maalum za Mzumbe, Ilboru, Kilakala, Tabora Boys, Tabora *Girls*, Pugu, Nganza, Mwenge, Same na Msalato.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina swali.

MWENYEKITI: Aah, huna swali. Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi linaulizia vitendea kazi vya elimu, ubora wa elimu, pamoja na mazingira yake yote ambayo ni elimu kwa wote, shirikishi na yenye ubora; mwaka 2013 tarehe 2 Machi siku ya Jumamosi, Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Sifuni Mchome ya kuangalia vigezo vyote hivi. Tarehe 31 hoja binafsi ilikuwa Bungeni kuhusu vigezo vyote hivi. Je, ni lini Serikali italeta ile ripoti ya Tume ya Sifuni Mchome hapa Bungeni ili Wabunge tuweze tukaishauri vizuri Serikali kuhusu ubora wa elimu Tanzania?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa *Engineer* Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli nafahamu kuna hiyo Tume ilikuwa imeundwa na kuna baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yameelezwa kwenye ile Tume; lakini baada ya hapo kuna *team* mbalimbali ziliundwa ambazo pia nyingine zilikuja kuona hata baadhi ya mapendekezo pengine hayako sawa; yaani hayaendani sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara tumekuwa tukiendelea kufanya marekebisha kulingana na mahitaji, kwa mfano katika suala la utoaji wa tuzo. Mwanzo zilikuwa zinatamia *GPA*, sasa hivi tumerudi tena kwenye *division*. Kwa hiyo, kuna mambo mengi tu ambayo yamekuwa yakifanyiwa kazi kila wakati. Hata hivyo, siyo tatizo kuweza kuwaonesha Waheshimiwa Wabunge nini kilikuwa kimezungumzwa kwenye Tume, lakini pia mabadiliko yanayoendana na uhalisia wa sasa yaliyofanyika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khadija.

MHE. KHADIJA N. ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa Tanzania, ni lini Wizara itaingiza mitaala ya masomo ya kilimo na ufugaji kwenye Sekta ya Elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Naibu Waziri, Mheshimiwa Jafo kwa kifupi twende mbele.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *concern* hiyo kweli imejitokeza wazi; na nakumbuka kipindi cha nyuma waliokuwa wanasoma sekondari, kulikuwa na somo moja linaitwa *Agricultural Science* na mambo ya *Nutrition*, lakini hapa katikati lilipotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza mitihani ya *Form Six* na ile ya *Form* ya *Four* mwaka 2016, somo hilo sasa limeshaanza kuingizwa. Utaratibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba somo hili la *Agricultural Science* na masomo mengine, kuhakikisha kwamba suala la kilimo linapatikana limeweza kufanyika hivyo. Nashukuru sana Walimu ambao wamejitokeza, nami nilienda kuwatembelea wakati ule wapo Hombolo wakifanya usahihishaji, wamesema vijana wametoa mwikio mkubwa sana, inaonekana tunaendelea vizuri. Kwa hiyo, hilo tuondoe shaka, Serikali inalifanya kazi vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali namba 131, linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Ulega. Aah, Mheshimiwa Dkt. samahani, karibu.

Na. 131

Huduma za Afya - Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa, huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya Bagamoyo zimekuwa dhaifu sana kutokana na upungufu mkubwa wa miundombinu, vitendea kazi, uhaba wa watumishi na ukosefu wa dawa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huduma za afya katika Hospitali hiyo kwa kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu bora, vitendea kazi, kuiongezea watumishi na dawa za kutosha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga shilingi 1.4 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambapo itahusisha kuboresha miundombinu ya Hospitali na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile zimetengwa shilingi 185,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutokana na ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya vituo vya kutolea huduma za afya, shilingi 59,790,600/= kutokana na mapato ya ndani kwa ajili ya upanuzi wa wodi ya wazazi, ukarabati wa kitengo cha wagonjwa wa nje (*OPD*) na eneo la kuhudumia wagonjwa wa dharura pamoja na kumaliza ukarabati wa wodi ya wanaume. Aidha, Serikali imetoa kibali cha kuajiri Madaktari na watumishi wengine wa afya ambapo Halmashauri hiyo pia itapewa kipaumbele. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kawambwa.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, isipokuwa nina maswali mawili ya nyongeza ya kuuliza. Moja, Mheshimiwa Waziri katika mwaka huu wa fedha 2016/2017, tulitengewa fedha jumla ya sh. 82,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa wodi kwenye Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo, lakini mpaka hapa tunapongea fedha hizi hazijapelekwa katika Halmashauri. Je, Mheshimiwa Waziri atatuhakikishia Bagamoyo kwamba fedha hizi zitaweza kutolewa kabla ya mwaka huu kumalizika ili tuweze kuboresha huduma katika hospitali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri amenijibu kuhusu ujenzi wa *OPD* kwa kutumia fedha za (*own source*) za kwetu wenyewe, lakini *OPD* hii ni mbovu sana; haina uwezo wa kuhudumia wagonjwa kwa kadri ambavyo ingeweza kutoa huduma ile ambayo wanasema

inafaa kwa wananchi wale wa Bagamoyo. Inahitaji ujenzi mpya kabisa. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari ku-*commit* kiasi cha fedha ili angalau tuweze kuijenga upya *OPD* hiyo?

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *commitment* ya Serikali katika bajeti ambayo mwaka huu tunaondoka nayo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba bado tuna mwezi mpaka tufike mwezi wa Sita. Lengo letu Serikali ni ile wodi iweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *OPD*, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwanza Bagamoyo tumeingiza katika *program* maalum ya *RBF* na hivi sasa tumewapelekea takriban shilingi milioni 150 kutokana na kuwepo kwa zahanati zao 15. Mpango huu utaenda takriban miaka mitatu kwa sababu tume-*site* kama ni sehemu ya mfano kuanzia na hiyo *program*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tunaenda na hizi *intervention*, kwa sababu lengo letu ni kupandisha vituo vyetu viwe na *star*. Bahati nzuri Jimbo lake ni miongoni mwa maeneo yaliyofanya vema. Katika vituo 15, vituo 11 vilipata *star*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wetu ni nini? Ni kwamba tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo, nami naifahamu *OPD* yaou pale Bagamoyo jinsi ilivyo, tutashirikiana kwa pamoja nini kifanyike tuhakikishe tunafanya marekebisho makubwa katika *OPD* ile, kwa sababu wagonjwa wengi sana ukiangalia katika jiografia ya pale wanatibiwa pale. Kwa hiyo, Serikali tutafanya kila liwezekano ili mradi tuweze kuweka mazingira yawe mazuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Owenya na mwisho Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Nina swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Tatizo la ukosefu wa dawa ni tatizo kubwa katika mahospitali mengi nchini, kuanzia Zahanati na Vituo vya Afya. *MSD* imeshalipwa zaidi ya shilingi bilioni 80. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba atueleze ni kwa nini *MSD* inashindwa kuagiza dawa wakati wana fedha katika akaunti zao? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI).

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba sasa hivi tunapeleka fedha nyingi sana. Kama nilivyosema hapa mara kadhaa katika Bunge letu hili, kupitia ule mfuko (*basket fund*) peke yake, tuna fedha nyingi ambazo tumezipoleka kule na nimekuwa nikihamasisha Halmashauri mbalimbali wafanye *procurement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumeweka utaratibu kwamba endapo dawa zinakosekana, kuna *prime vendors* ambao wanapatikana kwa ajili ya kuhakikisha dawa zinapatikana. Kwa hiyo, endapo dawa zimeonekana miongoni mwa dawa zilizoombwa kutoka *MSD* zimekosekana, basi tumewaelekeza wataalam wetu katika kanda kwamba waweze kutumia *prime vendors* ambao wamekuwa *identified* kabisa na Serikali, kuhakikisha kwamba tuna-*fast truck* katika suala la upatikanaji wa dawa. Lengo kubwa ni kwamba Hospitali zetu, Zahanati zetu na Vituo vya Afya viweze kupata dawa kwa ajili ya wananchi wetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami napenda niulize swali la nyongeza. Mikakati ya Serikali ni kuboresha afya katika maeneo yote na kupandisha hadhi baadhi ya Vituo vya Afya kuwa Hospitali. Katika Mkoa wa Mtwara tulikuwa tunapandisha hadhi Kituo cha Afya Nanguruwe na Kituo cha Afya Nanyumbu,

kuhakikisha inakuwa Hospitali na tumefikia hatua nzuri ya kufungua kuwa Hospitali. Hata hivyo, Naibu Katibu Mkuu kutoka TAMISEMI alipokuja alisema Vituo vya Afya viendeleo kuwa Vituo vya Afya na tuanze ujenzi upya. Sasa nataka kujua ile ni kauli yake au ni kauli ya Serikali? Kwa sababu Serikali siku zote imekuwa ikitusaidia kufikia hapo ili vituo hivyo viwe hospitali. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Kituo cha Afya cha Nanguruwe na Nanyumbu, Mheshimiwa Mbunge anakumbuka nilivyofika pale, Nanguruwe, Kituo cha Afya ambacho kina *facilities* nyingi sana, kilikuwa na suala zima la ahadi ya Mheshimiwa Rais kuifanya kuwa Hospitali ya Wilaya. Maana yake nini? Naibu Katibu Mkuu wetu alizungumza *technically* kwamba nini tunatakiwa kufanya? Kwamba tukiwa tuna upungufu wa mambo ya hospitali, lazima tujiwekeze katika suala zima la ujenzi wa hospitali zetu za Wilaya. Siyo kama ni kauli yake, isipokuwa ni kauli ya Serikali sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwamba tuvi-*convert* Vituo vya Afya kuwa Hospitali za Wilaya, maana yake tunafisha baadhi ya juhudi, lakini kuna maeneo mengine yana *special preferences*. Kwa mfano, pale Nanguruwe, Nanyumbu au maeneo mengine niliyotembelea, unakuta Vituo vya Afya vingine walikuwa katika *program* ya kufanya kuwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema tuna-*treat* maeneo mengine *case by case*. Kwa *case* kama pale Nanguruwe au Nanyumbu ambapo hata Mheshimiwa Rais mstaafu alipopita pale alitoa ahadi, ahadi ile itaendelea kuwepo pale pale. Lengo kubwa ni kuwasaidia wananchi wale na kwa kiwango kikubwa Serikali imesha-*invest* vya kutosha kukodi na vifaa vingine kuwasaidia wananchi wa eneo lile. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Ofisi hiyo hiyo ya Rais, TAMISEMI, swali namba 132, linaloulizwa na Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 132

Utaratibu wa Upelekaji Fedha katika Halmashauri

MHE. ROSE K. SUKUM aliuliza:-

Serikali hupeleka fedha kwenye Halmashauri baada ya kupokea mpango kazi wa maendeleo au matumizi ya kawaida kwa Halmashauri husika. Kama ikitokea fedha zaidi zimepelekwa katika Halmashauri, maana yake kuna Halmashauri imepelekewa kidogo:-

(a) Je, kwa nini fedha za ziada zisirudishwe Hazina na badala yake zinaombwa kutumiwa na Halmashauri ambayo haikuwa na mahitaji nazo?

(b) Je, Halmashauri ambazo zinakuwa zimepelekewa fedha kidogo zinafidiwa vipi ili kukidhi maombi ya mpango kazi wake?

(c) Je, kwa Halmashauri inayotumia fedha hizo bila ya kusubiri maelekezo kama ilivyo pale inapokuwa ziada kuwekwa kwenye Akaunti ya Amana kama *Memorandum* ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Kifungu Na. 9(2)(e) kinavyoelekeza, endapo itabainika, wanachukuliwa hatua gani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, upelekaji wa fedha katika Halmshauri huzingatia Mpango Kazi (*Action Plan*) ambao huandaliwa kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Fedha hizo hupelekwa na Hazina kila robo mwaka zikiwa na maelekezo ya matumizi. Uzoefu unatuonesha Halmashauri zimekuwa zikipokea pesa pungufu ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa sababu upelekaji wa fedha hizo huzingatia hali ya makusanyo kwa nchi nzima. Hata hivyo, pale inapobainika kuwa fedha zilizopokelewa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa na hakuna maelezo ya matumizi, ni wajibu wa Afisa Masuhuli kuuliza matumizi ya fedha hizo Hazina au Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kabla ya kuzitumia.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya jibu langu, kila Halmashauri hupelekewa fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na kwa kuzingatia mpango kazi. Fedha hupelekwa katika Halmashauri kwa kuzingatia hali ya makusanyo (*Cash Budget*). Kwa mantiki hiyo, hakuna utaratibu wa kufidia bajeti ambayo haikutolewa kwa mwaka husika. Mwongozo wa Bajeti huzitaka mamlaka husika kuzingatia maeneo ambayo hayakupata fedha katika vipaumbele vya bajeti inayofuata ili kupata fedha.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zote zinazotumwa katika Halmashauri huambatana na maelezo ya matumizi ya fedha hizo ambayo hupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa. Pale inapotokea maelezo yamechelewa kufika, ni wajibu kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika kufuatilia Hazina au Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kabla ya kuzitumia. Afisa Masuhuli atakayetumia fedha za ziada bila idhini, anakiuka sheria na taratibu za fedha na anastahili kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sukum.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, lakini nina maswai mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Afisa Masuhuli anayetumia fedha bila idhini ya TAMISEMI au ya Hazina, hastahili kutumia hizo fedha. Je, ni kwa nini ofisi yake haikutekeleza wajibu huo kwa Maafisa Masuhuli ambao wametumia hizo fedha bila idhini yake au bila idhini ya Ofisi yake pamoja na Hazina? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe umekiri kwamba fedha endapo itabainika imeongezwa, lakini (b) yake umesema kwamba hakuna bajeti inayoidhinishwa ikazidi kupelekwa kwenye Halmashauri: sasa ni ipi tuipokee kutoka kwako endapo fedha zimeongezeka? Unasema kwamba haziongezeki, nami nina uhakika kwamba fedha zinaongezeka; sasa naomba kuuliza. Je, kwa wale ambao wameongezewa fedha na wale ambao wamepunguziwa wanafidiwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atupatie majibu ambayo yanastahili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) majibu kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba kwa Afisa Masuhuli yeyote ambaye atakiuka utaratibu wa fedha, maana yake atachukuliwa hatua. Kwa sababu, Mheshimiwa Sukum hakunipa mfano halisi, lakini naomba nimhakikishie, kuna maamuzi mbalimbali ya kinidhamu tumeyachukua kwa Watendaji mbalimbali. Hata baadhi ya Wakurugenzi wengine ambao wameenda nje ya *system* sasa kutokuwa Wakurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kwa sababu mwanzo katika njia moja ama nyingine walikiuka utaratibu wa fedha na kufanya ufisadi mkubwa katika fedha hizo na ndiyo maana Serikali ilichukua hatua. Ni kwa sababu hatuwezi ku-*publicize* hapa kwamba nani na nani, lakini tumechukua

hatua mbalimbali kwa baadhi ya Wakurugenzi ambao ni Maafisa Masuhuli, walioko katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake lingine kwamba fedha sehemu nyingine zinaongezeka na nyingine zinapungua, nimezungumza wazi, hapa kila Mbunge akisimama anazungumza kwamba fedha haziji, fedha haziji. Ndiyo nimesema, kwa uzoefu tuliokuwa nao, mara nyingi sana fedha zile tunazozipanga, ndiyo maana hata Mheshimiwa Kawambwa hapa anaomba fedha za wodi yake hazijafika. Uzoefu uliokuwepo ni kwamba fedha zinazokwenda ni chache kuliko kile kilichopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kunatokea na *special case* kwamba kuna baadhi ya fedha zimeongezeka, ni lazima utaratibu ufuatwe kama nilivyoelekeza katika maelezo yangu ya awali, kwamba lazima atoe taarifa aidha Hazina au Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya ufuatiliaji, fedha hizo zirudishwe katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, Halmashauri mara nyingi tatizo la fedha ni shida kubwa sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia ni jinsi gani atahakikisha Ofisi yake inatimiza yale malengo ya fedha iliyoahidi kwenda kwenye Halmashauri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusu usimamizi, aseme kwa kina atazisimamiaje Halmashauri zake zisifanye ufisadi kwa kuwa, imekuwa ikijirudia mara kwa mara na kutuletea matatizo katika Halmashauri zetu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia suala zima la fedha na fedha hizi zinatafutwa kwa gharama kubwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi.

Naomba nimhakikishie, nilikuwa nikifanya ziara katika Halmashauri zote na nashukuru Mungu sasa nimebakiza chini ya Halmashauri 10 kuzipitia Tanzania nzima. Ajenda yetu ya kwanza ni suala la uadilifu katika usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaambia na nimetoa maelekezo katika maeneo yote kwamba Wakurugenzi na Waweka Hazina sasa lazima wanapokwenda katika Kikao cha Kamati ya Fedha ambapo Madiwani na Wabunge ni Wajumbe hapo, lazima watoe taarifa ya *transactions* katika Halmashauri zao, fedha zilizopokelewa na matumizi yake yalikuwaje. Siyo kupokea lile kabrasha la mapato na matumizi ambapo Mbunge au Diwani anashindwa kujua ndani kilichokuwemo. Kwa hiyo, tumetoa maelekezo haya vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge ambao sisi ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha kwamba tukiingia katika vikao vyetu, tuweze kuzisaidia Halmashauri hizi kwa sababu sisi ndio wafanya maamuzi ambao tunawawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwasihi Wabunge wote kwamba kwa moyo mkunjufu na moyo wa dhati tuzisimamie Halmashauri zetu, *compliance* iwepo na wananchi wetu wapate huduma na maendeleo.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea. Swali namba 133 linaulizwa na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge wa Bukombe.

Na. 133

Ujenzi wa Kilometa Tano Kwenye Mji wa Ushirombo

MHE. DOTO M. BITEKO aliuliza:-

Wakati wa Kampeni za Mwaka 2015, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kilometa tano kwenye Mji wa Ushirombo:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Mji wa Ushirombo zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imekusanya ahadi zote za viongozi na kuweka utaratibu wa jinsi ya kuzitekeleza, ikiwemo ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa tano zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2015, Mjini Ushirombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Serikali ya Awamu hii ya Tano ni kuhakikisha kuwa inatekeleza ahadi zake zote katika kipindi cha miaka mitano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Biteko, swali la nyongeza.

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Kwa kuwa, Serikali imesema kwamba imeshaweka utaratibu wa namna gani itatekeleza ahadi za viongozi, ikiwemo ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni ya ujenzi wa kilometa tano za lami kwenye Mji wa Ushirombo; wananchi wa Bukombe wanataka kujua tu sasa kwamba ni lini? Kwa sababu amesema ndani ya miaka mitano, basi waambiwe ni lini itaanza kutekelezwa katika kipindi cha miaka hii mitano, maana huu ni mwaka wa pili tayari tumeingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ndicho wananchi wanataka kusikia. Nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Biteko kwa kazi kubwa anayoifanya kufuatilia masuala ya miundombinu katika maeneo yake. Namwomba tu, yale ambayo tuliongea ofisini na yale ambayo tuliongea mbele ya Mheshimiwa Waziri wangu ni kweli tutayatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu tuliopewa, kitu cha kwanza ni kuhakikisha tunatekeleza ahadi zote, lakini wakati huo huo zina Wakandarasi *site* ili kuondoa matatizo ya kulipa *interest* pamoja na *idle time*. Hicho ndicho kipaumbele cha kwanza ili tuweze kupata hela nyingi zaidi za kuwekeza kwenye miundombinu badala ya kuwalipa watu ambao wanakaa tu hawafanyi kazi. Kwa hiyo, hicho ni kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha pili ni kuhakikisha ahadi zote za Mheshimiwa Rais na zilizoandikwa katika Ilani ya Uchaguzi tunazipangia ratiba. Sasa tunakwenda miaka kwa miaka; mwaka wa kwanza tumemaliza, mwaka huu mmeona kwamba mambo mengi tumeyaingiza ambayo ni mapya siyo yale ambayo tulikuwa tunategemea wakati ule kwa sababu tumeshapunguza kwa kiwango kikubwa yale madeni ambayo tulikuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ushirombo kwamba ahadi zote katika miaka hii mitatu iliyobakia tutatekeleza ahadi hii tuliyoitoa wakati wa uchaguzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa, jana mmejibiwa mambo mengi na Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na swali linalofuata. Swali namba 134 linaulizwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda.

Na. 134

**Barabara ya Masasi – Nachingwea Kujengwa
kwa Kiwango cha Lami**

MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE)
aliuliza:-

Barabara ya Masasi – Nachingwea imekuwa na matatizo kwa muda mrefu ya kupitika kwa shida:-

Je, barabara hiyo itajengwa lini kwa kiwango cha lami ili kufanya wananchi wa Jimbo la Ndanda waondoe imani kuwa wametengwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Masasi – Nachingwea hadi Nanganga yenye urefu wa kilometa 91 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, mradi huu umeombewa fedha za jumla ya sh. 3,515,394,000/= kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya barabara ya Masasi – Nachingwea yenye urefu wa kilometa 45 imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya kawaida na matengenezo ya muda maalum kila mwaka na inapitika vizuri katika kipindi cha mwaka mzima. Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali barabara hiyo ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka wakati barabara hii inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Masasi mpaka Nachingwea ni kama kilometa 42 na kutoka Masasi mpaka Ndanda ni kama kilometa 40; na kwenye bajeti iliyokuwa imeitengwa ambayo imeombwa mwaka 2017/2018 kama shilingi bilioni tatu, ni fedha ndogo ambayo haiwezi kukidhi kumaliza barabara hiyo. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kukamilisha barabara hiyo kwa kiwango cha lami kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alikuwa ameomba, kwa sababu fedha iliyotengwa ni ndogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali dogo la pili la nyongeza ni kwamba, matatizo ya Jimbo la Ndanda yanafanana kabisa na Jimbo la Momba kule; sasa naomba niulize kwamba barabara ya kutoka Kakozi kwenda Kapele mpaka Namchinka kilometa 50.1 imepandishwa hadhi na Wizara yako, lakini mpaka sasa haijawahi kuhudumiwa na hiyo barabara ni mbovu. Ni kwa nini barabara hizi mnazipandisha hadhi na hamzihudumii kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udogo wa fedha, kitu ninachojaribu kumweleza ni kwamba katika ule mpangilio wa kutekeleza ahadi sasa tumefikia kuanza utekelezaji wa ahadi ya barabara hii na tumeanzia na hizi fedha ndogo kutokana na bajeti tuliyopata mwaka unaokuja wa 2017/2018. Nimhakikishie, katika miaka yote inayofuata, barabara hii itakuwa inaendelea kupewa fedha za kutosha ili hatimaye katika kipindi chetu tulichoahidi, barabara hii itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Kakozi – Kapele na kuendelea ambayo imechukuliwa na *TANROAD*, nimhakikishie tu kwamba tutahakikisha *TANROAD* inapanga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa barabara hii kama ilivyokusudiwa kwa kupandishwa hadhi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Joseph Kakunda na wa mwisho Mheshimiwa Risala Kabongo.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba barabara ya Sikonge – Mibono – Kipili ilipandishwa hadhi tangu mwaka 2009 na hadi leo imetobolewa kwa kiwango cha kilometa 42 tu kati ya 282 ambayo ni kama kilometa tano kwa mwaka; ina maana kwamba hadi itakapokamilika barabara hiyo tunahitaji miaka 44. Je, Serikali iko tayari kuwaambia wananchi wa Sikonge kwamba itajenga barabara hiyo kwa kipindi cha miaka 44 ijayo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri. *Speed* ya ujenzi wa barabara hiyo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa fedha za Mfuko wa Barabara zinazogawiwa mikoani kwa ajili ya matengenezo, haturuhusiwi kutumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kutoboa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ombi lake tunalichukua na tutatafuta namna ya kuhakikisha barabara hii kipande hiki kipya cha kukitoboa tunakitoboa kwa haraka zaidi na naomba wananchi wote wa Sikonge wachukue hiyo ndiyo kama *commitment* ya Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Risala Kabongo.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Barabara ya kutoka Mlowo - Mbozi kwenda

Kamsamba - Momba haipitiki wakati wa mvua, je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami ili kuweza kusaidia uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Katavi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, yale ambayo tumeshayasema kabla ni ya kweli na tutayatekeleza. Tulichokiahidi, kitu cha kwanza ni kukamilisha daraja, tukishamaliza kukamilisha daraja tutashughulikia hii barabara katika kiwango cha lami. Tupeni fursa, hizo pesa ambazo tumezitenga kwa ajili ya daraja kwanza tukamilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika, maadam tunatenga fedha za utengenezaji wa hii barabara kuhakikisha inapitika karibu muda wote, naomba tupeni fursa tutekeleze kwa namna tulivyopanga.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali namba 135, linaulizwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa. Linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 135

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha
Ujenzi wa Barabara**

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE aliuliza:-

Barabara ya kutoka Mgakorongo, Kigarama mpaka Murongo iliwekwa kwenye ilani kuwa itajengwa kwa kiwango cha lami na wananchi waliokuwa ndani ya mradi waliowekewa alama ya 'X' wanashindwa kuendeleza maeneo yao wakisubiri fidia zaidi ya miaka mitano sasa:-

- (a) Je, ni lini wananchi hawa watapewa fidia ili waendelee na mambo ya kimaendeleo?
- (b) Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Sebba, Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Omugakorongo – Kigarama hadi Murongo ni barabara kuu inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Kagera na ina jumla ya kilometa 111. Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii kiuchumi na kijamii ndiyo maana imeiweka kwenye mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami. Hivi sasa upembuzi yakinifu wa barabara hii umekamilika, kazi inayoendelea ni usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania inaendelea na uhakiki wa fidia ya mali zitakazoathiriwa na mradi kulingana na sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Wananchi wote wanaostahili kulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 watalipa fidia mara zoezi la uhakiki litakapokamilika na Wizara yangu itahakikisha kuwa taratibu zote za malipo ya fidia na sheria zinafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kazi za ujenzi wa barabara ya Omugakorongo – Kigarama hadi Murongo zitaanza mara baada ya usanifu wa kina kukamilika na fedha za ujenzi kupatikana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bilakwate.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali

mawili ya nyongeza. Kwa kweli nasikitika sana kuona majibu ambayo ametoa Mheshimiwa Waziri. Hii ni mara yangu ya pili namwuliza hili swali. Mara ya kwanza alinijibu hapahapa Bungeni, akasema kabla ya mwezi wa Sita barabara hii itakuwa imeanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, anapotujibu siyo kuwajibu Wabunge kuwafurahisha, haya ni majibu ambayo tunakuja kuuliza kwa ajili ya wananchi wetu. Naomba Mheshimiwa Waziri atupe majibu ambayo ni ya uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; ni lini barabara hii ujenzi utaanza? Kwa sababu hii barabara ni ya muda mrefu tangu kipindi cha Mheshimiwa Rais Mkapa amestaafu; amekuja Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, sasa anakuja Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwenye bajeti ya mwaka 2017/2018, je, imetengwa pesa kwa ajili ya ujenzi huu kuanza na wananchi wapewe fidia?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie, tunapojibu hapa kwanza tunaonesha dhamira lakini pili, tunaonesha mipango ambayo ipo mbioni. Hatuwezi kuanza ujenzi wa barabara hii kabla ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika. Hakuna aina hiyo ya ujenzi ya barabara kuu na muhimu kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge atupe fursa tukamilishe upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa mwaka huu tunakamilisha kazi hizo mbili. Kwa hiyo, hatujatenga fedha za kuweza kujenga, tumetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha kazi hizo mbili. Nimhakikishie kwamba mara baada ya kazi hizo mbili kukamilika, ujenzi

utaanza, Serikali hii ya Awamu ya Tano inachosema inakusudia kukitekeleza na huwa inakitekeleza. (Makofi)

MWENYEKITI: Niangalie wa huko huko, Mheshimiwa Gashaza, Mbunge wa Ngara.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Dar es Salaam – Isaka – Rusumo, inayojulikana kama *central corridor* ni barabara inayohudumia nchi takriban nne ambazo zipo kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, lakini kipo kipande cha kilometa 150 kutoka Lusahunga kutoka Rusumo; Nyakasanza kwenda Kobelo mpaka Bujumbura. Kipande hiki kimekuwa ni kero kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana ambao ndiyo huu tunamalizia 2016/2017 barabara hii ilitengewa shilingi bilioni tano, lakini mpaka sasa hivi ukarabati unaofanyika ni mdogo na kwa bajeti hii ya 2017/2018 tumetengewa shilingi bilioni 1.19 tu kiasi kwamba haiwezi kufanya ukarabati unaoridhisha. Je, ni lini Serikali sasa itaweza kutenga fedha za kutosha ili kukarabati kipande hiki ambacho ni kero kwa Watanzania wanaotumia barabara hii na wageni wanaotoka kwenye nchi za Burudi na Rwanda, Kongo na Uganda ili barabara hii iweze kukidhi viwango na kukidhi mahitaji?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gashaza kwa sababu anapita hii barabara, anafahamu kazi kubwa inayofanywa kuirekebisha hiyo barabara kuanzia Isaka na kuendelea. Tunakwenda kwa hatua; mimi mwenyewe nimeona ukarabati ulioanzia Rusahunga kuelekea Rusumo. Nimeiona, nimepita hiyo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge, aridhike na hiki kinachofanyika na kwa vyovyote vile, baada ya kukamilisha hii, tutakwenda kukamilisha kipande kilichobakia. Suala siyo rahisi kupata fedha zote za kutosha kuikamilisha barabara yote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuikarabati barabara hii mpaka ikamilike. Tutafika Rusumo, tutafika hii njia inayokwenda Burundi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Savelina Mwijage.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa ahadi za barabara ya Karagwe kwenda mpaka Benako kutoka Nyakaanga zimekuwa kero kwa muda mrefu; nimeingia Bungeni mwaka 2005 barabara ya kwenda mpaka Mlongwe nimeiongea barabara ya kutoka Nyakaanga kwenda Benako nimeiongea:-

Ni lini Serikali itachagua moja; kutengeneza upande na mmoja kuimaliza na kuingia wa pili? Mnatafuta ma-*engineer* na Wakandarasi ambao hawana viwango. Barabara unatengeneza siku mbili, tatu, barabara inaharibika. Lini mtatafuta ma-*engineer* wa uhakika wa kutengeneza barabara zikawa za viwango? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Mbunge kwa makini anachokiongelea. Huwa naamini kwamba tunachagua Wakandarasi makini, ila kwa kauli yake inaonekana tunatakiwa tuongeze nguvu zaidi na macho yaangalie zaidi ili kuhakikisha kweli tunapata Wakandarasi wanaoweza kusaidia kufanya kazi bila kurudia rudia mara nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa ushauri wake.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali 136, linaulizwa na Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi, linaelekezwa kwa Waziri wa Mambo Katiba na Sheria.

Na. 136

Kukamatwa kwa Meli ya Uvuvi MFV Tawariq

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 Serikali ilikamata Meli ya Uvuvi MFV TAWARIQ, nahodha wake *Tsu Chin Tai* pamoja na watu wengine 36 walishtakiwa Mahakama Kuu kwa kesi ya Jinai Na. 38 ya mwaka 2009. Kwa amri ya Mahakama samaki tani 296.3 wenye thamani ya sh. 2,074,000,000/= waligawiwa bure. Aidha, meli hiyo ilizama ikiwa inashikiliwa kama kielelezo. Tarehe 23 Februari, 2012 watuhumiwa wawili walihukumiwa kifungo na walikata rufaa Mahakama ya Rufaa ambapo tarehe 25 Machi, 2014 waliachiwa huru na sasa ni miaka saba tangu meli hiyo ikamatwe.

Je, Serikali itarudisha lini sh. 2,07,000,000/= ambazo ni thamani ya samaki na fedha ambazo ni thamani ya meli kwa Mawakili wa Nahodha wa Meli hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mbunge wa Nungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 8 Machi, 2009 kikosi kazi kilichokuwa kikifanya doria katika ukanda wa kiuchumi wa Bahari Kuu ya nchi yetu (*Exclusive Economic Zone*) katika Bahari ya Hindi kilifanikiwa kukamata meli ya uvuvi iitwayo Na. 68 BU YOUNG ikivua katika bahari yetu bila

kibali. Meli hiyo ilikuwa ikiongozwa na nahodha aitwaye *TSU CHIN TAI*, raia wa Jamhuri ya Watu wa China na alikuwa pamoja na wenzake 36. Pamoja na kuwa jina la meli hiyo ni No. 68 *BU YOUNG*, meli hiyo ilikuwa inatumia pia jina la *TAWARO 1* na *TAWARIO 2* ili kuficha jina halisi na kuendeleza kufanya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahodha wa meli hiyo, yaani *TSU CHIN TAI* na wenzake walishtakiwa Mahakama Kuu katika kesi ya jinai Na. 38/2009 ambapo nahodha *Tsu Chin Tai* na *ZHAO HANQUING* aliyekuwa wakala wa meli hiyo, walitiwa hatiani. Wawili hawa waliomba rufaa Mahakama ya Rufani ambapo mwaka 2014 Mahakama hiyo ilibatilisha na kufuta mwenendo mzima wa kesi baada ya kubaini kuwa kulikuwa na kasoro katika taratibu za kuwafungulia mashtaka. Kwa ufupi, hawakuwahi kushinda kesi na Mahakama ya Rufani haikuwahi kutamka kuwa wako huru kwa sababu hawana hatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uamuzi huo wa Mahakama ya Rufani, Mkurugenzi wa Mashtaka alifungua mashtaka upya katika Mahakama ya Hakimku Mkazi Kisutu na baadaye kuondoa mashtaka dhidi yao tarehe 22/8/2014. Baada ya miaka miwili, yaani 2016 Wakili *Captain* Bendera alifanya maombi namba 108/2016 katika Mahakama Kuu akimwakilisha Bwana Said Ali Mohamed Al Aرامي ambaye hakuwa mmoja kati ya washtakiwa katika kesi ya msingi akiomba apewe meli au *USD 2,300,000.00* kama thamani ya meli hiyo na sh. 2,074,249,000/= kama thamani ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama Kuu baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, ilikubaliana na hoja za Jamhuri na kutupilia mbali maombi hayo. Katika uamuzi wake, Mahakama ilitamka yafuatayo, naomba kunukuu: "*this application was uncalled for, superfluous and amounts to abuse of court process, thus devoid of any merit.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la kisheria na wahusika wanaweza kuendelea kulishughulikia kupitia Mahakamani.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na mlolongo mrefu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa mbalimbali duniani wanapozikamata meli kama hizi wanazitaifisha kwa ajili ya kujenga uchumi wa ndani ya nchi yao. Ajabu sisi meli ile tumeiacha imezama mahali (bandarini) ambapo hapana upepo, hapana wimbi wala hapana dhoruba yoyote na kupoteza thamani kubwa ya meli ile. Je, Serikali inatamka tamko gani kuhusu suala hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa washtakiwa wameingizwa hatiani: Je, utaratibu gani uliotumika kuwaachia huru mpaka muda huu wakawa wako nje? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA (K.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ametolea mifano au ameelezea uzoefu wa nchi nyingine wanapokamata vyombo vya baharini au meli kama hizi. Kwanza, napenda tu kusema kwamba kwa Tanzania kufanya uamuzi ule waliouchukua imesaidia sana kukemea au ku-*deter* uvuvi haramu katika bahari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia matukio ya aina hii kuanzia mwaka 2009 tangu uamuzi huu ulipochukuliwa, kwa kweli hata Wizara ya Uvuvi itakuwa ni shahidi na vyombo vyetu vinavyofanya doria katika bahari zetu, matukio ya aina hii yamepungua sana. Kwa hiyo, kwa kweli na sisi Tanzania kama nchi tumeweka mfano, tumeweka *precedent* ili nchi

nyingine na watu wengine wenye masuala kama haya wasitumie bahari zetu kwa makosa na kuchezea rasilimali zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, kwamba ni utaratibu gani uliotumika katika kuwaachia huru watuhumiwa; kama nilivyoeleza, mwaka 2014 Mkurugenzi wa Mashtaka ali-*enter nolle* kupitia Kifungu cha 98 ambacho anayo mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na masuala mengine yaliyofuata hapo ilikuwa ni masuala ya diplomasia na waliweza kuachiwa huru.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali 137, linaulizwa na Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, linaelekezwa kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Na.137

Ujenzi wa Bomba la Maji Ruvu Juu - Kimara

MHE.SILVESTRY F. KOKA aliuza:-

Kazi kubwa ya ujenzi wa Mradi wa Bomba la Maji kutoka Ruvu Juu kupitia Kibaha Mkoani Pwani hadi Kimara Jijini Dar es Salaam, imeshafanyika.

Je, ni lini mradi huo kwa upande wa Kibaha Mjini utakamilika na wananchi waweze kupata maji ya uhakika?

NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutumia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India, imetekeleza mradi wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu, ulazaji wa bomba kuu la kutoka Mlandizi hadi Kimara na ujenzi wa tanki jipya la

Kibamba. Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu uliogharimu Dola za Marekani milioni 39.7 umeongeza uwezo wa mtambo wa kuzalisha maji kutoka lita milioni 82 hadi lita milioni 196 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na Ujenzi wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara kumeongeza uwezo wa kuzalisha maji ya kutosha na hivyo maeneo yenye mtandao wa mabomba ya usambazaji ya Mlandizi, Kibaha na Kiluvya pamoja na maeneo ya Kibamba, Mlonganzila, Mbezi kwa Yusufu, Mbezi mwisho, Kimara, Kilungule, Mavurunza, Baruti, Kibo, Kibangu, Tabata, Segerea, Kinyerezi, Vingunguti, Kipawa, *Airport* na Karakata yameanza kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DAWASCO* wako katika kampeni ya siku 90 ya kuunganisha wateja wote wanaohudumiwa na mtambo wa Ruvu Juu na Ruvu chini. Kwa upande wa Kibaha, *DAWASCO* wamepanga kuwaunganishia maji wateja wapya elfu 30. Ombi langu kwa wananchi, wapeleke maombi ya kuunganishiwa maji katika Ofisi za *DAWASCO* iliyoko katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara yangu itaendelea kutenga fedha kwenye programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Awamu ya Pili, ili kupanua mtandao wa mabomba ya kusambaza maji na kuweza kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Koka.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ya mradi huu mkubwa kwa takriban shilingi bilioni 90 ambao umekamilika. Pamoja na pongezi hizi, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Bado kuna tatizo la msukumo wa maji kutoka Ruvu Juu ili yaweze kuwa na *pressure* ya kutosha kuwafikia watejea, tatizo linalotokana na uhafifu wa umeme. Je, Serikali ina mpango gani wa

kurekebisha tatizo hili, ili mradi huu uweze kuwa na mafanikio makubwa zaidi hususan kwa wananchi wa Kibaha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; pamoja na kazi nzuri hii, lakini bado maeneo ya Kidenge, Muheza, Kidagulo, Kikalabaka, Mikongeni na Mbwawa hawajakamilishiwa mradi wa usambazaji wa maji ili waweze kufaidi mradi huu. Je, kupitia bajeti hii tunayokwenda nayo Mheshimiwa Waziri yupo tayari kushughulikia na kuhakikisha miradi hii inakamilika ili wananchi waweze kupata huduma hii nzuri kwa mradi huu ulio bora ambao umeshakamilika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Isack Kamwelwe, majibu.

NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Koka kwa jinsi ambayo anawapenda wananchi wake wa Kibaha Mjini. Kwa sababu mara zote anafuatilia kwa kupiga simu kwa kuja Ofisini moja kwa moja, kumwona Mheshimiwa Waziri pamoja na mimi kuhusiana na tatizo la maji la Mji wa Kibaha, kwa sababu Mji wa Kibaha kwa sasa unapanuka sana. Swali la kwanza, *pressure* ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji tuligundua kwamba hakukuwa na umeme wa kutosha ili kuweza kuendesha mtambo ule kwa sababu ni mkubwa. Kwa sababu hiyo, tulitenga fedha na tayari sasa kazi inafanyika na imeanza kukamilika ili kuwa na umeme wa kutosha ambao utaweza kuendesha mtambo uliojengwa ambao ni mtambo mkubwa. Kwa hiyo, hili suala Mheshimiwa Koka ni kwamba tunalimaliza muda wote wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama nilivyozungumza katika swali letu la msingi kwamba kupitia awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, tunatenga fedha kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Kibaha na maeneo yote yanayopitiwa na bomba kuu la kutoka Ruvu kwenda Dar es Salaam tutahakikisha kwamba

tunaweka miundombinu ya kutosha ili wananchi waweze kupata maji, umbali wa kilomita 12 kutoka eneo la bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba programu hiyo tunayo ambayo imeanza kutekelezwa kwenye mwaka wa fedha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Joseph Haule na wa mwisho Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika ziara yake Naibu Waziri pale Wilayani Kilosa alitembelea bwawa la Kidete na alijionea jinsi ambavyo limekuwa likileta madhara makubwa ya mafuriko na kuharibu mpaka reli kwenye Wilaya yetu ya Kilosa. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwawa hili la Kidete ambalo ni muhimu kwa wananchi wa Wilaya ya Kilosa? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kabisa nilitembelea hilo eneo na nikaenda kuona shida iliyoko katika lile bwawa. Palikuwa na mkataba lakini tayari Serikali imechukua hatua ya kuhakikisha kwamba sasa unafanyika usanifu upya na fedha ilishatengwa katika bajeti ya mwaka huu tunaokwenda nao. Kwa hiyo, wakati wowote tutatangaza tenda baada ya kukamilisha usanifu mpya ili tuweze kulijenga lile bwawa katika *standard* ile inayotakiwa isilete madhara tena kwa wananchi wa Kilosa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali moja tu dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa, Mkoa wetu wa lringa una mito kama Ruaha, Mto Lukosi na kadhalika, lakini wananchi wamekuwa wakipata shida sana kwa suala la maji hasa vijijini ikiwepo Kilolo na Mufindi. Ni kwa nini Serikali

sasa isitumie mito hii kuondoa huu upungufu ambao upo katika Mkoa wetu wa Iringa? (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mkoa wa Iringa una utajiri mkubwa sana wa mito ikiwepo Ruaha Mkuu, lakini bado kuna Ruaha Mdogo, kuna Mto Lukosi ambao unatokea maeneo ya Kilolo. Kutokana na utajiri huo wa kuwa na mito mingi, kwanza kabisa Mto Ruaha Iringa Mjini tumeutumia, maji yanapatikana kwa asilimia 100 katika Mji wa Iringa. Sasa hivi tunaanza kusambaza maji kuyapeleka nje ya Mji wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Mto Lukosi, nimeenda kule Kilolo, sasa hivi tunafanya utaratibu wa kuhakikisha tunasanifu mradi ili tuweze kutoa maji Mto Lukosi kuyapeleka maeneo yanayopitiwa na huo mto kuhakikisha kwamba maeneo mengi ya Iringa yanakuwa na maji ya kutosha ambayo ni safi na salama.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea tuyamalize haya maswali mawili yaliyobaki. Muda ndiyo huo. Swali namba 138, linaulizwa na Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, linaelekezwa kwa Waziri wa Afya.

Na. 138

Upungufu wa Dawa Katika Hospitali za Serikali

MHE. ILIVER D. SEMUGURUKA aliuliza:-

Upungufu wa dawa katika Hospitali mbalimbali za Serikali nchini umeleta athari kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Kagera na Wilaya zake zote:-

Je, Serikali inakiri uwepo wa upungufu wa dawa nchini? Kama inakiri hivyo, inawaambia nini wananchi kuhusu tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mojawapo ya vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni kuboresha upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa umma hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hii, Serikali ya Awamu ya Tano ilichukua juhudi za makusudi kwa kuongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 hadi kufikia shilingi bilioni 251.5 katika mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 jumla ya sh. 112,198,920,456/= zilishatolewa na kupelekwa Bohari ya Dawa ili kuviwezesha vituo vya kutolea huduma za afya vya umma kupata mahitaji yake ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ongezeko hilo la fedha, hali ya upatikanaji wa dawa nchini imeimarika na kumbukumbu zilizopo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zinaonesha kuwa hali ya upatikanaji wa dawa nchini imeimarika kwa kufikia asilimia 83. Kadhalika, hadi kufikia tarehe 15 mwezi Januari, 2017 Mkoa wa Kagera pekee umepokea kiasi cha sh. 4,150,767,216/= kupitia Fungu Namba 52, yaani Wizara ya Afya, kwa ajili ya kununulia dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Semuguruka.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa sasa *MSD* ina Bohari Kikanda. Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua Bohari ya *MSD* kila Mkoa ili kurahisisha usambazaji wa madawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Serikali imejiandaaje kudhibiti upotevu, wizi wa dawa kwa watumishi wasio waaminifu katika zahanati na vituo vya afya? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la kwanza kuhusu Serikali kujenga bohari za dawa kila mkoa; kwamba tuna mpango gani; kwa sasa hatujawa na mpango wa kufanya hivyo kwa sababu tunaamini utaratibu wa kuwa na bohari kwenye kila kanda bado haujakwama. Ni kwamba tunahitaji kufanya maboresho kidogo tu ili tuweze kuongeza tija na ufanisi kwenye kuhakikisha vituo vya umma vinapata dawa kadri ambavyo vinahitaji na kwa haraka kadri ambavyo inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mfumo wetu wa sasa hivi wa *Supply Chain Management*, tunaamini bado haujakwama na ndiyo maana tumeendelea kuuboresha. Tulikuwa na changamoto kidogo za kifedha, ambazo kama ambavyo sisi Wabunge ni mashahidi na naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa azma yake thabiti ya kuongeza upatikanaji wa dawa kwa kutuongozea bajeti kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, changamoto ya kifedha tuliyokuwanayo ambayo ilikuwa inashusha tija na

ufanisi, sasa inaelekea kuondoka na mfumo wa upatikanaji wa dawa umeimarika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu udhibiti, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote, Madiwani wote na Viongozi wote kuanzia Viongozi wa Mikoa na Wilaya washiriki kikamilifu katika kusimamia udhibiti wa mfumo wa upatikanaji wa dawa kwenye vituo vyetu kwa sababu, jambo hili haliwezi kuwa ni la sisi tu tuliopo Fungu 52, kwa maana ya Wizara ya Afya pekee. Kwa sababu, mfumo wetu wa udhibiti upo, kwamba kwenye kila zahanati, kila Kituo cha Afya na kwenye kila hospitali, kuna Kamati ya Udhibiti wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi ambapo ndani yake kuna viongozi wa kuchaguliwa na kuna watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba, mfumo huu hausimamiwi ipasavyo. Kama ungefanya kazi ipasavyo, kwa hakika, tungeweza kudhibiti wizi na ubadhirifu wa madawa ambao umekuwa ukitokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, kama kuna mtu ana taarifa yoyote ile ya mahali ambapo kuna wizi ama upotevu wa dawa ambao umejitokeza, atupe taarifa na sisi tutachukua hatua haraka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anna Gidarya na Mheshimiwa Bulembo wa mwisho.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ugonjwa wa *fistula* ni ugonjwa ambao umeenea karibu Tanzania nzima. Ugonjwa huu unawadhallisha akinamama, hususan mikoa yetu ambayo ina jamii ya wafugaji, watu ambao hawahudhuria mara nyingi kliniki. Je, Wizara ina mpango mkakati gani wa kutoa elimu hii kwa kila Wilaya, hasa kwa jamii hii ya wafugaji? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Gidarya kwamba ugonjwa wa *fistula* unawadhallisha sana mama zetu, shangazi zetu, dada zetu katika jamii. Ni jambo ambalo mwanaume yeyote ambaye anawapenda mama zetu na dada zetu hawezi kukubaliana nalo. Nami kama Balozi wa Wanawake nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kuboresha huduma za uzazi kwa sababu ndiyo kisababishi kikubwa cha ugonjwa wa *fistula* ili kupunguza *cases za fistula* ambazo zimekuwa zikijitokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango tulionao kwa sasa ni kutumia kliniki zetu za uzazi ambazo zipo kwenye kila kituo cha kutolea huduma za afya, kuanzia ngazi ya zahanati kwenda ngazi ya kituo cha afya, ngazi ya hospitali ya wilaya mpaka ngazi ya hospitali za rufaa, kutoa elimu kwa akinamama wote na akinababa wote ambao wanafika kuhudhuria kliniki za uzazi salama katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto zinazojitokeza za tiba zimekuwepo na tunaendelea kuzipunguza kwa kuendelea kutoa ujuzi, lakini pia elimu kwa umma juu ya kuwahi kupata huduma za uzazi ili wasipate madhara yanayotokana na mchakato wa uzazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulembo.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo linalozikabili zahanati nyingi nchini siyo upungufu wa dawa tu, bali pia huduma kwa akinamama wajawazito, hususan katika wodi zao huduma ni mbaya, ni hafifu, vifaa stahiki hakuna: Je, ni lini Serikali itahakikisha inaboresha afya kwa akinamama wajawazito katika hospitali na zahanati zote za Mkoa wa Kagera? (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Eeh, leo! Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, utoe majibu ya uhakika hapo, kama Balozi wa Wanawake. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nitoe majibu ya uhakika kwamba, kwanza nimkumbushe Mheshimiwa Halima Bulembo kwamba kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika vipaumbele vitano kwenye Sekta ya Afya ambavyo vimeandikwa mle ni pamoja na kuboresha huduma za akinamama wajawazito na watoto.

Kwa maana hiyo, naye kama Mwana-CCM mwenzangu lazima anafahamu kwamba jitihada za kupunguza matatizo na changamoto mbalimbali zilizopo kwenye huduma za akinamama wajawazito, zimekuwepo, zitaendelea kuwepo na ndiyo maana hata leo tutakapowasilisha bajeti yetu ataona tuna mikakati mahususi ambayo imejikita kwenye kuboresha huduma za uzazi kwa akinamama wajawazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili ni jambo ambalo Mheshimiwa Rais mwenyewe alilizungumza pia hapa Bungeni na sisi wakati anatukabidhi majukumu haya alituagiza tulisimamie kwa nguvu za kutosha. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa hakika hatulifanyii mzaha hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba huduma za uzazi zitakuwa bora na yeye atajifungua salama kadiri Mungu atakavyomsaidia. *(Kicheko/Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali letu la mwisho kwa leo. Swali namba 139, linaulizwa na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, linaelekezwa kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Na. 139

Ujenzi wa Jengo la Maktaba Chuo cha Ualimu Korogwe

MHE. MARY P. CHATANDA aliuliza:-

Mwaka 2001, Chuo cha Ualimu Korogwe kwa kushirikiana na wananchi, walianza ujenzi wa maktaba ambayo bado haijakamilika; na kwa kuwa wanachuo na wananchi wa Korogwe wanahitaji sana maktaba hiyo:-

Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia juhudi zilizokwishaanza ili kukamilisha jengo hilo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa maktaba hiyo kwa Wanajumuiya wa Chuo cha Ualimu Korogwe na wananchi kwa ujumla, Wizara yangu iko tayari kusaidia ujenzi wa maktaba hiyo na hivyo itatuma wataalam kwenda kufanya tathmini ya hatua iliyofikiwa na msaada unaohitajika ili ujenzi huo uweze kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na jinsi wananchi wa Korogwe wanavyoshirikiana vizuri na Mbunge wao, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuboresha elimu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mary Chatanda, swali la nyongeza.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nampongeza Waziri wa Elimu na Naibu

wake na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kufuatana nami ili aweze kuangalia lile jengo ili kusudi waweze kutoa kitu ambacho kinalingana na kazi ambayo inakusudiwa kumaliziwa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni ndiyoooo! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Haya, tumemaliza kwa leo. Ni sababu ya muda tu Waheshimiwa.

Matangazo ya wageni waliopo leo hapa Bungeni, kwenye Jukwaa la Spika, tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kutoka Wizara yake ambao ni Ndugu Sihaba Nkinga, Katibu Mkuu Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii. Tunaye pia Dkt. Mpoki Ulisubisya, Katibu Mkuu Idara Kuu ya Afya; na pia tunaye Dkt. Zainab Chaula, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), anayeshughulikia afya. Pia hawa wageni watatu wameambatana na Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi, Idara na Maafisa mbalimbali waliopo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Karibuni sana, leo ndiyo Wizara yetu. *(Makofi)*

Wageni wengine, sidhani kama wanamjumuisha na Mheshimiwa Halima Bulembo, lakini ni wajawazito 12 wanaowawakilisha wenzao Tanzania nzima. Nirudie? Eeh! *(Kicheko/Makofi)*

Wageni wengine ni wajawazito 12 wanaowawakilisha wenzao Tanzania nzima. Karibuni sana. Pia Wameambatana na Wauguzi wao wawili na Wajumbe wawili kutoka Muungano wa Utepe Mweupe wa Uzazi

Salama, wakiongozwa na Ndugu Rose Mlay, Mratibu wa Taifa wa *The White Ribbon Alliance for Safe Motherhood in Tanzania*. Karibuni sana. (Makofi)

Pia, tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliotembelea hapa Bungeni kwa ajili ya mafunzo.

Mheshimiwa Joseph Selasini, Mwenyekiti wa Jumuiya ya *St. Thomas More* hapa Bungeni anawatangazia Wakristo Wakatoliki wote, leo Jumatano, terehe 3 Mei, 2017 kutakuwa na Ibada ya Misa mara baada ya kuahirisha Bunge saa 7.00 mchana katika Kanisa Dogo lililopo ghorofa ya pili, Ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wengine pia mnakaribishwa kushiriki katika ibada hii takatifu.

Hayo ndio matangazo niliyonayo. Katibu!

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

MBUNGE FULANI: Kuhusu jambo la dharura.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Nitajie tu jina lako Mheshimiwa.

MHE. RHODA KUNCHELA: Rhoda Kunchela.

MWENYEKITI: Nitajie jina lako.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Innocent Bashungwa.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Rhoda Kunchela.

MWENYEKITI: Kwa hiyo, nina hawa Waheshimiwa Yussuf Hussein, Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Innocent.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Na Kakunda, hukuniona.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, nikisema msimame, basi msimame. Mheshimiwa Joseph Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7). Wakati nilipouliza swali la nyongeza kuhusu barabara ya Sikonge – Mibono – Kipili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali hairuhusiwi kuweka bajeti kubwa kwa ajili ya kutoboa barabara, lakini hapo hapo akaweka *commitment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na jibu hilo, naona kama siyo sahihi kwa sababu Serikali ninavyojua jinsi inavyohudumia watu, inaruhusiwa kupanga bajeti kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba utoe maelekezo tupate ufafanuzi wa kina jinsi Serikali itakavyotekeleza ile *commitment* ambayo wameisema hapa ili kusudi wananchi wangu wa Sikonge waweze kupata *commitment* ambayo inaridhisha. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutumia Kanuni ya 47(1) kuzungumzia jambo la dharura ambalo limetokea Jimboni kwangu Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Mguruka Kata ya Bwelanyange Jimbo la Karagwe hivi ninavyozungumza, kaya zaidi ya 300 zimepewa *Eviction Order* na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *Game Officers* wa Pori la Akiba la Kimisi, kwamba wananchi ambao wanaishi kwenye Vitongoji vya Mguruka, Rweizinga na Misenyi waondoke kwenye vitongoji hivyo ndani ya siku tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linasikitisha kwa sababu Kijiji cha Mguruka kimekuwepo kabla hili Pori la Akiba la Kimisi halijawa *gazetted* kisheria. Vitongoji hivi viko chini ya TAMISEMI kwa mujibu wa Sheria za TAMISEMI na vinapata huduma kama kawaida.

Kwa hiyo, *Eviction Order* hii ambayo imetolewa na Wizara ya Maliasili ni kandamizi, onevu na inawarudisha wananchi kwenye umaskini. Kwa sababu hivi ninavyozungumza, wananchi hao wamelima, wana mifugo na hivi sasa wameambiwa ndani ya siku tatu wawe wameondoka kwenye hayo maeneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hili jambo ni mahususi na changamoto za migogoro kati ya Vijiji na Mapori ya Akiba hayako Karagwe tu, ni nchi nzima, naomba kupitia Kanuni ya 47(1) nitoe hoja ili jambo hili lijadiliwe na Bunge na naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mniunge mkono. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea. Mheshimiwa Yussuf Hussein.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nina tatizo hapa na nimeshaliripoti kwa Watendaji mara tatu. Watendaji walichukua hatua wakaniambia wameshindwa. Nimeshaliripoti kwenye kiti chako mara tatu akiwepo Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti, Mheshimiwa Zungu, sijapata jibu. Jana nimeliripoti nikaambiwa nikiingia Bungeni jioni tatizo hilo litakuwa limerekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi sasa ninapozungumza, tatizo hilo halijarekebishwa. Kiti changu ninachokalia kimevuka hii *cover*, imekuwa kama teitei, inachafua nguo na kuharibu kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mwongozo wako, nitumie kanuni gani ili niweze kuingia na fundi humu ndani anitengenezee hiki kiti? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7), kwa sababu ya muda sitaisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea katika Mkoa wa Katavi, Manispaa ya Mpanda kuna wafanyakazi wanne wamelazwa hospitali; wawili wana *pressure* lakini wengine wametundikiwa *drip*. Hii ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alipokea ripoti ya majina ya watuhumiwa wanaotumia vyeti feki. Katika hao wagonjwa ambao wapo hospitali wengine walikuwa masomoni wametuhumiwa kwamba wana vyeti feki, lakini wengine ni wastaafu na wengine hawajamaliza wala hawajawahi kusoma sekondari lakini pia wametuhumiwa wana vyeti feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, kama ni Serikali ilitoa ripoti hii bila kuhakiki vizuri haya majina na hawa watuhumiwa ambao sasa wapo hospitali wengine wamelazwa na wengine wamezimia; nini tamko la Serikali kwamba hawa watu waliotuhumiwa na kwamba wameonewa na ikiwa kuna baadhi ya watu wanamzunguka Mheshimiwa Rais lakini pia hawajaguswa: Sasa hawa watu ambao wameonewa nini kifanyike ili wasafishwe na nini tamko la Serikali ili kuwanusuru hali yao ya kiafya. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nianze na hili la Mheshimiwa Yussuf Hussein. Niseme, kalieleza kwa uchungu, lakini naamini Waheshimiwa Wabunge wengine wangesimama. Jirani yangu hapo kwenye kiti changu ninapokaa Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, kiti chenyewe; na jirani yangu Mheshimiwa Mussa pale; naweza nikataja kule ambapo huwa napitia mimi kule.

Kwa hiyo, hili ni tatizo ambalo Ofisi ya Katibu wa Bunge wanalifanyia kazi. Wanaomba uvumilivu tu Waheshimiwa Wabunge; pia na Serikali watuelewe kwa hili kwa sababu Bunge liliahidi kulishughulikia suala hili na walitegemea zile fedha ambazo zilipaswa kuwa zimefika sasa kwamba washughulike, maana lilikuwa kwenye bajeti ya mwaka huu. Kwa hiyo, bado ni matarajio yetu kwamba hilo litatekelezwa na upande wa Serikali ili turejeshe heshima ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Hussein huhitaji kuingia humu na fundi wako, hapana. Bunge litatekeleza hayo ili muweze kukaa kwa staha, lakini pia nguo zenu ziendelee kuwa nadhifu na mavazi yenu yaendelee kuwa nadhifu. Kwa hiyo, hilo limekaa vizuri, tuvumiliane tu. Nami pia nitakwenda kumkumbushia Mheshimiwa Spika na Katibu wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Joseph Kakunda, nadhani kama hukujibiwa kikamilifu na Mheshimiwa Naibu Waziri, nisingependa sana nichukue muda wa Bunge hili kwenda kusoma *Hansard* ya jibu lililotolewa. Kwa vile Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Naibu wake aliyejibu swali kwa niaba yake yupo, suala hili mwongozo wangu ni kwamba hebu sasa wakupatie yale maelezo mazuri kuhusiana na matumizi ya fedha za barabara kwa wananchi wa Sikonge. Jana tu tumepitisha bajeti ya Wizara hii, nadhani ndiyo muda muafaka kuweza kulisemea suala hili kama kweli kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha sehemu ya barabara ambayo umeisemea imetengewa fedha.

Mheshimiwa Innocent Bashungwa, dharura. Nawavumilieni tu. Umesikika, lakini ni jambo ambalo halikutokea leo Bungeni hapa mapema, lakini Serikali imo

humu Bungeni na maeneo haya kama yanatambuliwa kisheria na Wizara yenyewe, wewe unasema wananchi hawa jana wamepewa *Eviction Order* waondoke ndani ya siku tatu, basi nadhani Serikali kwa ajili ya kuwapatia *comfort* wananchi hawa katika maeneo unayowakilisha wewe, mwongozo wangu ni kwamba Serikali ije itoe tu maelezo kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wa maeneo hayo na mengine ambayo yataguswa na operesheni hiyo ili waweze kujua ni nini ambacho kinaendelea. Hii operesheni naamini inaweza ikafika hata kwangu Bariadi kule Serengeti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuwe na uelewa wa pamoja kama viongozi wa nchi hii na kwa faida ya wananchi wetu wa maeneo hayo. Serikali itajipanga ni lini wanataka kutoa kauli hiyo katika Bunge hili. Kama Waziri anaweza akasimama baadaye akalisemea, itakuwa ni vyema tu.

Mheshimiwa Kunchela, hawa wagonjwa umesema ni mshtuko wa moyo wa vyeti! Sasa nadhani mwongozo wangu kwa hilo, Serikali hii ni makini sana, napenda kuamini hivyo na Waziri mwenye dhamana ya masuala haya yumo Bungeni. Nadhani anaweza akalitolea taarifa kwa hao ambao wameonewa au wanajiaminisha kwamba wameonewa au wanadhani kwamba wameonewa ni nini wafanye; na utaratibu gani ufuatwe? Nadhani ndicho kinachoweza kufanyika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huo ndiyo mwongozo wangu. Sasa kwa upande wa Serikali, kama Mheshimiwa Profesa Maghembe unataka kusema hapa, sawa. Mheshimiwa Angellah Kairuki. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumepokea miongozo hapa miwili, tunaona kwamba hiyo tunaweza tukaitolea maelezo. Kwa mwongozo unaohusu Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Waziri

ameridhia Mheshimiwa Naibu Waziri atoe maelezo sasa hivi. Mwongozo unaohusu masuala ya utumishi na vyeti atafuatia Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, basi tunaomba Serikali i-respond kwenye mambo hayo. (Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana *Chief Whip*. Mheshimiwa Dkt. Eng. Ramo Makani.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kutoa maelezo kwa ufupi kama ifuatavyo ili niweze kujenga mazingira ya kukuwezesha kutoa mwongozo kuhusu suala lililoletwa mbele yako na Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Innocent Bashungwa pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Kagera, lakini pia hata Mkoa wa jirani wa Kigoma kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakifuatilia masuala yanayohusiana na mahusiano baina ya wananchi na hifadhi zilizopo kwenye maeneo yao na hususan wahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo Mheshimiwa Mbunge amelileta mbele ya Bunge leo hii, liliwahi kuletwa pia na Mheshimiwa Magdalena Sakaya na maelezo yaliyotolewa awali yalikuwa kama ifuatavyo; na nitayatoa nikiwa nimeweka na nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa upande wa Serikali kwa sasa tunayo Kamati inayohusisha Wizara nne kwa kuanzia; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inachokifanya sasa hivi, inaratibu kazi ya awali itakayotoa mwongozo juu ya kuweza kutatua tatizo hili la mahusiano kati ya wananchi wanaoishi jirani ya hifadhi na hifadhi zenyewe. Sasa jambo

hili kama ambayo wewe na Wabunge wote kwa ujumla tunavyofahamu, kwanza ni la muda mrefu halafu ni kubwa na limekuwa gumu kwa muda mrefu na kwa hiyo, kama unaweka mfano wa ugonjwa ni kwamba na tiba yake pia lazima itafuata mkondo huo huo kwamba itakuwa ni kubwa na inahitaji pia muda wa kutosha kuweza kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho Serikali tulisema kwamba Kamati hii imefika mahali ambapo kazi yake ya awali imeshakabidhiwa kwenye Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na kwamba baada ya hatua hiyo, kazi hiyo itakwenda kwenye ngazi ya Baraza la Mawaziri na baadaye kwenye uongozi wa juu wa Serikali ili kuweza kutoa mwongozo kamili wa kutatua tatizo hili la muda mrefu, kubwa na gumu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kwamba matatizo au changamoto zinazohusiana na masuala ya uhifadhi hayako sawa nchi nzima. Yako maeneo mengine changamoto hizi ni kubwa zaidi, maeneo mengine ni wastani na pengine kuna maeneo ambayo hayana kabisa matatizo haya. Kwa hiyo, ufumbuzi wake pia unataka kuangalia maeneo kama yalivyo na kupata ufumbuzi mahususi kulingana na eneo jinsi lilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za Wilaya ya Karagwe na maeneo mengine yanayofanana nayo ni kwamba sasa hivi zoezi linaloendelea kwa upande wa Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, tunachokifanya ni kuweka mipaka kwenye hifadhi hizo. Zoezi la uwekaji wa mipaka ni uwekaji wa alama. Mipaka ipo tangu siku nyingi kwa mujibu wa sheria, lakini ipo kitaalam *GPS Coordinates* zipo kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa *GN* zilizounda maeneo hayo, lakini mipaka *physically* haikuwahi kuwekwa katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili linaendelea na katika baadhi ya maeneo uwekaji wa alama hizi ndiyo uliokuja kuleta changamoto kwamba wananchi wanafikiri kwamba alama hizo zinawekwa kwa mara ya kwanza na

kwa hiyo, wanaona kwamba pengine Serikali inaweka mipaka kwenye maeneo ambayo siyo ya hifadhi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Huku nyuma!

MWENYEKITI: Kwa nini usimwachie amalize? Endelea Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi yote hiyo ambayo inafanyika hivi sasa, nimesema kwamba kila eneo linakuwa na changamoto zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki ambacho kimetolewa taarifa sasa hivi ya kuomba mwongozo na Mheshimiwa Bashungwa ni tukio ambalo linahitaji kupata hali halisi kama ilivyo hivi sasa ili tuweze kuwianisha kati ya kazi ile ambayo ndiyo tulikuwa tunaifanya siku zote na hiki ambacho kimejitokeza pengine suala la kuhamisha watu kwa mtindo huu ambao ameuelezea ni suala ambalo sisi kama Serikali tunatakiwa kwenda kupata *first hand information* tulione jinsi lilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo mafupi yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI jana wakati akiwa anafafanua jambo linalofanana na hili, ni kwamba kama Serikali sasa jambo la kufanya katika kipindi hiki cha Bunge haraka iwezekanavyo, tutakachokifanya ni kukimbia kwenda kuona hali halisi jinsi ilivyo katika eneo hili linalotajwa kwa Mheshimiwa Bashungwa ili kuweza kuona namna ya kuweza kupata suluhisho la haraka la sasa hivi wakati tukiwa tunaendelea na suluhisho lile la muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kufupisha, niseme tu kwamba ili kuweza kufahamu uhalisia, tutajipanga kuweza kwenda kuona hali halisi jinsi ilivyo ili kuweza kwenda kutatua yale matatizo ambayo yanawezekana kutatua sasa hivi kwa haraka wakati tukiwa tunasubiri ufumbuzi wa muda mrefu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Fanyeni hivyo kwa haraka kwa sababu suala hili siyo dogo. Maelezo ni mazuri sana kwamba utatuzi wa suala hili utategemea hali halisi ya mahali tatizo lenyewe lilipo, lakini kwa vile linajirudia rudia, Serikali ingefanya kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii msiishie Karagwe tu, nendeni kwenye maeneo yote ambayo tunajua.

Nimeletewa *message* jana kwamba kuna operesheni inakuja kwenye maeneo ya mpaka wetu na Serengeti. Sasa kwa vile Mheshimiwa Bashungwa amesema kuna *Eviction Order*, sasa mimi sijui, siku nyingi sijaisoma sheria yetu hiyo, *Eviction Order* hiyo ni ya Mahakama? Kwa sababu kama ni ya Mahakama inachukua sura tofauti. Sasa ni vyema tukalifahamu vizuri suala hili kwa uharaka. Hata hivyo, nashukuru kwa maelezo hayo na uharaka wa Serikali wa kuweza kukubali kuelekea kwenye eneo la tukio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuweza kutoa ufafanuzi kuhusiana na mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili liko katika pande nyingi. Toka tarehe 28 tulipokabidhi taarifa ya uhakiki kwa Mheshimiwa Rais, wako wengi tu na hata wengine ni Waheshimiwa Wabunge, siyo kwamba wana vyeti feki lakini unakuta wamepiga wakifuatilia taarifa za ndugu zao na wengine wengi. Ila unapowabana kwa undani, unajua mtu anapopata taarifa kwa haraka wengine hawakubali, wako kwenye *denial* na *obviously* wengine, niseme baadhi maana yake bado nitakapoeleza utaratibu mwingine tutakuja kuhitimisha; kwa ndugu zao wanawaeleza kwamba wameonewa; lakini ukibana vizuri, Mheshimiwa Simbachawene amepokea, mimi nimepokea wengi na wengi tu nina uhakika wamepokea, wanakuja ku-*admit* kwamba kweli *somewhere somehow* kuna cheti niligushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kusema hivi, kwa kutambua hilo na kuweza kutoa fursa kwa hao waliolazwa na kwa wengine ambao wanaona hawajatendewa haki. Bahati nzuri leo hii Katibu Mkuu wangu atakuwa na *Press Conference* saa 5.00, ndani ya dakika 15 zijazo kutoa utaratibu wa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa kufanyika sasa, Mheshimiwa Rais alishaelekeza *by* tarehe 15, Mei kwa wale ambao watakuwa hawajajiondoa tunafuata taratibu nyingine katika sheria na vyombo vya dola.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Naomba tusikilizane, mliomba mwongozo, kwa hiyo, tusikilizane.

Kwa wale ambao wanaona wana lolote la kuripoti na kwamba wanaona taarifa za *NECTA* siyo sahihi, wanatakiwa kuandika barua ya kukata rufaa kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma, nakala iende Baraza la Mitihani na ipitishwe kwa mwajiri wao na iambatishe vyeti vilevile ambavyo viko katika jalada lake binafsi la kiutumishi na ambavyo ndivyo vilihakikiwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwajiri akishavipitisha, atavipeleka moja kwa moja Baraza la Mitihani halafu seti hiyo nyingine itapelekwa kwa Katibu Mkuu Utumishi. Tutavipitia kwa kina kuliko hata awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe tu kutoa angalizo, tusifanye nalo mzaha kwa wale ambao wanatusikiliza. Tunatoa ruhusa hiyo ya rufani lakini kweli iwe mtu ana uhakika anaona ameonewa, kwa sababu itakapotokea mtu ametumia fursa hii ya rufani na anaujua ukweli na matokeo yakarudi vilevile, kwa kweli adhabu itakuwa ni kali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yangu ni hayo. Tumetoa fursa hiyo na wafuatilie kwa karibu zaidi kupitia *portal* yetu ya *Human Capital Management Information System* au Taarifa za Kiutumishi na Mishahara maarufu kama *Lawson*, tangazo zima litakuwa limewekwa, waweze kufuatilia pia...

MBUNGE FULANI: Bashite!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: ...kwa Maafisa wao wa utumishi na wataweza kuona taarifa kamili na nini kinapaswa kufanyika lakini maelezo ya kina, saa 5.00 kamili Katibu Mkuu wangu atafanya *Press Conference* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naamini wahusika hao wala wasipandishe *pressure*, wawe na utulivu wa hali ya juu. Kama wanaona wana haki, haki yao wataipata, lakini kama wanaona kuna kuzungusha chochote, adhabu itakuwa kali zaidi.

MBUNGE FULANI: Daudi.

MWENYEKITI: Ahsante kwa ufafanuzi huo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea...

MBUNGE FULANI: Kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Unanipa mimi utaratibu? Mheshimiwa, unanipa mimi utaratibu?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni inasema wakati wowote naweza kuomba kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Nakuuliza, unanipa mimi utaratibu? Nimekiuka nini?

MBUNGE FULANI: Mwongozo. (*Kicheko*)

(*Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio*)

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Kiti.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nawavumilia tu.

MWENYEKITI: Sasa namwita Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla ya kuendelea, hotuba yangu yote iingie katika *Hansard* kama nilivyoiweka Mezani. La pili, nawaomba Waheshimiwa Wabunge katika ukurasa wa 100 wa hotuba yangu, kichwa cha habari cha jedwali lile ni Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Dawa kuanzia Mwaka 2015/2016 na Mwelekeo wa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilishwa Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka 2016/2017, vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2017/2018. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kawaida na Mpango wa Maendeleo wa Wizara kwa Mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama hapa, napenda kuchukua fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake imara kwa nchi yetu na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha huduma za afya, ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweka chachu katika kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya nchini ikiwa ni jitihada zake za kulinda afya za Watanzania hasa vijana ambao ndio nguvukazi ya Taifa letu. Kwa hali hiyo, Wizara yangu itaendelea kuelimisha na kuhimiza umma wa Watanzania kuhusu madhara yatokanayo na madawa ya kulevya lakini pia kuzingatia mfumo bora wa maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na ushauri wake wa dhati, hasa katika kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto na masuala ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Wizara yangu itaendelea kutumia taswira yake, ushawishi wake na uzoefu wake ili kujenga jamii ya Watanzania inayowajali, kuheshimu na kuwaendeleza wanawake na wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake ambao umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji ndani ya Wizara yangu. Pia nampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha ambayo imetoa dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe na Wenyeviti wote, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuendelea kulisimamia Bunge letu Tukufu. Nimalize pia kumpongeza Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa ushirikiano wake anaonipatia katika kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawashukuru kwa heshima na unyenyekevu mkubwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na Makamu

Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa ushauri na maelekezo yao. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri, maoni ambayo mmekuwa mkitupatia katika utendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu nimepongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioingia katika Bunge letu Tukufu katika kipindi cha 2016/2017, lakini pia nimetoa pole kwa Wabunge wenzetu waliotangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole pia kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani lakini pia wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Namwomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa niruhusu nizungumzie utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2016/2017, vipaumbele vya Wizara vya mwaka wa 2017/2018 pamoja na maombi ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunatekeleza majukumu yetu tumezingatia sera, mipango na mikakati mbalimbali ya Kitaifa, lakini nitaje tu kwamba tumezingatia Sera ya Afya ya 2007, Mpango Mkakati wa Pili wa Sekta ya Afya wa 2016 - 2020, Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi, lakini pia tumezingatia Sera ya Taifa ya Wazee, Sera ya Maendeleo ya Jamii, Sera ya Maendeleo ya Mtoto, Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia na Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Tumezingatia pia malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya chama changu, Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapato na matumizi kwa upande wa Fungu 52, hadi kufikia mwezi Machi, Wizara imekusanya takriban shilingi bilioni 118.7 sawa na asilimia 75 ya makadirio. Pia kwa upande wa mapokeo ya fedha, tumepokea shilingi bilioni 339.1 ambayo ni sawa na asilimia 43 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Wizara imepokea shilingi bilioni 133.8 sawa na asilimia 26 ya fedha zilizotengwa, lakini pia tumepokea vifaa tiba na dawa vyenye thamani ya shilingi bilioni 256.2 kutoka Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Fungu 53, Wizara imekusanya shilingi milioni 930.2 ambayo ni sawa na asilimia 39 ya makusanyo yaliyotarajiwa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, fedha za matumizi mengineyo zilizopokelewa ni shilingi bilioni 4.9 sawa na asilimia 28.4 ya bajeti iliyoidhinishwa na pia kwa upande wa miradi ya maendeleo, Wizara imepokea shilingi milioni 204.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi sasa nitazungumzia kazi maalum zilizotekelezwa, lakini sitazungumzia zote, nitajikita katika masuala muhimu. Suala la kwanza ni huduma za kinga. Lengo la kutoa huduma za kinga ni kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Kwa hiyo, tumefanya kazi katika maeneo ya chanjo, huduma za uzazi na mtoto, lische pamoja na utoaji elimu kwa afya ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chanjo, nimeeleza katika aya ya 18 ya hotuba yangu. Kupitia Mpango wa Taifa wa Chanjo tumehakikisha kuwepo kwa chanjo za kutosha kwa ajili ya huduma za chanjo kwa watoto na makundi mengine. Chanjo tulizonunua nimeziainisha katika aya ya 18 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo nataka Bunge lako litambue ni kwamba hatuna tatizo la uhaba wa chanjo za watoto katika nchi yetu na nchi yetu imekuwa ni miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri katika utoaji wa huduma za chanjo kwa mwaka 2016 ambapo tuliweza kuvuka lengo kwa kufikia kiwango cha asilimia 97. Tumenunua

magari tisa kwa ajili ya kuboresha huduma za usambazaji wa chanjo lakini pia tumenunua majokofu 317 ya kutunzia chanjo kwa ajili ya Vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafi wa mazingira; tumeendelea kuratibu kampeni ya Kitaifa ya usafi wa mazingira na nafurahi kulitaarifu Bunge lako kwamba kupitia kampeni hii kaya 391,337 zimejenga vyoo bora. Kati ya hizi, kaya 320,894 zina sehemu ya kunawia mikono mara baada ya kutoka chooni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza chachu ya ushindani katika kuboresha huduma za usafi wa mazingira, tumeweza kuendesha mashindano na kuitunuku Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa kuwa mshindi wa jumla Kitaifa ambapo tumeipatia gari aina ya *Toyota Land Cruiser Hard Top*. Pia tumenunua pikipiki 100 na kuzigawa katika Halmashauri 100 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia na jitihada za kudhibiti wagonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, kwa mfano matende, mabusha, usubi, *trachoma*, kichocho na minyoo katika Halmashauri 71 zenye maambukizi. Tumefanya pia upasuaji wa matende na mabusha bila malipo kwa wagonjwa takriban 805 katika Halmashauri za Temeke na Ilala na wagonjwa 100 katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malaria bado imeendelea kuwa ni changamoto katika nchi yetu, nimeeleza katika aya za 27, 28 na 29 hatua ambazo Serikali imechukua ikiwemo kusambaza dawa za kutibu malaria na vipimo vya kupima malaria katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Tumegawa vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu lakini pia tumepulizia dawa ukoka katika mikoa minne ya Kanda ya Ziwa ambayo ina maambukizi makubwa ya ugonjwa wa malaria ambayo ni Kagera, Mwanza, Mara na Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifua Kikuu na Ukoma tumeendelea na jitihada za kuimarisha huduma hizi. Kwa sasa kiwango cha wagonjwa wanaotibiwa na kupona Kifua Kikuu

ni asilimia 90. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwaomba tena wananchi wote wenye dalili za Kifua Kikuu kujitokeza ili waweze kupata huduma za tiba kwa sababu Kifua Kikuu kinatibika. Pia tumesogeza huduma za uchunguzi kutoka hospitali moja hadi hospitali 18 katika maeneo ambayo nimeyaainisha katika aya ya 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa UKIMWI; tumeendelea kutoa huduma za kupima pamoja na ushauri nasaha wa virusi vya VVU na UKIMWI ambapo Watanzania takribani milioni 7.4 walipata ushauri nasaha katika kipindi hiki. Pia jambo kubwa ambalo tumelifanya katika mwaka huu tunaomaliza, tumeanza kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI kwa Watanzania wanaozihitaji bila kujali kiwango cha *CD4*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwezi Oktoba mtu yeyote ambaye ana maambukizi ya VVU na UKIMWI na amepima, tumemwingiza katika mpango wa dawa. Pia tumenunua mashine 14 kwa ajili ya kupima wingi wa virusi vya damu na kuzisambaza katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea pia na jitihada ya kupunguza maambukizi ya UKIMWI kwa kutumia tohara kwa wanaume ambapo kuanzia Januari hadi Desemba, 2016 wanaume takribani 374,411 wamefanyiwa tohara na tunaendelea kuhamasisha tohara kwa wanaume katika mikoa ya kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa mfano magonjwa ya moyo, kisukari, shinikizo la damu, yameendelea kuongezeka katika nchi yetu, kwa hiyo mwaka huu tumeandaa mkakati wa Kitaifa wa kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambapo pia tumezindua kampeni chini ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan na kampeni yetu tumeipa jina la "Afya Yako, Mtaji Wako, Fanya Mazoezi, Linda Afya Yako."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara lakini pia kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa kwa ajili ya kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika hotuba yangu, Waheshimiwa Wabunge wataona karibu kurasa nyingi nimezungumzia huduma za afya ya uzazi na mtoto kwa sababu hicho ndiyo kimekuwa kipaumbele changu cha kwanza toka nimeteuliwa kuwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ambazo tumezitoa ni huduma kabla ya uzazi ambapo tumetoa huduma za uzazi wa mpango na sasa hivi tumeongeza idadi ya Watanzania wanaotumia huduma za uzazi wa mpango kutoka asilimia 27 hadi asilimia 32. Lengo letu ni kwamba ifikapo mwaka 2020 wanawake wanaotumia huduma za uzazi wa mpango wafikie asilimia 45. Pia tumeendelea kutoa huduma wakati wa ujauzito ikiwemo huduma za kupima na kuelimisha wanawake wajawazito kuhudhuria kliniki angalau mara nne kwa mwaka kama wataalam wanavyopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri, bado hatuko vizuri nchi yetu, ni asilimia 51 tu ya wanawake wajawazito wanaohudhuria kliniki angalau mara nne katika kipindi cha ujauzito wao. Lengo letu ni kufikia asilimia 70 ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma wakati wa kujifungua, tumeendelea kushirikiana na wadau ikiwemo Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuhamasisha na kuhimiza wanawake wajawazito kujifungulia katika Vituo vya Afya kwa sababu tafiti zinaonesha ukijifungulia katika Vituo vya Afya unaweza kupunguza changamoto za matatizo yanayokukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya ukarabati wa Vituo vya Afya nane katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu na Mara ili kusogeza huduma za dharura za uzazi ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni *(SEMOC)* lakini pia

tumeendelea kuhakikisha kwamba huduma za rufaa kwa wanawake wajawazito zinaendelea kuboreshwa ambapo Wizara imegawa magari ya kubebea wagonjwa (*ambulance*) 67 katika Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa ikiwemo Kigoma, lakini pia tumegawa katika mikoa mingine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegawa magari nane kwa ajili ya kuratibu shughuli za afya ya mama na mtoto katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa sababu ndiyo ina viashiria vya vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, tumeanzisha utaratibu kuanzia mwaka huu; kila kifo kinatakiwa kujadiliwa ndani ya masaa 24 toka kilipotokea ili kubaini chimbuko la kifo hicho. Pia nimeeleza katika aya ya 50 hadi 51 hatua ambazo tumezichukua katika kupunguza vifo vya watoto wachanga ikiwemo watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za lishe nimeongea katika aya ya 53 ya hotuba yangu na nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kiwango cha udumavu kwa watoto kimepungua kutoka asilimia 42 hadi asilimia 34 lakini uzito pungufu pia umepungua kutoka asilimia 16 hadi asilimia 14 na hii ni kutokana na jitihada ambazo tumezifanya ikiwemo kuhakikisha virutubisho muhimu kwa ukuaji wa mwili vinaongezwa katika unga wa mahindi na usindikaji wa mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia baadhi ya huduma za kinga tulizozitoa, napenda sasa kujikita katika huduma za tiba na nimeeleza katika aya ya 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama, tumeendelea kukusanya damu na kuzipima ambapo tumekusanya chupa za damu 145,300 sawa na asilimia 63 ya mahitaji, lakini pia kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI), tumeanzisha Benki za Damu za Mikoa katika Mikoa saba; Dar es Salaam, Lindi, Morogoro, Dodoma, Iringa, Kigoma na Shinyanga. Lengo letu kila Mkoa uwe na Benki ya

damu ili kuweza kusaidiana na Benki za Damu za Kanda. Huduma za Maabara na uchunguzi wa magonjwa nimezieleza katika hotuba yangu aya ya 56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri asubuhi alieleza suala la hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba. Kati ya jambo kubwa ambalo tunajivunia katika kutekeleza bajeti yetu ya 2016/2017, ni kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba. Wakati tunaanza bajeti ya 2016/2017, hali ya upatikanaji wa dawa ilikuwa ni asilimia 36. Tunaangalia dawa 30 muhimu ambazo zinatakiwa kuwepo katika Vituo vya Afya. Hadi mwezi Machi, 2017, asilimia 81 ya dawa muhimu sana (*essential medicine*) zinapatikana katika bohari ya dawa na vituo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeonesha katika hotuba yetu hali ya upatikanaji wa dawa katika Wilaya, katika Mikoa na katika Halmashauri mbalimbali. Hili limefanikiwa kutokana na uamuzi wa dhati wa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli wa kuongeza bajeti ya dawa kutoka bilioni 31 hadi bilioni 251.5 mwaka 2017 na hizi siyo fedha ambazo ziko katika makaratasi; hadi mwezi Machi, Wizara imeshapokea shilingi bilioni 112.1 kwa ajili ya dawa ukilinganisha na shilingi bilioni 24 ambazo zilitolewa kwa ajili ya dawa kwa mwaka wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tumefanikiwa ni kusambaza kwa kila Halmashauri vitanda vya kawaida 20, vitanda vya kujifungulia vitano, magodoro 25 na mashuka 50 ikiwa ni kuhakikisha kila kituo cha afya nchini kinakuwa na vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za matibabu ya Kibingwa; hili ndiyo eneo la pili ambalo tunajivunia sana kwamba tumefanikiwa. Tumepunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi kwa asilimia 35. Mwaka 2015/2016 wagonjwa waliopewa rufaa kwenda nje ya nchi walikuwa 553 hadi mwezi Machi tumetoa rufaa 357. Maana yake, hospitali zetu zimejenga uwezo wa kutibu magonjwa ikiwemo yanayohitaji huduma za kibobezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ambayo yanaongoza kupeleka watu nje ya nchi ni saratani, magonjwa ya moyo na figo. Nitaeleza kwa ufupi kazi zilizofanywa na hospitali yetu ya Taifa Muhimbili ambapo wao wamekarabati wodi za wagonjwa mahututi na sasa hivi watakuwa na uwezo wa kuwa na vitanda 75 kutoka vitanda 21. Pia Muhimbili imeshaanza kazi ya kukarabati jengo la upasuaji wa akinamama wajawazito ambapo vitanda vitaongezeka kutoka vitanda sita hadi vitanda 19, lakini pia zimeanza jitihada za kupanua jengo la kusafisha figo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya Mifupa Muhimbili (*MOI*) imeendelea na juhudi za kupanua wigo wa huduma ya upasuaji wa mifupa ikiwemo migongo ya watoto iliyopinda. *MOI* kwa kushirikiana na Taasisi ya *GSM Foundation* imetoa huduma za upasuaji wa vichwa vikubwa vikubwa na mgongo wazi kwa watoto takriban 2,020 na pia watoto 250 walifanyiwa upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hospitali ambayo imefanikiwa sana na kuleta mabadiliko makubwa ni hospitali ya moyo ya Jakaya Kikwete. Sasa hivi ina uwezo wa kufanyia upasuaji wagonjwa 30 kwa mwezi kutoka wagonjwa 15 mwaka 2015/2016. Sasa hivi imejenga uwezo, wanapasua wagonjwa kwa kupitia tundu dogo, wagonjwa 608, mwaka uliopita walikuwa ni wagonjwa 190. Kwa kupitia Taasisi ya *JKC* tumeweza kupunguza gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Saratani ya *Ocean Road* imeendelea kutoa huduma na kubwa tumeboresha jengo la kutolea tiba ya dawa (*Chemotherapy*) sasa hivi ina uwezo wa kuwaweka wagonjwa kwa pamoja 100 kutoka wagonjwa 40. Lingine ambalo tumelifanyia maboresho makubwa, muda wa kusubiri kuanza tiba ya mionzi (*Radiotherapy*) tumepunguza kutoka miezi mitatu hadi wiki sita na lengo letu ni kuhakikisha ndani ya siku 14, mgonjwa anayetakiwa kupata matibabu ya mionzi ya saratani (*Radiotherapy*) anapata huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za dawa za saratani zimeboreshwa kutoka 5% mwaka 2015/2016 hadi 60% kufikia mwezi Machi, 2017. Kwa baadhi ya saratani dawa zinapatikana kwa asilimia 100 ikiwemo saratani ya mlango wa kizazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kazi zilizotekelezwa na Hospitali Maalum ya Kibong'oto, Hospitali yetu ya Mirembe, lakini pia na sambamba na Hospitali za Rufaa za Kanda za Juu Kusini, Mbeya; Hospitali yetu ya Kanda ya Benjamin Mkapa, Dodoma; Hospitali yetu ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa, Bugando na Hospitali yetu ya Rufaa ya Kanda za Kaskazini, *KCMC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa, hospitali hizi zimeweza kutoa huduma za matibabu ya kibingwa ili kupunguza usumbufu wa wananchi kwenda Dar es Salaam kupata huduma hizi. Huduma za moyo, huduma za saratani ikiwemo tiba ya maji zinapatikana sasa hivi *KCMC* na Bugando. Pia ikiwemo kusafisha damu. Sasa hivi kusafisha figo huduma zimeanza kupatikana katika hospitali zetu za rufaa za Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia pia katika hotuba yangu, kazi zinazofanywa na Wizara katika kusimamia ubora wa huduma za afya ambapo tumeendelea na zoezi tunaliita la *star rating*, (kutoa nyota) kwa aili ya Vituo vya Afya na zoezi hili limefanyika katika Mikoa sita ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Kilimanjaro na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 52 ya vituo tulivyovifanyia tathmini vimepata nyota sifuri. Ni asilimia 4.1 tu ya vituo vilivyofanyiwa tathmini ndiyo vimepata nyota tatu na nyota nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu katika Sekta ya Afya; tumeendelea kuimarisha miundombinu katika Vyuo vya Afya lakini pia tumeongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu. Nimeonesha wataalam tuliozalisha katika mwaka 2016/2017 lakini pia tunamshukuru sana Mheshimiwa

Rais Dkt. John Pombe Magufuli ambaye amewezesha kupatikana kwa Madaktari 258 na hadi ninavyosema tumeshawagawa katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imekamilisha maandalizi ya mkakati wa kugharamia huduma za afya, lengo ni kuhakikisha tunapata rasilimali fedha za kutosha kwa ajili ya huduma za afya na kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya tumeongeza idadi ya wanachama wa Bima kutoka wanachama 702,598 hadi wanachama 792,986. Pia wanachama wa *CHF* wameongezeka kutoka milioni 1.4 hadi milioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KFW*), tumetekeleza mpango wa kuwapa Bima ya afya wanawake wajawazito kwa jina la "*Tumaini la Mama*" ambapo wanawake wajawazito 147 tumewapa Bima na hivyo kupata huduma za afya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite sasa katika kutekeleza bajeti kwa upande wa Fungu 53 - Maendeleo ya Jamii. Kubwa ambalo tumelifanya ni kuwezesha na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya maendeleo ya jamii hususan katika kutoa hamasa kwa jamii kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo kupitia miongozo mbalimbali; lakini pia tumeendelea kutoa wataalam wa kada ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali katika Vyuo vyetu nane vya Maendeleo ya Jamii pamoja na Taasisi ya Maendeleo Tengeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maendeleo ya jinsia tumeendelea na jitihada za kuwezesha wanawake kiuchumi kupitia Benki ya Wanawake na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, shilingi milioni 156 zimekopeshwa katika Halmashauri tano za Kisarawe, Busokelo, Gairo, Iringa Manispaa, Masasi na Mtwara Vijijini lakini pia tumeendelea

kushirikiana na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuhamasisha Halmashauri kuchangia asilimia tano ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuzipongeza Halmashauri zote zilizotenga na kutoa asilimia tano ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake; lakini nazilaani Halmashauri zote ambazo hazikuchangia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na naamini Mheshimiwa Simbachawene atachukua hatua kuziwajibisha Halmashauri zote ambazo hazijatenga Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi hapa tuko Bungeni kwa sababu ya kura za wanawake, lakini pia wote tunajua kwamba wanawake ndiyo msingi wa maendeleo ya familia, maendeleo ya Taifa na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake imetoa mikopo kwa wajasiriamali 6,959 yenye thamani ya shilingi bilioni 10, lakini pia tumeongeza vituo vya kutoa huduma. Benki ya wanawake imewasaidia wanawake 223 katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea na jitihada za kusimamia na kulinda haki za mtoto ambapo tumeendelea kupinga na kujenga hamasa kuhusu mimba na ndoa za utotoni; na katika hotuba yangu nimeonesha Mikoa inayoongoza kwa ndoa za utotoni ambapo ni Shinyanga, Tabora, Mara, Dodoma na Lindi; lakini pia nimeonyesha Mikoa inayoongoza kwa mimba za utotoni ikiwemo Katavi, Tabora, Simiyu, Geita na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya utafiti wa kubaini vyanzo vya ndoa na mimba za utotoni. Katika kumwendeleza mtoto wa kike, tumewezesha kuanzishwa kwa *Club* za Wasichana na Wavulana 105. Tumetoa huduma za ustawi wa jamii kwa ajili ya watoto walio katika mazingira hatarishi, watoto walio katika mkinzano na sheria, watu wenye ulemavu na wazee ikiwemo familia zenye migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa haki na ustawi wa wazee; nimeeleza katika hotuba yangu hatua tulizochukua ikiwemo kutoa elimu kwa jamii kuwaheshimu na kuwathamini wazee, lakini pia tumefurahi kwamba kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, mauaji ya wazee yamepungua kutoka 190 mwaka 2015 hadi 135 mwaka 2016. Tumeendelea kutoa huduma kwa wazee 456 wasiojiweza katika Makazi 17 yanayoendesha na Serikali. Huduma hizi ni pamoja na chakula, malazi na matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru wadau wote waliochangia katika kuhakikisha huduma bora kwa wazee nchini. Kipekee namshukuru mke wa Rais, Mheshimiwa Mama Janet Magufuli kwa kuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia wazee wanaotunzwa katika makazi ya wazee hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa jamii kuiga mfano wa mama yetu, sote ni wazee watarajiwa tunahitaji kuwaenzi, kuwaheshimu na kuwatunza wazee wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza pia wataalam wa ustawi wa jamii ambao wameendelea kuzalishwa na Taasisi yetu ya Ustawi wa Jamii katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu nimeeleza pia kuanzia aya ya 164 kazi zilizotekelezwa na Taasisi za Wizara ikiwemo Taasisi ya Chakula na Lishe, Bohari ya Dawa, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Uchunguzi wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)*. Naomba Waheshimiwa Wabunge wapitie kazi hizo zilizofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijikite katika sehemu ya tatu ya hotuba yangu ambayo nitazungumzia vipaumbele vya Wizara na bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fungu 52; Wizara itakeleza vipaumbele vifuatavyo:-

(i) Kuimarisha huduma za kinga, tiba na kuongeza usawa katika kutoa huduma za afya.

(ii) Tutaimarsha huduma za afya ya uzazi na mtoto ili kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto. Lengo letu ni kupunguza vifo hivi kutoka 556 katika kila vizazi hai 100,000 na kufikia vifo 290 ifikapo mwaka 2020.

(iii) Tutaimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Vituo vya Umma.

(iv) Tutaimarisha miundombinu katika vituo vya mafunzo.

(v) Tutaimarisha matibabu ya kibingwa nchini kwa kuendeleza ujenzi, upanuzi na kununua vifaa vya kisasa katika Hospitali yetu ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (*MOI*), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Hospitali ya Benjamin Mkapa, Hospitali zetu za Rufaa za *KCMC*, Bugando na Mbeya, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto.

(vi) Tutaimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo.

(vii) Tutaimarisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika kuboresha huduma za afya.

(viii) Tutahamasisha wananchi kwa nia ya kuongeza idadi ya wanaojiunga na Mifuko ya Afya, bado hatufanyi vizuri. Ni asilimia 27 tu takriban ya Watanzania ambao wanatumia Bima ya Afya.

(ix) Kwa upande wa maendeleo ya jamii kupitia Fungu 53, tutaendelea kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo.

(x) Tutawezesha utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa mwaka 2018 mpaka 2020/2021.

(xi) Tutaimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya watoto.

(xii) Tutakuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.

(xiii) Tutaimarisha huduma za ustawi pamoja na haki na ustawi wa wazee na watoto na ushiriki wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika maendeleo ya jamii.

(xiv) Vile vile tutaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi yetu ya maendeleo Tengeru, Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii pamoja na Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kufikia malengo hayo, nitaeleza tu masuala makubwa machache. Mkiniuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, bajeti yako ya 2017/2018 inajibu vitu gani? Bajeti yetu inajibu mambo makubwa matatu:-

Jambo la kwanza; tunataka kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa ili kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi ili tuweze kupunguza hizo gharama. Kupitia hospitali yetu ya Taifa Muhimbili, itaanza kutoa huduma za kupandikiza figo (*Renal transparent*) ambapo tukipeleka Mtanzania mmoja nje ya nchi kwa ajili ya kupandikizwa figo, tunatumia takriban Shilingi milioni 80. Huduma hii ikianza kupatikana Muhimbili, gharama zitapungua hadi kufikia milioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Hospitali ya Muhimbili itaanza kutoa huduma za kupandikiza vifaa vya kusaidia kusikia, kwa kitaalamu inaitwa *cochlear implants*. Tunakimpeleka mgonjwa nje ya nchi tunatumia takribani milioni 30. Huduma hii ikitolewa hapa nchini si tu Serikali lakini wananchi wengi wataweza kumudu huduma hizi kwa sababu gharama hizi zitapungu kwa zaidi ya asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Watanzania wengi sasa hivi wana imani na huduma zinazotolewa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Hivyo tumeamua katika mwaka unaokuja tutajenga jengo la wagonjwa binafsi (*private wing*), tumetenga shilingi bilioni 14.5 kwa sababu watu wengi wanataka kwenda Muhimbili lakini wanashindwa kwenda kwa sababu pia ya mazingira. Kwa hiyo, nawapongeza sana Watanzania wote walioamua kutumia huduma za hospitali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesem sa tunajibu kero za kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo tunawekeza kwa mwaka 2017/2018. Kupitia Taasisi yetu ya Saratani ya *Ocean Road* tunanunua mtambo wa kisasa kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya saratani unaitwa *PET Scan* ambapo tumetenga shilingi bilioni 14.5. Kifaa hiki hakipo Kenya, hakipo Uganda, hakipo Malawi, hakipo Zambia, kwa mara ya kwanza Tanzania itaanza kutoa huduma za vipimo vya saratani (*PET-Scan*). Tunategemea kupitia uamuzi huu tutaokoa takribani shilingi bilioni tano kwa mwaka. Kwa sababu kupeleka mgonjwa kwa ajili ya kipimo hiki inagharimu milioni 100. Huduma hii sasa itaweza kupatikana nchini kwa takribani shilingi milioni kumi na mbili. Hayo ndiyo maeneo makubwa ya kujibu hoja za kupeleka rufaa nje ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutaendelea kuimarisha hospitali yetu ya *MOI*, Hospitali ya Jakaya Kikwete ambayo imewekeza sana katika matibabu ya moyo. Sambamba na hayo tutajenga uwezo katika hospitali zetu za Rufaa za

Kanda ya Benjamin Mkapa. Kama mnavyofahamu, Serikali imehamia Dodoma, tumeshamaliza kusimika mitambo ya kisasa. Kwa hiyo lengo letu huduma zote za kibingwa pia zitapatikana katika hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara ambapo tumetenga shilingi bilioni mbili. Lakini pia tutawekeza katika Hospitali za Mbeya, Bugando na KCMC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za tiba tutaendelea kutoa chanjo, na labda niliweke wazi, ukiangalia bajeti ya dawa ya mwaka jana na mwaka huu, mwaka huu ni shilingi bilioni 236, mwaka jana bajeti ya dawa tuliweka shilingi bilioni 251. Vilevile kulikuwemo na fedha za chanjo. Kwa hiyo, katika kuhakikisha kwamba hatutetereki katika kutoa huduma za chanjo hasa chanjo za watoto, tumeamua kutenganisha fedha za dawa na fedha za chanjo. Kwa hiyo tumetenga shilingi bilioni 33 kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wametuelekeza, kila dola moja inayowekezwa kwenye chanjo ya mtoto maana yake tunaokoa angalau dola nane mpaka dola 44 katika kutibu magonjwa ya watoto hao. Kwa hiyo, bajeti ya dawa haijapungua lakini tumetenga fedha za dawa, vifaa na vifaa tiba na kuziweka tofauti na fedha za chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya afya ya uzazi na mtoto, tutaendelea kununua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango. Haya ni maboresho makubwa, tumekuwa tukitegemea wafadhili wa nje kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango. Wataalam wanatuambia tukitumia huduma za uzazi wa mpango tunaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 40. Kwa hiyo, tumetenga kwa mara ya kwanza shilingi bilioni 14 za ndani kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutanunua, kusambaza na kutoa bila malipo, dawa kwa ajili ya uzazi salama katika

vituo vya umma. Nimeona wanawake wajawazito ambao mpo hapa, nataka kuwathibitishia, chini ya Serikali ya Awamu ya Tano kupitia bajeti hii hakuna mwanamke mjamzito atafariki kwa kukosa dawa ya kuzuia kuvuja damu (*oxytocin*).
(*Makofi*)

Nataka kupitia Bunge hili kuwathibitishia wajawazito wote kupitia bajeti hii hakuna mwanamke mjamzito atafariki kwa sababu amekosa dawa ya *magnesium sulphate* kwa ajili ya kuzuia kifafa cha mimba. Kwa mara ya kwanza dawa hizi tutazitoa bure na tutahakikisha kila mwanamke mjamzito anayejifungua katika vituo vya umma anapata dawa; tumetenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya huduma hii.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tutaendelea kuboresha huduma za uchunguzi za uzazi salama kwa kununua mashine za *Ultra Sound 65*, tutazipeleka katika vituo vya afya ili viweze sasa kufanya huduma za uchunguzi. Kupitia bajeti hii tutawakatia Bima ya Afya wanawake wajawazito 150,000 ili kuweza kupata huduma za afya katika hospitali za umma. Lakini kwa kupitia bajeti hii tutaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni ambapo tutaboresha vituo vya afya 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshawasiliana na wenzetu wa TAMISEMI watuletee mapendekezo ya vituo hivyo na tayari timu ya TAMISEMI na timu ya Wizara ya Afya imepita katika Halmashauri mbalimbali kwa hiyo nasubiri kuletewa orodha ya mwisho ya vituo hivyo. Ninachotaka kuwathibitishia, tumesherehekea takriban miaka 50 ya Uhuru vituo vya afya vya Serikali vinavyotoa huduma za dharura za uzazi ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto (*CEMOC*) ni vituo vya afya 117 tu, ambayo ni sawa na asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia bajeti hii tutaongeza vituo vya afya 150 ndani ya mwaka mmoja, vitaweza kutoa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto. Tutaboresha upatikanaji wa damu salama, ambapo

tutajenga benki za damu katika Mikoa ya Katavi, Rukwa, Ruvuma, Njombe na Manyara ambapo tumetenga shilingi bilioni mbili. Hayo ndiyo mambo makubwa ambayo tutayafanya kupitia sekta ya afya, na kama nilivyosema yanajibu kero kubwa tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia sekta ya maendeleo ya jamii tutaendelea kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za kujitea maendeleo, tutawezesha utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, tutaimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi, kuimarisha huduma za ustawi wa jamii na wazee, lakini pia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, juzi wakati anawasilisha hotuba yake, amezungumzia kuhusu Sheria ya Ndoa. Nikiwa mlezi na msimamizi mkuu wa haki na maendeleo ya wasichana nataka kukiri mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba zipo changamoto mbalimbali zinazoleta mimba na ndoa za utotoni, lakini Sheria ya Ndoa nayo ni kikwazo. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Katiba na Sheria kuhakikisha kwamba tunafanyia marekebisho sheria ya ndoa ili kuwawezesha wasichana waweze kuendelea na masomo badala ya kuwaoza mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kushughulikia masuala ya maendeleo ya jinsia tutaendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi ili kutoa mikopo kupitia Benki ya Wanawake katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma, Ruvuma na Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya mtoto kama nilivyosema tutaendelea kuimarisha utendaji wa Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mtoto, kwa huduma za ustawi wa jamii tutaendelea kuhakikisha tunatoa huduma za wazee pamoja na wazee wanaokaa katika makazi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi lakini naomba kwa sababu ya muda nitoe shukrani kwa wadau wetu wakubwa ambao wamewezesha kutekelezwa kwa miradi mbalimbali ya sekta ya afya. Kipekee niwashukuru sana nchi rafiki na mashirika ya kimataifa yanayosaidia kuboresha huduma za afya kupitia Mfuko wa Pamoja wa Kugharamia Huduma za Afya (*Health Basket Fund*) ambazo ni Denmark, Uswis, Ireland, Canada, Benki ya Dunia, *UNICEF* na Korea. Tunawashukuru sana kwa sababu mchango wenu ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzishukuru nchi za Canada, China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa ambazo zimeendelea kusaidia Wizara ya Afya katika maeneo mahsus. Nayashukuru mashirika ya kimataifa, asasi za kiraia, sekta binafsi, vyuo vikuu, taasisi za kitafiti na vyama vya kitaaluma, wadau wote nimewaainisha katika hotuba yangu kuanzia aya ya 219 hadi 223. Pia ningependa kutamka kwamba *Global Fund for HIV/AIDS, Malaria and TB* tunawashukuru sana, *African Development Bank, BADEA, EU, Global Alliance on Vaccine, US AID, PEPFAR, UN-Women* na *UNFPA* tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha utendaji wa kazi zangu, nikiwa Waziri nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mbunge na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuwashukuru Dkt. Mpoki Ulusubisya - Katibu Mkuu Afya na Bibi Sihaba Nkinga Katibu Mkuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mchango wao. Ninamshukuru sana Profesa Mohamed Kambi Bakari - Mganga Mkuu wa Serikali kwa mchango wake mkubwa katika utendaji wa kazi zangu, nawashukuru

Makamishna, Wakurugenzi na Viongozi wa vitengo vya Wizara. Nawashukuru Wakurugenzi wa Hospitali zetu ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Profesa Museru tunakushukuru sana, MOI, JKCI - Profesa Janabi, Ocean road, Mirembe, Kibong'oto na Hospitali za Rufaa ya Kanda ya Mbeya, Benjamini Mkapa - Dodoma, Bugando na KCMC na taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri katika Bunge lako Tukufu kwamba mimi si daktari lakini siku hizi nimekuwa *bush doctor* kwa sababu ya msaada na mchango mkubwa ambao nimekuwa nikiupata kutoka katika timu yangu ya wataalam. Nawashukuru sana kwa kuniwezesha kusimamia Wizara vizuri. (Makofi)

Aidha niwashukuru Waganga Wakuu wa Mkoa wote, Waganga Wakuu wa Wilaya, Waganga Wafadhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na Mashirika ya Dini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watumishi wenzangu wa sekta ya afya, nawashukuru sana, sana sana kwa sababu mmeendelea kutoa huduma katika mazingira yenye changamoto mbalimbali, lakini bado mmeendelea kutoa huduma, niendelea kuwasihi madaktari, wauguzi, wafamasia, watumishi wote wa sekta ya afya muendeleo kutoa huduma kwa kuzingatia miiko na maadili ya kazi ya kutoa huduma za afya ili mwisho wa siku tuweze kulipeleka mbele Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu na ustahimilivu wao mkubwa sana, bila wao nisingekuwa naendelea kuwa vizuri katika kazi zangu kwa kujitoa na kujituma. Vilevile kwa wananchi hasa wanawake wa UWT wa Mkoa wa Tanga, ninawashukuru sana kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika utendaji wa kazi zangu. Ninaahidi kwamba nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya kweli na ya haraka katika Mkoa wetu wa Tanga. Tanga inapendeza na tumeamua kuwa iwe ni Tanga ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba ninywe maji sasa kusudi niombe fedha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Fungu 52 - Afya katika mwaka 2017/2018 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya shilingi 225,038,495,525, kati ya fedha hizo shilingi 207,472,729,612 zitakusanywa kutoka katika mashirika na taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 17,565,765,913 ni kutoka makao makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida kupitia Fungu 52 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 291,895,940,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 64,063,937,000 zitatumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 227,823,003,000 zitatumika kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara shilingi 49,360,787,000 ni kwa ajili ya watumishi wa Wizara Makao Makuu na shilingi 178,795,217,000 ni kwa ajili watumishi wa taasisi, mashirika na wakala zilizo chini ya Wizara. Kwa upande wa miradi ya maendeleo Fungu 52 linakadiria kutumia shilingi 785,805,952,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya fedha hizo fedha za ndani ni shilingi 336,300,000,000 na fedha za nje ni shilingi bilioni 449,505,952,278.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya makadirio ya bajeti kwa mwaka 2017/2018 kwa Fungu 52 ni shilingi 1,077,701,892,000. Kwa upande wa Fungu 53 Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, makadirio ya makusanyo ya maduhuli na matumizi kwa mwaka ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa makusanyo ya maduhuli Wizara inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 2,101,874,000 ambazo ni ada za wanafunzi kutoka vyo vyanane kutoka maendeleo ya jamii, ada za mashirika yasiyo ya kiserikali na mauzo ya vitabu vya zabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2017/2018 ni shilingi 35,300,602,090 ambapo mishahara ni shilingi 19,142,252,240, na shilingi 16,158,449,850 ni matumizi mengineyo. Aidha, Fungu 53 kwa upande wa miradi ya maendeleo inakadiriwa kutumia kiasi cha shilingi 2,606,278,000 kati ya fedha hizo shilingi 2,000,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 606,278,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima jumla ya makadirio ya bajeti kwa Fungu 53 ni shilingi 37,906,880,090. Jumla ya fedha zote ambazo ninaliomba Bunge lako Tukufu lipitishwe kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni shilingi 1,115,680,772,090.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo nashukuru kwa kunipa fursa hii na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante! Hoja imetolewa na imeungwa mkono, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho lako zuri.

HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHE. UMMY A. MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

I. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba sasa

Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2016/17 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2017/18. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2017/18.

2. Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa, napenda kuchukua fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake imara kwa nchi yetu na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na katika kuimarisha huduma za Afya na ustawi ya jamii nchini. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweka msingi wa kudhibiti matumizi ya madawa ya kulevya nchini ikiwa ni katika jitihada zake za kulinda afya za Watanzania hasa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu. Kwa jinsi hiyo, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhimiza umma wa Watanzania kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya madawa ya kulevya sambamba na kuzingatia mfumo bora wa maisha.

3. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na ushauri wake wa dhati hasa katika kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto na masuala ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Wizara yangu itaendelea kutumia taswira, ushawishi na uzoefu wake ili kujenga jamii ya watanzania inayowajali, kuwaheshimu na kuwaendeleza wanawake na wasichana kwa ajili ya kuwa na maendeleo ya kweli na endelevu katika nchi yetu

4. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake ambao umesaidia kuongeza ufanisi katika

utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa na Wizara yangu. Aidha, naomba nimpongeze kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge hili ambayo imetoa dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka 2017/18.

5. *Mheshimiwa Spika*, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuendelea kutekeleza majukumu yako kwa weledi katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.)** kwa ushirikiano wake kwako, katika kutekeleza majukumu yako. Vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

6. *Mheshimiwa Spika*, napenda nimshukuru **Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb)** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wake uliowezesha kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini hasa afya ya msingi. Pia, nawashukuru Mawaziri wa Wizara nyingine zote ambazo ushirikiano wao na Wizara yangu umechangia katika utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii.

7. *Mheshimiwa Spika*, kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb)**, na Makamu Mwenyekiti, **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyotoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha nawashukuru *Mheshimiwa Wabunge* wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Ninawashukuru sana! Ninawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia wananchi ndani na nje ya Bunge.

8. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo (Mb), Mheshimiwa Anna Kilango Malecela (Mb), Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Mheshimiwa Juma Ali Juma (Mb), Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete (Mb) na Mheshimiwa Getrude Pangalile Rwakatare (Mb) kwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha nampongeza **Prof. Kabudi** kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Ninawaahidi kuwapa ushirikiano ili tuendeleo kuwatumikia wananchi kwa pamoja.

9. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa familia na wananchi wa Jimbo la Dimani kwa kifo cha **Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir** na **Dkt. Ely Marko Macha** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, CHADEMA. Aidha, natoa pole kwako na watanzania wote, ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza ndugu na jamaa zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga. Pia, natoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

10. *Mheshimiwa Spika*, Baada ya kusema hayo, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka 2016/17, Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2017/18 pamoja na maombi ya fedha ambazo zitaiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yetu.

II. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

11. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Sera, Mipango na Mikakati

mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030), Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), Sera ya Afya (2007), Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2016 - 2020) na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM 2007 – 2017). Aidha tumezingatia Sera ya Taifa ya Wazee (2003), Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008), Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000), Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001). Vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020.

Mapato na Matumizi ya Fedha - Fungu 52 (Afya)

12. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Fungu 52 (Afya) hukusanya mapato yake kupitia Bodi na Mabaraza mbalimbali, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi wa vitabu vya maombi ya zabuni, pamoja na makusanyo yatokanayo na utoaji wa huduma katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Hadi kufikia mwezi Machi 2017, Wizara imekusanya jumla ya Shilingi **118,701,870,697.00** ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi **157,786,384,366.00** yaliyoidhinishwa kwa mwaka 2016/17. Makusanyo haya ni sawa na asilimia **75** ya makadirio ya makusanyo ambapo usimamizi thabiti pamoja na matumizi ya mifumo ya Kielektroniki vimechangia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa ufanisi huu.

13. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, jumla ya Shilingi **796,115,856,780.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kati ya fedha hizo, Shilingi **277,629,895,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **518,511,683,780.00** ikiwa ni kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, jumla ya Shilingi **339,194,232,240.85.00**

zilipokelewa ikiwa ni **asilimia 43** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 205,321,959,485.85 sawa na asilimia 74** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 133,872,272,755.00 sawa na asilimia 26** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. tumepokea vifaa, vifaa tiba na dawa vyenye thamani ya shilingi 256,238,088, 964 kutoka mfuko wa dunia wa kupambana na UKIMWI, malaria na kifua kikuu ikiwa ni sehemu ua utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo.

Fungu 53 - Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

14. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Fungu 53, ilitarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 2,382,679,000**. Vyanzo vya mapato ikiwa ni ada za wanafunzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na ada za Mashirika Yasio ya Kiserikali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, makusanyo yalifikia **Shilingi 930,281,152** sawa na **asilimia 39.0**.

15. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, jumla ya **Shilingi 49,857,955,920** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara kupitia Fungu hili. Kati ya hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 41,009,372,644** yakijumuisha **Shilingi 18,669,129,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 22,340,243,644** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bajeti ya matumizi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa ilikuwa **Shilingi 8,848,583,276** kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,365,400,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,483,183,276** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Machi, fedha za Matumizi Mengineyo **Shilingi 4,950,097,864** zilipokelewa sawa na **asilimia 28.4** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Shilingi 7,866,426,933** za Mishahara zilipokelewa sawa na **asilimia 42.1** ya bajeti iliyoidhinishwa. Vilevile, katika bajeti ya miradi ya Maendeleo, **Shilingi 497,718,250** zilipokelewa ambapo **Shilingi 204,217,000** (3.8%) ni fedha za ndani na **Shilingi 293,501,250** (8.4%) ni fedha za nje.

16. Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni taarifa kuhusu majukumu yaliyotekelezwa na Wizara katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017;

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA SEKTA YA AFYA

HUDUMA ZA KINGA

Udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza na Yasiyo ya kuambukiza

17. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma za kinga nchini ambazo zinajumuisha udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyo ya kuambukiza, huduma za uzazi na mtoto, lishe pamoja na utoaji wa elimu ya afya kwa umma. Katika kipindi cha 2016/17 Wizara ilitekeleza afua mbalimbali za huduma za kinga ikiwa ni pamoja na;

Huduma za Chanjo

18. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma za Chanjo kulingana na Sera na Miongozo. Aidha, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Chanjo, imehakikisha kuwepo kwa chanjo za kutosha kwa ajili ya **huduma za chanjo kwa watoto** na makundi mengine kwa kununua na kusambaza chanjo katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Serikali ilitumia jumla ya **shilingi bilioni 18 kununulia chanjo na vifaa vya kutolea chanjo**. Chanjo zilizoununuliwa kwa mwaka 2016/2017 zilikuwa **BCG** (chanjo ya kifua kikuu) dozi 6,000,000, **Polio** dozi 6,000,000, **Penta** (chanjo ya dondakoo, kifaduro, homa ya ini, Preumonia, homa ya uti wa mgongo na kichomi) dozi 5,975,500, **PCV** (chanjo ya homa ya nimonia na homa ya uti wa mgongo) dozi 5,082,200, **Rota** (chanjo dhidi ya ugonjwa wa kuharisha) dozi 3,303,400, **TT** (chanjo ya Pepo punda kwa wajawazito) dozi 2,480,000, **Surua Rubella** dozi 4,797,600 na **HPV** (chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi) dozi 67,100. Hii imewezesha nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi zilizofanya vizuri katika utoaji wa huduma za chanjo kwa mwaka 2016, ambapo tuliweza kuvuka lengo kwa kufikia kiwango cha chanjo cha asilimia 97.

19. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa chanjo **imenunua magari 9**

kwa ajili ya kuboresha huduma za usambazaji wa chanjo, usimamizi elekezi na ufuatiliaji wa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. Kati ya magari hayo, manne ni ya tani 3.5 na yana vyumba vya ubaridi. Aidha, Wizara ilinunua na **kusambaza majokofu 317 ya kutunzia chanjo** kwenye vituo vya huduma za afya ambapo majokofu 70 yanatumia mionzi ya jua na 247 yanatumia gesi. Vilevile Wizara **imeanzisha mfumo wa kukusanya taarifa za chanjo ikiwa** ni pamoja na ufuatiliaji wa chanjo kutoka ngazi ya Taifa hadi kwenye vituo vya kutolea chanjo (Vaccination Immunization Management System (VIMS)). Mfumo huu umeshapelekwa kwenye mikoa saba ambayo ni Dar es salaam, Lindi, Njombe, Arusha, Mtwara, Tabora na Mwanza.

Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko

20. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa yanayotolewa taarifa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko. Katika mwaka 2016/17 nchi yetu ilikumbwa na **ugonjwa unaosababishwa na sumu kuvu (Aflatoxicosis)**. Hata hivyo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilidhibiti ugonjwa huo. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo kwa watumishi wa afya mipakani, bandarini, viwanja vya ndege na bandari kavu kuhusu namna ya kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza ikiwemo **Ebola**. Mafunzo haya yalishirikisha watumishi na wadau 110. Vilevile, Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Milipuko na Majanga ili kulinda usalama wa nchi kiafya (National Health Security Plan, 2017-2021). Utekelezaji wa Mpango huo umeshaanza.

21. Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kipindupindu uliendelea kutolewa taarifa na kudhibitiwa kwa kiasi kikubwa ambapo hadi Machi 2017, jumla ya wagonjwa 2,927 waliripotiwa na vifo 46 viliripotiwa. Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI katika kupanga mikakati ya kudhibiti ugonjwa huo na magonjwa yote ya milipuko ambapo mafunzo yalitolewa kwa Mikoa na Halmashauri zilizoathiriwa na ugonjwa huo. Mafunzo hayo yalijielekeza zaidi katika matumizi ya maji safi na salama, usafi wa

mazingira na usafi binafsi wa mwili. Aidha, jumla ya **tani 50 za dawa ya kutibu maji ya kunywa (Chlorine)** ilisambazwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Pwani, Morogoro, Iringa, Mwanza, Mara, Kagera, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dodoma, Mbeya, Rukwa, Singida, Kigoma na Manyara ambayo iliathiriwa zaidi na ugonjwa wa kipindupindu. Visima virefu 18 vya maji vilichimbwa katika Mikoa ya Mara na Mwanza kupitia msaada wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO).

22. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha udhibiti wa **ugonjwa wa homa ya manjano**, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi wanaotegemea kusafiri nje ya nchi kuhusu umuhimu wa kupatiwa chanjo ya ugonjwa huo siku 14 kabla hawajasafiri ambapo kati ya Julai 2016 hadi Machi 2017 **wananchi 26,045 wamepatiwa chanjo** hiyo. Sambamba na uhamasishaji huo, Wizara imezindua **vyeti vipya vya Homa ya Manjano** vilivyoboreshwa vyenye alama maalum ya siri ambayo itazuia kughushi vyeti hivyo, ambapo kuanzia mwezi Agost 2016 mpaka sasa jumla ya **vyeti 34,000** vimebadilishwa kote nchini.

Usafi wa Mazingira

23. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuratibu awamu ya pili ya Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira (2016-2021) ambapo katika mwaka 2016/17, jumla ya kaya **391,937** zimejenga vyoo bora, kati ya hizi, kaya **320,894** zina sehemu maalum ya kunawa mikono mara baada ya kutoka chooni.

24. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza chachu ya ushindani katika kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira, Wizara iliendesha mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira na kutoa zawadi mbalimbali kwa Halmashauri zilizofanya vyema. Katika mashindano hayo, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe iliibuka mshindi wa jumla kitaifa na kukabidhiwa zawadi ya gari jipya aina ya Toyota Hardtop 4WD. Zawadi nyingine zilizotolewa kwa washindi ni pamoja na pikipiki 17, vyeti na vikombe. Aidha, katika kujenga uwezo wa Halmashauri kusimamia na kufuatilia shughuli za afya

mazingira, Wizara ilinunua na kugawa jumla ya pikipiki kwa Halmashauri 100 nchini hususani za vijijini (*Kiambatisho Na. 1*).

Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele

25. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele imeendelea kugawa dawa za kingatiba za matende, mabusha, usubi, trakoma, kichocho na minyoo ya tumbo katika Halmashauri zote zenye maambukizi haya . Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, mpango umegawa dawa katika **Halmashauri 71 na kufikia watu milioni 14.3** katika mikoa ya Dar Es Salaam, Pwani, Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Dodoma, Singida, Tanga, Tabora, Manyara, Mtwara, Lindi na Morogoro. Katika zoezi hilo serikali imesambaza **vidonge milioni 54.5** vya dawa ya Mectizan kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa usubi na Matende, **vidonge milioni 23.8** vya albendazole kwa ajili kuzuia maambukizi ya ugonjwa waminyoo ya tumbo, **vidonge milioni 13.3** vya dawa ya Prazquantel kwa ajili kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa kichocho na **dozi million 8.7 ya dawa ya Mectzan** kwa ajili kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa trakoma.

26. Mheshimiwa Spika Serikali imefanya **kambi za upasuaji kwa wagonjwa 805 wa matende na mabusha** bila malipo ambapo 705 ni katika Halmashauri ya Temeke na Ilala jijini Dar es salaam na 100 katika mkoa wa Mtwara. Wizara ilifanya tathmini ya kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa matende na mabusha katika Halmashauri 27 za mikoa ya Dodoma, Katavi, Rukwa, Singida, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani. Matokeo ya tathmini hii yameonesha kushuka kwa kiwango cha maambukizi katika Halmashauri zote na hivyo hazihitaji tena ugawaji dawa wa kingatiba; isipokuwa katika Halmashauri ya Kondo na Chemba.

Udhibiti wa Malaria

27. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea na juhudi za udhibiti wa malaria nchini, kwa kutekeleza afua mbalimbali zinazopendekezwa kimataifa, ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata kinga na matibabu pale wanapothibitika kuwa na vimelea vya malaria.

28. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendelea na mapambano dhidi ya Malaria, Wizara imesambaza **dawa za kutibu malaria na vipimo vya kupima malaria (mRDT)** kwenye mikoa 26 ya Tanzania Bara. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya **dozi za ALU 12,530,040 na Vitepe vya mRDT 15,511,500** vimenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya huduma za afya nchini. Aidha, uhamasishaji wa jamii juu ya matumizi ya kipimo cha mRDT na matibabu sahihi ya malaria kupitia kampeni ya “SIO KILA HOMA NI MALARIA NENDA UKAPIME” umeendelea kufanyika katika mikoa yote nchini.

29. *Mheshimiwa Spika*, unyunyiziaji wa dawa ukoka umefanyika katika mikoa minne ya Kanda ya Ziwa ambayo ina maambukizi makubwa zaidi ya malaria hapa nchini ambayo ni (Kagera, Mwanza, Mara na Geita). Pia kampeni ya ugawaji wa vyandarua vyenye viuatilifu vya muda mrefu imetekelezwa katika Halmashauri ya Kilombero Mkoa wa Morogoro na Halmashauri zote za Mkoa wa DSM. **Jumla ya vyandarua 2,617,465** vilinunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri hizo. Hivyo kukamilisha jumla ya Mikoa 23 ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Manyara, Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Arusha, kilimanjaro, Mara, Simiyu, Mwanza, Geita, Kagera na Morogoro ambayo ilikuwa imelengwa na kampeni ambapo jumla ya vyandarua 27,189,572 vimesambazwa kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017.

Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma

30. Mheshimiwa Spika, huduma za kifua kikuu na Ukoma zimeendelea kuimarika nchini ambapo mafanikio makubwa yameendelea kupatikana. **Kwa hivi sasa kiwango cha wagonjwa wanaotibiwa na kupona ni asilimia 90 kati ya waliogunduliwa kuugua kifua kikuu.** Wizara imeendelea kuboresha huduma za vipimo kwa kuimarisha maabara 4 za Kanda ya Mbeya (Hospitali ya Rufaa Mbeya), Mwanza (Bugando Medical Centre), Dodoma (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa) na Kilimanjaro (Hospitali ya Kibong'oto) ambazo zimeweza kufunguliwa na kuanza kutoa huduma za uchunguzi wa vimelea vya kifua kikuu. Hapo awali huduma hii ilikuwa inapatikana katika maabara moja tu iliyopo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

31. Mheshimiwa Spika, huduma za uchunguzi na matibabu ya **kifua kikuu sugu** zimeimarishwa na kusogezwa karibu na wananchi. Awali huduma hizi zilikuwa zinatolewa katika hospitali ya Kibong'oto (Kilimanjaro) pekee, ambapo kuanzia Mwezi Desemba 2016 jumla ya vituo 18 vimeanza kutoa huduma hiyo. Vituo hivyo ni Tambuka reli, Bukombe, Mbogwe (Geita), Hospitali Amana, Ukonga, Rangi tatu na Sinza (Dar es salaam), Newala (Mtwara), Ifakara-Kibaoni (Morogoro), Bagamoyo (Pwani), Hospital ya Rufaa ya Kanda Mbeya, Ruanda, Mana (Mbeya), Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera, Rubya, Kamachumu (Kagera), Tanga Mjini (Tanga) na Bariadi (Simiyu). Aidha, shughuli mbalimbali za uelimishaji na uhamasishaji jamii kuhusu Kifua Kikuu zilitekelezwa ikiwemo kuendesha Kampeni kupitia vyombo vya habari (TV, Radio) yenye lengo la kuibua wagonjwa wapya wa kifua kikuu kwa kuwa ni asilimia **39 tu** kati ya **wagonjwa 162,000** waliopo nchini ndio waliopo katika matibabu. Tunamshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuongoza mapambano dhidi ya kifua kikuu.

32. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendesha Semina kwa Waheshimiwa Wabunge mwezi Novemba, 2016, ambayo iliwezesha kuanzishwa rasmi kwa **Umoja/Mtandao**

wa Wabunge wanaofuatilia masuala ya Kifua Kikuu, (Tanzania Parliamentary TB Caucus) ikiwa ni utekelezaji wa maazimio ya kimataifa. Nitumie fursa hii kumpongeza Dkt. Faustine Ndugulile kwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Tanzania Parliamentary TB Caucus. Aidha, nawapongeza wabunge wote kwa kuwa chachu ya mapambano dhidi ya kifua kikuu. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Viongozi wa Dini, Madiwani na jamii kwa ujumla kuhimiza wananchi wote wenye dalili za ugonjwa wa kifua kikuu kupata tiba mara moja. Tusipofanya hivyo tunaiweka nchi katika hatari zaidi ya kuwa na wagonjwa wengi wa kifua kikuu kwa kuwa mtu mmoja anayeugua na hajanza tiba anauwezo wa kuambukiza hadi watu 20 kwa mwaka. Nisisitize kuwa **Kifua Kikuu Kinatibika na Huduma za Kupima na Matibabu hutolewa bila Malipo.**

33. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha tunaibua wagonjwa wapya wa kifua kikuu, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi inatekeleza Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma wa 2015-2020 **wa kuibua wagonjwa wa kifua kikuu kupitia sekta binafsi;** ambapo mwaka 2016 jumla ya wagonjwa 7,090 kati ya 65,785 sawa na asilimia 11 waliibuliwa kupitia vituo vya afya vinavyomilikiwa na Sekta Binafsi. Aidha, Wizara ilishirikisha maduka ya dawa muhimu (ADDO) katika kuibua wagonjwa wa Kifua kikuu, jumla ya wauza dawa 300 kutoka mikoa 10 walipatiwa mafunzo ya mfumo wa utoaji wa rufaa za wahisiwa wa ugonjwa wa kifua kikuu. Vilevile, Wizara imeongeza wigo wa utoaji huduma za kifua kikuu katika vituo binafsi vya afya kutoka asilimia 10 mwaka 2014 hadi asilimia 15 mwaka 2016.

34. Mheshimiwa Spika, kuhusu jitiada za **kutokomeza ugonjwa wa ukoma,** Wizara imeendelea kufanya kampeni maalum ya utoaji elimu kwa jamii kuhusu dalili za ukoma na namna ya kutambua mapema wagonjwa katika hatua za awali za ugonjwa. Kampeni hiyo imetekelezwa katika wilaya za Kilombero, Liwale na Nanyumbu ambapo jumla ya wagonjwa 61 waligunduliwa. Hii inaonesha kuwa bado kuna uwepo wa ugonjwa huu katika wilaya hizi.

Udhibiti wa UKIMWI

35. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2016/17, Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti UKIMWI kwa kutoa ushauri nasaha na kupima virusi vya UKIMWI (VVU). Kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2016 jumla ya **wateja wapya 7,447,102 walipata ushauri nasaha na kupima VVU**. Aidha, Wizara imepanua wigo wa utoaji huduma za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU. Hadi kufikia Desemba 2016, vituo **6,155** vilikuwa vinatoa huduma za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU. Kati ya vituo hivyo vituo **5,690 (92%)** vinatoa huduma za maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Vilevile, Wizara **imeanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa watoto wachanga waliozaliwa na mama wenye maambukizi ya VVU**. Programu hii imeweza kufanya majaribio ya mfumo mpya uitwao “Mother baby cohort monitoring system” katika mikoa 5 ya Iringa, Mbeya, Pwani, Tanga na Tabora ambapo tathmini yake imeonyesha kuwa mfumo huu unafaa kuanza kutumika katika mikoa yote nchini. Mpango huu utasaidia katika kubaini mapema watoto walioathirika na VVU.

36. Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Oktoba 2016, Wizara ilianza **kutoa dawa za ARV** kwa watu wenye maambukizi ya Virusi vya VVU/UKIMWI (WAVIU) **bila kujali kiwango cha CD4** ambapo hadi Machi 2017 jumla ya WAVIU wanaotumia ART/ARV ni 849,594 ambayo ni sawa na asilimia 60 ya watu million 1.4 wanaokadiriwa kuwa na maambukizi ya VVU nchini. Kati ya hao watoto 55,670 wako kwenye matibabu ya ARV ambayo ni asilimia 50% ya lengo. Aidha, huduma mkoba za UKIMWI na Kifua kikuu zimeendelea kutolewa, na hadi Desemba 2016 asilimia **96** ya WAVIU wanaohudhuria kliniki za Tiba na matunzo wamepimwa hali zao za maambukizi ya kifua kikuu na dawa za **Isonizidi** ya kuzuia maambukizi ya Kifua kikuu kwa WAVIU inatolewa katika vituo **512** sawa na asilimia **30** ya vituo vya matunzo na Tiba kwa WAVIU. Pia, Wizara imefunga mashine mpya **14** za kupima uwingi wa virusi vya UKIMWI {viral load} katika damu katika hospitali za rufaa za mikoa ya Mtwara, Dodoma, Tabora, Iringa, Morogoro, Arusha, Ruvuma, Kagera na Rukwa

Hospitali za Rufaa za Kanda - Bugando, Mbeya, KCMC, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Maabara ya Taifa ya Viwango na Ubora.

37. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza afua ya **tohara kwa wanaume** kama mojawapo ya afua ya kupambana na maambukizi ya VVU. Kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2016 jumla ya wanaume **374,411** kati ya lengo la wanaume **492,844** wenye umri wa kati ya miaka 10 hadi 49 wamepata huduma ya Tohara kutoka mikoa 14 ya kipaumbele (Mbeya, Songwe, Katavi, Rukwa, Ruvuma Njombe, Iringa, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Geita, Simiyu, Mara (Wilaya ya Rorya) na Kagera na kufikisha jumla ya wanaume **2,203,230** waliokwisha kupata huduma hiyo tangu ilipozinduliwa nchini mwaka 2010. Idadi hiyo ni sawa na asilimia **79** ya wanaume **2,800,000** wanaopaswa kufikiwa ifikapo mwaka 2017.

38. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau imebuni kifungashio kipya kwa kondom ya kiume ambayo imekuwa ikitolewa na serikali na kuipa jina la ZANA. **Kondom ya ZANA** ilizinduliwa kitaifa katika mkoa wa **Mbeya** na kutambulishwa kwa umma na hali kadhalika, uzinduzi ulifanyika pia katika mikoa ya **Mwanza, Arusha, Tanga, Dodoma, Mtwara, Kigoma na Morogoro**. Jumla ya kondom za **ZANA 21, 000,000** ziliagizwa na kusambazwa katika mikoa yote kupitia Bohari ya Dawa.

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza Nchini

39. Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko kubwa la Magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile Kisukari, Shinikizo la Damu na Magonjwa ya Moyo, Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa kupambana na magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza wa 2016 – 2020 ambao ulizinduliwa Dodoma mwezi Novemba 2016. Hatua hiyo ilifuatiwa na kuanzishwa kwa Kampeni ya Kitaifa inayolenga katika kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi na kupima afya mara kwa mara na kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa. Kampeni hiyo

ilizinduliwa na **Mhe. Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan** mwezi Desemba 2016 jijini Dar es Salaam, ambapo pamoja na mambo mengine Mhe. Makamu wa Rais aliagiza kuwa kila Jumamosi ya Pili ya Mwezi iwe ni Siku ya Hamasa ya Kufanya Mazoezi.

40. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa agizo hilo umeanza mara moja ambapo Mikoa/Halmashauri mbalimbali inaandaa mazoezi ya pamoja angalau mara moja kwa mwezi lengo likiwa ni kujenga utamaduni kwa wananchi hasa wanaoishi mijini na wanaofanya kazi za ofisini kufanya mazoezi ya mwili mara kwa mara na hivyo kupunguza maradhi, ulemavu na vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Sambamba na kampeni ya mazoezi, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kuzingatia mfumo bora wa maisha ikiwemo ulaji wa vyakula unaofaa, kupunguza unywaji wa pombe kupita kiasi, kujiepusha na matumizi ya sigara na bidhaa za tumbaku pamoja na kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara. Inategemewa kuwa, kutekelezwa kikamilifu kwa mikakati hii kutapunguza kwa kiasi kikubwa kasi ya kuongezeka kwa magonjwa haya nchini.

Udhibiti wa Matumizi ya Tumbaku na Kilevi

41. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuelimisha wananchi juu ya madhara ya Tumbaku, pamoja na kusimamia Sheria na Kanuni zinazohusu Uvutaji Sigara na matumizi ya mazao ya Tumbaku nchini kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Katika kutekeleza hilo, Wizara imehakikisha kuwa Pakiti za Sigara zinazouzwa nchini hivi sasa zina maandishi ya onyo "Uvutaji wa Sigara una athari katika Afya" yanayoonekana kwa urahisi (yenye ukubwa wa asilimia 30). Aidha, kanuni za mwaka 2014 za kudhibiti matumizi ya tumbaku zilifanyiwa mapitio na kuongeza suala la udhibiti wa matumizi ya Shisha. Kanuni hizi zinatarajiwa kuanza kutumika rasmi kuanzia mwezi Julai 2017.

Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto

42. *Mheshimiwa Spika*, Upatikanaji wa huduma inayofikiwa na wanawake wote, kabla ya ujauzito, wakati wa ujauzito, na wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua ni muhimili muhimu wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Hata hivyo, tatizo la vifo vitokanavyo na uzazi bado ni changamoto. Tafiti zilizofanyika hapa nchini mwaka 2015 zinaonyesha kwamba vifo vitokanavyo na uzazi havijapungua, ambapo takwimu zinaonesha idadi ya vifo ni 556 kwa kila vizazi hai 100,000. Katika kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto nchini, Wizara imeandaa Mpango Mkakati unaotekelezwa kuanzia mwaka 2016 hadi 2020 unaolenga kuboresha afya ya uzazi, watoto na vijana pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 292 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2020. Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imezingatia maeneo makuu matatu: ambayo ni: huduma ya uzazi wa mpango, huduma wakati wa ujauzito na huduma wakati wa kujifungua.

43. *Mheshimiwa Spika*, **uzazi wa mpango** ni eneo muhimu katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na kuhakikisha afya nzuri kwa mama na mtoto. **Tafiti zinaonyesha kwamba uzazi wa mpango ukitumiwa kikamilifu, unaweza kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa asilimia 30.** Hivyo, Wizara yangu imekuwa ikitekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana kwa wote wanaohitaji. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya **wateja 357,244** walifikiwa kupitia huduma za mkoba na **2,509,280** walifikiwa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya. Wizara kwa kushirikiana na wadau imetoa mafunzo kwa watoa huduma **3,233** ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma za aina mbalimbali za uzazi wa mpango. Aidha, Wizara imenunua na kusambaza dawa za uzazi wa mpango ikiwa ni pamoja na **“Depo-provera” vichupa 4,973,811**, **“Microval” mizunguko (cycles) 743,615 na Kondomu za Kiume 13,096,916.** Utekelezaji wa afua hizo umewezesha kiwango cha kutumia uzazi wa mpango kupanda kutoka asilimia 27 mwaka 2010 hadi asilimia 32 mwaka 2015/16 (TDHS). Lengo ni kufikia asilimia 45 mwaka 2020.

44. Mheshimiwa Spika, kuhusu **huduma wakati wa ujauzito** imebainika kuwa matatizo mengi wakati wa ujauzito yanaweza kuzuilika, kugundulika na kutibiwa kama wanawake wajawazito watahudhuria kliniki ya wajawazito na kupimwa na wahudumu wenye ujuzi. Huduma zinazopaswa kutolewa katika kliniki za wajawazito ni pamoja na; chanjo ya pepopunda, kupimwa wingi wa damu, kupimwa protini kwenye mkojo, kupimwa kama kunauambukizo wa VVU na vimelea vya kaswende na kupewa matibabu. Huduma nyingine zinazotolewa ni kugundua dalili za hatari na kutoa matibabu mapema wakati wa ujauzito. Katika kipindi cha 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendelea kuhakikisha huduma hizi zinapatikana sambamba na kuelimisha wajawazito kuhudhuria kliniki. **Kulingana na tafiti zilizofanyika mwaka 2015/16 asilimia 98 ya wajawazito wote walihudhuria kliniki angalau mara moja na asilimia 51 walihudhuria angalau mara 4** ambacho ni kiwango cha chini cha mahudhurio kinachopendekezwa. Lengo ni kufikisha asilimia 70 ya wanawake wajawazito kuhudhuria kliniki angalau mara 4 katika kipindi cha ujauzito ifikapo mwaka 2020. **Nitumie fursa hii kuwahimiza akinamama wajawazito kuhudhuria kliniki kama inavyoshauriwa.**

45. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa **huduma wakati wa kujifungua** ikiwemo huduma ya dharura wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua, ni muhimu sana ili kuepuka vifo vitokanavyo na uzazi. Huduma kwa matatizo haya hupatikana tu kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya na mtoa huduma mwenye ujuzi. Katika mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhamasisha na kuhimiza wanawake wajawazito kujifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma. Idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma imeongezeka kutoka **asilimia 51 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 64 mwaka 2015/16**. Napenda kutoa wito kwa wanawake wajawazito wote nchini wajifungulie kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya ili kupunguza vifo na changamoto za uzazi kwa mama na mtoto. Aidha, Wizara imetoa mafunzo mbalimbali ya uzazi salama na

huduma za dharura wakati wa ujauzito na kujifungua kwa watoa huduma 1,300 nchini.

46. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kusogeza huduma karibu na wananchi, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI, imekamilisha **ukarabati wa vituo vya afya 8** katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Simiyu na Mara ili viweze kutoa huduma za uzazi wa dharura ikiwemo upasuaji wa kutoa mtoto tumboni (CEmONC). Hadi sasa vituo vya Afya 171 vinatoa huduma za upasuaji na kati ya hivyo, 117 vinamilikiwa na Serikali ambapo ni sawa na asilimia 21 ya vituo vya afya **473** vinavyomilikiwa na Serikali. Aidha vituo vya afya 145 viko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji ili kuweza kutoa huduma za dharura za uzazi ikiwemo upasuaji wa kutoa mtoto. Lengo la serikali ni kuhakikisha angalau asilimia 50 ya vituo vya afya nchini vinatoa huduma kamili za uzazi wa dharura ifikapo mwaka 2020.

47. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kukabiliana na tatizo la uhaba wa damu hasa kwa wanawake wajawazito. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeanzisha utaratibu wa kuwa na vituo vya benki za damu kwenye ngazi ya mikoa hapa ili visaidaine na benki za damu za kanda katika kuboresha upatikanaji wa damu salama. Hadi sasa Benki za damu za Mikoa **7** zimeanzishwa katika mikoa ya Dar es salaam, Lindi, Morogoro, Dodoma, Iringa, Kigoma na Shinyanga. Aidha, uanzishwaji wa benki hizo katika mikoa ya Mara na Kagera upo katika hatua za mwisho. Lengo ni kuhakikisha kila Mkoa una Benki ya Damu ikiwa ni jitihada za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

48. Mheshimiwa Spika, Huduma za Rufaa kwa Wajawazito zimeendelea kuboreshwa ambapo Wizara imegawa **magari ya kubebea wagonjwa (Ambulance) 67** katika Halmashauri za Mikoa yote ya Kanda ya Ziwa na Kigoma na mikoa mingine hapa nchini. Aidha, Wizara imegawa **magari 8** kwa ajili ya kuratibu shughuli za afya ya mama na mtoto katika Kanda ya Ziwa, Kati, Magharibi, OR - TAMISEMI Dodoma, na magari 2 katika kitengo cha Afya ya mama na Mtoto Wizarani. Hatua hiyo itatoa msukumo na

kuimarisha juhudi za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi katika mikoa hiyo ambayo takwimu zimeonesha kuwa wana vifo vingi zaidi kuliko mikoa mingine nchini.

49. Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua kwa ajili ya **kuongeza uwajibikaji** kwa ngazi zote ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa kutaka kila kifo cha mama na mtoto kinachotokana na matatizo ya uzazi kijadiliwe ndani ya saa 24 katika kituo/hospitali husika kwa lengo la kubaini chimbuko la kifo hicho na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuboreshwa zaidi kwa huduma zinazotolewa katika kituo husika. Miongozo imeandaliwa na mafunzo ya kujenga uwezo yamefanyika kwa mikoa yote nchini. Sambamba na hilo **Wizara kuanzia mwezi Oktoba 2016 imeanzisha utaratibu wa kutaka kila halmashauri na mikoa nchini kutoa taarifa ya vifo vitokanavyo na uzazi kila mwezi**. Taarifa hizi zinafanyiwa kazi na hatua stahiki zimekuwa zikichukuliwa na mrejesho kutolewa kwa Mikoa na Halmashauri husika.

50. Mheshimiwa Spika, kuhusu **vifo vya watoto**, kupitia Mpango Mkakati wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa 2016-2020, Serikali imedhamiria kuwa ifikapo 2020 kupunguza vifo vya watoto wa chini ya mwezi mmoja kutoka 21 hadi 16 katika kila vizazi hai 1,000; vifo vya watoto wa chini ya umri wa mwaka mmoja kutoka 45 hadi 25 katika kila vizazi hai 1,000 na vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano kutoka 54 hadi 40 katika kila vizazi hai. Katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watoa huduma ya afya 241 katika wilaya tano za mkoa wa Iringa. Aidha katika kupunguza vifo vya watoto waliozaliwa na uzito pungufu, Wizara ilitoa mafunzo kwa watoa huduma 143 jinsi ya kumtunza mtoto mchanga kwa njia ya Kangaroo.

51. Mheshimiwa Spika, Jamii ni sehemu muhimu katika mikakati ya kuboresha afya ya uzazi na mtoto. Hivyo katika mwaka 2016/17 Wizara imetoa mafunzo ya afya ya uzazi na mtoto kwa wahudumu 1,649 wa afya kwa ngazi ya jamii (Community Health care Workers program) ambao wanatumika kuhamasisha na kuelimisha jamii wanapoishi.

Aidha Wizara imeanzisha mpango maalum wa kuwa na kada ya watoa huduma ngazi ya jamii watakaoajiriwa baada ya kupata mafunzo rasmi yaliyopitishwa na NACTE. Katika mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya wahudumu 3,688 walihitimu mafunzo yao.

52. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti saratani za via vya uzazi (Reproductive cancers) ikiwemo saratani ya mlango ya kizazi, saratani ya matiti na saratani ya Tezidume. Katika kuhakikisha kuhakikisha upatianaji wa **huduma za kupima na matibabu ya Mabadiliko ya awali ya Saratani ya Mlango wa kizazi na saratani ya matiti** ambazo ndizo zinazoongoza nchini, vituo 360 vya kupima dalili za awali ya Saratani ya mlango wa kizazi vimeanzishwa na kutoa huduma hiyo katika mwaka wa fedha 2016/17. Aidha Taasisi za Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yameendesha kampeni za kuelimisha jamii juu ya kudhibiti saratani za via vya uzazi sambamba na kuandaa kambi na huduma za kupima saratani za uzazi katika maeneo mbalimbali nchini.

Huduma za Lishe

53. Mheshimiwa Spika katika mwaka 2016/17, Wizara inaendelea kushirikiana na asasi mbalimbali za Serikali na zisizo za kiserikali kuhakikisha virutubishi muhimu kwa ukuaji wa mwili na akili vinaendelea kupatikana kote nchini. Kwa sasa urutubishaji unaoendelea ni ule wa uongezaji wa virutubishi muhimu kwenye unga wa mahindi na unafanyika katika mikoa ya Morogoro, Dodoma na Dar es Salaam wakati mikoa ya Iringa (Kilolo na Iringa vijijini), Njombe (Njombe mjini) na Arusha (Monduli, Karatu na Meru) inaendelea na mradi wa urutubishaji vijijini. Aidha usindikaji wa mafuta ya alizeti kwa kuongeza vitamini A unaendelea katika mikoa ya Singida na Manyara. Jumla ya mikoa 11 (Dodoma, Arusha, Morogoro, Dar es Salaam, Lindi, Iringa, Mbeya, Tabora, Rukwa, Mara na Simiyu) imefikwa kupitia mpango wa urutubishaji chakula kwa kutumia virutubishi nyongeza kwenye chakula cha kawaida kwa watoto wenye umri wa miezi 6 hadi 59 katika ngazi ya jamii (Home food

Fortification). Kwa mujibu wa takwimu za TDHS 2015/16 kaya zinazotumia chumvi yenye madinijoto kwa viwango vilivyowekwa kisheria zimeongezeka na kufikia asilimia 61 kutoka asilimia 47 mwaka 2010.

Elimu ya Afya kwa Umma

54. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/17, Wizara iliendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza afya zao dhidi ya magonjwa na kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara. Wizara iliendelea kuelimisha jamii kujikinga na ugonjwa wa kipindupindu kupitia matangazo ya Radio, Runinga, simu za kiganjani kwa kupiga simu nambari 117 bila malipo. Aidha Wizara ilitayarisha na kusambaza kupitia mitandao ya kijamii elimu kuhusu magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyo ya kuambukiza. Vilevile, Wizara ilihakiki matangazo na vielelezo mbalimbali vilivyotayarishwa na wadau, kuhusu ubora unaotakiwa ikiwa ni pamoja na kuzingatia Sera na Miongozo ya Wizara. Matangazo na Vielelezo hivyo vilihusu uzazi wa mpango, afya ya uzazi na mtoto, saratani ya mlango wa kizazi, lishe, chanjo, UKIMWI, kifua kikuu, afya ya mazingira, magonjwa yanayoambukiza na yasiyo ya kuambukiza, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, malaria, afya ya kinywa na meno pamoja na macho. Wizara imekamilisha ujenzi wa studio ya radio na runinga ambazo zitaiwezesha Wizara kurekodi vipindi vya kuelimisha na kuhamasisha jamii.

HUDUMA ZA TIBA

Huduma za Damu Salama

55. Mheshimiwa Spika Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama imeendelea kutekeleza jukumu la ukusanyaji na usambazaji wa Damu Salama nchini, ambapo katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya chupa za damu **145,300** zilikusanywa, sawa na asilimia **63** ya lengo la kukusanya chupa **230,000** kwa mwaka. Chupa zote za damu zilizokusanywa ziliweza kupimwa kwa ufasaha magonjwa yote manne ambayo ni VVU, kaswende, homa

ya ini aina B na C pamoja na kuangalia makundi ya damu, ambapo jumla ya chupa **130,408 sawa na asilimia 90** zilionekana kutokuwa na maambukizi ya aina yoyote na hatimaye kusambazwa hospitalini kwa ajili ya kupewa wagonjwa wahitaji.

Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

56. Mheshimiwa Spika; Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kuboresha upatikanaji wa dawa kwa kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika mwaka 2016/17, Wizara ilitenga **Shilingi 251,500,000,000.00** kwa ajili ya kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba, na vitendanishi ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 31,000,000,000.00** kilichotengwa mwaka 2015/16. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya **Shilingi 112,198,920,456** zilipokelewa ambazo ni sawa na **asilimia 45**. Hadi kufikia mwezi Machi 2017 mikoa/halmashauri/hospitali zimepokea zaidi ya asilimia 95 ya fedha za dawa. (*Kiambatisho Na. 2*) Upatikanaji wa fedha hizi umeboresha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba nchini ikilinganishwa na kipindi kilichopita. Nitumie furusa hii kuzitaka mamlaka za halmashauri na mikoa/hospitali kuhakikisha uwepo wa mifuko maalum ya dawa (drung revolving fund) katika maeneo yao ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa fedha za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

57. Mheshimiwa Spika; Hadi kufikia Machi, 2017, asilimia **81 ya dawa muhimu zaidi (essential medical items) zinapatikana katika Bohari ya Dawa**. Ongezeko hili la upatikanaji wa dawa kutoka **asilimia 36** kipindi cha mwezi Juni 2016 na kufikia **asilimia 81** mwezi Machi, 2017 limetokana na uamuzi wa Serikali wa kuongeza bajeti ya dawa na kuhakikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya dawa, vifaa, vifaa tiba, na vitendanishi. Aidha, katika kuboresha upatikanaji wa dawa, Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeanza kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo **ununuzi wa dawa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji** kwa lengo la kupunguza gharama za dawa na kuongeza uwezo wa

MSD kununua dawa nyingi zaidi ambapo Zabuni 6 za wazalishaji zimekamilika. Kukamilika kwa zabuni hizi, kutawezesha upatikanaji wa dawa muhimu zaidi kutoka moja kwa moja kwa wazalishaji kwa asilimia 76. **Lengo la Wizara ni kuhakikisha hali ya upatikanaji wa dawa inafikia asilimia 90 ifikapo mwishoni mwa mwaka wa fedha 2016/17.**

58. Mheshimiwa Spika; kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, na vitendanishi katika Bohari ya Dawa kumeongeza **upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za Afya afya nchini.** Kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa kutoka katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini, hali ya upatikanaji wa dawa kwenye vituo inakadiriwa kuwa wastani wa **asilimia 83** kufikia mwishoni wa Machi 2017 (**Kiambatisho Na. 3**). Wizara itaendelea kukusanya taarifa za upatikanaji wa dawa kutoka Halmashauri na Mikoa kila mwezi ili kujiridhisha zaidi juu ya hali halisi ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma hasa ngazi ya zahanati na vituo vya afya. Hata hivyo, bado zipo changamoto mbalimbali katika upatikanaji wa dawa ikiwemo baadhi ya **Halmashauri /Hospitali kutowasilisha mahitaji yao ya dawa kwa wakati** na hivyo kusababisha tatizo la upatikanaji wa dawa katika vituo. Vilevile, kuna usimamizi hafifu wa matumizi ya dawa, makusanyo na matumizi ya fedha zitokanazo na uchangiaji wa huduma za afya na matumizi ya mifumo na utunzaji taarifa za dawa na vifaa tiba. Wizara imejipanga kukabiliana na changamoto hizi kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI. Moja ya hatua tulizochukua ni kuamua kuwa kuanzia Julai 2017 fedha za dawa kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund) zitapelekwa moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma. Nitumie fursa hii kuzitaka mamlaka za halmashauri na mikoa kuhakikisha wanasimamia fedha hizo ikiwemo makusanyo na matumizi ya fedha zitokanazo na uchangiaji wa huduma za afya sambamba na kutoa taarifa sahihi za hali ya upatikanaji wa dawa.

59. Mheshimiwa Spika; kwa kutambua changamoto zilizopo katika mfumo wa ugavi na usambazaji

wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo nchini, Wizara imefanya mapitio ya mfumo (Holistic Supply Chain Review) kwa lengo la kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji ili kuwa na mfumo madhubuti wenye kukidhi mahitaji ya nchi.

60. Mheshimiwa Spika; Wizara pia imetekeleza ahadi ya **Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli** ya kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya cha umma kinakuwa na vifaa vya kutosha. Katika mwaka 2016/17, **Wizara imenunua na kuanza kusambaza kwa kila Halmashauri vitanda vya kawaida 20, vitanda vya kujifungulia 5, magodoro 25 na mashuka 50.** Uzinduzi wa zoezi hili umefanyika mwezi Aprili 2017 katika halmashauri ya Kongwa Dodoma. Jumla ya vitanda vya kawaida (Hospital beds) 3,680, vitanda vya kujifungulia (delivery beds) 920, magodoro 4,600 na mashuka 9,200 vimenunuliwa ambapo thamani yake ni **Shilingi 2,933,125,600.00**

61. Mheshimiwa Spika, Usugu wa dawa aina ya antibiotiki ni tatizo kubwa ambalo linaikabili dunia kwa sasa. Hali ya Dunia ya utumiaji wa dawa aina ya antibiotiki kwa mwaka 2015 inaonyesha kwamba matumizi ya dawa hizo kwa ukuzaji wa kuku, ng'ombe na nguruwe, husababisha Usugu wa dawa kwa vimelea vya bakteria ambavyo vinaenea kwa binadamu. Aidha, utafiti uliofanyika hapa nchini umeonesha kuongezeka kwa usugu wa dawa za antibiotiki katika kutibu magonjwa ya kuambukiza kwa binadamu, wanyama na mazingira.

62. Mheshimiwa Spika, Katika kupambana na usugu wa dawa hizo, Serikali imeitikia tamko la Mkutano Mkuu wa 68 wa Shirika la Afya Duniani uliofanyika mwaka 2015 ambapo nchi Wanachama walikubaliana kufanya juhudi za dhati za kupambana na usugu wa dawa hizo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na uvuvi na Wadau wengine imeandaa mpango wa miaka mitano wa kupambana na usugu wa dawa hizo kwa binadamu, mifugo na kilimo. Mpango huu umekamilika na kuzinduliwa mwezi Aprili, 2017.

63. Mheshimiwa Spika Mpango huo pamoja na mambo mengine umelenga kuhamasisha na kuelimisha wataalam wa afya na wananchi kwa ujumla juu ya madhara yatokanayo na utumiaji wa dawa za antibiotiki usio sahihi kwa binadamu, mifugo na kwenye kilimo na jinsi ya kutatua changamoto hizo. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utumiaji ulio sahihi wa dawa aina ya antibiotiki hasa kwa kufuata sheria na kanuni zilizowekwa na inapobidi kuandaa sheria mpya; Kuzuia maambukizi ya vimelea vya bakteria kwa kuzingatia usafi wa mazingira hasa sehemu za kutolea huduma na katika kukuza mifugo.

Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya kibingwa

64. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, moja ya jukumu la kipaumbele kwa Wizara ilikuwa ni kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma za kibingwa zitolewazo nchini. Maboresho hayo, yanalenga katika kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi ili kupunguza gharama kubwa ambazo serikali inaingia katika kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Hadi kufikia Machi 2017, **idadi ya Wagonjwa waliopewa rufaa ya Matibabu nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 35** kutoka wagonjwa **553** mwaka 2015/16 hadi Wagonjwa **357** mwaka **2016/17**. Mafanikio haya ni kutokana na maboresho yaliyofanyika katika Hospitali zilizo chini ya Wizara zinazotoa huduma za Kibingwa ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), MOI na Ocean Road. Takwimu za mwaka 2016/17 zinaonyesha kuwa magonjwa yanayoongozwa kwa rufaa nje ya nchi ni Saratani (36%), Moyo (17%), Masikio, pua na koo (15%), mishipa ya fahamu (8%), mifupa (4%) na mengineyo (5%).

Hospitali ya Taifa Muhimbili

65. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, **Hospitali ya Taifa Muhimbili** imewahudumia jumla ya wagonjwa wa nje 317,660 ikilinganishwa na wagonjwa 357,343 waliopatiwa huduma mwaka 2015/2016. Aidha, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa waliolazwa

39,418 ikilinganishwa na wagonjwa 51,698 mwaka 2015/2016. Pia, ukusanyaji wa mapato ya Hospitali umeongezeka na kufikia kiasi cha **shilingi 39,793,000,000** kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017 ikilinganishwa na **shilingi 30,145,000,000** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho 2015/16 ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 32**.

66. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa Muhimbili imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za kibingwa. Hatua hizo ni pamoja na kufanya ukarabati wa Wodi mbalimbali kwa lengo la kuongeza uwezo wa kuhudumia wagonjwa wengi, ambapo jumla ya wadi 5 za ICU zimefanyiwa ukarabati. **Ukarabati huo utaongeza vitanda vya ICU kutoka 21 na kufikia 75**. Aidha, mashine **14** za upasuaji (Diathermy Machines), mashine kubwa mbili (**2**) za utakasishaji vifaa zenye thamani ya **Shilingi milioni 717.6** zimenunuliwa. Vilevile, Hospitali imenunua mashine ya **CT-Scan** mpya yenye uwezo wa "slice" **128**, ambayo imegharimu **Shilingi bilioni 3.9**. Pia Hospitali imefanya ukarabati wa mashine za *ventilators, monitors na anaesthesia* kwa jumla ya **Shilingi milioni 213**. Hospitali imeanza kukarabati jengo kuu la upasuaji wa kina mama wajawazito na jengo la upasuaji wa watoto; ukarabati huo utaongeza vyumba vya upasuaji **6** na kufanya Hospitali iwe na jumla ya vyumba **19**. **Upanuzi wa jengo la kusafisha figo** unafanyika ambao utaongeza vitanda **27** na kufikia jumla ya vitanda **42** ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 1.02** zitatumika. Aidha, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imepeleka jumla ya wataalamu saba (7) nchini India kwa ajili ya mafunzo ya upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia (Cochlear Implants) kwa wagonjwa wenye matatizo ya kusikia. Jumla ya **Shilingi milioni 75.8** zimetumika katika mafunzo haya. Vilevile katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kubadilisha figo nchini, wataalamu ishirini (20) wakiwemo Madaktari, Wauguzi, Wataalamu wa Maabara wamepatiwa mafunzo nchini India kwa gharama ya **Shilingi milioni 700**.

67. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili pia imepanua sehemu ya kutoa huduma za dharura ili kuendana

na ongezeko la wagonjwa sambamba na kuwa na sehemu ya dharura kwa ajili ya watoto. Upanuzi huo umeshakamilika kwa asilimia **60** na utagharimu **Shilingi bilioni 1**. Aidha, Hospitali imekarabati Wadi ya Sewahaji namba 18 kwa ajili ya wagonjwa wa kulipia yenye vitanda 13 kwa kutumia **Shilingi milioni 250 ambazo zimetokana na** vyanzo vya ndani. Aidha, upatikanaji wa Dawa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili umeongezeka na kufikia zaidi ya asilimia **95**. Vilevile Hospitali imeanzisha mfuko wa fedha za kununulia dawa (**Revolving Fund**) ambao sasa umefikia **Shilingi 1,000,000,000** inayolipwa kila mwezi ili kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa dawa.

68. Mheshimiwa Spika, Hospitali kwa kushirikiana na Mpango wa Damu Salama ilianzisha huduma za kuchangia damu katika jamii zoezi ambalo limepunguza kwa kiasi kikubwa sana ukosefu wa damu Hospitalini. Hospitali imeanzisha mpango wa uchunguzi na tiba kwa ugonjwa sugu wa homa ya ini ambao utatoa fursa kwa watazania kupata huduma hiyo. Mpango huo utawezesha vituo vingine kujifunza na kuweza kutoa huduma hiyo.

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

69. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)** imewahudumia jumla ya wagonjwa wa nje 119,580 ikilinganishwa na wagonjwa 79,927 waliopatiwa huduma mwaka 2015/2016. Aidha, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa waliolazwa 6,830 ikilinganishwa na wagonjwa 8,355 mwaka 2015/2016. Pia, kutokana na matumizi ya mfumo wa kieletroniki (HMIS) ukusanyaji wa mapato, umeongezeka kwa asilimia 8.5 na **kufikia shilingi 6,707,172,559.43 kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Februari, 2017** ikilinganishwa na shilingi **6,134,667,970.65** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho 2015/16.

70. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya MOI imeendelea na juhudi za kupanua wigo wa huduma za kibingwa ambapo katika kipindi cha Julai 2016 - Machi 2017, imeanza kutoa

huduma ya upasuaji wa migongo ya watoto iliyopinda (paediatric scoliotic spine correction) ikishirikiana na *Centre of Disease Excellence in Orthopaedics (COEDN)* ya Marekani pamoja na kuanzisha mafunzo ya upasuaji huo. Aidha, Taasisi hiyo imetoa huduma za upasuaji mkubwa kwa wagonjwa 496, wakijumuisha wagonjwa 67 waliofanyiwa upasuaji wa nyonga, 62 mgongo, 55 Ubongo, 262 watoto wenye vichwa vikubwa na 50 watoto wenye mgongo wazi.

71. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya MOI kwa kushirikiana na GSM Foundation imetoa huduma ya upasuaji wa vichwa vikubwa na mgongo wazi kwa watoto kupitia kambi Tiba katika mikoa 18 ya Tanzania Bara na hospitali ya Mnazi Mmoja – Zanzibar. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya watoto **2,200 walifanyiwa uchunguzi na watoto 250 walifanyiwa upasuaji kwa** mafanikio na kutoa mafunzo kwa Madaktari wa upasuaji wa kawaida katika hospitali za rufaa za mikoa/kanda nchini. Kwa sasa Taasisi ipo kwenye mpango wa kuchukua madaktari wa upasuaji toka hospitali husika kuja Dar es Salaam kujifunza zaidi upasuaji huo. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Weil Cornell na California San Francisco vya Marekani, inafanya utafiti wa kuboresha matibabu kwa wagonjwa wa ajali ya Kichwa, mfupa wa paja na Ugoko.

Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)

72. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai 2016 hadi 2017, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKC) imewahudumia jumla ya wagonjwa wa moyo wanaotibiwa na kurudi nyumbani **37,199** ikilinganishwa na wagonjwa **24,570** waliopatiwa huduma hiyo mwaka 2015/2016. Taasisi ilifanya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa **236** kwa gharama ya **shilingi 1,555,500,000.00** ambapo kama upasuaji huo ungefanyika India ungegharimu takribani **shilingi 5,307,000,000.00**, hivyo kuokoa kiasi cha **shilingi 3,751,500,000.00**. Idadi hii ni sawa na **wastani wa wagonjwa 30 kwa mwezi**, ikiwa ni ongezeko la asilimia 100 ukilinganisha na **wastani wa wagonjwa 15 kwa mwezi** katika mwaka wa fedha 2015/16. Kati ya wagonjwa 236 waliofanyiwa upasuaji,

watu wazima walikuwa 74 wakati watoto walikuwa 162. Asilimia 49 ya wagonjwa walifanyiwa upasuaji na madaktari wa JKCI na asilimia 51 walifanyiwa kwa kushirikiana na madaktari kutoka nje ya nchi kupitia kambi za upasuaji wa pamoja. Aidha jumla ya **wagonjwa 608** walipatiwa matibabu maalum kupitia **tundu dogo kwa kutumia mtambo wa kisasa - catheterization laboratory** (stents, percutaneous intervention, device closure, pacemaker). Idadi hii ni ongezeko la **asilimia 190** ukilinganisha na **wagonjwa 290 waliohudumiwa katika mwaka wa fedha 2015/16**. Kati ya wagonjwa hao, **asilimia 82.6** walikuwa watu wazima na **asilimia 17.4** walikuwa watoto. **Asilimia 89** ya huduma ya matibabu maalum ya moyo kwa kutumia mtambo wa kisasa – *catheterization laboratory* zimefanywa na madaktari wa Taasisi na **asilimia 11** zilifanywa kwa kushirikiana na wataalam kutoka nje ya nchi.

73. Mheshimiwa Spika, Vilevile, JKCI ilifanya kambi 3 za upasuaji kwa kushirikiana na mataifa rafiki (Israel, Germany na Australia). Hatua hiyo imesaidia kujenga uwezo wa madaktari wazawa kwa kupata utaalam wa kupasua wagonjwa kutumia tundu dogo (hii inasaidia wagonjwa kupona mapema na kuruhusiwa kurudi nyumbani ndani ya siku chache). Vilevile, **JKCI** kwa kushirikiana na Wizara imeweza kupeleka madaktari 9 kwenye masomo ya juu katika fani ya moyo (2 Afrika ya Kusini, 2 Israel, 1 India, 1 China na 3 MUHAS). Pia imeweza kuchapisha matokeo ya chunguzi zake kwenye majarida ya kimataifa machapisho 3 (3 peered reviewed publications).

Taasisi ya Saratani Ocean Road

74. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, **Taasisi ya Saratani Ocean Road** iliendelea kutoa huduma za uchunguzi, matibabu, kinga, mafunzo na utafiti wa saratani. Katika kipindi hicho, Taasisi imehudumia jumla ya wagonjwa **19,244** ambapo **3,982** ni wagonjwa wapya wa Saratani, **13,109** ni wagonjwa wa marudio wa saratani, na **2,133** ni wagonjwa wasio wa saratani ikilinganishwa na

wagonjwa 31,075 walipatiwa huduma na Taasisi katika mwaka 2015/2016. Aidha, jumla ya wanawake **6,717** walifanyiwa uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi na matiti na wanaume **534** walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya tezi dume. Katika uchunguzi huo, jumla ya wanawake **451** waligunduliwa kuwa na dalili za awali za saratani ya mlango wa kizazi na **267** walikutwa na dalili za saratani ya matiti. Vilevile, wananchi **1,204** walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi, saratani ya matiti na saratani ya tezi dume katika kampeni ya mkoa wa Dar es Salaam iliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja pamoja iliyofanyika kwa Waheshimiwa wabunge, Dodoma mwezi Februari 2017.

75. Mheshimiwa Spika, Taasisi iliendelea kutoa huduma za mkoba katika mikoa mbalimbali ambapo jumla ya wagonjwa **3,215** walipatiwa matibabu na rufaa kufuatana na mwongozo wa huduma. Aidha, jumla ya wananchi **16,433** walifanyiwa upimaji wa saratani katika mashirika mbalimbali ya serikali na yasiyo ya kiserikali katika huduma ya elimu na upimaji. Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) iliendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi **43** wa Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Saratani kwa Mionzi na wanafunzi **17** wa Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Tiba ya Saratani. Wanafunzi **2** walihitimu Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Tiba ya Saratani na wanafunzi **3** Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Saratani kwa Mionzi. Pia, Taasisi imeendelea kushirikiana na wadau wa ndani na nje katika utafiti wa Saratani na katika kipindi husika jumla ya machapisho **matatu (3)** yalichapishwa katika majarida ya kisayansi duniani (peer-reviewed journals).

76. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Saratani Ocean Road imekamilisha ukarabati wa jengo la kutolea tiba ya dawa (chemotherapy) pamoja na kununua vifaa na vitanda ambapo idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa imeongezeka kutoka wastani wa wagonjwa 40 hadi kufikia wagonjwa 100 kwa wakati mmoja. Aidha, Taasisi imeweza kupunguza muda wa kusubiri kuanza tiba za mionzi (radiotherapy) kutoka miezi 3 hadi wiki 6; kwa

kuhakikisha wagonjwa wanapata tiba mara mbili kwa wiki na kufanya matengenezo ya mashine kwa haraka. Lengo la Wiraza ni kupunguza muda huo uwe chini ya wiki 2 pindi mashine mpya za LINAC zitakaposimikwa.

77. Mheshimiwa Spika, upatikanajii wa dawa za saratani umeboreshwa kutoka asilimia 4 mwaka 2015/16 hadi kufikia asilimia 60 mwezi Machi, 2017; na kwa baadhi ya saratani kama ya mlango wa kizazi, saratani ya koo, tezi dume na dawa za dripu (chemotherapy) zinapatikana kwa asilimia 100. Aidha, upatikanaji wa dawa za mionzi hasa radioactive iodine kwa sasa zinapatikana kwa asilimia 100 na ununuzi wa dawa hizo unafanywa kutoka kiwandani nchini Afrika Kusini kupitia MSD. Taasisi imeanzisha duka la dawa la jamii ambalo limeongeza wigo wa upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa na hasa wale wa Bima na kuongeza mapato ya dawa kutoka Milioni 30 kwa mwezi hadi kufikia Milioni 700 kwa mwezi.

78. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Saratani Ocean Road ilikamilisha ujenzi wa jengo la 'bunker' ambapo mashine za mionzi za LINAC pamoja na CT Simulator zitasimikwa. Aidha, Taasisi inakamilisha taratibu za manunuzi ili kununua mashine hizo ambazo zinategemewa kusimikwa mwezi Juni 2017.

Hospitali ya Rufaa Benjamin Mkapa - DODOMA

79. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Hospitali ya Rufaa Benjamin Mkapa ilihudumia jumla ya wagonjwa 21,662 ambapo wagonjwa wa nje walikuwa 20,812 na waliolazwa 850 ikilinganishwa na wagojwa 6,450 waliohudumiwa mwaka 2015/2016. Aidha, uchunguzi wa matibabu ya Macho kwa ushirikiano na timu ya wataalamu kutoka Marekani ulifanyika katika Hospitali kwa wagonjwa 3,500 na kati ya hao wagonjwa 500 walifanyiwa upasuaji na waliobaki walipata matibabu mengine ikiwemo utoaji wa miwani na ushauri mbalimbali. Vilevile, kulifanyika huduma za uchunguzi wa figo mwezi Machi 2017 ambapo wagonjwa 754 walichunguzwa na kupewa ushauri. Pia, Hospitali imekabidhiwa gari la kubebea

wagonjwa na Wizara ili kukidhi mahitaji ya huduma kwa wagonjwa.

80. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza na kuboresha utoaji wa huduma za afya, Hospitali imefunga mitambo ya Uchunguzi wa magonjwa mbalimbali kama vile MRI, CT-Scan, Mammography, General Purpose X-ray, Fluoroscopy, Ultrasound na Dental Unit and Dental X-ray machine. Huduma zitaanza kutolewa baada ya Tume ya Taifa ya Mionzi kutoa leseni. Aidha, hospitali ipo katika hatua za mwisho za ukamilishwaji wa maabara ya kisasa *Cath-lab* kwa ajili ya matibabu ya moyo pamoja na Maabara yenye uwezo wa kuchunguza vinasaba ambapo hadi mwezi Machi 2017 baadhi ya vifaa vimenunuliwa ikiwemo DNA, Analyser, Dignator PCR na Conventional PCR. Vilevile, hospitali imeboresha na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Wodi za wagonjwa, jengo la huduma za kinywa na Meno, Vyumba vya upasuaji na Chumba cha Wagonjwa mahututi.

Hospitali ya Mirembe

81. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 **Hospitali ya Mirembe** ilihudumia jumla ya wagonjwa wa akili 2,111 kati yao wanaume 1,511 na wanawake 600 na pia ilihudumia wagonjwa wa magonjwa ya kawaida 364. Aidha, hospitali ilihudumia wagonjwa wa akili wa kutibiwa na kuondoka 8,363 ambao kati yao wanaume walikua 3,023 na wanawake 5,340. Wagonjwa wa magonjwa mengine 12,633 walihudumiwa katika mwaka 2016/17; ikilinganishwa na wagonjwa 33,900 waliopewa huduma mwaka 2015/2016.

82. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 2002 na Sheria ya Afya ya Akili ya mwaka 2008, **Hospitali** ilihudumia jumla ya wagonjwa wa akili wahalifu 374 waliopokelewa katika Taasisi ya Isanga ambapo wanaume walikuwa 297 na wanawake 77. Aidha, Hospitali iliandaa ripoti za kisheria kwa wagonjwa wa akili wahalifu 75 ambao walihisiwa kutenda makosa

wakati wakiwa na ugonjwa wa akili, kati yao wanaume 66 na wanawake 9. Wagonjwa hao walichunguzwa na taarifa za kitaalamu zilitumwa katika Mahakama Kuu na Mahakama za Wilaya ili kuzisaidia katika kufikia maamuzi ya kisheria. Taasisi pia, ilipokea hati za ruhusa kwa wagonjwa 62 wa kundi maalum (Category C) wakiwemo wanaume 53 na wanawake 9. Wagonjwa hao ni wale waliopona na kumaliza muda wao wa matibabu wa miaka 3 kwa mujibu wa Sheria.

Hospitali Maalumu ya Kibong'oto

83. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Hospitali iliendelea kutoa huduma kwa wagonjwa **18,441** wa nje na kati ya hao wagonjwa wa Kifua Kikuu na UKIMWI ni **283**, Kifua Kikuu Sugu waliolazwa **112**, Kifua Kikuu cha kawaida **159** na wagonjwa 17,887 wa magonjwa mengine ikilinganishwa na wagojwa **22,348** kwa mwaka 2015/2016. Katika kufuatilia mwenendo wa magonjwa ya kuambukiza, Hospitali imeweza kupima sampuli za makohozi kwa wagonjwa 1,961 na kupata wagonjwa 367 (asilimia 33.5) na kati yao wagonjwa 30 walikuwa na Kifua Kikuu Sugu. Aidha hospitali imepata mashine ya kupima usugu wa vimelea vya Kifua Kikuu kwa dawa daraja la pili (Secondline anti tuberculosis drug susceptibility testing) na kupunguza muda wa uchunguzi wa Kifua Kikuu Sugu Zaidi (Extensive drug Resistant TB) chini ya siku 90.

84. Mheshimiwa Spika, Hospitali pia iliendelea kutoa elimu kwa watoa huduma kutoka Hospitali mbalimbali nchini kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuanzisha matibabu ya Kifua Kikuu Sugu nchini. Vituo **19** katika Mikoa **14** wamejengewa uwezo wa kutibu wagonjwa na kuwafuatilia matibabu. **Kwa hivi sasa hospitali imeweza kufupisha muda wa kuanza Tiba kutoka siku 14 mpaka siku 3 tangu mgonjwa kugundulika kuwa na kifua Kikuu Sugu hivyo kupunguza maambukizi kwa jamii.** Aidha, Hospitali ilifanya tafiti mbalimbali za kusaidia kujua changamoto zinazoikabili sekta ya afya katika mfumo mzima wa ugunduzi na tiba ya Kifua Kikuu na UKIMWI kwa kushirikiana na taasisi za utafiti nchini na nchi za nje. Vilevile,

Hospitali imechapisha machapisho matatu ya kisayansi kifua kikuu na kifua kikuu sugu.

85. Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa bajeti ya 2016/17, **Hospitali ya Kibong'oto** kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Nelson Mandela imeandaa andiko la kuanzisha mafunzo ya shahada za uzamili na uzamivu katika magonjwa ya kuambukiza ikiwa na lengo la kuongeza wataalam wabobezi wenye uwezo wa ugunduzi wa vipimo kwa magonjwa haya nchini. Kwa makubaliano hayo wafanyakazi wawili (Madaktari; 1 shahada ya uzamivu na 1 shahada ya uzamili) wamejiunga na Chuo cha Nelson Mandela kusomea Sayansi ya Magonjwa ya Kuambukiza.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya)

86. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 **Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mbeya** imewahudumia jumla ya wagonjwa wa nje **175,478** ikilinganishwa na wagonjwa 198,219 waliopatiwa huduma mwaka 2015/2016. Aidha, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa waliolazwa **24,927** ikilinganishwa na wagonjwa **29,162** mwaka 2015/2016.

87. Mheshimiwa Spika, **Hospitali** imeendelea kuimarisha huduma za kibingwa, ambapo hadi kufikia Machi 2017, jumla ya wagonjwa 37 walifanyiwa upasuaji kwa kutumia tundu dogo. Aidha, Hospitali kwa kushirikiana na Taasisi ya Mifupa Muhimbili imefanya upasuaji kwa watoto wenye matatizo ya mgongo wazi na vichwa vikubwa. Jumla ya Wagonjwa 10 wamewekewa *Arteriovenous Fistula* kwa ajili ya kuchujia damu (*dialysis*).

88. Mheshimiwa Spika, Hospitali imeendelea kuboresha na kupanua wigo wa huduma zinazotolewa kwa kukarabati jengo la daraja la kwanza na **kukamilisha ujenzi wa jengo la watoto**. Kukamilika kwa jengo jipya la Idara ya Watoto kutatoa nafasi kwa Idara ya upasuaji (mifupa na ajali, njia ya mkojo na tezi dume pamoja na upasuaji wa jumla) na

hivyo kumaliza tatizo la wagonjwa kulala chini. Kukamilika kwa miradi hiyo miwili kutaongeza uwezo kwa hospitali kutoka **vitanda 477 vya sasa mpaka vitanda 605**.

89. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Hospitali imeanzisha idara ya **matibabu ya pua, koo na masikio (ENT)** na hivyo kuwaondolea wananchi mzigo wa kusafiri kufuata huduma hizo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Hadi kufikia mwezi Machi 2017 wagonjwa 883 wenye matatizo ya pua, koo na masikio wamehudumiwa. Aidha, Idara ya Mifupa imeimarishwa baada ya kupata vifaa kama *sign nails sets* hivyo kupunguza sana muda wa wagonjwa walio vunjika kukaa wodini ambapo kwa sasa mgonjwa hukaa wodini kwa muda wa chini ya siku tatu ikilinganishwa na siku 42 ilivyokuwa hapo awali. Vilevile, Huduma ya kusafisha figo (dialysis) imeimarishwa kwa kununua vitanda vipya 3 na hivyo kufikisha idadi ya vitanda 6. Pia, hospitali imepata mashine za kisasa za maabara (cobas machine), *histopathology* na mashine ya kutolea dawa ya usingizi, vyote vikiwa na thamani ya **shilingi milioni 340**, pamoja na kununua mashine ya vipimo vya damu (Hematology) kupitia fedha zake za ndani iliyogharimu kiasi cha **shilingi milion 57**. Aidha, mchakato wa kukamilisha ujenzi wa jengo la radiologia unaendelea ambapo tayari shilingi bilioni 1.5 zimepokelewa kutoka Hazina.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa – Bugando

90. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, **Hospitali ya Bugando** iliwahudumia jumla ya wagonjwa 117,992 ambapo wagonjwa wa nje walikuwa 89,091 na waliolazwa walikuwa 28,901 ikilinganishwa na wagonjwa 327,080 mwaka 2015/2016. Hospitali pia imeendelea kutoa huduma za kifua na moyo ambapo jumla ya wagonjwa 1,347 walihudumiwa na 26 walifanyiwa upasuaji mkubwa. Aidha, **huduma za moyo kwa watoto zimeanza kutolewa kuanzia mwezi Januari 2017** na hadi sasa watoto 250 wamepata huduma hizo. Hospitali imetoa huduma kwa **akinamama 174 wenye fistula**. Vilevile, Hospitali imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya kutolea

huduma ikiwa ni pamoja na kliniki za wagonjwa wa nje, jengo la Saratani, na kukamilisha ujenzi wa kliniki ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

91. Mheshimiwa Spika, Hospitali imekamilisha ufungaji wa CT-Scan simulator ambayo hutumika kupanga matibabu ya mionzi ya saratani. Huduma zitaanza kutolewa baada ya Tume ya Mionzi ya Taifa (TAEC) kutoa leseni. Kukamilika kwa usimikaji wa mitambo hiyo na kuanza kutolewa kwa matibabu ya saratani kwa njia ya mionzi itakuwa ni ukombozi na faraja kubwa kwa wagonjwa wa saratani wa Kanda ya Ziwa ambao wamekuwa wakilazimika kusafiri hadi Dar es Salaam ili kupata huduma hiyo katika Taasisi ya Saratani Ocean Road. Hospitali ya Bugando pia imeweza **kuanzisha kituo cha kusafisha damu** (Haemodialysis Unit) ambacho kinaweza kutoa huduma kwa wagonjwa 10 kwa wakati mmoja. Kituo hiki ambacho kilianza mwezi Julai 2016 hadi sasa kimeweza kuhudumia wagonjwa 30 katika mizunguko (sessions) 2,107.

Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – KCMC

92. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi kufikia Machi 2017, **Hospitali ya KCMC** ilihudumia jumla ya wagonjwa 162,078 ikilinganishwa na wagonjwa 223,198 waliohudumiwa mwaka 2015/16. Hospitali kwa kushirikikiana na Taasisi za *Foundation for Cancer Care in Tanzania* (FCCT) na *Tanzania Cancer Care Foundation* (TCCF) ambao ni marafiki wa Shirika la Msamaria Mwema Tanzania imekamilisha **ujenzi wa kituo cha tiba za saratani** awamu ya kwanza kati ya nne. Awamu hiyo ilijumuisha ujenzi wa jengo la kliniki kwa ajili ya wagonjwa wa saratani na jengo la tiba ya dawa (Chemotherapy). Utoaji wa huduma katika kituo hiki umerahisisha upatikanaji wa matibabu ya saratani karibu na wananchi wa mikoa ya Tanga, Manyara, Singida, Arusha, na Kilimanjaro.

93. Mheshimiwa Spika, wagonjwa waliohudumiwa na kituo cha tiba za saratani ni 415, kati yao watu wazima walikuwa ni 367 (wanawake 189 na wanaume 178) na watoto

ni 48. Watu wazima 160 na watoto 19 walikuwa wakiendelea na tiba ya dawa. Aidha Hospitali imekamilisha ujenzi wa Wodi mpya kwa ajili ya wagonjwa walioungua moto na kemikali. Wodi hizo zina uwezo wa kulaza wagonjwa 24 kwa wakati mmoja. Vilevile, **Kitengo cha ICU kwa ajili ya watoto kimefunguliwa tangu Oktoba 2016** ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2017, jumla ya watoto 91 wamepata huduma. Hospitali pia imeanza kutoa **huduma za kusafisha figo tangu Desemba 2016** baada ya kufunga mashine nne za kusafisha figo. Kati ya Januari na Machi 2017, jumla ya wagonjwa 32 wameshapata huduma hii.

Usimamizi wa utoaji wa Huduma za Tiba Nchini

94. Mheshimiwa Spika, Wizara ikiwa na dhamana ya kusimamia utoaji wa huduma za afya nchini imeendelea kutoa miongozo na maelekezo yenye lengo la kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi unazingatiwa. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inaendelea kusisitiza kwa vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya nchini kuweka utaratibu mwepesi kwa wananchi kufikisha malalamiko yao pindi wanapoona kwamba hawakupatiwa huduma za afya kwa kiwango stahiki. Aidha, Wizara imeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko na kero za wananchi juu ya huduma zinazotolewa. Kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017 malalamiko kuhusu utoaji wa huduma kwa vituo binafsi na huduma kwa vituo vya Umma yalipokelewa na kupatiwa ufumbuzi. Vilevile **magari 10 ya wagonjwa** kutoka katika Serikali ya Qatar yalitolewa kwa hospitali mbalimbali nchini ili kuimarisha huduma za rufaa kwa wagonjwa.

95. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara pia imeendelea kuratibu utolewaji wa huduma ya matibabu bure kwa wazee. Katika kutekeleza azma hiyo, Halmashauri ziliendelea kuhimizwa kutenga fedha kwa ajili ya kulipia matibabu ya wazee kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii na kuwanunulia dawa na vifaa tiba.

Huduma za Maabara za Uchunguzi wa Magonjwa

96. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kuboresha huduma za maabara ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2017, jumla ya maabara **66** ambazo zipo katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Vituo vya Afya, zilishiriki kwenye utaratibu wa Shirika la Afya Duniani wa kutoa Ithibati hatua kwa hatua, kwa kutoa nyota za viwango vya ubora wa huduma za maabara. Maabara **33** zilipata kati ya nyota moja **(1)** mpaka Tatu **(3)** za viwango vya ubora. Aidha, Maabara ya Taifa na zile za Kanda sita **(6)** zimepata ithibati ya SADCAS ya kiwango cha kimataifa yaani **ISO 15189:2012**. Maabara hizo ni Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (NHLQATC), Hospitali ya Kanda Bugando (BMC), Hospitali ya Kanda Mbeya (MRH), Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC). Pia, Wizara inaendelea na ujenzi wa maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii katika eneo la Mabibo, Dar es salaam. Mradi huo hadi kukamilika unatarajiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 7,493,193,434.97.00**.

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

97. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala Na. 23 ya Mwaka 2002, kanuni zake na miongozo mbalimbali. Katika kutekeleza majukumu ya Kisheria, Wizara imeandaa na kuchapisha nakala 4,950 za mpango mkakati wa tiba asili na tiba mbadala **2016/17-2021/22**. Vitabu hivyo vitatoa msaada kwa waganga wakuu wa mikoa na Halmashauri kuweza kupanga mipango itakayo husu tiba asili na tiba mbadala katika maeneo yao. Aidha, Wizara inaendelea kuwakumbusha wamiliki wa vyombo vya habari kuzingatia Sheria ya Tiba Asili na Tiba Mbadala Na. 23 ya Mwaka 2002, kanuni zake katika utoaji wa matangazo ya Tiba Asili na Tiba Mbadala. Vilevile, Wizara iliratibu mafunzo kwa waganga 25 wa tiba asili yaliyofanyika mwezi Februari 2017 katika chuo kikuu cha MUHAS na wanachuo 44 katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa.

HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA

98. *Mheshimiwa Spika*, Katika kuhakikisha kuwa huduma za Uuguzi na Ukunga zinaimarika, Wizara imezindua Mpango Mkakati kwa ajili huduma za Uuguzi na Ukunga. Lengo la Mpango huo ni kutoa dira inayolenga katika kuboresha huduma za Uuguzi na Ukunga nchini. Aidha, Wizara imezindua mwongozo wa maabara ya mafunzo ya Uuguzi na Ukunga nchini, mwongozo huo unalenga katika kuboresha mafunzo ya vitendo yatolewayo katika vyuo vya uuguzi na ukunga, ili kuongeza weledi, maarifa, na stadi za kuhudumia wananchi kwa ubora zaidi. Katika kuimarisha umahiri kwa wauguzi na wakunga, Wizara imetayarisha na kuzindua mwongozo wa mafunzo sehemu za kazi kwa ajili ya kuwaongoza wakufunzi wa vitendo katika kusimamia mafunzo yatolewayo kwa wanafunzi sehemu za kazi. Vilevile, **Wizara imeendelea kusisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili ya Uuguzi na Ukunga** kwa kutumia fursa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya usimamizi shirikishi, mikutano ya wauguzi na ile ya wasimamizi wao

UHAKIKI UBORA WA HUDUMA ZA AFYA

Uhakiki na Ukaguzi

99. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/17, Wizara imekamilisha zoezi la kufanya tathmini ya awali ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya ya msingi (Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali) katika Halmashauri zote za mikoa 6 iliyosalia ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Kilimanjaro na Arusha. Vituo vilipewa hadhi ya nyota kulingana na ubora wa huduma zinazotolewa. Jumla ya vituo 1,665 vimefanyiwa tathmini, ambapo kati ya vituo hivyo, 446 (27%) vilipata nyota sifuri, 862 (52%) vilipata nyota moja, 272 (16.3%) vilipata nyota mbili, 63 (4%) vilipata nyota tatu na 2 (0.12%) vilipata nyota nne. Mipango ya Uimarishaji Ubora wa huduma za afya kwa kila Kituo iliandaliwa na utekelezaji unaendelea kwa kushirikiana na Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri. Aidha, katika utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango ya uboreshaji wa huduma za afya, Wizara ilitoa kiasi cha **3,040,000,000** katika

mikoa 4 ambapo jumla ya vituo 304 (Dodoma 118, Kigoma 135, Singida 32 na Tanga 19) vilivyokuwa na nyota sifuri vilipatiwa Shilingi **10,000,000** kwa kila Kituo.

100. Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya tathmini ya marudio kwa vituo 52 katika mkoa wa Shinyanga. Ukilinganisha matokeo ya awali na matokeo ya tathmini ya marudio, vituo vimeonyesha mabadiliko makubwa katika utekelezaji wa mipango ya uboreshaji wa huduma ambapo kati ya vituo 40 vilivyokuwa na nyota sifuri, ni vituo 3 tu (7.5%) ndivyo vimebaki katika hadhi ya nyota sifuri.

Aidha, Wizara imefanya usimamizi shirikishi kwenye eneo la Kukinga na Kudhibiti Maambukizi (infectious, prevention and control) katika vituo vya kutolea huduma vya mikoa 22 (**Kiambatanisho Na. 4**) ya Tanzania bara. Vilevile, Jitihada za Kukinga na Kudhibiti Maambukizi zimeimarishwa katika utoaji huduma za dharura na Maafa ili kuzuia kuenea kwa maambukizi wakati wa utoaji wa huduma hizo.

Dharura na Maafa

101. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara imetekeleza mikakati ya kujenga utayari wa kisékta wa kukabiliana na dharura kwa kuwapatia mafunzo ya kukabiliana na dharura na maafa timu za dharura katika mikoa 23 ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Lindi, Mtwara, Mbeya, Iringa, Rukwa, Tabora, Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Geita, Simiyu Shinyanga na Katavi ambapo jumla ya watoa huduma 120 walipata mafunzo hayo. Aidha, Wizara imeandaa na kuchapisha miongozo ya kutoa huduma za dharura pamoja na kufanya tathmini ya viashiria vya dharura "*Vulnerability Risk Assessment and Mapping*" kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu nchini ili kusaidia kuimarisha mikakati ya kukabiliana na ugonjwa huo.

102. Mheshimiwa Spika, Aidha, Wizara imeanza maandalizi ya kuanzisha huduma za dharura katika barabara kuu kutoka Dar es Salaam hadi mpaka wa Tanzania na

Malawi, kwa kupitia mradi wa *South Africa Trade and Transport Facilitation* (SATT). Awamu ya kwanza ya mradi huo utanzia Dar Es Salaam hadi mpakani mwa Morogoro na Iringa katika eneo la Ruaha Mbuyuni. Aidha, Wizara inashirikiana na wadau wa usalama barabarani kutekeleza mikakati ya kupunguza ajali za barabarani kwa kupitia Mradi wa "*Bloomberg Initiative for Road Safety* (2015-2019)". Katika Mradi huo, Wizara inaratibu Wadau wa Usalama Barabarani, kuhamasisha uboreshaji wa sheria, utoaji wa taarifa za kuhamasisha masuala ya usalama barabarani na mafunzo ya kujenga uwezo kwa wanasheria na waandishi wa habari.

103. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeshiriki katika kukabiliana na dharura mbalimbali pamoja na kuratibu ushiriki wa wadau katika kukabiliana na dharura. Kwa kupitia kituo cha uratibu wa Operesheni za Dharura na Maafa, Wizara imeratibu utoaji wa huduma za afya katika dharura ikiwemo matukio ya tetemeko la ardhi mkoani Kagera, mlipuko wa magonjwa ya kipindupindu na sumu kuvu. Shughuli hizo zimefanyika kwa njia ya kutuma wataalamu, kupeleka dawa, vifaa na vifaa tiba na kuratibu mikutano ya wadau mbalimbali katika ngazi ya Taifa na Mkoa.

URATIBU, UFUATILIAJI NA UGHARAMIAJI HUDUMA ZA AFYA

Tathmini, Ufuatiliaji na Usimamizi wa huduma za Afya

104. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi na uwajibikaji katika kutekeleza vipaumbele vya Sekta ya Afya, Wizara imeendelea kufanya tathmini shirikishi kwa kutumia nyenzo ya kijamii (Community Score Card) ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa lengo la kuboresha kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Tathmini hiyo imefanyika katika ngazi ya jamii inayohudumiwa na vituo vya afya 227 vya umma katika Halmashauri 14 (Mkoa wa Pwani halmashauri 8 na Kilimanjaro halmashauri 6). Matokeo ya tathmini hizo yametumika kuandaa mipango kabambe ya Halmashauri ya uboreshaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma.

105. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika mipango na utawala bora katika sekta ya afya, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imefanya usimamizi shirikishi katika mikoa yote na kubaini uwepo wa Bodi za Usimamizi wa Huduma za Afya za Halmashauri katika Halmashauri 45 za mikoa ya Singida, Dodoma, Mbeya, Songwe, Tanga na Tabora ambazo hazifanyi kazi vizuri. Katika kuhakikisha Bodi hizo zinatekeleza majukumu yake ipasavyo, Wizara kupitia zoezi la usimamizi shirikishi ilitoa mafunzo elekezi, miongozo ya namna bora ya kutatua changamoto za usimamizi wa shughuli za afya za Halmashauri.

106. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kuboresha upatikanaji wa takwimu za afya kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Uboreshaji huo unatokana na kuimarishwa kwa mfumo wa kielektroniki wa kutoa taarifa za vituo vya afya nchini yaani “Health Facility Registry” na uboreshaji wa mtandao wa kutoa taarifa za afya kupitia anuani ya hmisportal.moh.go.tz

107. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuimarisha mfumo wake wa Takwimu za kila siku katika kila kituo kinachotoa huduma za Afya unaoitwa “Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA) na pia kusimamia mfumo wake wa kielektroniki unaoitwa “District Health Information System (DHIS2)”. Mfumo huu umezisaidia Halmashauri, Mikoa pamoja na ngazi ya Taifa katika kuchambua na kutumia taarifa hizo katika kuandaa mipango ya utoaji wa huduma za afya. Aidha, Wizara imeingiza Mafunzo ya MTUHA kwenye mitaala ya kufundishia katika Vyuo ya Mafunzo ya Afya Nchini.

TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

108. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuelekeza matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa taasisi zilizo chini yake ili kuondoa matumizi ya karatasi na kuimarisha taarifa za wagonjwa na mtoa huduma. Kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Wizara imekamilisha kufunga mfumo wa

kielektroniki wa hospitali (paperless) ikiwa ni pamoja na kusimamia mapato katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Hospitali za Mkoa za Singida na Tabora, usimikaji unaendelea katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya Kanda ya Rufaa ya Mbeya, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Mirembe na Hospitali ya Kibong'oto.

109. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikia na OR-TAMISEMI na wadau mbalimbali imetengeneza Mpango Mkakati wa uwekezaji katika mifumo ya TEHAMA (Investment Recommendation Plan), mpango huu umewezesha Serikali na Wadau kubaini maeneo ya uwekezaji. Pamoja na kuharakisha uunganishaji wa mifumo katika sekta ya Afya.

110. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mkakati wa TEHAMA katika Sekta ya Afya (ehealth Strategy 2013-2018). Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Wizara imefanya tathmini ya mifumo ya kielektroniki iliyofungwa kwenye hospitali zote za rufaa katika ngazi ya Mkoa na hospitali za Wilaya ili kujua kama inakidhi miongozo na viwango vilivyotolewa na Wizara pamoja na Wakala ya Serikali Mtandao. Tathmini ilionyesha kuwa mifumo iliyopo inakidhi vigezo kwa kati ya asilimia 18 hadi 92. Kufuatia matokeo ya tathimini hiyo, Wizara ilielekeza kuwa, Mifumo ambayo haikufikia vigezo kwa asilimia 60 isitumike na ile iliyofikia zaidi ya asilimia 60 iboreshwe kufikia asilimia 100. Aidha, Wizara inakamilisha mfumo wa kupokea maoni ya wananchi juu ya ubora wa huduma zinazotolewa katika vituo vya Afya nchini, ambapo mgonjwa ataweza kutoa taarifa kupitia code namba *152*05#.

RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

111. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu uzalishaji wa wataalamu kutoka vyuoni ambao wameendelea kuwa nguzo muhimu ya utoaji huduma za afya nchini. Uzalishaji huu umeendelea kuimarika kutokana na ongezeko la wanafunzi watarajali wanaodahiliwa katika vyuo vya afya kutoka wanafunzi **13,002** mwaka 2015/16 hadi

wanafunzi 13,632 mwaka 2016/17. **Serikali imevuka lengo la Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) la kudahili wanafunzi 10,000 waliotarajiwa kudahiliwa ifikapo mwaka 2017.** Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Wizara inasimamia utoaji wa **mafunzo kwa vitendo (internship) kwa wahitimu 1,798** wa vyuo vikuu katika fani mbalimbali za afya ikiwemo madaktari (1,072), wafamasia (186), wauguzi (265), maafisa mazingira (46), Radiologia na Radiografia (9), na maabara (220). Wanafunzi hao wanatarajia kukamilisha mafunzo hayo mwezi Oktoba, 2017.

112. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na jitihada za kupunguza uhaba wa wataalam wanaotoa huduma za kibingwa nchini kwa kutekeleza mpango wake wa **kugharamia masomo ya uzamili** kwa wataalamu 404 wa afya katika nyanja mbalimbali. Hadi Machi 2017, wanafunzi 387 walikuwa wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali ndani ya nchi na wanafunzi 17 katika vyuo vya nje ya nchi.

113. Mheshimiwa Spika, Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha vyuo vyake vya Mafunzo kwa kuvifanyia ukarabati mkubwa pamoja na ujenzi wa majengo mapya. Katika mwaka 2016/17, vyuo **14** vimeboreshewa miundombinu yake kupitia ufadhili wa Mfuko wa Dunia (Global Fund) na kati ya hivyo vyuo 12 vimekamiliika na kukabidhiwa kwa watumiaji. Vyuo hivyo ni Lindi CATC, Songea CATC, Njombe NTC, PHI Iringa, Rukwa CATC, Mpanda CATC, Kigoma CATC, Musoma NTC, Nzega NTC, PHN Morogoro, Tanga NTC na Mtwara COTC. Vyuo viwili ambavyo havijakamilika ni Mirembe NTC na Mvumi TI ambavyo vinategemea kukamilika mwaka wa fedha 2017/18. Wizara pia imenunua vifaa vya Maabara za vitendo kwa ajili ya kufundishia kwa vyuo 10 vya utabibu, uuguzi na ukunga.

114. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na kituo cha kudhibiti magonjwa cha Marekani "Centre for Disease Control (CDC)" inatekeleza mpango wa uimarishaji mifumo ya huduma za Afya. Katika mwaka 2016/17, Wizara imejenga Kituo kipya cha Elimu kwa njia ya Masafa eneo la Mkundi

Manispaa ya Morogoro kitakachoweza kutoa elimu kwa Kada za Afya. Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi hadi 300 kwa wakati mmoja. Vilevile, Mpango huo wa uimarishaji mifumo ya huduma za Afya umewezesha kutoa ajira za mkataba kwa wauguzi (97) na Tabibu wasaidizi (95) ambao wamesambazwa kwenda kutoa huduma kwenye vituo vya Afya na Zahanati katika Halmashauri 40 hapa nchini. **(Kiambatisho Na 5)**

115. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jitihada za kuajiri watumishi wa afya ambapo katika mwaka 2016/17, **kibali cha kuajiri madaktari 258 kimepatikana. Hatua hii itasaidia kupunguza pengo la watumishi hasa katika ngazi ya vituo, Hospitali za wilaya na mikoa.** Hata hivyo, Sekta ya afya bado inakabiliwa na upungufu wa watumishi wa afya, kwa takribani asilimia 49. Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha upungufu huu unaisha ili kuhakikisha huduma bora za afya kwa wananchi wote zinapatikana hasa kwenye zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Wilaya na Hospitali za Rufaa za Mikoa.

116. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau wakiwemo Taasisi ya Benjamini Mka pa imeendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba **200** za watumishi katika Mikoa 9 ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Tanga, Manyara, Pwani na Simiyu. Chini ya udhamini wa Mfuko wa Dunia (Global Fund), Ujenzi wa nyumba **132** umekamilika na nyumba **68** ujenzi unaendelea. Kukamilika kwa nyumba hizo kutaongeza idadi ya nyumba za watumishi zilizojengwa kupitia mradi huu na kufika nyumba **480** katika maeneo yenye mazingira magumu.

UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO YA AFYA YA MSINGI

117. Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha utekelezaji wa Mpango wa miaka kumi wa Maendeleo wa Afya ya Msingi unaokamilika mwaka 2017. Katika utekelezaji wa mpango huo, Vituo vya kutolea huduma vimeendelea kuongezeka kutoka jumla ya **vituo 5,172** mwaka 2005 na kufikia jumla ya

vituo 7,232 mwaka 2016. Hii ni ongezeko la **vituo 2,060** sawa na asilimia 40. Kati ya vituo vyote vilivyopo nchini, **vituo 5,414** sawa na asilimia 75 ni vya Serikali na 1,818 ni vya taasisi binafsi. Aidha kupitia MMAM, Serikali iliingia Mkataba na watoa huduma binafsi (Service Level Agreement) ili kupunguza ulazima wa Halmashauri kujenga vituo vipya vya huduma za afya sehemu ambazo kuna vituo binafsi. Katika makubaliano hayo jumla ya Halmashauri 39 zinatumiya hospitali teule.

118. Mheshimiwa Spika, kutokana na kipindi cha utekelezaji wa MMAM kufikia ukingoni, Wizara imeanza maandalizi ya kufanya tathimini ya utekelezaji wa mpango huo ili kupima mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake na kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuandaa na kutekeleza mpango mwingine.

UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA NCHINI

119. Mheshimiwa Spika, Utoaji wa huduma za afya nchini unasimamiwa na Sera ya Afya ya mwaka 2007. Sera hii ni ya muda mrefu hivyo katika mwaka 2016/17 Wizara ilifanya mapitio ya Sera na kubaini kuwa kuna maeneo mengi ya Sera ambayo yametokeleza kwa ufanisi mkubwa na maeneo machache ambayo hayakutekeleza kikamilifu. Kufuatia matokeo haya, Wizara imeanza maandalizi ya kutunga Sera mpya ya Afya itakayokidhi mabadiliko katika Sekta ya Afya. Maandalizi ya Sera hiyo yanatarajiwa kukamilika katika mwaka 2017/18. Maandalizi ya Sera hii yamekuwa shirikishi na nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa Wizara kwa kutoa maoni na ushauri katika ukamilishwaji wa Sera hiyo.

120. Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilikamilisha maandalizi ya Mkakati wa Ugharamiaji huduma za afya nchini. Lengo kuu la Mkakati huu ni kutafuta vyanzo mbalimbali vya uhakika vya kuongeza rasilimali fedha katika Sekta ya afya. Mkakati huo una maeneo mengi ya Kiseru ambayo bado yanafanyiwa kazi na wadau kabla ya kuanza kutekelezwa. Utekelezaji wa

mkakati huu utasaidia kuimarisha upatikanaji wa Rasilimali Fedha katika Sekta ya Afya na kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa huduma bora za Afya pindi wanapozihitaji hasa wananchi wasio na uwezo na wenye mahitaji maalum.

121. Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Bima ya Taifa ya Afya na kwa kushirikiana na Benki ya Ujerumani (KfW) inatekeleza Mpango wa NHIF/CHF kwa Wanawake Wajawazito na Watoto ujulikanao kama **Tumaini la Mama**. Mpango huo wenye lengo la kupunguza vifo vya akinamama na watoto ulianza kutekelezwa mwaka 2012 ambapo akina mama wajawazito hulipiwa kadi za NHIF/CHF ili kuwa na uhakika wa matibabu katika kipindi chote cha ujauzito na miezi sita baada ya kujifungua kwa mama na mtoto. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi kufikia mwezi Machi 2017, wanawake **wajawazito 147,615 walijisajiliwa na** hivyo kufanya jumla ya wanufaika kufikia wanawake **572,576** katika mikoa ya **Mbeya, Tanga, Lindi, Mtwara na Songwe**.

122. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya imepanga kutekeleza mpango wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa ili kuhakikisha watanzania wanapata huduma bora na kwa urahisi kwa kuzingatia uwezo wa kifedha wa mwanachama. Kupitia mpango huo, mwanachama ataweza kupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya mkoa bila kujali Kituo/Halmashauri alipojisajili tofauti na ilivyo sasa ambapo mwanachama wa CHF hupata huduma kutoka ngazi ya zahanati hadi ngazi ya Halmashauri aliyojisajili tu.

123. Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi, kupitia Mpango huu wa CHF iliyoboreshwa, Halmashauri zitabaki na jukumu la kutoa huduma (**service provider**) na Mfuko/NHIF utakuwa na jukumu la kuandikisha wanufaika, kukusanya fedha za wanachama na kulipa watoa huduma (**purchaser**). Aidha, katika kuimarisha ushirikishwaji wa wananchi, vikao vya kijiji vitapewa fursa ya kuteua maafisa watakaokuwa na jukumu la kusajili wananchama na kuwahamasisha pamoja na kukusanya michango. Mpango

huo utatekelezwa kwa kuanzia katika **halmashauri 50** za mikoa ya **Kagera, Mwanza, Singida, Mara, Tabora, Pwani, Ruvuma** na baadae utasambazwa katika mikoa yote nchini. Uzinduzi rasmi wa mpango huu unatarajiwa kufanyika katika mkoa wa Singida kabla ya mwisho wa fedha 2016/17. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa nafasi zao na ushawishi mkubwa walionao katika jamii tunayoishi, kuendelea kuwaelimisha wananchi wote umuhimu wa kujunga na bima ya afya ili waweze kupata huduma za tiba bila kikwazo cha fedha.

Uratibu wa Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund)

124. Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa na jukumu la kuratibu **Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund)** ulioanzishwa mwaka 1996. Kupitia Sekretarieti ya Uratibu wa Mfuko, Vikao mbalimbali vya majadiliano kati ya Serikali na Wadau vimekuwa vikifanywa ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya Serikali jinsi inavyotekeleza kazi zinazogharamiwa na fedha za Wadau. Kwa hivi sasa Mfuko huo unachangiwa na Wadau (8) ambao ni Denmark, Uswisi (SDC), Ireland, Canada, Benki ya Dunia, UNICEF, UNFPA na Korea Kusini. Wizara inaendelea na juhudi za kuwaleta pamoja wadau wengine zaidi ili wachangie katika Mfuko huo ili kuleta ufanisi na matokea makubwa katika utekelezaji wa miradi ya afya nchini.

125. Mheshimiwa Spika, wanufaika wa Mfuko huu ni OR - TAMISEMI, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto (Idara kuu ya Afya), Mikoa na Halmashauri zote nchini. Fedha hizo hugawiwa kwa fomula kwa kuzingatia makubaliano kati ya Serikali na Wadau wanaochangia Mfuko. Asilimia 90 ya fedha zote hupelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, asilimia 6 ya fedha hizo hutumika katika Wizara ya Afya kwa ajili ya masuala ya uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Kiseru katika Sekta ya Afya. Aidha, asilimia 3 ya fedha hizo hupelekekwa katika Mikoa kwa ajili ya kugharamia ufuatiliaji katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa na asilimia 1 ya

fedha zote hupelekwa Makao Makuu ya OR- TAMISEMI kwa ajili ya kugharamia ufuatiliaji katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

126. Mheshimiwa Spika, Hadi robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2016/17, kiasi cha **shilingi bilioni 88.8 kimepokelewa** kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 5.6 zilipokelewa na Wizara ya Afya (Fungu 52), shilingi milioni 865.05 zilipokelewa na OR-TAMISEMI, shilingi bilioni 2.6 zilipokelewa na Mikoa na kiasi cha shilingi bilioni 79.7 zilipokelewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Fedha hizi hutumika kadiri ya Mkataba wa Makubaliano kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo, ambapo asilimia 33 ya fedha zinazopelekwa katika Halmashauri zinatakiwa kutumika kama nyongeza ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na asilimia 67 ni kwa ajili ya utekelezaji wa afua mbalimbali ambazo zinalenga kuboresha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kugharamia usambazaji na ufuatiliaji wa chanjo kwa kuimarisha mnyororo baridi (cold chain), uimarishaji wa huduma za dharura za mama na mtoto (CEmOC), udhibiti wa magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza pamoja na yale yasiyopewa kipaumbele na kuwajengea uwezo watoa huduma za afya.

127. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzingatia vigezo vya usawa katika kugawanya fedha za Mfuko, muelekeo wa Wadau kwa sasa ni kutoa umuhimu kwa ufanisi katika utekelezaji wa kazi zilizokubaliwa ili kuongeza ufanisi katika kazi zinazokubaliwa. Na ili kuviwezesha vituo vya kutolea huduma za afya kupata fedha kwa wakati na kuweza kufanya maamuzi ya haraka ya kutumia fedha hizo kulingana na mahitaji ya kituo husika, Wizara imeandaa utaratibu wa kuwezesha fedha za Mfuko kutumwa moja kwa moja kwa vituo vya kutolea huduma za afya ili kuviwezesha vituo kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji yao kwa haraka. Halmashauri zitabaki na jukumu la kusimamia na kufuatilia matumizi ya fedha hizo. Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia fursa hii kuwaomba waheshimiwa wabunge pia kufuatilia matumizi ya fedha hizi.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (FUNGU 53)

MAENDELEO YA JAMII

128. Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo ya Jamii ya 1996 inasisitiza ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka kuleta mabadiliko chanya katika jamii. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara katika kipindi cha 2016/17 iliendelea kuwezesha na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Maendeleo ya Jamii hususan katika kutoa hamasa kwa jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo kupitia miongozo mbalimbali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuandaa Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa shughuli za Maendeleo na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuhakikisha shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii zinatekelezwa kwa ufanisi na kuwanufaisha wananchi ipasavyo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na hivyo kuharakisha kufikiwa kwa malengo mbalimbali ya maendeleo. Kazi hii ilifanyika kwa kushirikiana na OR- TAMISEMI.

129. Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ni muhimu wakatamika ipasavyo katika kufanikisha Malengo ya Sera mbalimbali za Maendeleo ya nchi yetu. Wataalamu hawa ni muhimu katika kuandaa wananchi kushiriki katika kupanga na kutekeleza programu za Kilimo, Elimu, Maji, Barabara, Afya, Mifugo na Hifadhi ya Mazingira. Wizara ina jukumu la kuandaa wataalam wa kada ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali za elimu kupitia Vyuo 8 vya Mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii na taasisi moja ambayo ni Taasisi ya Maendeleo Tengeru. Katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Vyuo hivi imeendelea kuzalisha wataalamu hao ambapo jumla ya wataalam 1,685 walihitimu na wanachuo 2,216 walidahiliwa katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, katika kuboresha utoaji wa mafunzo katika chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba, Wizara imewezesha kukirejeshea chuo eneo lenye ukubwa wa hekari

175 lililokuwa na mgogoro na wanakijiji wa Rungemba, ambapo jumla ya Shilingi milioni 193,384,000.00 zimelipwa kwa wananchi 39. Hatua hii inatoa fursa ya kuhifadhi eneo la chuo kwa ajili ya upanuzi.

MAENDELEO YA JINSIA

130. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali kwa lengo la kufikia usawa wa jinsia na kuwawezesha wanawake nchini. Utekelezaji huo ulizingatia maeneo manne ya kipaumbele ambayo ni Uwezeshaji wanawake kiuchumi; Kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia ikiwemo Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto; Kuwawezesha wanawake kushiriki katika uongozi na ngazi za maamuzi; na uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, mikakati na mipango ya kisekta na kitaifa.

Uwezeshaji Wanawake kiuchumi

131. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea na jitihada za kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwapatia mikopo kupitia **Benki ya Wanawake Tanzania** na **Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake** ili waweze kushiriki na kunufaika na ukuaji wa pato la kaya na taifa sawa na wanaume.

132. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Wizara imeendelea kuratibu Mfuko huu kwa lengo la kuwawezesha wanawake wajasiriamali wadogo. Katika mwaka 2016/17, jumla ya **shilingi milioni 156** zilikopeshwa kwa Halmashauri tano za Kisarawe, Busokelo, Gairo, Iringa Manispaa, Masasi na Mtwara vijijini kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi 61 vyenye wanawake wajasiriamali 658.

133. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake unawafikia wanawake wengi, Wizara kwa kushirikiana na OR TAMISEMI imeendelea kuzihamasisha Halmashauri kuchangia asilimia tano (5%) ya

mapato yao ya ndani katika Mfuko huo. Katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2016, jumla ya Halmashauri 147 zilichangia jumla ya **Shilingi 7,826,722,946**. Pamoja na kuongezeka kwa mwamko wa Halmashauri kuchangia katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, Halmashauri 39 hazikuchangia. **Kiambatisho Na. 6**_Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza Halmashauri zote ambazo zimechangia katika Mfuko huu. Aidha, natoa wito kwa Halmashauri ambazo hazijachangia zichangie Mfuko huu ili kuharakisha kufikiwa kwa malengo ya maendeleo jumuishi ambayo nchi imejiwekea. Vilevile, natoa rai kwenu wabunge wenzangu kuhakikisha Halmashauri zetu zinachangia ipasavyo Mfuko huu.

134. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Benki ya Wanawake Tanzania**, mikopo kwa wajasiriamali 6,956 yenye thamani ya shilingi bilioni 10,469,282,000 (wanawake 4,596 na wanaume 2,360) imetolewa. Hivyo, mikopo iliyotolewa na Benki imeongezeka kutoka shilingi 112,473,600,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia shilingi 121,796,840,000 mwaka 2016/17. Aidha, idadi ya wajasiriamali walionufaika na mikopo inayotolewa na benki imeongezeka kutoka wajasiriamali 79,983 mwaka 2015/16 hadi kufikia wajasiriamali 86,939 mwaka 2016/17 ambapo asilimia 75 ya wanufaika ni wanawake.

135. Mheshimiwa Spika, Aidha, Benki imeongeza vituo vya kutolea mikopo na mafunzo kutoka vituo 184 mwaka 2015/16 hadi kufikia vituo 252 mwaka 2016/17. Aidha, Benki iliwezesha jumla ya wanawake 223 kati ya wanufaika 560 kumiliki ardhi katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Benki pia katika kumwezesha mwanamke wa kipato cha chini kupata huduma za mikopo yenye riba nafuu, Benki imeanzisha Akaunti ya Malaika ambayo ilizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan. Lengo la akaunti hiyo ni kutoa mikopo yenye riba nafuu isiyozidi asilimia 10.

136. Mheshimiwa Spika, vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI iliratibu uanzishwaji na uzinduzi wa

majukwaa ya uwezesaji wanawake kiuchumi katika mikoa ya Kigoma, Singida na Dar es Salaam. Uanzishwaji wa majukwaa haya unalenga kuendeleza jitahada za **Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan** ambaye alizindua Jukwaa la Uwezesaji Wanawake Kiuchumi Tanzania kwa ngazi ya taifa.

137. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika mwezi Machi, 2017 ambapo hapa nchini yalifanyika katika ngazi ya mkoa kwa mikoa yote. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa '**Tanzania ya Viwanda: Wanawake ni Msingi wa Mabadiliko ya Kiuchumi**'. Maadhimisho hayo yametoa fursa kwa wadau kutafakari, kubadilishana uzoefu kuhusu mafanikio yaliyofikiwa na kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake katika kufikia ukombozi wa kiuchumi.

Jitihada za Kuzuia na Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia

138. Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na watoto, Wizara kwa kushirikiana na wadau imendaa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22) ambao uliozinduliwa mwezi Disemba, 2016. Uzinduzi huo ulishirikisha Mawaziri 10 kutoka katika wizara mbalimbali ambao waliahidi kuutekeleza Mpango huo kwa manufaa ya wanawake na Watoto wa Tanzania. Katika Aidha, yamefanyika maandalizi ya awali ya utekelezaji wa mpango huu ambayo yalikusisha: kutoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa mikoa 25, Maafisa wa Madawati ya Jinsia 25 kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali. Aidha, mwongozo wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto katika ngazi mbalimbali umeandaliwa.

Ushiriki wa Wanawake katika Ngazi za Uongozi na Maamuzi

139. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha wanawake kushiriki katika ngazi mbalimbali za uongozi na

maamuzi. Katika kutekeleza hilo, wizara kwa kushirikana na shirika la TGNP imeandaa Kanzidata inayoonesha wasifu wa wanawake kwa ajili ya kuwawezesha kushiriki katika fursa za uongozi, ngazi za maamuzi na ajira. Kanzidata hii pia itasaidia kuwatambua wanawake wajasiriamali. Katika kanzidata hii tumebainisha uwepo wa wanawake wasomi, wataalam wenye uwezo katika fani mbalimbali ikiwemo engineers, wahasibu, Madaktari, Wachumi na Wataalam wa Maendeleo wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii. Wizara itaendelea kuhimiza waajiri na mamlaka za uteuzi kutumia kanzidata hii.

Kuimarisha haki ya Mwanamke Kunyonyesha Wakati ya Kazi

140. Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja kati ya nchi zilizoridhia matamko na mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu haki ya unyonyeshaji wa Watoto. Miongoni mwa mikataba na matamko ya kimataifa ambayo imeridhiwa na Tanzania ni pamoja na '*Innocent Declaration on the Protection, Promotion and Support of Breastfeeding na Maternity Protection Convention, 2000 (No. 183)*'. Katika mwaka 2016/17, Serikali imefanya mapitio ya Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini hususan kifungu cha 33(10) na kuifanyia marekebisho kupitia Kanuni zake mpya zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali la Na. 47 la tarehe 24/2/2017 ambapo kwa sasa imewekwa wazi haki ya mama kunyonyesha muda wa masaa mawili katika muda wa kazi kwa kipindi cha miezi 6 baada likizo ya uzazi. Kabla ya marekebisho haya, haki ya mama kunyonyesha baada ya likizo ya uzazi haikuwa imefafanuliwa ni kwa kipindi cha muda gani. Kifungu hiki sasa kinasomeka '***Where an employee is breast-feeding a child, the employer shall allow the employee to feed the child during working hours up to a maximum of two hours per day, for a period of 6 months after maternity leave***', badala ya kusomeka '***Where an employee is breast-feeding a child, the employer shall allow the employee to feed the child during working hours up to a maximum of two hours per day.***' Marekebisho hayo yatasaidia kuimarisha upatikanaji wa haki za wanawake katika uzazi na kuhakikisha haki na

maendeleo ya mtoto mchanga. Nitumie fursa hii kuwataka waajiri wa sekta binafsi na wa umma kuzingatia matakwa haya ya kisheria. Aidha, pia ninapenda kuwahamasisha wanawake kuitumia fursa hii kwa ajili ya kuweka msingi imara wa maendeleo ya awali ya watoto wao.

Uingizaji wa Masuala ya Jinsia Katika Sera Sheria na Mipango ya Kisekta na Taifa

141. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sera na Mipango, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Taarifa ya Hali ya Jinsia Nchini ya mwaka 2016. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la UN-Women imeandaa viashiria vya jinsia katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu hapa nchini. Uwepo wa viashiria hivi utasaidia kuhakikisha upangaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa malengo hayo unazingatia masuala ya jinsia na uwezeshaji wanawake.

MAENDELEO YA MTOTO

142. *Mheshimiwa Spika*, Maendeleo endelevu ya Taifa lolote, yanategemea uwekezaji katika makuzi, malezi, na maendeleo ya mtoto. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, **idadi ya watoto ni asilimia 51.6 ya watanzania wote**. Hali hii inaonesha umuhimu wa kulinda na kusimamia utekelezaji wa haki za msingi za mtoto ambazo ni; kuishi, kuendelezwa, kulindwa, kushiriki na kutobaguliwa.

Ukatili dhidi ya watoto

143. *Mheshimiwa Spika*, kumekuwa na ongezeko la taarifa za vitendo vya ukatili vinavyofanywa dhidi ya watoto. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, vitendo vya ukatili dhidi ya Watoto kwa mwaka 2016 vilivyoripotiwa ni 10,551 ikilinganisha na vitendo 9,541 mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 9.6%. Vitendo hivyo vinasababishwa kwa kiasi kikubwa na hali ya umaskini na uwepo wa mila na desturi zenye madhara. Utolewaji wa

taarifa za vitendo vya ukatili ni mojawapo ya mikakati ya Kupunguza vitendo hivyo katika jamii. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kupokea taarifa juu ya vitendo husika na kuchukua hatua. Taarifa kupitia mtandao wa huduma ya simu ya kusaidia kuripoti taarifa za ukatili dhidi ya watoto kupitia namba ya simu 116 (Child Helpline) zimeongezeka kutoka 33,675 mwaka 2015/16 hadi kufikia simu 37,888 mwaka 2016/17, ongezeko hili sawa na asilimia 12.5 ya simu zilizopokelewa. Kuongezeka kwa idadi hii ya simu ni matokeo ya mwamko wa jamii katika kutoa taarifa za masuala ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ikiwemo ulawiti na ubakaji. Nitumie fursa hii kutoa rai kwa jamii, wazazi, walezi na watoto kutosita kutoa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili katika maeneo yao.

144. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imetoa mafunzo juu ya mbinu za kushirikisha wazazi na walezi kubadili mitazamo kuhusu mila na desturi zenye madhara kwa watoto na umuhimu wa kuwekeza katika malezi yenye mwelekeo wa kumlinda na kumwendeleza mtoto hasa mtoto wa kike. Mafunzo hayo yalitolewa wa kipindi cha Julai 2016 mpaka Machi 2017 kwa maafisa maendeleo ya jamii 505, walimu 40 na maafisa ustawi wa jamii 39 katika Halmashauri 72 nchini.

Mimba na ndoa za utotoni

145. Mheshimiwa Spika, mimba na ndoa za utotoni bado ni kikwazo katika kufikia maendeleo endelevu ya nchi yetu. Kwa mujibu wa Utafiti wa Taasisi ya Takwimu ya Taifa kiwango cha **ndoa za utotoni nchini ni asilimia 37**. Mikoa inayoongoza kwa ndoa za utotoni ni Shinyanga (59%) Tabora (58%), Mara (34%), Dodoma (51%) na Lindi (48%). Aidha Takwimu hizo pia zinaonesha kuwa **asilimia 27 ya watoto wanaathirika na mimba za utotoni** nchini, mikoa inayoongoza ni Katavi (36.8%), Tabora (36.5%), Simiyu (32.1%), Geita (31.6%) na Shinyanga (31.2%). Katika kukabiliana na ndoa na mimba za utotoni, Wizara kwa mwaka 2016/17 ilishirikiana na wadau kufanya utafiti katika mikoa 10 na halmashauri 20 na kubaini kuwa **vyanzo vikubwa vya ndoa na mimba za utotoni ni umaskini na mila potofu**. Utafiti huu umesaidia Serikali na wadau

wengine kuendesha kampeni na programu za kupinga ndoa za utotoni ili kupunguza tatizo hili. Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendesha Kampeni maalum ya kupinga ndoa za utotoni mkoani Shinyanga ambayo iliwafikia wananchi zaidi ya 800 na kuokoa Watoto wa kike 102 waliokuwa katika hatua za kuoreshwa.

Maendeleo ya Mtoto wa Kike

146. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha kuwa mtoto wa kike anapata fursa ya kujiendeleza, Wizara imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa klabu za wasichana shuleni ambazo zinawapa fursa ya kujitambua, kujua haki zao na kutoa taarifa ya ukiukwaji wa haki zao. Vilevile, klabu hizi ni sehemu ambayo watoto wanakutana na kubadilishana mawazo kuhusu maendeleo yao kielimu. Katika Mwaka 2016/17, Wizara imehamasisha na kuwezesha **kuanzishwa kwa klabu 105 za watoto wa kike na kiume shuleni** katika wilaya ya Tarime, Shinyanga vijini na Kahama.

Ushiriki wa Mtoto katika Maendeleo

147. Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kusimamia upatikanaji wa haki ya ushiriki wa mtoto kupitia mabaraza ya watoto. Katika mwaka 2016/17, Wizara iliwawezesha viongozi wa Kamati Kuu ya Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya ziara ya mafunzo kwenye mabaraza yanayotekeleza majukumu yake vizuri. Mikoa iliyotembelewa ni pamoja na Mwanza, Lindi, Iringa, Mjini Magharibi, Mkoa wa kusini na Mkoa wa Kaskazini. Lengo la ziara hii ni kupata ujuzi, kuboresha mabaraza na ushiriki wa Watoto katika shughuli za maendeleo. Hadi sasa, jumla za Halmashauri zilizoanzisha Mabaraza ya Watoto ni 108 na Mikoa yenye Mabaraza za Watoto ni 21 **Kiambatisho Na. 7**

HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

148. Mheshimiwa Spika, huduma za ustawi wa jamii zinalenga kuyawezesha makundi maalum kupata huduma za msingi na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo.

Makundi haya ni pamoja na watoto walio katika mazingira hatarishi, watoto walio katika mkinzano na sheria, watu wenye ulemavu na wazee. Makundi mengine ni yale ambayo yanakosa au yapo katika hatari ya kukosa fursa ya kushiriki kikamilfu katika shughuli za maendeleo mfano familia zenye migogoro, wakimbizi, waathirika wa matumizi mabaya ya pombe na madawa ya kulevya.

Huduma za Ustawi kwa Watoto, Watoto Walio katika mazingira Hatarishi na Walio katika Mkinzano wa Sheria

149. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuweka mifumo ya matunzo, malezi na ulinzi wa watoto yenye misingi ya kijamii. Mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau imehamasisha na kuzijengea uwezo Halmashauri 18 kuanzisha timu za ulinzi na usalama wa mtoto ambapo idadi ya Halmashauri zenye timu za ulinzi na usalama imeongezeka kutoka 33 mwaka 2015/16 hadi kufikia Halmashauri 51 mwaka 2016/17. Vilevile, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi 2017 Wizara imeendelea na zoezi la kuziwezesha Halmashauri kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi ili kuwa na takwimu sahihi zitakazotumiwa na wadau kutoa huduma. Jumla ya watoto 131,304 (wavulana 66,965 na wasichana 64,339) walitambuliwa na kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo chakula, mavazi, mahitaji ya shule na msaada wa kisaikolojia.

150. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeandaa mwongozo wa mfumo wa kushughulikia masuala ya watoto walio katika mazingira hatarishi. Mfumo huu utawezesha kushughulikia masuala ya watoto kwa wakati. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau, wizara imewajengea uwezo watoa huduma za ustawi wa jamii na watoa huduma za kujitolea 2,974, ili waweze kutoa huduma katika ngazi za kata na vijiji/mitaa.

151. Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilitoa leseni 18 za uendeshaji wa makao ya watoto na kufanya **Makao ya Watoto** yaliyoajiliwa kufikia 195. Aidha, Wizara imeendelea

kutoa huduma za chakula, malazi na huduma za afya kwa watoto 115 waliotunzwa katika Makao ya Taifa ya Watoto Kurasini.

152. Mheshimiwa Spika, Ili kuwezesha watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kulelewa katika familia, Wizara inatekeleza mpango wa kuwatumia walezi wa kuaminiwa, walezi mbadala, huduma ya malezi ya kambo na kuasili. Kwa mwaka 2016/17, jumla ya watoto 53 (Me 19, Ke 24) waliwekwa katika malezi ya kambo na watoto 20 (Me 7, Ke 13) waliasiliwa. Katika kipindi hicho Wataalamu wa Ustawi wa Jamii 35 walijengewa uwezo kuhusu kuwatambua walezi wa kuaminika ambao watatoa huduma ya muda kwa watoto hao.

Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto

153. Mheshimiwa Spika, Malezi Changamshi ya awali kwa mtoto yameendelea kuratibiwa. Kwa mwaka 2016/17, vituo 75 vya kulelea watoto wadogo mchana vimesajiliwa na kufanya idadi ya vituo hivyo kuongezeka kutoka vituo 782 mwaka 2015/16 hadi kufikia vituo 856 mwaka 2016/17. Aidha, jumla ya walezi wa watoto 1,211 walidahiliwa katika vyuo 23 vya malezi ya watoto. Vilevile, Wizara iliwajengea uwezo wa malezi na makuzi ya mtoto wataalam wa afya na wahudumu wa afya ngazi ya jamii 401 katika Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Nzega na Igunga.

Huduma kwa Watoto walio katika Mkinzano na Sheria na Marekebisho ya Tabia.

154. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa matunzo na maadilisho kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu za watoto za Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Moshi na Tanga na Shule ya Maadilisho Irambo. Katika mwaka 2016/17, Wizara imetoa huduma za chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu na elimu kwa watoto 375 (wavulana 345, wasichana 30) walio katika mahabusu za watoto na waadiliwa (wavulana 72) katika shule ya Maadilisho Irambo. Aidha, Wizara imewachepusha

watoto 882 kutoka katika mfumo wa makosa ya jinai. Kati yao, watoto 353 wamepitia mpango wa jamii wa marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria na watoto 529 waliotuhumiwa kufanya makosa ya jinai kutoka katika Vituo vya Polisi na kuunganishwa na familia zao.

155. Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara ili wajengea uwezo maafisa 228 wanaosimamia haki za Watoto. Mafunzo yalihusu utekelezaji na usimamizi wa amri za mahakama ili kuboresha upatikanaji wa haki kwa wakati. Kati ya hao, Mahakimu 46, Maafisa Ustawi wa Jamii 135 na Waendesha Mashtaka 47.

Maendeleo na Ustawi wa Familia

156. Mheshimiwa Spika, familia ni kitovu cha maendeleo ya binadamu na Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha utulivu na uimara wa familia ambao ni msingi wa jamii, Wizara imeendelea kutoa huduma za unasihi na usuluhishi wa migogoro ya ndoa. Katika mwaka 2016/17, jumla ya mashauri ya ndoa 6,819 yalipokelewa ambapo mashauri 2,727 yalisuluhishwa na mengine 4,092 yalipelekwa mahakamani kwa utatuzi wa kisheria.

157. Mheshimiwa Spika, Wizara imewajengea uwezo wataalam wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii 402 kuhusu elimu ya malezi bora katika ngazi ya familia. Mafunzo hayo yalitolewa katika Halmashauri na Kata za Temeke, Mafinga na Mufindi. Mafunzo hayo yanatarajiwa kuwawezesha wataalam hao kuwajengea uwezo wazazi na walezi kuhusu malezi bora ya watoto.

HAKI NA USTAWI WA WAZEE

158. Mheshimiwa Spika, wazee ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya taifa kutokana na uzoefu na ujuzi walionao katika nyanja mbalimbali. Kwa mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu haki na ustawi wa wazee kupitia vyombo vya habari

na maadhimisho ya siku ya wazee. Elimu hii imesaidia kuongezeka kwa idadi ya wazee wanaopata huduma za afya na kupungua kwa vitendo vya ukatili. Kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mauaji ya wazee yamepungua kutoka 190 (me 66, ke 124) mwaka 2015 hadi 135 (me 44, ke 91) mwaka 2016.

159. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI imewezesha kuwatambua wazee 69,100 na kufanya idadi ya wazee waliotambuliwa kufikia 367,889. Kati yao, wazee 16,990 walipatiwa vitambulisho vya msamaha wa matibabu na kufanya idadi ya wazee wenye vitambulisho hivyo kufikia 74,590. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau imewezesha kufanyika kwa ukarabati katika makazi ya wazee ya Kailima. Wizara pia imeboresha miundombinu kwa kuanza ujenzi wa bweni katika makazi ya Kolandoto (Mkoa wa 17)Vilevile, Wizara imeendelea kutoa huduma kwa wazee 456 wasiojiweza katika makazi 17 yanayoendeshwa na Serikali. Huduma hizi ni pamoja na chakula, malazi na matibabu.

160. Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali waliochangia katika kuhakikisha huduma bora kwa wazee nchini. Kipekee napenda kumshukuru **Mke wa Rais, Mhe, Mama Janet Magufuli** kwa kuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia wazee wanaotunzwa katika makazi ya wazee hapa nchini. Natoa wito kwa jamii kuiga mfano wa mama yetu huyu. Sote ni wazee watarajiwa tunahitaji kuwaenzi, kuwaheshimu na kuwatunza wazee wetu.

Wataalam wa Ustawi wa Jamii

161. Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Ustawi wa Jamii ni muhimu katika kuhakikisha utengamano wa familia na jamii. Katika kuhakikisha tunakua na wataalam hao katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara kupitia **Taasisi ya Ustawi wa Jamii** imeendelea kuzalisha wataalam hao kupitia mafunzo katika fani za Ustawi wa Jamii na fani

nyingine ikiwemo Rasilimali Watu na Mahusiano Kazini kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Kwa kipindi cha mwaka 2016/17, jumla ya wataalamu 1,164 walihitimu. Aidha, katika kuboresha mafunzo hayo, Taasisi imeendelea na ujenzi wa Maktaba ya kisasa.

MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

162. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchangia kufikiwa kwa maendeleo na ustawi wa jamii. Katika kutekeleza hilo, Wizara iliendelea kusajili, kufuatilia na kuratibu shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini ambapo, katika kipindi cha 2016/17, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 264 yalisajiliwa. Kati ya hayo mashirika 26 ni ngazi ya Kimataifa, 218 ngazi ya Kitaifa, 5 ngazi ya Mkoa na 15 ni ngazi ya Wilaya. Usajili huo umeongeza idadi ya mashirika kutoka 8,047 mwezi Julai, 2016 hadi kufikia 8,144 mwezi Machi, 2017 (**Kiambatisho Na.8**).

163. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2016/17, Wizara ilifuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Katika ufuatiliaji huo, jumla ya miradi 79 ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliyopo katika mikoa ya Rukwa, Katavi, Geita, Mara, Tanga na Mtwara ilitembelewa na kukaguliwa. Wizara pia ilifanya tathmini ya taarifa za utekelezaji kutoka katika mashirika 267. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali umezidi kuimarika hasa katika maeneo ya; afya, hifadhi ya mazingira, elimu, jinsia, utawala bora, utetezi wa haki za binadamu, hifadhi ya jamii na kilimo.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya ufuatiliaji na tathmini pia ilibainisha kuwa, jumla ya Mashirika 100 hayakuzingatia miongozo ya kisera, sheria, kanuni na katiba ya mashirika husika na hivyo kufutiwa usajili.

**UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/17 KWA
TAASISI NYINGINE ZILIZO CHINI YA WIZARA**

TAASISI YA CHAKULA NA LISHE (TFNC)

164. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Chakula na lishe ina jukumu la kuratibu, kutoa miongozo, kujenga uwezo kwa wataalamu, kufanya tafiti na kuishauri Serikali na wananchi kwa ujumla juu ya lishe bora na namna ya kuutokomeza utapiamlo. Taasisi imeendelea na jitihada za kupambana na utapiamlo kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na wanawake walioko kwenye umri wa kuzaa. Aidha, Utafiti wa Maendeleo ya Afya Nchini wa mwaka 2016 umebaini kuwa tatizo la udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano limepungua kutoka asilimia 42 hadi 34, uzito pungufu umepungua kutoka asilimia 16 hadi 14. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa afua mbalimbali. Vilevile, Taasisi ilikamilisha maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa masuala ya lishe 2016/17 – 2020/21. Mpango huo ni mbadala wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Lishe wa mwaka 2011/12-2015/16 ambao umekwisha muda wake.

165. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Taasisi ilifanya mafunzo kwa wakufunzi wa Taifa wa Afya na Lishe ya watoto. Mafunzo yalikusisha wajumbe wa Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Halmashauri kwa Halmashauri zote 184 nchini. Mafunzo yalilenga kutathmini zoezi la Afya na Lishe ya watoto la mwezi Juni 2016, kuangalia changamoto zinazowakabili, ili kuwapa wajumbe wa Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Halmashauri ujuzi zaidi na mbinu za utekelezaji wa afua za Afya na Lishe ya watoto. Aidha, Taasisi imeendelea kukusanya taarifa za ufanisi wa utoaji huduma za mwezi wa Afya na Lishe ya Mtoto kwa mwezi Desemba 2016 kutoka mikoa yote nchini ili kujua idadi ya watoto waliofikiwa na huduma za matone ya vitamini A (miezi 6 – 59), utoaji wa dawa za kutibu maambukizi ya minyoo (miezi 12 – 59) na upimaji wa hali ya lishe ya watoto wenye umri wa miezi 6 -59 pamoja na kutoa rufaa kwa watoto wenye utapiamlo.

BOHARI YA DAWA (MSD)

166. Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa imetekeleza majukumu yake ya msingi ya ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba, Vitendanishi na chanjo ili kuwezesha upatikanaji endelevu katika vituo vya kutolea huduma za afya zaidi ya **vituo 5,414** nchini. Wastani wa upatikanaji wa dawa muhimu katika Bohari ya Dawa umeimarika. Hali hiyo inatokana na ongezeko la bajeti ya dawa kutoka Shilingi bilioni 31 mwaka 2015/16 hadi kiasi cha Shilingi bilioni 251.5 mwaka 2016/17. Aidha, Katika kipindi cha Julai 2015 mpaka Machi 2016, Bohari ilipokea ni **Shilingi bilioni 24** tu kwa ajili ya dawa. Kwa mwaka mzima ikilinganishwa na kipindi cha 2016/17 hadi kufikia Machi 2017 ambapo Bohari tayari imeshapokea kiasi cha **shilingi bilioni 112.198**.

167. Mheshimiwa Spika, MSD inaendelea kuimarisha mfumo wa ugavi ambapo imefunga viambato vya kielektroniki (Barcode Scanners) katika maeneo yote ya usambazaji dawa ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za dawa, vifaa na vifaa tiba katika maghala wakati wote. Aidha, Kwa upande wa miradi msonge, MSD imetunza na kusambaza dawa zenye thamani ya zaidi ya **Shilingi bilioni 202** katika kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi, 2017. Hali hiyo, imeweza kuimarika kwa upatikanaji wa dawa za Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma nchi nzima. Vilevile, MSD imenunua, kutunza na kusambaza vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vyenye thamani ya zaidi ya **Shilingi bilioni 57** kwa ajili ya kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa ya Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma nchi nzima.

168. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa kiwango cha kutosha nchini, Serikali kupitia mpango wa ushirikishwaji wa sekta binafsi imeanza kutekeleza mkakati wa ujenzi wa viwanda vitakavyozalisha dawa na vifaa Tiba hapa nchini ambapo MSD imetengewa eneo la Ekari 100 Mkoani Pwani. Aidha, MSD imeendelea kupanua uwezo wa maghala katika kanda zake ambapo katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017, maandalizi ya ujenzi wa ghala la Kanda ya Dar es Salaam ujenzi wake

unategemewa kuwa umekamilika ifikapo June 2018. Kukamilika kwa ujenzi huo kutasaidia kuondoa gharama ya **shilingi milioni 800** zinazotumika katika ukodishaji wa maghalaya kuhifadhia dawa kutoka sekta binafsi kwa mwaka.

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)

169. *Mheshimiwa Spika*, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali hususan kuongeza wigo wa wanufaika wa bima ya afya. Idadi ya wanachama wachangiaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, imeongezeka kutoka wanachama **702,598** waliokuwa wameandikishwa mwaka 2015/16 hadi kufikia **wanachama 792,987** mwezi Machi 2017. Aidha, idadi ya wanufaika nayo iliongezeka kutoka **3,377,023** mwaka 2015/16 hadi kufikia **wanufaika 3,880,088** mwezi Machi 2017. Hii inaonyesha kuwa wanachama wa Mfuo wameongezeka kwa wastani wa asilimia 11 na wanufaika wameongezeka kwa wastani wa asilimia 8 katika kipindi cha miaka mitano (**Kiambatisho Na.9**). Mafanikio hayo yameweza kupatikana kutokana na juhudi zinazofanywa na Mfuko za kuelimisha watanania pamoja na kubuni mbinu mbalimbali za kuongeza wigo wa wanachama, kama kuanzishwa kwa mpango wa **KIKOA** (unaojumuisha kundi la wajasiriamali, vikundi vya vikoba, saccos na wavuvi), **TOTO AFYA KADI** (unaojumuisha watoto chini ya miaka 18), Wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya Juu, Wastaafu na wanachama binafsi.

MFUKO WA AFYA YA JAMII (CHF)

170. *Mheshimiwa Spika*, Hadi kufikia Machi 2017 Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulikuwa na jumla ya kaya **1,595,651** zilizojiunga ukilinganisha na kaya **1,452,855** zilizokuwa zimejiunga mwaka 2015/16. Aidha, wanufaika wameongezeka kutoka **8,717,130** mwaka 2015/16 hadi kufikia wanufaika **9,573,906** Machi 2017. (**Kiambatisho Na.10**). Katika kuchangia juhudi za wananchi wanaochangia CHF na kuboresha huduma zitolewazo, Serikali hutoa malipo ya tele kwa tele kwenye Halmashauri kulingana na kiwango cha

makusanyo ya CHF. Malipo yaliyofanyika kwa Halmashauri kwa kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi 2017 ni **Shilingi bilioni 3.5**. na hivyo kuwezesha jumla ya **Shilingi bilioni 12.3** kulipwa kwa Halmashauri mbalimbali nchini tangu Mfuko ulipokabidhiwa jukumu hili mwezi Julai 2009. Vilevile, Mfuko umefanya mapitio ya Tiba kwa Kadi (TIKA) ili Huduma hiyo iimarike Mijini, Utaratibu wa uanzishaji wa TIKA uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji katika Manispaa za jiji la Dar-es-salaam, Kibaha Mji na Babati Mjini. Matarajio ya Mfuko ni kuwa Halmashauri zote za Miji zitajielekeza katika kutekeleza TIKA.

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (TFDA)

171. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa imeendelea na shughuli za udhibiti wa ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ambapo Mamlaka inakamilisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wake wa miaka mitano wa 2012 – 2017. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2016/17, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi ya usajili wa viwanda vipya 767 (chakula 739, dawa 1, vipodozi 27) na vyote vilitathminiwa na kukaguliwa ambapo viwanda 635 (chakula 613, dawa 1 na vipodozi 21) sawa na **asilimia 82.8** vilisajiliwa baada ya kukidhi vigezo. Vilevile, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 8,023 ya usajili wa majengo na maeneo ya biashara ambapo maeneo 7,873 sawa na **asilimia 98.4** yalikitidhi vigezo na kusajiliwa.

172. Mheshimiwa Spika, Katika kujiridhisha na usalama na ubora wa bidhaa katika soko, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa majengo 13,461 (6,743 ya chakula, 2,553 dawa, 3,957 vipodozi na 208 vifaa tiba) ambapo majengo 11,923 sawa na **asilimia 89** yalikitidhi vigezo na hivyo kuhuishiwa vibali vyao vya biashara kwa mwaka 2016/17. Aidha, kupitia mfumo wa ufuatiliaji wa ubora na usalama wa bidhaa katika soko, jumla ya sampuli 462 zilichukuliwa katika soko na kuchunguzwa katika maabara ambapo sampuli 451 sawa na **asilimia 98** zilifaulu na sampuli 11 hazikitidhi vigezo na hivyo bidhaa husika ziliondolewa katika soko. Aidha, Mamlaka ilipokea maombi 5,802 kwa ajili ya usajili wa bidhaa za dawa,

chakula, vifaa tiba na vipodozi ambapo bidhaa 4,322 sawa na **asilimia** 75 yalisajiliwa. Vilevile, Mamlaka ilifanya uchunguzi wa jumla ya sampuli 2,860. *Kati ya sampuli zilizochunguzwa, sampuli 2,396 sawa na asilimia 84 zilifaulu vigezo vya ubora na usalama na asilimia 16 hazikukidhi vigezo na hivyo bidhaa husika hazikusajiliwa na nyingine kuondolewa.*

173. Mheshimiwa Spika; Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa jumla ya tani 631.7 za bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba, zenye thamani ya takriban Shilingi 797,312,103.15 kutokana na kutofaa kwa matumizi ya binadamu. Aidha, vipodozi vyenye viambato sumu vya thamani ya takriban Shilingi milioni 616 vilikamatwa katika maghala ya kificho na viwanda bubu jijini Dar es Salaam na matenka ya kubebea mafuta mkoani Njombe ambapo vipodozi hivyo vinasubiri hatua za kisheria kukamilika kabla ya kuteketezwa. Vilevile, Mamlaka imetoa Elimu kwa Umma kwa makundi mbalimbali ya wananchi na mihadhara katika vyuo na shule za sekondari ambapo wanafunzi na walimu 51,835 katika mkoa ya Ruvuma, Lindi, Pwani, Mwanza, Shinyanga, Geita, Mbeya, Rukwa, Tanga, Simiyu na Songwe walielimishwa.

174. Mheshimiwa Spika; Ili kusogeza huduma karibu na wananchi, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa ofisi na maabara ya Kanda ya Ziwa katika eneo la Nyakato, jijini Mwanza. Kukamilika kwa ofisi na maabara hiyo kutaongeza ufanisi wa utoaji huduma na hivyo kuimarisha uhibititi. Aidha, Mamlaka imeimarisha mfumo wa kielektroniki wa kupokea taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa kwa njia ya simu ya kiganjani ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za madhara ya dawa kwa haraka. Kupitia mfumo huo jumla ya taarifa **mpya 71** sawa na asilimia 44 ya taarifa zote zimepokelewa. Vilevile, Mamlaka imeanzisha mfumo wa kuweka taarifa za bidhaa zote zilizosajiliwa nchini kwenye mtandao ambao unasaidia wananchi na wateja kwa ujumla kuona bidhaa zilizosajiliwa na tarehe za kuisha muda wa usajili.

WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI (GCLA)

175. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali imenunua mtambo wa *Liquid Chromatography Mass Spectrometer* kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.6. Mtambo huo utatumika katika kufanya uchunguzi wa sampuli mbalimbali, zikiwemo za sumu, kilimo, uvuvi, mifugo, maji, dawa za binadamu, gesi, mafuta n.k. Aidha, mtambo utatumika kuchunguza dawa za kulevya na kutoa mchango katika juhudi za Serikali kupambana na matumizi ya dawa za kulevya. Vilevile, katika kuboresha huduma za uchunguzi wa kimaabara Wakala imenunua na kusimika mtambo wa kisasa (**ED-XRF**) katika Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya. Mtambo huo utatumika kutambua ubora na usalama wa bidhaa mbalimbali za viwandani na kilimo, kutambua uwepo wa madini ya thamani kwenye udongo na bidhaa za vito na sampuli zinazohusiana na usalama wa afya na mazingira.

176. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2016/17, Wakala ilikagua na kusajili makampuni 261 yanayojihusisha na shughuli za kemikali nchini sawa na asilimia 70 ya lengo. Aidha, Wakala ilikagua viwanda na maghala 346 ambayo ni sawa na asilimia 65 ya lengo hadi kufikia Machi, 2017. Vilevile, Wakala ilifanya uchunguzi na kutoa taarifa ya sampuli **25,632**, sawa na asilimia 194 ya lengo la kuchunguza sampuli **13,170**. Sampuli hizo ni za Vinasaba, Sumu, Dawa za Kulevya, Vyakula, Dawa asilia, Kemikali, Maji, Vilainishi vya Mitambo na sampuli za mazingira. Pia, Wakala umeendelea na ujenzi wa Maabara ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya ambao hadi mwezi Machi jengo hilo limeshapauliwa na **Shilingi 180,000,000.00** sawa na asilimia 60 ya gharama zote zimetumika.

TAASISI YA TAIFA YA UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU (NIMR)

177. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu imeendelea na utafiti wa

chanjo dhidi ya virusi vya HPV vinavyosababisha Saratani ya mlango wa kizazi. Utafiti huo unalenga kubaini kama dozi moja ya chanjo hiyo inaweza kutoa kinga sawa na dozi mbili au tatu. Utafiti unashirikisha wasichana walio na umri wa miaka kati ya 9 na 14 walio katika shule za umma za kutwa za msingi na sekondari zilizopo jijini Mwanza. Utafiti huo utashirikisha wasichana 900, watakaofuatiliwa kwa miezi 36 tangu walipopata dozi ya kwanza na unategemewa kukamilika mwaka 2021.

178. Mheshimiwa Spika; Taasisi kwa kushirikiana na Taasisi kutoka nchi za Kenya, Uganda na Ghana zilishiriki katika utafiti wa awali wa chanjo dhidi ya virusi vya Ebola. Madhumuni ya utafiti huo ilikuwa ni kutathmini usalama, ubora na uwezo wa kutengeneza kinga dhidi ya virusi vya Ebola. Aidha, utafiti huo ulifanyika katika jiji la Mwanza kwa kushirikisha watu wazima 25 wasiokuwa na matatizo ya kiafya waliohiari kushiriki, wakiwemo wanaume 23 na wanawake Wawili. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa chanjo hiyo kuwa ni salama. Uchambuzi wa takwimu unaendelea ili kuweza kubaini ubora wa chanjo hiyo katika kufanya mwili utengeneze kinga dhidi ya virusi vya Ebola. Matokeo haya yatawasilishwa pale uchambuzi wa takwimu utakapokamilika.

179. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2016/17, Taasisi ilifanya utafiti katika tiba asilia ili kubaini uwezo na usalama wa dawa za asili zinazotumiwa na jamii mbalimbali hapa nchini. Aidha, Taasisi imefanya utafiti wa dawa za asili zinazotumika kwa ajili ya tiba ya magonjwa ya malaria, UKIMWI na magonjwa nyemelezi, ugonjwa wa ini, shinikizo la damu, kisukari na kupunguza mafuta lehemu mwilini pamoja na uvimbe wa tezi dume kwa wanaume na dawa inayoongeza nguvu za kiume. Taasisi iko katika hatua za mwisho za kukamilisha usajili wa dawa asilia 11 ili ziweze kuingizwa sokoni.

MABARAZA YA KITAALUMA

180. Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa taaluma mbalimbali zilizomo katika sekta ya afya. Kwa

kuzingatia hilo Serikali imetunga sheria mbalimbali za kusimamia wanataaluma wa taaluma hizo. Hadi Machi 2017, Wizara imetunga sheria nane zinazosimamia taaluma za udaktari na udaktari wa meno; uuguzi na ukunga; ufamasia; wataalam wa maabara; wataalam wa afya; optometria; radiolojia na tiba asili. Aidha, Wizara inasimamia utoaji wa huduma kupitia hospitali na maabara binafsi nchini.

181. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2016/17, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limeendelea kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini na kuhakikisha jamii inapata huduma za uuguzi na ukunga zilizo bora na salama. Aidha, awamu ya kwanza ya **Ujenzi wa Kituo cha kuwaendeleza Wauguzi na Wakunga** kitaaluma nchini katika eneo la **mjini Kibaha (Pwani)** kwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani **umekamilika**. Lengo la mradi huo ni kuwawezesha wauguzi na wakunga nchini kupata nafasi ya kujiendeleza kitaaluma kwa kupitia mafunzo ya masafa yatakayokuwa yakiratibiwa katika jengo hilo. Mradi huo umegharamiwa kwa mapato ya ndani ya Baraza ambapo unatarajia kukamilika kabla ya Mwezi Juni, 2017 na kiasi cha **Shilingi bilioni 2.674** kimetumika.

182. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2016/17, **Baraza la Famasi** liliendelea kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali kufanya kaguzi katika maduka ya jumla na rejareja ya dawa ambapo jumla ya maduka ya dawa **721** yalikaguliwa na maduka **396 asilimia 54.9** yalikutwa na makosa mbalimbali. Baadhi ya makosa yaliyobainika ni pamoja na utoaji huduma ikiwemo kuendesha biashara ya dawa pasipo usimamizi wa mfamasia na uuzaji wa dawa zisizoruhusiwa kwa maduka ya dawa muhimu. Aidha, Baraza limetoa vibali kwa famasi **190** na maduka ya dawa muhimu **1,009** katika Halmashauri mbalimbali ambapo hadi kufikia Machi 2017 jumla ya famasi **1,432** na maduka ya ADDO **11,517 yalikuwa yamesajiliwa** nchini kote.

183. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, **Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala** kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imewasajili waganga wa tiba asili na tiba mbadala

5,298 kutoka mikoa yote nchini na hivyo kufikisha waganga 15,960 waliosajiliwa, vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa ni 45 na hivyo kufikisha jumla ya vituo 228. Aidha, Baraza lilifanya ufuatiliaji wa huduma za tiba asili katika Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Iringa na Songwe na kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni, Miongozo mbalimbali kwa waratibu 17 wa mikoa hiyo pamoja na baadhi ya waganga 373 wa tiba asili.

184. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, **Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi** imesajili vituo 45, makampuni 13 na kuandaa Mkataba wa Huduma kwa Wateja. Aidha, **Bodi ya Maabara Binafsi za Afya** ilifanya ukaguzi wa jumla ya bidhaa 309 zilizoingizwa nchini.

III. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

185. Mheshimiwa Spika Katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara kupitia fungu 52 itatekeleza vipaumbele vifuatavyo:

- i. Kuimarisha Huduma za Kinga, Tiba, na kuongeza usawa katika kutoa huduma za afya
- ii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto ili kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto,
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya,
- iv. Kuimarisha miundombinu kwenye vyuo vya mafunzo ya afya kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu,
- v. Kuimarisha matibabu ya kibigwa nchini kwa kuendeleza ujenzi, upanuzi, ukarabati wa miundombinu na kufunga mitambo ya kisasa

- ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Benjamini Mkapa - Dodoma, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto; pia Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando, KCMC, Mbeya na Mtwara.
- vi. Kuimarisha mazingira ya ubia na ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi (PPP) katika utoaji wa huduma za afya,
 - vii. Kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo vya kutolea Huduma za Afya,
 - viii. Uimarishaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha huduma za afya.
 - ix. Kuhamasisha wananchi kwa nia ya kuongeza idadi ya wanaojunga na Mifuko ya Bima za Afya.

186. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Fungu 53 imepanga kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo;

- i. Kuamsha ari ya wananchi kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo
- ii. Kuwezesha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa mwaka 2017/18 – 2021/22;
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya Mtoto;

- iv. Kukuza usawa wa jinsia na uwezesaji wa wanawake kiuchumi;
- v. Kuimarisha huduma za ustawi wa Mtoto na Wazee;
- vi. Kuimarisha ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya jamii kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi; na
- vii. Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii pamoja na Taasisi ya Ustawi wa Jamii

187. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2017/18, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

HUDUMA ZA KINGA

188. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2017/18, Wizara itaendelea kutekeleza afua mbalimbali za huduma za kinga ikiwa ni pamoja na;

- i. Kununua na kusambaza chanjo kulingana na mahitaji ya nchi ambapo **jumla ya shilingi bilioni 33** zimetengwa.
- ii. kununua na kusambaza **majokofu 1,710** ya kutunzia chanjo yatakayotumika katika ngazi ya wilaya na vituo vya huduma.
- iii. Kuendelea kutekeleza Kampeni ya uhamasishaji na uelimishaji umma (***Behaviour Change and Communication-BCC***) kuhusu usafi wa mazingira nchini.

- iv. Kuendelea kugawa dawa kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa usubi na Matende, minyoo ya tumbo, kichocho na ugonjwa wa trakoma katika Halmashauri za mikoa ambayo haikupatiwa dawa hizo kwa mwaka 2016/2017.
- v. Kuendela kugawa vyandarua kupitia kliniki za wajawazito na watoto (RCH) katika mikoa 9 ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Geita, Mwanza, Kagera, Mara, Simiyu na Kigoma na baadaa kujumuisha Mikoa mingine iliyobaki hadi kukamilisha mikoa yote kwa awamu
- vi. Kuendelea kuhakikisha upatikanaji wa vitendanishi (mRDT) kwa ajili ya kupima uwepo wa vimelea vya malaria na dawa mseto katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini.
- vii. Kuongeza wigo na kasi ya uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu katika mikoa yote nchini.
- viii. Kusambaza mashine 90 za GenXpert zitakazotumika kufanyia uchunguzi wa vimelea vya Kifua kikuu nchini
- ix. Kufanya kampeni maalum za uchunguzi na uibuaji wa wagonjwa wapya wa ukoma katika wilaya zenye viwango vikubwa vya maambukizi zikiwemo wilaya za Liwale, Kilombero, Chato, Nanyumbu, Mkinga na Muheza.
- x. Kuendelea kutoa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI kwa jumla ya watu **2,253,836** nchini.
- xi. Kufunga mashine mpya **80** za kupima uwingi wa virusi vya UKIMWI, TB na Utambuzi wa Virusi

vya UKIMWI kwa watoto wadogo wenye umri chini ya miezi 18 katika hospitali za mikoa ambayo haijapatiwa huduma hii na hasa katika wilaya zenye idadi kubwa ya WAVIU.

- xii. Kuendelea kuhamasisha wananchi kuzingatia mfumo bora wa maisha ikiwemo kufanya mazoezi mara kwa mara, kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa, kupunguza unywaji wa pombe kupita kiasi, kujiepusha na matumizi ya sigara na bidhaa za tumbaku pamoja na kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara.
- xiii. Kuanza mchakato wa kutunga sheria mpya inayoendana na *Framework of the convention on tobacco control* badala ya sheria ya Tumbaku ya mwaka 2003 inayotumika sasa.

Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

- i.* Kuendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kununua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango nchini ambapo **Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 14**
- ii.* Kuendelea kununua, kusambaza na kutoa bila malipo dawa kwa ajili ya uzazi salama katika vituo vya umma vya kutolea huduma ikiwemo oxytocin (dawa ya kuzuia kutokwa na damu baada ya kujifungua), magnesium sulphate (kwa ajili ya kifafa cha mimba), Fefol (kwa ajili ya kuongeza damu) ambapo jumla ya **shilingi bilioni 7 zimetengwa**.
- iii.* Kuendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki kwa akinamama wajawazito nchini na kujifungulia

katika Vituo vya kutolea huduma badala ya kujifungulia nyumbani.

- iv.* Kuendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo kwa kulipia kadi za Bima ya Afya kwa wanawake wajawazito wa kipato cha chini 150,000 kupitia Mradi wa Tumaini la Mama ambapo **jumla ya shilingi milioni 600 zimetengwa**
- v.* Kuboresha huduma za uchunguzi za uzazi salama kwa kununua mashine 65 za *ultrasound* kwa ajili ya vituo vya afya ili kuwezesha kutoa huduma maalum za dharura kwa kinamama wajawazito ambapo **jumla ya shilingi 5,412,500 zimetengwa**
- vi.* Kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za uzazi za dharura ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni kwa kuboresha vituo vya afya 150 **ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.8 kutoka vyanzo vya ndani zimetengwa.**
- vii.* Kuendelea kuboresha upatikanaji wa damu salama kwa kuongeza vituo 5 vya benki za damu katika mikoa yenye takwimu za vifo vingi vitokanavyo na uzazi ikiwemo mikoa ya Katavi, Rukwa, Ruvuma, Njombe na Manyara **jumla ya shilingi bilioni 2 zimetengwa.**
- viii.* Kuongeza upatikanaji wa huduma za kupima na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na saratani ya matiti katika Vituo vya afya na zahanati 100 nchini.
- ix.* Kuhakikisha wodi za watoto wachanga (neo natal ward) zinaanzishwa katika hospitali zote za Rufaa za mikoa na wilaya nchini.

- x. Kuendelea kutoa huduma za urutubishaji wa unga, mafuta na uongezaji wa madinjoto katika chumvi kwa mikoa yote nchini.
- xi. Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya kiafya kupitia njia zote za mawasiliano, ikiwemo machapisho, vyombo vya habari, simu za kiganjani na mitandao ya kijamii.

HUDUMA ZA TIBA

Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi.

189. *Mheshimiwa Spika*, Katika kipindi cha 2017/18, Wizara itaendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi nchini kwa kununua na kuvisambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya. **Jumla ya shilingi bilioni 236 zimetengwa.**

Huduma za Damu Salama

190. *Mheshimiwa Spika* katika mwaka 2017/18, Wizara imetenga jumla ya **shilingi bilioni 3.5** ili kuendelea kukabiliana na tatizo la uhaba wa damu salama kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kukusanya chupa za damu salama 230,000 kukidhi mahitaji ya damu salama nchini
- ii. Kuendesha kampeni ya ukusanyaji wa damu kutoka katika makundi mbalimbali katika jamii

Uimarishaji wa Huduma za kibingwa

191. *Mheshimiwa Spika* katika mwaka 2017/18, *Wizara itaendelea* kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za kibingwa nchini. Kupitia **Hospitali ya Taifa Muhimbili** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuanzisha huduma za kubadilisha figo (renal transplant)
- ii. Kuanzisha huduma za upandikizaji wa vifaa vya kusaidia kusikia ambapo jumla ya **shilingi milioni 206.3** zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa vya kusaidia kusikia.(cochlear implant)
- iii. Kuanza ujenzi wa jengo maalum kwa wagonjwa wanaolipia (private wing) ambapo jumla ya **shilingi bilioni 14.5** zimetengwa.
- iv. Kununua Vifaa, Vitendanishi na Vifaa Tiba kwa lengo la kuboresha huduma za kibingwa ambapo jumla ya shilingi bilioni 4 zimetengwa.

192. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**, katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kuendelea kutoa matibabu kwa maradhi yote ya Mgongo, mishipa ya fahamu na mifupa.
- ii. Kuwaongezea ujuzi wataalam wa upasuaji wa kubadilisha Nyonga na Goti.
- iii. Kuanza upasuaji wa vivimbe kwenye mishipa ya damu ya ubongo.
- iv. Kuboresha utoaji wa huduma kwa kununua vifaa na vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya jengo la MOI awamu ya tatu ambapo jumla ya shilingi bilioni 2 zimetengwa, na
- v. Kuendelea kurejesha Mkopu uliotumika kugharamia ujenzi wa jengo hilo ambapo jumla ya **shilingi bilioni 1.8** zimetengwa.

193. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, **Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete** itaendelea kuboresha huduma za matibabu ya moyo kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja kununua vifaa tiba kwa ajili ya chumba cha upasuaji ambapo jumla ya **shilingi bilioni 2** zimetengwa, na
- ii. Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam.
- iii. Kuandaa kambi mbalimbali za upasuaji kwa kushirikiana na madaktari bigwa kutoka nje ya nchi

194. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, **Taasisi ya Saratani Ocean Road** itaendelea kuimarisha huduma za kinga, uchunguzi, mafunzo na tiba ya saratani kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kununua vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ikiwa ni pamoja na PET Scan **ambapo kiasi cha shilingi bilioni 14.5 zimetengwa**. Hatua hii inatarajiwa kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi zaidi ya asilimia 60 na hivyo kuokoa pesa za Serikali kiasi cha shilingi billioni 5 kwa mwaka zinazotumika kulipia matibabu ya wagonjwa nje ya nchi
- ii. Kuimarisha huduma za mkoba hasa katika maeneo ambayo yanaonekana kuwa na idadi kubwa ya watu waliogundulika kuwa na saratani.
- iii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani ili kupunguza mzigo kwa wagonjwa hasa wa kipato cha chini.

195. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za afya za kibingwa katika **Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma** kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kununua vifaa na vifaa tiba ili kuboresha utoaji wa huduma za kibingwa ambapo jumla ya **shilingi bilioni 1** zimetengwa
- ii. Kuongeza wataalam wa fani mbalimbali na kuwajengea uwezo walilopo.
- iii. Kuanzisha maabara ya kisasa (cath lab) kwa ajili ya matibabu ya moyo pamoja na maabara yenye uwezo wa kuchunguza vinasaba.
- iv. Kuanzisha huduma ya matibabu ya magonjwa ya Figo na njia ya mkojo (Dialysis) na upandikizaji wa Figo (Renal Transplant)

196. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia **Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe** itaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma ya tiba ya afya ya akili katika kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kununua vifaa na vifaa tiba **ambapo jumla ya shilingi bilioni 1 zimetengwa.**
- ii. Kujenga uzio kuzunguka eneo la hospitali
- iii. Kuendelea na ukarabati wa wodi za wagonjwa

197. Mheshimiwa Spika, **Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya** itatekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kuboresha na kupanua wigo wa huduma zinazotolewa kwa kufanya ukarabati jengo la daraja la kwanza na kukamilisha ujenzi wa jengo la watoto hivyo kuongeza uwezo kwa hospitali kutoka **vitanda 477** vya sasa mpaka vitanda **605**.

- ii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la kutoa huduma za radiolojia (Radiology) **ambapo jumla ya shilingi bilioni 2 zimetengwa.**

198. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando itatekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwa pamoja na kliniki za wagonjwa wa nje, jengo la Saratani,
- ii. Kukamilisha ujenzi wa kliniki ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.
- iii. Kununua mashine ya Brachytherapy kwa ajili ya matibabu bora zaidi ya saratani.

199. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18 Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini KCMC, sambamba na kuendelea kutoa huduma itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kutekeleza awamu ya pili ya ujenzi wa wodi na hosteli za wagonjwa wa saratani utakaogharimu **shilingi bilioni 2.**
- ii. Kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kusafisha figo.

200. Mheshimiwa Spika, Hospitali Maalumu ya Kibong'oto itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na ukarabati wa wodi za wagonjwa na maabara. Jumla ya shilingi bilioni 1 zitatumika kutekeleza kazi hizo
- ii. Kutoa elimu kwa wataalam mbalimbali kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuanzisha matibabu ya kifua kikuu sungu.

201. Mheshimiwa Spika, katika kuimalisha Huduma za uchunguzi wa magonjwa Wizara itaendelea na ujenzi wa maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii katika eneo la Mabibo, Dar es salaam. Mradi huo hadi kukamilika unatarajiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 7,493,193,434.97.00**.

202. Mheshimiwa Spika, kuhusu Tiba Asili na Tiba Mbadala Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma na waganga kupitia vyombo vya habari kuhusu usajili wa dawa za asili na maeneo ya kuzalishia dawa hizo.

203. Mheshimiwa Spika; katika mwaka, 2017/18, Wizara inakusudia kuboresha utoaji wa **huduma za uuguzi na ukunga** unaozingatia maadili, utu, na heshima ya mteja "respective care". Aidha, Wizara inapanga kuandaa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu zitolewazo na Wauguzi na Wakunga.

204. Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea **kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na upatikanaji wa takwimu za afya kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini**.kwa kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kutoa taarifa za vituo vya afya nchini yaani (**HMIS/DHIS2**) na uboreshaji wa mtandao wa kutoa taarifa za afya kupitia anuani ya **hmisportal.moh.go.tz**

205. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI inatarajia kuimarisha mfumo wa mawasiliano kwa kutekeleza yafuatayo:

- i. Kufunga awamu ya kwanza ya mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za wagonjwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya na kutoa mafunzo ya matumizi ya mfumo huo.
- ii. Kuanza kutumia TEHAMA katika kufuatilia wagonjwa na taarifa zao katika ngazi ya jamii hususan taarifa za vifo, uzazi, magonjwa ya

mlipuko na magonjwa sugu kama kifua kikuu na UKIMWI (self-assessment) kwa kutumia mfumo wa simu za kiganjani.

- iii. Kuanzisha mfumo wa CHF mobile app ambao utarahisisha upatikanaji wa huduma za bima ya afya katika jamii.

RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

206. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kusimamia eneo la rasilmali watu katika sekta ya afya ambapo katika mwaka 2017/18 kazi zifuatazo zitatekelezwa:

- i. Kudahili wanafunzi watarajari 13,632 katika vyuo vya afya vilivyoko chini ya Wizara
- ii. Kuendelea kugharamia mafunzo ya uzamili na uzamivu kwa wataalam wa kada mbalimbali za afya.
- iii. Kuendelea kuboresha miundombinu katika Vyuo vya Afya kwa kufanya ukarabati na upanuzi wa vyuo ambapo jumla ya **shilingi bilioni 3** zimetengwa.

207. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2017/18, kazi zitakazotekelezwa na fungu 53 ni zifuatavyo;

MAENDELEO YA JAMII

208. *Mheshimiwa Spika*, ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya nchi ya kufikia Uchumi wa kati kupitia wataalam hawa, Wizara katika mwaka 2017/18 itatekeleza yafuatayo:

- i. Kuendelea kuhamasisha Halmashauri na Mikoa kuajiri watumishi wa fani ya Maendeleo ya Jamii;

- ii. Kuendelea kuboresha utekelezaji wa shughuli za Maendeleo ya Jamii ikiwemo kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii katika ngazi za Sekretarieti za Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mtaa. Uimarishaji wa mfumo huu utawezesha serikali kupata taarifa sahihi za ushiriki wa Jamii katika kuleta maendeleo ya nchi yetu;
- iii. Kuendelea kuwajengea uwezo Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa kusimamia sera na miongozo ya Wizara ili waweze kuishirikisha jamii katika kujiletea maendeleo;
- iv. Kuendelea kuwezesha vyuo kuandaa na kutoa wataalam wa maendeleo ya jamii katika Vyuo 8 na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili.
- v. Kuboresha miundombinu ya vyuo na mazingira ya kujifunzia na kufundishia; na
- vi. Kuimarisha ubora wa wataalam wa maendeleo ya jamii wanaozalishwa na Taasisi kwa kuandaa mitaala ya NTA level 4 & 9 itakayozingatia hali halisi ya mabadiliko na mahitaji ya jamii.

MAENDELEO YA JINSIA

209. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kusimamia maendeleo ya jinsia kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kuwawezesha wanawake kiuchumi

- i. Kupitia Benki ya Wanawake Tanzania kutoa Mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 12 kwa wajasiriamali wanawake 9,650 katika mikoa ya Dares Salaam, Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma, Ruvuma, Pwani na Mwanza.
- ii. Kuwezesha Akaunti ya Malaika kufanya kazi kwa ufanisi na kuwafikia wanawake wajasiriamali walengwa;
- iii. Kuhamasisha uanzishwaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi katika mikoa yote ya Tanzania Bara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI.
- iv. Kuendelea kuhakikisha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake unawafikia wanawake wengi. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika mwaka 2017/18, itaendelea kuhamasisha Halmashauri kuchangia asilimia tano (5%) ya mapato yao ya ndani katika Mfuko.
- v. Kuboresha mfumo wa taarifa za mikopo na wanufaika wa mfuko, kazi itafanyika kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI;
- vi. Kusambaza mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko ulioboreshwa kwa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini; na
- vii. Kuzijengea uwezo Kamati za Mikopo za Mfuko katika Halmashauri 15 kuhusu uendeshaji na usimamizi wa Mfuko ili kuimarisha utendaji na usimamizi wake kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Kuzuia na Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia

- viii. Kusambaza na kuwezesha kuanza kutumika kwa Daftari la kutunza taarifa za ukatili wa kijinsia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa ili kuimarisha upatikanaji na ubora wa taarifa na takwimu za ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto;
- ix. Kuimarisha Kamati 51 za Ulinzi wa Wanawake na Watoto; na
- x. Kufuatilia utekelezaji wa afua za kuzuia ukatili wa kijinsia hususan dhidi ya wanawake na watoto.

Ushiriki wa Wanawake katika Ngazi za Uongozi na Maamuzi

- xi. Kuendelea kuhuisha Kanzidata inayoonesha wasifu wa wanawake kwa ajili ya kuwawezesha kushiriki katika fursa za uongozi, ngazi za maamuzi na ajira; na
- xii. Kuziwezesha taasisi mbalimbali kutumia taarifa katika kanzidata kuajiri, kufanya uteuzi na maamuzi mbalimbali ya kiseru.

Uingizaji wa Masuala ya Jinsia Katika Sera, Sheria na Mipango ya Kisekta na Taifa

- xiii. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000 pamoja na Mkakati wake. Mapitio ya Sera hiyo yatawezesha kuzingatiwa kwa masuala muhimu ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu, Agenda ya Afrika Tuitakayo 2063, Mpango wa Taifa wa Maendeleo Miaka Mitano na kukidhi mahitaji ya sasa ya kufikia

usawa wa kijinsia na uwezesaji wanawake nchini.

- xiv. Kupitia Mwongozo wa uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sekta zote pamoja na kuandaa Kanzidata kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za hali ya jinsia nchini.

MAENDELEO YA MTOTO

Ukatili dhidi ya watoto

210. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, kupitia Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto, Wizara itatekeleza yafuatayo katika kutokomeza ukatili dhidi ya mtoto

- i. Kuimarisha utendaji wa kamati za ulinzi wa mtoto katika Mamlaka za Serikali ya Mitaa kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata na Halmashauri za Wilaya;
- ii. Kuendelea kutoa mafunzo kuhusu malezi chanya na athari za ukatili dhidi ya watoto katika Halmashauri 12 za Mikoa ya Lindi na Mtwara;
- iii. Kuhamasisha kuanzishwa kwa mfumo wa ulinzi wa mtoto katika shule za msingi kwa ajili ya kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya mtoto katika mazingira ya shule;
- iv. Kuendelea kuelimisha wazazi, walezi na jamii kutokomeza mila na desturi zinazoathiri afya na maendeleo ya mtoto wa kike na kumnyima haki kuendelea na masomo na hivyo kufifisha ndoto zake;
- v. Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa klabu katika shule za msingi na sekondari; na

- vi. Kuendelea kusimamia upatikanaji wa haki ya ushiriki wa mtoto kupitia mabaraza ya watoto. Kwa mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kuhamasisha Halmashauri kuanzisha mabaraza ya Watoto ili kuongeza idadi kutoka 108 iliyopo sasa hadi kufikia 140 na kuyawezesha kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

211. Mheshimiwa Spika Wizara imeendelea kuweka mifumo ya matunzo, malezi na ulinzi wa watoto yenye misingi ya kijamii. Kwa mwaka 2017/18, pamoja na mambo mengine itafanya yafuatayo:

- i. Kuendelea kuzijengea uwezo Halmashauri na wadau wengine kuweka mifumo imara ya matunzo na ulinzi kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi;
- ii. Kuhamasisha na kuelimisha waajiri kuzingatia marekebisho ya Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini hususan kifungu cha 33(10) na kuzifanyia marekebisho kupitia Kanuni zake mpya kwa kutoa fursa kwa waajiriwa wanawake kupata haki ya kunyonyesha watoto wao;
- iii. Kuendelea kuratibu na kusimamia uanzishwaji na uendeshaji wa vituo vya malezi ya watoto pamoja na kuwajengea uwezo watoa huduma za malezi na makuzi ya awali ya Watoto;
- iv. Kuendelea kuwajengea uwezo watoa huduma kwa watoto wanaokinzana na sheria ili kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wakati;

- v. Kuendelea kuwezesha utoaji wa huduma za usuluhishi na ushauri nasaha ili kuleta utulivu na uimara katika ndoa kwa maendeleo na ustawi wa taifa;
- vi. Kuendelea kuwajengea uwezo wataalam wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii katika Halmashauri ili kuboresha makuzi na malezi katika familia kwa lengo la kupunguza vitendo vya ukatili wa watoto kwenye jamii;
- vii. Kuendelea kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika fani mbalimbali; na
- viii. kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia na kuanzisha kituo cha utafiti na ubunifu katika fani ya ustawi wa jamii ili kuongeza ufanisi katika kufundisha.

HAKI NA USTAWI WA WAZEE

212. *Mheshimiwa Spika*, wazee ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya taifa kutokana na uzoefu na ujuzi walionao katika nyanja mbalimbali. Katika mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kuboresha huduma, makazi ya wazee na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wazee kote nchini na kutokomeza mauaji ya wazee.

MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

213. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchangia kufikiwa kwa maendeleo na ustawi wa jamii. Kwa mwaka 2017/18, Wizara itaendelea kusajili na kuratibu utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhakikisha yanatoa mchango unaotarajiwa kwa maendeleo na ustawi wa jamii.

214. Mheshimiwa Spika, aidha Taasisi zilizo chini ya Wizara zitaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma kwa kutekeleza na Mipango ya Maendeleo ikiwa ni pamoja na:

- i. Kupanua maghala ya MSD katika Kanda ya Dar es Salaam
- ii. Kufanya upanuzi wa maabara ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Chakula na Dawa ili kuongeza ufanisi katika uchunguzi wa bidhaa,
- iii. Kuanza udhibiti wa vitendanishi na vifaa vya maabara, kukamilisha ununuzi wa vifaa vya maabara ya kisasa ya TFDA Kanda ya Ziwa, Mwanza
- iv. Kuanza ujenzi wa jengo la Maabara na ofisi za TFDA kwa ajili ya kanda ya Kati - Dodoma.
- v. Kununua mitambo na vifaa mbalimbali vya maabara ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo jumla ya shilingi **bilioni 10 zimetengwa.**
- vi. Kukamilisha ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu na Ofisi ya Kanda ya Kaskazini - Arusha,
- vii. Kukarabati maabara ya Vinasaba vya Binadamu ya Mkemia Mkuu wa Serikali iliyopo Dar es Salaam
- viii. Kuboresha utafiti na uzalishaji wa dawa za asili katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kwa kununua mashine za kisasa kwa ajili ya kiwanda cha kuzalisha dawa za asili Mabibo. Jumla ya **shilingi milioni 800 zimetengwa.**

Taasisi za Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii

215. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia **Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru** itaendelea kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani mbalimbali. Aidha, Wizara itaboresha miundombinu ya vyuo; na mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Vilevile, itaimarisha ubora wa wataalam wa maendeleo ya jamii wanaozalishwa na Taasisi kwa kuandaa mitaala ya NTA level 4 & 9 itakayozingatia hali halisi ya mabadiliko na mahitaji ya jamii.

Aidha, Wizara itaendelea kuratibu utoaji wa mafunzo ya maendeleo ya jamii kupitia **Vyuo (8) vya Maendeleo ya Jamii** pamoja na kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Lengo ni kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojunga na mafunzo katika vyuo hivyo ikiwa ni pamoja na kudurusu Mtaala wa Mafunzo kwa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira na kuwawezesha wahitimu kujajiri.

Taasisi ya Ustawi wa Jamii

216. Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha tunakua na wataalam wa Ustawi wa Jamii katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara kupitia Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kuzalisha wataalam hao kupitia mafunzo katika fani za Ustawi wa Jamii na fani nyingine ikiwemo Rasilimali Watu na Mahusiano Kazini kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Katika mwaka 2017/18, Taasisi itaendelea kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika fani mbalimbali, kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia na kuanzisha kituo cha utafiti na ubunifu katika fani ya ustawi wa jamii ili kuongeza ufanisi katika kufundisha. Aidha, Taasisi inatarajia kukamilisha mchakato wa kuanzisha shahada ya uzamili katika fani ya rasilimali watu na shahada ya maendeleo ya jamii.

MABARAZA YA KITAALUMA

217. *Mheshimiwa Spika*, Serikali itaendelea kutambua umuhimu wa taaluma mbalimbali zilizomo katika sekta ya afya; kwa kuzingatia hilo, Serikali itasimamia sheria mbalimbali za wanataaluma wa taaluma hizo. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utoaji wa huduma kupitia hospitali na maabara binafsi nchini.

USHIRIKIANO WA NDANI NA NJE YA NCHI

218. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kushirikiana na nchi rafiki katika kuimarisha Sekta ya Afya nchini. Aidha, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye mikutano ya jumuiya za kikanda za SADC, EAC, ECSA-HC na mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa na katika kutekeleza maamuzi ya pamoja yenye manufaa kwa taifa. Katika mwaka 2017/18, Wizara itaimarisha ushirikiano na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayosaidia Wizara yangu. Aidha, itaimarisha ushirikiano na sekta nyingine ambazo zinachangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na mikoa na wadau wa sekta itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za afya za kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuhamasisha na kufikisha ujumbe kwa umma. Baadhi ya siku hizo ni za Afya, Malaria Afrika, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Wazee, Kutotumia Tumbaku, Tiba Asili ya Mwafrika, Wachangia Damu, Utepe Mweupe, Siku ya Wauguzi na Fimbo Nyeupe na Siku ya Mtoto Njiti duniani.

IV: SHUKRANI

219. *Mheshimiwa Spika*, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark (DANIDA), Uswisi (SDC), na Ireland (Irish Aid), Canada (DFATD) na Mashirika ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, na UNFPA kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Aidha, naishukuru na kuipongeza Korea Kusini kupitia shirika lake la Maendeleo (KOICA) kwa kuamua kujiunga na

nchi zinazochangia fedha katika Mfuko wa pamoja kwa ajili ya huduma za afya kuanzia mwaka 2016/17. Pia, napenda kuzishukuru nchi za Canada, China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa njia mbalimbali.

220. Mheshimiwa Spika, vilevile nayashukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Mfuko wa Dunia Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (*GFATM*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Afrika (BADEA), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Global Alliance on Vaccine (GAVI), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo (UNDP), UNFPA, UN-Women, Shirika la Afya Duniani (WHO) na Benki ya Dunia (WB). Wengine ni Abbott Fund, BASIC NEED (UK), ACF – Canada, Baylor College of Medicine ya Marekani, Canadian Bar Association, CDC, CORDAID (Netherlands), CUAMM, DANIDA, DFID, Engender Health (USA), EED, Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF), Family Health International (FHI360), FINIDA, GIZ, Good Samaritan Foundation (GSF), German TB and Leprosy Relief Association (GLRA), HelpAge International, ILO, Jane Adams School of Social Work ya Chuo Kikuu cha Illinois Marekani, John Snow Incorporation (JSI), JICA, KOICA, KfW, Global Partnership for Education (GPE), Madaktari Afrika na Madaktari Wasio na Mipaka (Medicins Sans Frontieres – MSF), MSERIOR, ORIO, P4H, SAREC, SDC, SIDA (Sweden), Shirika la Upasuaji la Spain, SIGN la Marekani, na Shirika la Human Resource Capacity Project, Touch Foundation, USAID na, Children Investment Foundation Fund (CIFF), World Lung Foundation.

221. Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Wadau wa Maendeleo ambao ni African Programme for Orchorcerciasis Control, *Africare*, *Axios International*, *Aids Relief Consortium*, *AIHA*, *ASCP*, *ASM*, *APHL*, *Balm and Gillead Foundation*, *Bill*

and Melinda Gates Foundation, Clinton Health Access Initiative, CLSI, CMB, Christoffel Blinden Mission (CBM), Christian Relief Services (CRS), Citi Bank, Department of Defence ya Marekani, Community of Saint Egidio (DREAM), Duke University, ECSA, Futures Group, Glaxo Smith Kline (GSK), General Electric (GE – USA), Havard University na University of Maryland, Helen Keller International, Henry Jackson Foundation, IMA, ICAP, International Trachoma Initiative, Intrahealth, International Eye Foundation, I-TECH, Jhpiego, Johns Hopkins University, Labiofarm Industry, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Management Science for Health (MSH), MEDA, Merck & Company, Malaria No More, Military Advancement for Medical Research, NOVARTIS, Pathfinder, PATH, President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR), Pharm Access International, PactWorld, Plan International, Pfizer, Qiagen, Research Triangle Institute (RTI), Regional Psychosocial Support Initiatives (REPSSI), Saint Thomas Hospital- London, Save the Children, SightSavers International, Supply Chain Management Systems (SCMS) na University of Columbia, URC, USA-Presidential Malaria Initiative (PMI), World Vision, FXB, Walter REED Army Institute of Research (WRAIR) na World Education Inc.

222. Mheshimiwa Spika, ninawashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, Benjamin William Mkapa HIV/AIDS Foundation, CCBRT, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, MEWATA, MUKIKUTE, FAWETA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Assosiation (TSA), Tanzania Society of Anaesthesiologist of Tanzania (SATA), Association of Gynaecologists and Obstetricians of Tanzania (AGOTA), Association of Paedricians of Tanzania (PAT), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, Mabaraza yote ya

Kitaaluma, Mashirika, hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii nchini pamoja na vyama vyote vya kitaaluma vya sekta ya afya.

223. Mheshimiwa Spika, navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na maendeleo ya jamii.

224. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha naomba kuwashukuru **Dkt. Mpoki M. Ulisubisya** Katibu Mkuu (Afya) na **Bibi Sihaba Nkinga** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Muhammad Bakari Kambi**, Mganga Mkuu wa Serikali Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara yangu. Nawashukuru pia Wakurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, MOI, JKCI, ORCI, BMH, Mirembe, Kibongoto na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda za Mbeya, Bugando, na KCMC na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na watumishi wote wa wizara, Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote

ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa sekta ya afya, maendeleo na ustawi wa jamii wakiwemo madaktari, wauguzi na wakunga kwa kuendelea kutoa huduma kwa wananchi. Naomba waendeleo kuzingatia misingi ya kutoa huduma bora, maadili ya kazi na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu

225. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa Viongozi na Wananchi hasa wanawake wa Mkoa wa Tanga ninawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Mkoa wetu.

V: MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2017/18

Fungu 52 – Afya

Mapato

226. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18 Wizara imekadiria kukusanya mapato ya **Shilingi 225,038,495,525.00** kati ya fedha hizo **Shilingi 207,472,729,612.00** zitakusanywa katika mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara na **Shilingi 17,565,765,913.00** ni kutoka katika vyanzo vya makao makuu. Vyanzo hivyo vinatokana na makusanyo ya uchangiaji wa huduma za afya, tozo na ada mbalimbali, usajili wa vituo binafsi vya kutolea huduma, maabara binafsi na Mabaraza ya Kitaaluma.

Matumizi ya Kawaida

227. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 291,895,940,000.00** kwa

ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 64,063,937,000.00** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 227,832,003,000.00** zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara **Shilingi 49,036,786,000.00** ni kwa ajili ya watumishi wa Wizara, Makao Makuu na **Shilingi 178,795,217,000.00** ni kwa ajili ya watumishi wa Taasisi, Mashirika na Wakala zilizo chini ya Wizara.

Miradi ya Maendeleo

228. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/18 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 785,805,952,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 336,300,000,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 449,505,952,278.00**. Jumla ya Makadirio ya Bajeti kwa 2017/18 kwa Fungu 52 ni **Shilingi**

Fungu 53 – Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

229. Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na Matumizi kwa Mwaka 2017/18 kwa Fungu – 53 ni kama ifuatavyo:

Makusanyo ya Maduhuli

Wizara inataraji kukusanya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 2,101,874,000.00** ambazo ni kutokana na ada za wanafunzi kutoka Vyuu 8 vya Maendeleo ya Jamii, ada za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mauzo ya vitabu ya zabuni.

Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2017/18, ni **Shilingi 35,300,602,090.00** ambapo Mishahara ni **Shilingi 19,142,252,240.00** na **Shilingi 16,158,349,850.00** ni Matumizi Mengineyo. Aidha, Miradi ya Maendeleo inakadiriwa kutumia kiasi cha **Shilingi 2,606,278,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 606,278,000** ni fedha za nje.

Jumla ya Makadirio ya ya Bajeti kwa 2017/18 kwa Fungu 53 ni **Shilingi 37,906,880,090**

230. Mheshimiwa Spika, Jumla ya fedha zote zinazoombwa ni shilingi **1,115,608,772,090**.

231. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto www.moh.go.tz na www.mcdgc.go.tz.

232. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja

MWENYEKITI: Tunaendelea na mtiririko wetu, namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Mheshimiwa Peter Serukamba. (*Makofi*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nina omba hotuba yangu yote ingie kwenye *Hansard* kama ilivyo, hapa nimefanya *summary* kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili, uchambuzi katika masuala mbalimbali. Katika maoni ushauri na mapendekezo yaliyo tolewa na Kamati iliyopita yapo maoni yaliyoweza kutekelezwa kikamilifu, yanayoendelea kutekelezwa na Wizara na ambayo hayajatekelezwa. Katika ushauri tulioutoa Kamati inaipongeza Serikali na Wizara kwa jitihada hizo na yale ambayo yanaendelea kutekelezwa Kamati inaiomba Wizara iendelee kusimamia ili yatekelezwe kama tulivyoshauri na yale ambayo hayajatekelezwa kwa

sababu ya kutopata fedha kutoka Serikalini Kamati inaiagiza Wizara kufuatilia fedha hizo na kuyatekeleza mara moja kabla ya mwaka 2016/2017 haujaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2016/2017; Kamati ilifanya mapitio na mwenendo wa makusanyo maduhuli ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017, na kufanya ulinganisho wa makadirio wa maduhuli wa mwaka 2017/2018 na kuona mwenendo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ilikadiri kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 170 kutoka Fungu 52 - Idara Kuu ya Afya na kufikia mwezi Machi, 2017 Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 157 sawa na asilimia 75.5

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa mwaka 2016/2017; upatikanaji wa fedha katika Wizara haujawa wa kuridhisha kwani fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi, 2017 ilikuwa haijafika asilimia 50. Katika Fungu 52 hadi kufika mwezi Machi, 2017 ni kiasi cha shilingi bilioni 314.67 sawa na asilimia 40 kati ya shilingi bilioni 796.11 kilichokuwa kimeidhinishwa na Bunge lako Tukufu kilikuwa kimepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Fungu namba 53 hadi kufika mwezi Machi, 2017 Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto ilikuwa imepokea shilingi bilioni 16.23 sawa na asilimia 39.57 kati ya shilingi 41,000,000,000 kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kamati inaona kwamba Serikali haijaamua kulipa kipaumbele suala la afya, kwanza kwa kutokutenga fedha za kutosha katika sekta hii, pili kutotoa fedha za utekelezaji wa shughuli zake kwa wakati.

Kamati inaona kwamba hata mafanikio ya nayopataika katika Wizara hii, ni kutokana na uzalendo mkubwa walionao Wizara, watendaji wakuu pamoja na wasaidizi wao katika kutafuta vyanzo vingine vya fedha na si fedha za Serikali ambazo zimetengwa na bajeti yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyekuwa mpigania uhuru na baba wa taifa la India *Mahatma Gandhi* aliwahi kusema; *"It is health that is real wealth and not pieces of gold and silver."* Hivyo Serikali haina budi kuhakikisha afya za Watanzania ndicho kipaumbele na ndio utajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaisihi Serikali kuipa kipaumbele cha pekee Wizara hii kwa kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zikiwemo shughuli za kutoa huduma za kuzia magonjwa (*prevention services*), matibabu (*curative services*), hata *promotion service*. Kwa kutekeleza haya hatuta lazimika kutenga fedha nyingi kwa masuala ya dawa kwani magonjwa yatakayohitaji dawa yatakuwa tayari ya mekwisha zuliwa katika huduma ya kinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo kuhusu miradi ya maendeleo iliyokaguliwa ni kuwa mwaka 2016/2017 Fungu 52 lilitengewa shilingi 518,000,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 320,000,000 sawa na asilimia 40.2 ni kutoka vyanzo vya ndani na kiasi cha shilingi bilioni hizo ni vyanzo vya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi wa miradi ni kuwa Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi iliyotengewa jumla ya shilingi bilioni tano kwa ajili ya kununua mashine mpya za kisasa za kutibia saratani. Gharama za mashine hizi zilikuwa ni bilioni 9.5 ambapo katika mwaka wa fedha 2015/2016 taasisi ilitengewa shilingi bilioni 4.5 ambazo imeshapokelewa.

Aidha, hadi kufikia siku Kamati inakagua mradi huu, Tasisi ilikuwa imeshapokea bilioni tano, sawa na asilimia 100, fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kamati imejulishwa kuwa Taasisi imekamilisha kuandaa makabrasha ya zabuni na mashine zinatarajiwa kufika mwezi Mei, 2017.

Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa mradi huu, kwani utasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Taasisi hii, wanaokwenda kupata matibabu ya

saratani. Kamati inasisitiza Taasisi chini ya usimamizi wa Wizara iharakishe mchakato wa manunuzi ya vifaa tiba hivyo ili viweze kuanza kutoa huduma haraka kwa wagonjwa wa saratani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa ununuzi wa mitambo ya vifaa tiba katika Taasisi ya Mifupa (MOI); Mradi huu ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni 4.8 ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.8 ni kwa ajili ya kulipa mkopo wa *NHIF* na shilingi bilioni tatu ni kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na vifaa tiba. Hadi Kamati inatembelea MOI hakuna fedha iliyokuwa imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Taasisi ya MOI ni Taasisi nyeti sana kutokana na utoaji wake wa huduma ya mifupa hususani kutokana na ongezeko kubwa la wahitaji wa huduma ya mifupa katika Taasisi hiyo. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa ajali hapa nchini zikihusisha magari, pikipiki na vyombo vya moto ambavyo hupelekea watu kuvunjika miguu ama mwisho wa siku huduma yake hupatikana katika Taasisi ya Moi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa sana na hali ya kutotolea kwa fedha kwani MOI ni moja ya Taasisi muhimu sana nchini na ndiyo Taasisi pekee inayotoa tiba ya mifupa hapa nchini. Taasisi hii inatumia mapato yake ya ndani kwa ajili ya kununua vifaa tiba na kutoa huduma kwa ajili ya wananchi. Pia ikumbukwe kwamba kuna kundi linapewa msamaha katika gharama za matibabu, ikiwemo wazee na watoto walio chini ya miaka mitano. Hawa wote wanategemea fedha za matibabu kutoka Serikalini ambazo haziletwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna mtoto aliyepata matibabu ya kunyooshwa mgongo wake kwa sababu ulipinda. Mgonjwa huyu alipatiwa matibabu kwa kuwekewa vifaa tiba 12 ambapo kila kimoja gharama yake ni dola 60 ambayo ni sawa sawa na 132,000, jumla ya vifaa tu ni shilingi 1,584,000. Gharama hii ni vifaa tuu ambapo kwa mujibu wa sera, mgonjwa huyu anatakiwa apewe matibabu

bila ya malipo yoyote. Sasa je ni wagonjwa wangapi wa namna hii wanaolipiwa na hawatalipiwa katika taasisi? Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inapeleka fedha hizo katika Taasisi ya MOI kabla hatujamaliza bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifaa tiba Muhimbili, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 4,000,000,000. Hadi Kamati inatembelea kulikuwa hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa ajili ya kununua vifaa tiba kama ilivyokuwa imepangwa, hivyo kupelekea hospitali kushindwa kutekeleza ununuzi wa vifaa tiba. Aidha, pamoja na kutopokea fedha hizo za maendeleo kutoka Serikalini bado hospitali hii ilihitaji kuendelea kutoa huduma kwa wahitaji wagonjwa, hivyo ilipelekea hospitali kutumia fedha zake za ndani, fedha kutoka kwa wahisani pamoja na mikopo kutoka *NHIF* zaidi ya shilingi bilioni 7.8 yenye riba nafuu ili kuendesha shughuli za hospitali ikiwemo ukarabati wa wodi na vyumba vya upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na hali hii kwani Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ni hospitali kongwe nchini na ndiyo hospitali inayotegemewa na Taifa. Wagonjwa kutoka sehemu mbalimbali nchini wamekuwa wakipelekwa kupata rufaa Muhimbili ili kupata huduma na idadi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano mwaka 2015 wagonjwa 191,241 walihudumiwa Muhimbili, mwaka 2016 wagonjwa 238,000 walihudumiwa, sawa na ongezeko la asilimia 20. Ongezeko hili la wagonjwa wakiwemo wagonjwa wanaopata huduma bila malipo kwa mujibu wa sera wa kiwemo Watoto chini ya umri wa miaka mitano na Wazee lilihitaji uwepo wa rasilimali fedha za kutosha ili kuweza kuwa hudumia. Serikali lazima iamue kutoa kipaumbele kwenye huduma za afya ili kulinda wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa ununuzi wa mitambo katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa (*NIMRI*); katika majadiliano na uchambuzi wa bajeti ya mwaka 2016/2017 Kamati ilikubaliana na Kamati ya Bajeti pamoja na Wizara

kwamba ifanye uhamisho wa fedha kutoka katika vifungu vingine, Fungu namba 52 (*Re-allocation*) ili iweza kuipatia Taasisi ya utafiti ya magonjwa ya binadamu (*NIMRI*) kiasi cha shilingi 800,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo. Hadi siku Kamati inakwenda kufanya ukaguzi wa maendeleo wa miradi hiyo hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe inapeleka fedha shilingi 800,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ili Taasisi ianze utekelezaji wa dawa za asilia kabla mwaka huu haujaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa makadirio 2017/2018; pamoja na malengo mengi ambayo Wizara kupitia Fungu 52 na 53 imeyapanga malengo haya yanaonekana kuwa yana tija katika suala zima la uboreshaji wa sekta za afya kwa kuzingatia mipango mikakati mbalimbali pamoja na makubaliano ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara hii yenye mafungu mawili inatarajia kukusanya maduhuli yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 52 inatarajia kukusanya shilingi bilioni 245.038 ikiwa ni ongezeko la shilingi 87,000,000,000 sawa na asilimia 35 ya kiasi cha shilingi 157,000,000,000 zilizokadiliwa kwa mwaka 2016/2017. Ongezeko hii ni kutokana na uimarishaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na utoaji wa huduma za afya katika vituo vyote vya kutolea huduma. Katika Fungu 52 Wizara inakadiria kukusanya shilingi 2,000,000,000 ikiwa ni pungufu ya shilingi 280,000,000, sawa na asilimia 11.8 kiasi cha shilingi bilioni 2.3 kilichotakiwa kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 52 imepanga kutumia shilingi 1,078,754,221,478 ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 291.9 sawa ya asilimia 27 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikiwa ni pamoja na mishahara na watumishi. Aidha, shilingi bilioni 786.8, sawa

na asilimia 73 kinachoombwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, na hapa tunawapongeza sana Wizara kwa kutenga fedha nyingi kwa ajili ya fedha za maendeleo.

Kwa upande wa Fungu 53 Wizara imepanga kutumia shilingi 40,000,000,000, kati ya fedha hizo shilingi 4,000,000,000 sawa na asilimia 12 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, 35,000,000,000 sawa na asilimia 88 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio haya ya matumizi ya fedha yanaonyesha kuongezeka kwa asilimia 25.9 hasa kwa Fungu 52 kwa mwaka 2017/2018 ikilinganishwa na makadirio ya matumizi ya mwaka 2017/2018. Pamoja na kuongezewa fedha, Kamati inajiuliza je, bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha iliyopokelewa mpaka sasa sawa na asilimia 50 je, asilimia hizi 73 zitaweza kupatikana kwa ajili ya mwaka kesho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ya taarifa inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Mwaka 2016/2017 Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 796,000,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Hata hivyo hadi kufika mwezi Machi Wizara ilipokea kiasi cha shilingi 314,000,000,000, sawa na asilimia 40 tu ya fedha ambazo zilitakiwa kupokelewa na Wizara hii. Kamati inahoji ni lini sasa Serikali itatekeleza haya ambayo yalitakiwa yatekelezwa kwa mwaka 2016/2017 kwani sasa tunaelekea mwaka mwingine wa fedha, ni vyema sasa Serikali ikajipanga na kuhakikisha bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge inatolewa yote kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya afya; katika bajeti ya mwaka 2017/2018 iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Fungu 52 na 53 inaonekana kuongezeka kwa asilimia karibia 30. Hata hivyo bajeti hii bado haijafanikiwa kufika asilimia 100 ya bajeti nzima ambayo imetengwa kwa asilimia 10 ya bajeti nzima ambayo imetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Afya. Bajeti ya mwaka wa Wizara hii ni sawa na asilimia 3.5 tu ya bajeti ya Serikali ya

trilioni 31.9. Bajeti hii ni ndogo kwani bado hatujatekeleza makubalino ya Mkutano wa Azimio la Abuja (*Abuja declaration*) ya mwaka 2001 ya kwamba nchi zipange asilimia 15 ya Bajeti kwenye sekta ya afya. Kamati inaona imefika wakati sasa Serikali ikaamua kwa dhati kulipa kipaumbele suala afya na kutenga Bajeti ya kutosha, angalau kufika asilimia 10 ya Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bima ya Afya kwa Mtanzania; katika kutekeleza ahadi kwa wananchi ni lazima kuangalia suala la afya katika mapana yake, hasa kwa kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anakuwa na uhakika wa kupata huduma za afya wakati wowote mahali popote inapohitajika. Kutokana na hali hii, Kamati inatoa ushauri kwamba Serikali ilipe kipaumbele cha pekee suala zima la bima ya afya kwa Watanzania ili ijiwekee malengo ambayo yanaambatana na mpango kazi wa kutekeleza azma hiyo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa fedha kutoka kwa wahisani - Bajeti ya Wizara ya Afya imekuwa ikitegemea sana fedha kutoka kwa wahisani. Madhalani mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ilitegemea fedha kutoka kwa wahisani zaidi ya asilimia 59.8 ya Bajeti nzima ya maendeleo ambapo hadi kufika mwezi Machi ni asilimia sita tu ya fedha iliyotengwa na wahisani ilikuwa imetolewa kwa ajili ya shughuli hiyo. Pamoja na kutopatikana kwa fedha hizo kutoka kwa wahisani bado Wizara imeendelea kutenga asilimia 94 ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa kutegemea kwa wahisani, ambao ni sawa na asilimia 57.2 ya bajeti nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imerejea baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo inategemea wafadhili kutoka nje kwa asilimia 100. Miradi hiyo ya maendeleo ni pamoja Udhhibiti wa Virusi vya UKIMWI (*HIV/Aids Control Programme*) pamoja na Mradi wa Udhhibiti wa Kifua Kikuu. Kwenye miradi hii hakuna hata shilingi moja ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya usimamizi wa utekelezaji wa magonjwa haya. Kamati inajiuliza, je, magonjwa haya ni kipaumbele katika

kupambana nayo hapa nchini? Au je, Serikali imeamua kutoa reheni ya afya za wananchi katika magonjwa haya ambayo ndiyo kati ya magonjwa yanayowasumbua wananchi wa Tanzania bila kujali umri, dini, cheo, itikadi wala siasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha katika masuala haya pamoja na miradi mingine ya maendeleo ili iache kutegemea fedha za wahisani na wafadhili wa nje kwa ajili ya kuokoa maisha ya Watanzania kama wafadhili hawataleta fedha hizo kwa mwaka 2016/2017 basi tuwe na miradi endelevu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vifaa tiba na vilainishi; uotoaji wa huduma bora nchini ni pamoja na uwepo wa vitendea kazi katika vituo vya huduma za afya. Kumekuwa na malalamiko ya upungufu wa dawa vitendanishi, vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha itakayotosha kununua vifaa hivi na kuvisambaza katika vituo vyote vya kutolea huduma hapa Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jamii kumekuwa na makundi mbalimbali ambayo yapo katika mazingira magumu likiwemo kundi la watoto yatima ambalo linatokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo vitokanavyo na ugonjwa wa UKIMWI.

Katika kuhakikisha kwamba kundi hili linapata huduma za afya kama walivyo watoto wengine, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha leseni zinapatikana kwa urahisi ili hawa wanaojitolea kutoa huduma hizi za watoto yatima wasikate tamaa, kwani juhudi hizi zote ni kwa ajili ya kuisaidia Serikali pale ambapo inaonekana imeelemewa na jukumu la kutunza watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutenga fungu kwa ajili ya msamaha wa matibabu, nchi yetu imetengeneza sera nzuri sana, sera ya mwaka 2007 ambapo katika sera hiyo imeanishwa bayana makundi ambayo yamepewa

msamaha wa gharama ya matibabu, likiwemo kundi la watoto wa umri wa miaka tano, wajawazito pamoja na wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera hii imegeuka kuwa changamoto kwa taasisi zinazotoa huduma za afya kwa makundi haya na kupelekea kuwa kero kwa makundi hayo na hata kwa taasisi husika inayotoa huduma kwa kuwa na uhaba wa rasilmali fedha kwa ajili ya kununua dawa pamoja na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kupewa taarifa kwamba, kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2015 zaidi ya shilingi bilioni 1.6 ilitoka kwa ajili ya watoto hawa ambao ni kwa ajili ya msamaha. Mwaka wa fedha 2016/2017 Taasisi ya Mifupa - MOI ilitoa huduma kwenye zaidi ya Mikoa 18 Tanzania Bara na Zanzibar kwa watoto 2,200 na kati ya watoto hao wenye vichwa vikubwa walipata huduma ya upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha maalum (*separate vote*) ambayo ni kwa ajili ya kutoa huduma bora ya afya kwa ajili ya msamaha wa gharama za matibabu ili kuweza kuwa na gharama endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Taasisi ya Jakaya Kikwete. Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete imekuwa ikitoa huduma ya matibabu ya moyo kwa Watanzania. Taasisi hii imetoa huduma kwa mazingira magumu sana. Kamati inashangazwa na kitendo cha taasisi inayookoa fedha nyingi kwa kutopeleka wagonjwa nje lakini bado fedha zinazoombwa hazipelekwi katika Taasisi hiyo. Kamati inaishauri bajeti ya *JKC* itolewe yote na kwa wakati ili iweze kusaidia kuoko fedha nyingi ambazo zingetumika kupeleka wagonjwa kwenye matibabu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ripoti ya ukaguzi wa Benki ya Wanawake, Kamati inaishauri Serikali kupitia Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuifanyia ukaguzi wa kimahesabu benki hii ili kubaini kiasi cha mtaji wake, nini kikwazo cha

benki hiyo kutokuwa kama benki nyingine, na kuna namna gani inaweza kuibuliwa kwa kukuzwa ili kuweza kushindana na benki nyingine kwa ajili ya kuwasaidia wanawake Wakitanzania lakini pamoja na wanaume kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utoaji wa zabuni za utoaji huduma katika Taasisi ya Afya Muhimbili. Utoaji wa huduma ya afya katika taasisi kubwa kama vile Muhimbili imekuwa ni changamoto kubwa kutokana na uhaba wa vifaa, vifaa tiba, dawa na vitendanishi kama nilivyoeleza hapo awali. Aidha, upungufu huo unapelekea kuwa na msongamano mkubwa katika sehemu ya vipimo vya wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hiyo ya ugumu wa upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya vipimo na dawa; kutokana na taasisi kukosa fedha za kununulia vifaa na dawa, Kamati inaishauri Serikali kuruhusu huduma hizo za vipimo na dawa zitolewe na mzabuni wa nje (*Taasisi Service Outsourcing*) ambaye ataweza kuwekeza katika maeneo hayo; ambapo mbia huyo ataleta vifaa vyake kwa ajili ya upimaji wa wagonjwa mbalimbali lakini pia utoaji wa dawa kwa wagonjwa katika taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri hivyo kwa kuwa kuna faida kubwa katika kutekeleza hayo. Kwanza itapungumza mzigo mkubwa wa Serikali na Taasisi hiyo katika suala zima la ukarabati (*maintenance*) wa vifaa hivyo, itapunguza shughuli ya uagizaji wa dawa katika Taasisi hiyo, pia hata teknolojia ya vifaa itabadilika kwa kuwa jukumu la mzabuni huyo litakuwa ni hubadilisha na kwamba jukumu halitakuwa la Serikali tena kama ilivyo sasa. Hii itaifanya nchi yetu kuendana na mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea katika ulimwengu wa suala zima la afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kutopelekwa kwa fedha zilizotengwa kwa mradi wa maendeleo, tunaomba sana Serikali fedha hizo zinazotengwa za maendeleo ziweze kwenda kwa wakati. Vyuo vya Maendeleo

ya Jamii vipelekwe Wizara ya Elimu, Kamati inashauri vyuo hivyo vyote vilivyo chini ya Fungu namba 53 vihamishiwe na kupelekwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ilivyo vyuo vikuu vingine hapa nchini. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kufuatilia ubora wa elimu itolewayo na vyuo hivyo vya maendeleo ya jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bohari Kuu ya Dawa, Kamati inashauri Bohari hiyo kufanyiwa ukaguzi wa kina kwa ajili ya kubaini, mafanikio (*strength*), changamoto (*challenges*) na mahitaji (*demands*) ili kuweze kubaini namna ya kuboresha usambazaji wa dawa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Ndoa na ndoa za utotoni, Kamati inaishauri Serikali pamoja na ugumu unaojaribu kuwekwa na taasisi za kidini, na mila na desturi za mahali husika, Kamati inaamini Serikali ina mamlaka juu ya kulinda haki na ustawi wa jamii zetu, hasa kulinda haki za watoto hapa nchini. Serikali ilinde haki za watoto hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza idadi ya makundi maalum; makundi maalum yanajumuisha watu wanaojidunga dawa za kulevya, wanaofanya biashara ya ngono, wanaofanya mapenzi ya jinsia moja (*men who sex with the men; the women who sex with the women; and trans gender*). Makundi haya yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku katika jamii yetu. Imekuwa ni tishio kubwa hasa katika suala zima la ongezeko la virusi vya UKIMWI.

Ongezeko la kundi hili ni kutokana na mabadiliko ya jamii yetu ikiwemo suala zima la malezi katika ngazi za familia, shuleni na katika jamii kwa ujumla. Matendo haya yamekuwa yakifanyika majumbani mwetu, shuleni kutwa, hata mabwenini kwetu. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inaajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii, katika kila kata, ambao watasaidia kutekeleza mambo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifo vya akina mama, Kamati inaishauri Serikali kuwanusuru akina mama hawa

katika matatizo ya uzazi na kuwatengea na kutoa fedha za kutosha katika bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za Bima ya Afya (NHIF); Kamati inaishauri Serikali kuupa muda Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa kujiandaa vyema ili uweze kutoa huduma bora kwa wateja wake ili hata mashirika hayo yajiunge nayo, tofauti ya upatikanaji wa huduma walizokuwa wanapata kabla ya kujiunga katika mifuko mingine ya bima ya afya. Kwa kufanya hivyo kutaondoa malalamiko, pia kuwapa uwezo kuendana na soko la utoaji wa huduma za afya kama mifuko mingine inavyotoa huduma za afya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa vituo vya afya; Kamati inaishauri Serikali kwa ujumla wake kuhakikisha vituo vya afya vinajengwa vya kutosha ili kusaidia kutoa huduma za afya hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TFDA* Kamati inaishauri Serikali izianganalie Sheria zinazounda taasisi hizi ambazo zinaainisha majukumu hayo pale kwenye tatizo linapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vikwazo katika msaada kwa wahisani, Kamati inaishauri Serikali kupitia *TFDA* ifanye jukumu lake bila kutoza kiasi chochote kwa Wizara kwani hilo ndilo jukumu ambalo limepangiwa katika vajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magonjwa yatokanayo na kukosekana kwa matumizi bora ya vyoo na maji na salama; Kamati inashauri Serikali ihimize ujengaji wa vyoo nchini pamoja na kuhakikisha kwamba Wizara ya Afya inatoa maji katika vyoo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia

Wazee na Watoto, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (Mbunge) pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati hasa Kamati ilipokuwa ikijadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Vilevile napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara, Idara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wazee pamoja na Maafisa Waandamizi wao, Wizara na Taasisi zote kwa ushirikiano wanaotoa katika Kamati yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru wadau wetu wote wa sekta ya afya kwa kazi nzuri wanayoifanya, kwa ushirikiano wao mkubwa wanautoa kwa Serikali yetu katika kuendelea kutoa huduma bora za afya hapa nchini. Naomba kuwataja baadhi na wachache tu ambao wanatoa huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *TGNP, Tanzania Women Lawyers (TAWLA), Shirika la Utepe Mwekundu, Tanzania Health Promotion (HDT), Tanzania Water and Sanitation Network* na Mashirika mengine Yasiyo ya Kiserikali kwa juhudi wanazoendelea kufanya hapa Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee kabisa naomba niwashukuru wajumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua makadirio na mapato ya matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2017/2018. Pamoja na ufinyu wa muda walikuwa tayari kutekeleza jukumu hili kubwa na hatimaye kukamilisha uchambuzi wa bajeti hii kwa weledi mkubwa na kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Dkt. Thomas Kashilillah Katibu wa Bunge, Ndugu Athumani Hussein Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zao

vizuri. Kipekee kabisa naomba niwashukuru Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Agnes Nkwela Makatibu wa Kamati yangu na ndugu Gaitana Chima kwa msaada wao mkubwa katika Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto na Taasisi zake kwa mwaka 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. Fungu 52 jumla ya shilingi 1,078,344,282,000; Fungu 53 jumla ya shilingi bilioni 40,130,215,784.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa taarifa uliyowasilisha kwa niaba ya Kamati yako, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWAMWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 6(5)(a) na 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Bajeti ya Wizara hii. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni hizo, Kamati hii inao wajibu pia wa kushughulikia Bajeti ya kila Mwaka ya Wizara hii.

Vile vile, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyopo chini ya usimamizi wa Kamati hii ambazo ni tatu (3) ikiwemo Wizara hii.

Naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ilifanya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha chini ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kufanya Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo ni Fungu 52- Idara Kuu ya Afya na Fungu 53- Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, naomba kutoa taarifa hii ambayo inafafanua mambo manne (4) yafuatayo:-

- i. Hali halisi katika Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka unaoisha;
- ii. Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo

- iii. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na
- iv. Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI KATIKA MASUALA MBALIMBALI

2.1 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kufanya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilifanya Mapitio ya Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha Bajeti ya Mwaka 2016/2017. Jumla ya Mapendekezo Ishirini na mbili (22) yalitolewa.

Mheshimiwa Spika, Katika Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati iliyopita, yapo maoni yaliyoweza kutekelezwa kikamilifu, yanayoendelea kutekelezwa na ambayo hayajatekelezwa kabisa na Wizara. Katika ushauri uliotekelezwa, Kamati inaipongeza Serikali na Wizara kwa jitihada hizo na yale ambayo yanaendelea kutekelezwa Kamati inaiomba Wizara kuendelea kusimamia ili yatekelezwe kama ilivyoshauriwa. Na yale ambayo hayajatekelezwa kwa sababu ya kutopata Fedha toka Serikalini Kamati inaiagiza Wizara kufuatilia Fedha hizo na kuyatekeleza mara moja kabla ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 haujamalizika. **(Rejea Kiambatisho Namba 1).**

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 kadiri

zilivyokuwa zimepangwa katika kutekeleza majukumu yake. Kamati ilijikita katika kufanya Uchambuzi wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 katika kikao kilichofanyika **tarehe 31 Machi na 1 Aprili 2017** kwa kufanya mapitio katika taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati wakati wa kujadili taarifa za utekelezaji pamoja na taarifa zilizowasilishwa wakati wa vikao vya Kamati katika kutekeleza shughuli za Kamati kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya mapitio ya mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha unaofuata wa 2017/2018 ili kuona mwenendo wake.

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedhawa 2016/2017, Wizara ilikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi **Bilioni 170.01** kutoka **Fungu 52 (Idara Kuu Afya)**, hadi kufikia mwezi Machi 2017 Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi **Bilioni 157.801** sawa na **asilimia 75.48**.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Fungu 53- Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**, ilikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi **Bilioni 2.38**, hadi kufikia mwezi Machi 2017 Idara hii imekusanya kiasi cha shilingi **Millioni 930.28** sawa na **asilimia 39.04** ya lengo.

Mheshimiwa Spika, hadi Kamati inakutana na Wizara hakuna hata Fungu moja ambalo limekamilisha ukusanyaji wa Maduhuli kwa asilimia 100. Kamati inaamini kwamba kwa muda uliobaki **Idara Kuu Afya (Fungu 52)** itaweza kukamilisha Makadirio ya Makusanyo yao kadiri ilivyojiwekea malengo yake, kwani hadi kufikia mwezi Machi 2017 Idara Kuu hii ilifanikiwa kwa zaidi ya **asilimia 75**.

Aidha, kwa upande wa **Fungu 53 Idara Kuu Maendeleo ya Jami**impaka wakati Kamati inapokea taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2016/2017, makusanyo hayajafika hata nusu ya lengo kwa maana ya asilimia 50. Hali hii imepelekea kupunguza makadirio ya makusanyo ya mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa **asilimia 13** kwa sababu zilezile zilizoainishwa mwaka uliopita kwa maana ya kupungua kwa makusanyo ya ada kutoka kwa wanafunzi wa vyuo vyao kama chanzo kikuu cha makusanyo ya mapato yake. **Kamati inaitaka Wizara kuangalia tena Idara Kuu hii ili kuweza kubuni vyanzo vingine vya mapato yake na kuweza kugundua sababu zinazoipelekea Idara kuporomoka kwa kiwango cha Makadirio ya Mapato yake kila mwaka.**

Mheshimiwa Spika, Idara Kuu Afya inaendelea kufanya vizuri katika Makusanyo yake kwa kuweza kutekeleza Makadirio ya Makusanyo ya Mapato yake na kuweza kuongeza Makadirio ya makusanyo kila mwaka na Kamati inatambua juhudi hizo kubwa. **Kamati inaipongeza Wizara na Idara Kuu Afya kwa ufanisi huo mkubwa na kuiomba Wizara kutumia mbinu hizo katika Idara Kuu Maendeleo ya Jamii ili nayo iweze kupiga hatua mbele kutoka pale ilipo na kuweza kufanya Makusanyo makubwa zaidi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na hata miaka mingine ijayo.**

Kielelezo Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Fungu	Mwaka wa Fedha 2016/2017			Mwaka wa Fedha 2017/2018	
	Makadirio	Makusanyo	%	Makadirio	% Tofauti
52	Bilioni 170.011	Bilioni 157.801	75.48	Bilioni 245.038	+36
53	Bilioni 2.382	Milioni 930.281	39.04	Bilioni 2.101	-13

Chanzo: Taarifa ya Wizara kuhusu utekeleaji wa Majukumu kwa Mwaka 2016/2017

3.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa shughuli za Wizara katika kuboresha Afya na Ustawishaji wa Jamii nzima ya Watanzania unategemea upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini kwa

asilimia 100. Kamati ilifanya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa mafungu yote mawili (**52 & 53**) kabla ya kufanya Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa fedha katika Wizara haujawa wa kuridhisha kwani fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Machi 2017 hazijafika hata **asilimia 50**. Katika **Fungu 52** hadi kufikia mwezi Machi 2017 ni kiasi cha shilingi **Bilioni 314.67 sawa na asilimia 40** kati ya shilingi **Bilioni 796.11** kilichokuwakimeidhinishwa na Bunge lako Tukufu kilikuwa kimepatikana. Aidha, kuhusu **Fungu 53**, hadi kufikia mwezi Machi 2017 Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **Bilioni 16.23** sawa na **asilimia 39.57** kati ya kiasi cha shilingi **Bilioni 41.00** kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. (**Rejea Kielelezo Na. 2**)

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi huo, Kamati inaona kwamba utoaji wa fedha kwa ajili ya Wizara hii ni wa kusuasua kila mwaka licha ya kutengewa fedha kidogo kila lakini hata hicho kiasi kidogo kimekuwa hakitolewi hata kwa asilimia 50 kama siyo 75 kama ilivyo matarajio kwa watu wote ambao wanaona Afya ni kipaumbele katika nchi yoyote.


Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba Serikali hajaamua kulipa kipaumbele suala la Afya, kwanza kwa kutotenga fedha za kutosha katika Sekta hii na pili kwa kutotoa fedha za utekelezaji wa shughuli zake kwa wakati. Kamati inaona pia kwamba, hata mafanikio yanayopatikana katika Wizara hii ni kutokana na Uzalendo mkubwa walionao Watendaji Wakuu pamoja na wasaidizi wao kwa kutafuta vyanzo vingine vya fedha na siyo fedha au jitihada ambazo zinawekwa na Serikali kwa ajili ya uboreshaji wa Afyaza Watanzania. Aliyekuwa Mpigania Uhuru na Baba wa Taifa la India Mahatma Gandhi aliwahi kusema **"It is Health that is real Wealth and not pieces of gold and silver"** hivyo Serikali haina budi kuhakikisha afya za Watanzania ndiyo kipaumbele kwani ndiyo utajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaisihi Serikali kuipa kipaumbele cha pekee Wizara hii kwa kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake zikiwemo shughuli za kutoa huduma za kuzuia magonjwa (*Prevention Services*), Matibabu (*Curative Services*) na hata uraghabishaji (*Promotion Services*). Kwa kutekeleza haya hatutalazimika kutenga fedha nyingi katika masuala ya dawa kwani magonjwa yatakayohitaji dawa yatakuwa tayari yamekwisha zuliwa na huduma za kinga.

Aidha, Kamati inashauri Serikali pia kuiangalia Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu 53) ili Idara hii iweze kutimiza wajibu wake wa kuifanya jamii istawi vilivyo ikiambatana na kutoa ajira ya kwa ajili ya Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa awaliKamati inaona kwamba Serikali kutokupeleka Fedha kwa wakati kunakwamisha Wizara katika kutekeleza majukumu yake.

Kielelezo: Na.2: Ulinganishwa Bajeti iliyochinishwa na kiasi cha Fedha Kilichopatikana



Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

3.2 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto-**Idara Kuu Afya Fungu 52**, ilitengewa kiasi cha **shilingi 518,511,683,780/=** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Kati ya fedha hizo **shilingi 320,134,600,000/=** sawa na asilimia **40.2** ni kutoka vyanzo vya ndani na kiasi cha **shilingi 198,377,083,780/=** kutoka vyanzo vya nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanikiwa kukagua jumla ya Miradi minne iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 licha ya ukweli kwamba Miradi iliyotengewa fedha ilikuwa 28. Ukaguzi wa Miradi hii michache ulitokana na ufinyu wa muda lakini pia uwezo wa kifedha. Miradi iliyokaguliwa na Kamati imeanishwa kwenye Taarifa hii.

3.2.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa awali, Kamati ilifanya ukaguzi wa jumla ya Miradi ya Maendeleo minne (4) iliyo chini ya Wizara hii ambayo ilitengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Miradi hiyo ni pamoja na:-

3.2.2 Mradi wa Ununuzi wa Mashine ya kupima ugonjwa wa Saratani katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* (ORCI)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya Ziara ya Ukaguzi wa Mradi huu mnamo tarehe 20 Machi, 2017. Mradi hu ulitengewa jumla ya shilingi **Bilioni 5** kwa ajili ya kununua mashine mpya na za kisasa za kutibu Saratani (*Linear Accelerator –LINAC* na *CT Simulator*). Gharama za mashine hizi zilikuwa ni shilingi **Bilioni 9.5** ambapo katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Taasisi ilitengewa shilingi **Bilioni 4.5** na zilishapokelewa.

Aidha, katika Mwaka huu wa Fedha 2016/2017, hadi kufikia siku Kamati inakagua mradi huu Taasisi ilikuwa imekwisha kupokea fedha zilizokuwa zimetengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 5** sawa na **asilimia 100** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kamati imejulishwa kuwa Taasisi imekamilisha kuandaa makabrasha ya Zabuni na mashine zinatarajiwa kufika nchini ifikapo mwezi huu wa Mei, 2017. ***Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa Mradi huu kwani utasaidia kupunguza msongamano wa Wagonjwa katika Taasisi hii wanaokwenda kupata matibabu ya Saratani, pamoja na hili, Kamati inasisitiza kuwa Taasisi chini ya usimamizi wa Wizara waharakishe mchakato wa manunuzi wa vifaa tiba hivyo ili iweze kuanza kutoa huduma ya haraka kwa wagonjwa wa Saratani.***

3.3.2 Mradi wa Ununuzi wa Mitambo na Vifaa Tiba katika Taasisi ya Mifupa (MOI) (Namba ya Mradi-5491)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Mradi huu siku ya tarehe 23 Machi, 2017. Mradi huu ulitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 4.8** ambapo kati ya fedha hizo shilingi **Bilioni 1.8**ni kwaajili ya kulipa mkopo NHIF na shilingi **Bilioni 3** ni kwaajili ya manunuzi ya mitambo na vifaa tiba. Hadi Kamati inatembelea MOI hakuna fedha iliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kwamba Taasisi ya MOI ni Taasisi nyeti sana kutokana na utoaji wake wa huduma ya mifupa na hususan kutokana na ongezeko kubwa la wahitaji wa huduma ya mifupa katika Taasisi hiyo. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa ajali kila siku hapa nchini zikihusisha magari, pikipiki na vyombo vingine vya moto ambavyo hupelekea watu kuvunjika viungo ambapo mwisho wa siku huduma yake hupatikana katika Taasisi ya MOI.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa sana na hali hii ya kutotolewa fedha kwani MOI ni moja ya Taasisi muhimu sana nchini na ndiyo Taasisi pekee inayotoa tiba ya mifupa hapa nchini. Taasisi hii inatumia mapato yake ya ndani kwa ajili ya kununua vifaa tiba na kutoa huduma kwa ajili ya wananchi. Pia ikumbukwe kwamba, kuna kundi ambalo limepewa msamaha katika gharama za matibabu wakiwemo wazee na watoto walio chini ya miaka mitano (5) hawa wote wanategemea fedha za matibabu kutoka Serikalini ambazo haziletwi kabisa. Mfano kuna mtoto aliyepata matibabu ya kunyooshwa mgongo wake kwa sababu ulipinda, mgonjwa huyu alipatiwa matibabu kwa kuwekewa vifaa tiba 12 ambapo kila kimoja gramama yake ni **dola za Kimarekani 60 (60 USD)** ambayo ni sawa na **shilingi 132,000/=** na jumla ya vifaa tu ni **shilingi 1,584,000/=**, gharama hii ni vifaa tu ambapo kwa mujibu wa sera mgonjwa huyu anatakiwa apewe matibabu bila ya malipo yoyote. Sasa je ni wagonjwa wangapi wa namna hii hata wale wanaolipa wanatibiwa katika Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inapeleka fedha hizo katika Taasisi ya MOI kabla ya Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 haujaisha.

3.3.3 Mradi wa Ununuzi wa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Mradi huu mnamo tarehe 23 Machi, 2017. Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi **Bilioni 4**. Hadi Kamati inatembelea kulikuwa hakuna fedha yoyote iliyopokelewa kwa ajili ya kununua Vifaa tiba kama ilivyokuwa imepangwa. Hivyo kupelekea Hospitali kushindwa kutekeleza ununuzi wa vifaa tiba hivyo.

Aidha, pamoja na kutopokea fedha hizo za maendeleo kutoka Serikalini bado Hospitali ilihitaji kuendelea kutoa huduma kwa wahitaji (Wagonjwa) hali iliyopelekea Hospitali kutumia fedha zake za ndani, fedha kutoka kwa Wahisani, pamoja na mkopo kutoka NHIF kiasi cha shilingi **Bilioni 7.89 (wenye riba nafuu)** ili kuendesha shughuli za hospitali ikiwemo ukarabati wa wodi na vyumba vya upasuaji.

Kamati imesikitishwa na hali hii kwani Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ni Hospitali kongwe nchini na ndiyo Hospitali kubwa inayotegemewa na Taifa. Wagonjwa kutoka sehemu mbalimbali nchini wamekuwa wakipewa rufaa kuja Muhimbili kupata huduma na idadi yao imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano Mwaka 2015 jumla ya wagonjwa 191,241 walihudumiwa ikilinganishwa na Mwaka 2016 ambapo wagonjwa 238,026 waliohudumiwa sawa na ongezeko la wagonjwa 46,785 sawa na asilimia 20. Ongezeko hili la wagonjwa wakiwemo wagonjwa wanaopata huduma bila malipo kwa mujibu wa Sera wakiwemo watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) na wazee linahitaji uwepo wa rasilimali fedha za kutosha ili kuweza kuwahudumia. Serikali lazima iamue kutoa kipaumbele kwenye huduma za afya nchini ili kuwalinda wananchi wake.

3.3.4 Mradi wa Ununuzi wa Mitambo katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)

Mheshimiwa Spika, Katika majadiliano ya Uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 Kamati ilikubaliana na Kamati ya Bajeti pamoja na Wizara kwamba ifanye uhamisho wa fedha kutoka katika vifungu vingine ndani ya Fungu 52 (*Re-allocation*) ili iweze kuipatia Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kiasi cha shilingi **Milioni 800** kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kutengeneza dawa zitokanazo na miti dawa.

Mheshimiwa Spika, Mpaka kufikia siku Kamati inakwenda kufanya ukaguzi wa maendeleo ya mradi, hakuna fedha yoyote iliyokuwa imepelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati inahoji Serikali, je kwanini hakuna fedha iliyopelekwa katika mradi huu? Je, ni kwa kuwa utengenezaji wa dawa asilia hauna umuhimu katika afya za wananchi wetu, au ni nini kinapelekea Serikali kutoupa kipaumbele mradi huu wa ununuzi wa mitambo ya utengenezaji wa dawa asilia.

Mheshimiwa Spika, *Kamati inashauri Serikali ihakikishe inapeleka fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 800 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ili Taasisi ianze utengenezaji wa dawa hizo asilia kabla ya Mwaka huu wa Fedha 2016/2017 haujaisha.*

3.3 Matokeo na Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa awali kwamba Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi minne kati ya Miradi 28 iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kutokana na hali iliyoikuta kwenye Miradi hiyo, Kamati inatoa Ushauri ufuatao:-

i) Kamati inashauri Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa kwaajili ya ununuzi wa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Ikumbukwe kwamba hii ni Hospitali

ya Taifa ambayo Rufaa zote nchini zinaelekezwa katika Hospitali hii. Kutoipa fedha za maendeleo ni kuirudisha nyuma kimaendeleo. Hadi siku Kamati inaitembelea Taasisi hii hakuna fedha iliyopelekanakulazimu Taasisi hii kutekeleza shughuli zake kwa kutumia fedha zake za ndani.

ii) Kamati inashauri Serikali kuipa dhamana Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ajili ya kukasimisha huduma nyingine kwa wadau wengine wa afya (*Services Outsourcing*) ikiwemo huduma za dawa pamoja na vipimo, ambapo ulimwengu wa sasa ndicho kinachofanyika katika Sekta ya afya. Kwa kufanya hivyo, Taasisi itaondokana na masuala mazima ya ukosekanaji wa Dawa na hata kufanya matengenezo ya vifaa vya upimaji wa magonjwa mbalimbali.

iii) Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha za maendeleo kiasi cha shilingi **Bilioni 4.8** kwa ajili ya ununuzi wa Vifaa Tiba katika Taasisi ya Mifupa MOI ili kuiwezesha Taasisi hiyo kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi, kwani hadi Kamati inaitembelea Taasisi hiyo hakuna hata shilingi moja iliyokuwa imekwisha pelekwa na Serikali. Ikumbukwe kwamba kuna kundi kubwa la watu ambao wanatibiwa bila malipo kwa mujibu wa Sera ya Afya (Wazee na Watoto) ambapo unakuta vifaa vyake ni gharama kubwa sana hali inayopelekea Taasisi kubebe mzigo mkubwa ambao ungeweza kutekelezwa kwa fedha zilizotengwa na Serikali na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

iv) Kamati inashauri Serikali ihakikishe inasimamia vyema Taasisi ya Saratani ya ***Ocean Road*** katika uharakishaji wa mchakato wa ununuzi wa Vifaa Tiba ambavyo vimepatiwa fedha kiasi cha shilingi **Bilioni 5** ili kuepuka usumbufu utakaotokana na mabadiliko ya thamani ya fedha (***Inflation***). Aidha, kuharakisha kwa mchakato huo kutapelekea upatikanaji wa vifaa tiba hivyo kwa haraka ambako kutatatua msongamano wa wagonjwa wanaohitaji huduma ya matibabu ya mionzi katika Taasisi ya ***Ocean Road***.

v) Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu kiasi cha shilingi **Milioni 800** zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Ununuzi na Ufungaji wa mitambo ya kutengeneza dawa zitokanazo na Miti Dawa ili Taasisi hiyo iendelee kuzalisha Dawa hizo zinazogundulika kutokana na Utafiti wao. Aidha, Kamati inashauri pia kuongeza eneo la kujenga kiwanda hicho cha utengenezaji wa Dawa asilia kwani sasa hivi kipo katikati ya makazi ya watu (**Mabibo External**) ambapo Kamati inaona ni eneo dogo na linaweza kuleta usumbufu hapo mbeleni kama Taasisi hiyo itakua katika uzalishaji wa dawa asilia.

vi) Kutokana na Serikali kupeleka fedha za maendeleo kiasi cha shilingi **Bilioni 133.872** sawa na **asilimia 25.82** tu (Fungu 52) nakiasi cha shilingi **Milioni 204.217** sawa na **asilimia 2** tu (Fungu 53) ya kiasi kilichopangwa, Kamati inashauri Serikali kupeleka fedha katika miradi yote iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 angalau kwa **asilimia 50** hadi ifikapo tarehe 30 June, 2017 ili Miradi hiyo ianze kutekelezwa.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Wizara inatarajia kutekeleza malengo mbalimbali katika Mwakawa Fedha 2017/2018 kwa **Fungu 52 & 53**. Kati ya Malengo hayo ni pamoja na;

1. Kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake Kiuchumi
2. Kuimarisha upatikanaji wa haki na huduma za Ustawi wa Jamii kwa Wazee na Watoto
3. Kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto wa Mwaka 2017/2018-2021/2022

4. Kusimamia Sera ya Afya na kutoa huduma za Kinga na Tiba
5. Kuendesha ukaguzi wa wa huduma za afya zitolewazo katika ngazi mbalimbali
6. Kuandaa na kusimamia mpango wa mafunzo ya wataalamu wa afya na kuwaendeleza kitaaluma watumishi wa sekta ya Afya
7. Kuinua kiwango cha ushirikiano kati ya Wizara, Sekta binafsi, Idara mbalimbali na kuimarisha ubora wa huduma za Afya
8. Kuratibu, Kutekeleza na kusimamia masuala ya lische nchini
9. Kuendesha utafiti wa magonjwa ya binadamu na kutumia matokeo hayo kwa manufaa ya wananchi
10. Kuongoza na kusimamia Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara-Afya

Mheshimiwa Spika,Pamoja na malengo mengi ambayo Wizara kupitia Fungu 52 na 53 imeyapanga, Malengo hayo yameonekana kuwa yana tija katika suala zima la uboreshaji wa Sekta ya Afya kwa kuzingatia Mipango Mikakati mbalimbali pamoja na makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa Huduma ya Afya nchini. Malengo ambayo Wizara inatarajia kutekeleza ni yale ambayo yameainishwa katika miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Muda Kati 2016/2017-2020/2021, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017-2020/21), Malengo ya Maendeleo Endelevu (***Sustainable Development Goals 2030***), Sera ya Afya (2007) Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2015-2020). Aidha, Malengo haya yote yanalenga katika kuhakikisha kuwa huduma za afya zenye

uwiano wa kijiografia, viwango vya ubora wa hali ya juu, gharama nafuu lakini pia huduma ambazo ni endelevu. Kwa kutekeleza Malengo haya ya Afya kutapelekea kuwa na jamii yenye afya bora na Ustawi wa Jamii ambao utachangia kupelekea Jamii iliyo bora katika Ustawi wa jamii kwa ujumla.

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara hii ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye mafungu mawili inataraji kukusanya maduhuli yake kama ifuatavyo:- Kwa upande wa **Fungu 52** (Idara Kuu Afya) inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi **245,038,495,525/=** ikiwa ni ongezeko la **shilingi 87,237,111,159/=**, sawa na **asilimia 35** ya kiasi cha shilingi **157,801,384,366/=** zilizokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Ongezeko hilo ni kutokana na uimarishaji wa mifumo ya ukusanyaji wa Mapato yatoanayo na utoaji wa Huduma za afya katika vituo vyote vya kutolea huduma.


Mheshimiwa Spika, Katika Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) Wizara inakadiri kukusanya kiasi cha **shilingi 2,101,874,000/=** ikiwa ni pungufu kwa shilingi **280,805,000/=**, sawa na **asilimia 11.8** ya kiasi cha **shilingi 2,382,679,000/=** kilichokadiriwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 52 (Idara Kuu Afya) imepanga kutumia kiasi cha **shilingi 1,078,754,221,478/=** ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Idara Kuu Afya. Kati ya fedha hizo kiasi cha **shilingi 291,932,052,000/=** sawa na **asilimia 27** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ikiwa ni pamoja na Mishahara ya Watumishi. Aidha, kiasi cha **shilingi 786,822,169,478.62/=** sawa na **asilimia 73** kinaombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto), Wizara imepanga kutumia kiasi cha **shilingi Bilioni 40,130,215,784/=**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi **4,829,613,784/=** sawa na **asilimia 12** ni kwa ajili Miradi ya Maendeleo na **shilingi 35,300,602,000/=** sawa na **asilimia 88** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Kielelezo Na. 3: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018



Chanzo: Randama ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Makadirio haya ya Matumizi ya Fedha yanaonesha kuongezekakwaasilimia **25.9** hasa kwa Fungu 52 kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ikilinganishwa na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. **Kamati inaona kwamba pamoja na Fungu hili kuongezewa fedha, Kamati inaona haina tija sana kwani hata Bajeti ya**

Mwaka wa Fedha unaoisha imepelekwa chini ya asilimia 50. Kamati inajiuliza kama kiasi kidogo cha mwaka uliopita hakikwenda, je kiasi hiki chenye ongezeko la asilimia 25.9 kitakwenda?

SEHEMU YA TATU

5.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua fursa hii kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 katika maeneo yafuatayo:-

5.1 Bajeti ya 2016/2017 haijatekelezeka kwa asilimia 60

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizarailitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 796.115** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zake. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30, Machi 2017 Wizara ilipokea kiasi cha shilingi **Bilioni 314.673** sawa na **asilimia 40** tu ya fedha zote ambazo zilitakiwa kuletwa katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, *Kamati inahoji ni lini sasa Serikali itatekeleza haya ambayo yalitakiwa kutekelezeka kwa Mwaka wa Fedha unaoisha (2016/2017) kwani sasa tunaelekea Mwaka wa Fedha mwingine? Ni vyema sasa Serikali ikajipanga na kuhakikisha Bajeti yote inayoidhinishwa na Bunge inatolewa yote na kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.*

5.2 Bajeti ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Fungu 52 &53 inaonekana kuongezeka kwa **asilimia 25.9**. Hata hivyo, bajeti hii bado haijafanikiwa kufikia hata **asilimia 10** ya bajeti nzima ya nchi ambayo imetengwa kwa ajili ya

utekelezaji wa shughuli za Wizara. Bajeti ya Mwaka huu ya Wizara hii ni sawa na **asilimia 3.5** tu ya Bajeti nzima ya Serikali ya shilingi **Trilioni 31.9**. Bajeti hii ni ndogo kwani bado haijatekeleza makubaliano ya Mkutano wa Azimio la Abuja (*Abuja Declaration, 2001*) ya kwamba nchi zipange **asilimia 15** ya Bajeti ya nchi kwenye Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ni wakati sasa Serikali ikaamuakwa dhati kulipa kipaumbele suala la Afya kwa kutenga Bajeti ya kutosha angalau kufikia asilimia 10 ya Bajeti Kuu ya Serikali.

5.3 Bima ya Afya kwa kila Mtanzania

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza ahadi kwa Wananchi wa Tanzania ni lazima kuangalia suala la afya katika mapana yake hasa katika kuhahakikisha kuwa kila Mtanzania anakuwa na uhakika wa kupata huduma za afya wakati wowote na mahali popote anapohitaji kuzipata.

Mheshimiwa Spika, suala la bima ya afya kwa wote si suala geni katika nchi za Afrika Mashariki, jirani zetu Rwanda wamefanikiwa katika suala hilo na hakuna mwananchi ambaye ana wasiwasi na suala la kupata huduma ya Afya iwapo atakosa fedha taslimu.

Kutokana na hali hii, Kamati inatoa ushauri kwamba Serikali iipe kipaumbele cha kipekee suala la bima ya afya kwa kila mtanzania na ijiwekee malengo ambayo yataambatana na Mpango kazi wa kutekeleza azma hiyo kwa Watanzania.

5.4 Kupungua kwa Fedha kutoka kwa Wahisani

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara ya Afya imekuwa ikitegemea sana fedha kutoka kwa Wahisani. Mathlani, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ilitegemea fedha kutoka kwa hisani kwa **asilimia 59.8** ya bajeti nzima ya Maendeleo ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2017, ni **asilimia 6** tu ya fedha iliyotegemewa na Wahisani ndiyo iliyotolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutopatikana kwa fedha hizo kutoka kwa Wahisani kwa **asilimia 94**, lakini bado bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 imeendelea kutegemea fedha kutoka kwa Wahisani hao hao kwa **asilimia 57.2** ya bajeti nzima.

Mheshimiwa Spika, Kamati imerejea baadhi ya Miradi ya Maendeleo ambayo inategemea ufadhili wa nje kwa **asilimia 100**, Miradi hiyo ya Maendeleo ni pamoja na Udhhibiti wa Virusi vya UKIMWI na UKIMWI (*HIV/AIDS Control Programme*), Mradi wa Udhhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma (*Support to TB/Leprosy Control Programme*), katika Miradi hii hakuna hata shilingi moja ya fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa magonjwa haya. Kamati inajaribu kuhoji Serikali je, magonjwa haya si ya kipaumbele katika kukabiliana nayo hapa nchini? Au je, Serikali imeamua kutoa rehani ya afya za wananchi katika magonjwa haya ambayo ndiyo kati ya magonjwa yanayosumbua wananchi wa Tanzania bila kujali umri, dini, cheo, itikadi za siasa wala za kidini.

Mheshimiwa Spika, *Kamati inashauri Serikali kutenga fedha katika masuala haya pamoja na Miradi mingine ya Maendeleo ili itekelezeke kwa kutegemea fedha za ndani badala ya kutegemea ufadhili wa nje kwa ajili ya kuokoa maisha ya watanzania hata kama Wafadhili hawataleta fedha zao kama mwaka huu (2016/2017) basi tuwe na miradi endelevu katika Wizara hii.*

5.5 Upungufu wa Vifaa, Vifaa Tiba, Vitendanishi na Dawa nchini

Mheshimiwa Spika, Utoaji wa huduma bora nchini ni pamoja na uwepo wa vitendea kazi katika vituo vya kutolea huduma ya afya. Kumekuwa na malalamiko ya upungufu wa dawa, vitendanishi, vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti inayotosheleza kuweza kununua vifaa hivi na kuvisambaza katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini.

5.6 Urasimu wa Upatikanaji wa Leseni kwa ajili ya Vituo vya kulelea Watoto Yatima

Mheshimiwa Spika, Katika jamii kumekuwa na makundi mbalimbali ambayo yapo katika mazingira magumu likiwemo kundi la watoto yatima ambao wametokana nasababu mbalimbali ikiwemo vifo vitokanavyo na ugonjwa wa **UKIMWI**. Jamii katika kuhakikisha kundi hili linapata huduma za jamii kama walivyo watoto wengine, kuna Mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotoa huduma hizi kwa watoto hao yatima. Changamoto kubwa ni katika upatikanaji wa leseni za kuanzisha vituo vya kuwalelea watoto hao ili wapate huduma umekuwa mgumu na wenye urasimu mkubwa.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha leseni hizi zinapatikana kwa urahisi ili wanaojitolea kutoa huduma hizo kwa watoto yatima wasipate kukata tamaa kwani juhudi hizi zote ni kwa ajili ya kuisaidia Serikali pale ambapo inaonekana kuelemea na jukumu la kuwatunza watoto hao.

5.7 Kutenga Fungu kwa ajili ya Msamaha wa Matibabu

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu imetengeneza Sera nzuri sana(Sera ya Afya 2007) ambayo katika Sera hiyo imeainisha bayana makundi ambayo yamepewa msamaha wa gharama za matibabu likiwemo kundi la Watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5), Wajawazito pamoja na Wazee wenye umri zaidi ya miaka 60. Katika kutekeleza Sera hii imegeuka kuwa changamoto kwa Taasisi zinazotoa huduma za afya kwa makundi haya na kupelekea kuwa kero kwa makundi hayo na hata kwa taasisi husika inayotoa huduma kwa kuwa na uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya kununua Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi kwa ajili ya kuwapa huduma bora za afya kwa makundi husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Hospitali ya Taifa Muhimbili na kupewa taarifa kwamba kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba 2015 Taasisi ilitumia kiasi cha shilingi **Bilioni 1.640** kwa ajili ya kutoa huduma kwa msamaha na

kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 Taasisi hiyo kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba 2016 ilitumia kiasi cha **shilingi Bilioni 1.560** kwa wagonjwa walio na sifa za kupata matibabu kwa msamaha. Hii ni kwa kipindi cha miezi sita (6) tu katika miaka hiyo miwili mfululizo Taasisi hiyo imekuwa ikitumia fedha zake kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa makundi ya msamaha ambazo zinakusanywa na Taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI) ilitoa huduma katika mkoa 18 ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa watoto **2200** na kati hao watoto **202** wenye vichwa vikubwa walipata huduma ya upasuaji na katika huduma hiyo iliyotolewa fedha zilizotumika ni kutokana na vyanzo vya mapato ya ndani ya Taasisi. Kwa mantiki hii, Taasisi hizi zimekuwa zikifanya kazi kubwa ambayo inalazimika kutumia mapato ya ndani na hata hivyo kusababisha kufanya kazi kwa kiasi kidogo kutokana na uhaba wa rasilimali fedha ambazo kama Taasisi inahangaika kuzikusanya na kuzigawanya katika utoaji wa huduma kwa makundi yenye msamaha.

Mheshimiwa Spika, *Kamati inashauri Serikali, kutenga Fungu lake maalumu (Separate Vote) ambalo litatengwa kwa ajili ya kutoa huduma bora za afya kwa makundi hayo ya msamaha wa gharama za matibabu ili kuweza kuwa na huduma endelevu.*

5.8 Bajeti ndogo ya Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete imekuwa ikitoa huduma ya matibabu ya Moyo kwa Watanzania. Taasisi hii imekuwa ikitoa huduma katika mazingira magumu sana kutokana na kuongezeka kwa wagonjwa na upande mwingine Serikali kutopeleka fedha kama ilivyokuwa imepangwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Mathlani, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Taasisi hii ilitengewa kiasi cha **shilingi Bilioni 4** lakini mpaka kufikia mwezi Machi 2017 Taasisi hii ilikuwa imepokea kiasi

cha shilingi **Milioni 500** tu sawa na **asilimia 12.5** ya fedha zote zilizotengwa. Wakati huo huo Taasisi hii imeokoa kiasi cha **shilingi Bilioni 3.75**kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 iwapo wagonjwa hao wangepelekwa nje ya nchi hasa India kwa ajili ya matibabu hayo ya Moyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashangazwa na kitendo cha Taasisi inayookoa fedha nyingi kwa kutokupeleka wagonjwa nje lakini bado fedha zinazoombwa hazipelekwi katika Taasisi hiyo. Kamati inashauri bajeti ya JKCI itolewe yote na kwa wakati ili iweze kuisaidia Serikali kuokoa fedha nyingi ambazo ingetumia kupeleka wagonjwa kwenye matibabu nje ya nchi.

5.9 Ripoti ya Ukaguzi wa Benki ya Wanawake ya Tanzania (TWB)

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake ya Tanzania (*Tanzania Women Bank*) ipo chini ya Wizara ya Afya na Benki hii imekuwa ikisuasua katika ukuaji wake na hata kutofikia maeneo mengine ya nchi kwa maana ya mikoa ya pembezoni na kujikuta imebakia katika mkoa wa Dar es Salaam peke yake.

Kamati inaishauri Serikali kupitia Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuifanyia ukaguzi wa kimahesabu Benki hiyo ili kubaini kiasi cha mtaji wake, nini kikwazo cha Benki hiyo kutokukua kama Benki nyingine na kuona namna gani inaweza kuibuliwa na kukuzwa ili kuweza kushindana na Benki nyingine kwa ajili ya kuwasaidia Wanawake wa Kitanzania lakini pamoja na Wanaume kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

5.10 Utoaji wa zabuni za utoaji wa Huduma katika Taasisi za Afya.

Mheshimiwa Spika, Utoaji wa Huduma za Afya katika Taasisi kubwa kama vile Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa (MOI) imekuwa ni changamoto kubwa kutokana na uhaba wa Vifaa, Vifaa Tiba, Dawa na Vitendanishi kama ilivyoelezwa hapo awali. Aidha, upungufu huo unapelekea

kuwa na msongamano mkubwa katika sehemu ya vipimo na hata kupelekea wagonjwa kwenda kununua dawa nje ya Taasisi kwa gharama kubwa kwa kuwa hazijaweza kupatikana ndani ya Taasisi ambayo mgonjwa amekuwa akipata matibabu yake. Hali hii inapelekea hata wagonjwa wengine kurejea nyumbani wakiwa wamekosa vipimo, dawa au fedha za kupata huduma nje ya Taasisi hizo. Hili limekuwa linaleta usumbufu na hata kupoteza maisha yao kwa maradhi ambayo yamekuwa yakiwasumbua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizo za ugumu wa upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya vipimo na dawa kutokana na Taasisi kukosa fedha za kununulia vifaa na dawa Kamati inaishauri Serikali kuruhusu huduma hizo hasa za Vipimo na dawa zitolewe na Mzabuni wa nje ya Taasisi (Services Outsourcing) ambaye ataweza kuwekeza katika maeneo hayo ambapo mbia huyo ataleta vifaa vyake kwa ajili ya upimaji wa magonjwa mbalimbali lakini pia utoaji wa dawa kwa wagonjwa katika Taasisi husika. Kamati inashauri hivyo kwakuwa kuna faida kubwa katika kutekeleza hayo, kwanza, itaipunguzia mzigo mkubwa kwa Serikali na Taasisi hiyo katika suala zima la ukarabati (Maintenance) ya vifaa hivyo, itapunguza shughuli ya uagizaji wa dawa katika Taasisi lakini pia hata kama teknolojia ya vifaa itabadilika itabaki kuwa jukumu la Mzabuni huyo kubadilisha na si jukumu la Serikali tena kama ilivyo sasa na zaidi tena kuifanya nchi yetu kuendana na mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea kutokea ulimwenguni katika suala zima la afya.

5.11 Kutopelekwa kwa fedha zilizotengwa katika Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Maendeleo ya Afya ndiyo msingi mkubwa wa kuwekeza katika Sekta ya Afya kwa mustakabli wa afya za wananchi wa Tanzania, ikiwemo miradi ya Lishe, Kifua Kikuu na UKIMWI, Maendeleo ya masuala ya Utafiti ya Magonjwa ya Binadamu. Kamati imesikitishwa kuona katika Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017 Wizara imepokea asilimia 25 tu ya fedha za Miradi ya Maendeleo. Kuna Msemu

usemao " *Nothing happens without Focus, Don't try to do everything at once, Take it one step at a time*".

Kamati inaona ni wakati sasa umefika Serikali iamue kuchagua Miradi michache ya Kipaumbele kulingana na uwezo wake wa kifedha ili iweze kuitekeleza.

5.12 Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii vipelekwe Wizara ya Elimu

Mheshimiwa Spika, Wizara hii katika Fungu 53 (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) inasimamia Vyuvo vinavyotoa Elimu kwa ajili ya kupata Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii kikiwemo chuo cha Tengeru-Arusha, Rungemba-Iringa, Mondoli, Uyole, Misungwi na vingine vingi. Katika suala hili Taaluma hii imekuwa si katika ubora ule ambao unatarajiwa kutolewa na vyuvo hivyo.

Kamati inashauri vyuvo hivi vyote vilivyoko chini ya Fungu 53 vihamishwe na kupelekwa chini ya uangalizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ilivyo vyuvo vikuu vingine hapa nchini. Kwa kufanya hivi kutasaidia kufuatilia ubora wa Elimu itolewayo na vyuvo hivyo vya Maendeleo ya Jamii.

5.13 Bohari Kuu ya Dawa

Mheshimiwa Spika, Bohari ya Dawa hapa nchini ndiyo wanaohusika katika Uagizaji na Usambazaji wa Dawa hapa nchini. Katika kutekeleza suala hili Bohari ya Dawa imekuwa ikilalamikiwa sana katika kutotekeleza majukumu yake ikiwa kutopeleka Dawa katika vituo kwa wakati hali inayopelekea wagonjwa kutopata matibabu yanayotakikana.

Kamati inashauri Bohari hiyo kufanyiwa ukaguzi wa kina kwa ajili ya kubaini mafanikio (Strength), Changamoto (Challenges), Mahitaji (Demands) ili kuweza kubaini namna gani ya kuboresha usambazaji wa dawa nchini.

5.14 Mabadiliko ya Sheria ya ndoa na Ndoa za utotoni

Mheshimiwa Spika, Katika suala la ndoa kuna Sheria inayosimamia masuala ya ndoa ya Mwaka 1971. Sheria hiyo imeonekana kuwa namapungufu mengi hasa katika **Kifungu cha 13 na 17**. Kifungu cha 17 kinahusu wanaotaka kufunga ndoa wawe wameridhiana na kama yupo chini ya miaka 18 ridhaa itatoka kwa baba na kama baba amefariki ridhaa itatoka kwa mama na kama wazazi wote wamefariki basi ridhaa hiyo itatoka kwa mlezi wa mtoto huyo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi mojawapo ya nchi ambazo zinaongoza kwa ndoa za utotoni duniani ambapo kwa wastani kati ya watoto wakike watano (5) watoto wawili (2) huolewa kabla ya umri na takwimu za Utafiti wa Afya na Watu (*Demographic Health Survey 2015/2016*) inaonesha kuwa **asilimia 30.5%** ya wanawake kati ya umri wa miaka 20-24 inaonesha waliolewa chini ya umri wa miaka 18.

Mheshimiwa Spika, Mkoa inayoongoza kwa ndoa za utotoni kwa zaidi ya **asilimia 50** ni pamoja na **Shinyanga** (asilimia 59), **Tabora** (asilimia 58), **Mara** (asilimia 55) na mkoa wa **Dodoma** (asilimia 51). Ndoa hizi za chini ya umri wa miaka 18 zinapelekea watoto hao kupata athari nyingi zikiwemo za kiafya na hata kukosa haki yao ya kupata Elimu na hata kupata athari za kisaikolojia.

Kamati inashauri Serikali pamoja na ugumu unaojaribu kuwekwa na Taasisi za kidini na mila na desturi za mahali husika, Kamati inaamini Serikali ina mamlaka juu ya kulinda haki na ustawi wa jamii zetu hasa kulinda haki za watoto hapa nchini Serikali ilinde haki hizo za watoto.

5.15 Kuongezeka kwa Idadi ya Makundi Maalum (*Key Populations*) katika Jamii

Mheshimiwa Spika, Makundi maalum (*Key Populations*) inajumuisha watu wanaojidunga madawa ya kulevya (IDUs), Wanaofanya biashara ya ngono (wakike na kiume) na wanaofanya mapenzi ya jinsia moja (*Men who Sex with*

Menand women who sex with women and Trans-Gender). Makundi haya yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku katika jamii zetu na imekuwa tishio kubwa hasa katika suala zima la ongezeko la Virusi vya UKIMWI. Ongezeko la kundi hili ni kutokana na mabadiliko ya jamii zetu ikiwemo katika suala la malezi kuanzia katika ngazi ya familia, shuleni na hata katika jamii kwa ujumla. Matendo haya yamekuwa yakifanyika majumbani, shuleni za kutwa na hata bweni.

Mheshimiwa Spika, Kuna athari nyingi zitokanazo na makundi haya maalumu ikiwemo za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, Homa ya ini, kupoteza nguvu kazi ya Taifa katika jamii na hata watoto kukatisha masomo yao na kujiingiza katika makundi hayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaajiri Maafisa maendeleo ya jamii, katika kila kata ambao watasaidia katika kutekeleza afua mbalimbali na hata kuwapa miongozo wanajamii ya namna gani ya kuenenda ili kudhibiti suala hili la makundi maalumu, kwani imethibitika kwamba katika maeneo mengi kuna upungufu mkubwa wa Watumishi wa hao pamoja na Halmashauri nyingine lakini hata Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kwako Mheshimiwa Spika kuna upungufu wa Maafisa hao wa maendeleo ya Jamii kwa asilimia 82, Kondoa asilimia 100, Ruangwa (Waziri Mkuu) upungufu ni asilimia 100, Mji wa Bunda na Halmashauri nyingine nyingi hapa nchini. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali itimize wajibu wake wakuajiri Maafisa maendeleo na Ustawi wa Jamii ili kuweza kupunguza ongezeko la makundi haya.

5.16 Vifo vya akina Mama vitokanavyo na Uzazi

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba Serikalii bado haijatilia mkazo suala la vifo vya akina mama vitokanavyo uzazi na akina mama hapa nchini. Suala hili lilielezwa na Kamati katika Taarifa ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwamba, kumekuwa na vifo vingi vitokanavyo na masuala ya uzazi, ikiwemo wakati wakati wa ujauzito,

wakati wa kujifungia na hata ndani ya siku arobaini (40) baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, Takwimu zinazoonesha vifo vya akina mama zipo juu kila mwaka pamoja na jitihada zote za Serikali katika kupunguza au kumaliza tatizo hili. Vifo hivi vinatokana na sababu mbalimbali ikiwemo umbali wa vituo vya kutolea huduma za afya ya uzazi, kukosekana kwa huduma za uzazi wa mpango takwimu zinaonesha kuwa katika kila wanawake Watano (5) wa Kitanzania mwanamke mmoja (1) ana mahitaji yasiyofikiwa. Aidha, kutokana na kutopatikana kwa huduma hizo za Uzazi wa Mpango kila mwaka wanawake wa Kitanzania **Milioni moja (1,000,000)** hupata mimba zisizotarajiwa ambazo kati ya hizo **asilimia 39 (Wanawake 390,000)** huishia kwenye utoaji wa mimba hizo tena kwa usiri mkubwa na kupelekea kupata matatizo ambayo yanahitajimatibabu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwanusuru akina mama hawa katika matatizo ya uzazi kwa kuwatengea na kutoa fedha za kutosha kwani Bajeti yao imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka. Kwa mfano katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 Masuala ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi (Support to Maternal Mortality Reduction) ilitengewa kiasi cha shilingi Bilioni 13 na Mwaka wa Fedha 2017/2018 fedha zimetengwa shilingi ni shilingi Bilioni 8.6. Upungufu huu ni sawa na asilimia 33.8. Kamati inaona hii si sawa hata kidogo kwani inaonesha Serikali kukosa nia thabiti ya kutatua tatizo hili.

5.17 Huduma za Bima ya Afya ya Taifa (NHIF)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ni Mfuko ambao unatumika kukusanya makato ya Watumishi wa Serikali na Taasisi zake kutoka katika mishahara yao na kukusanya fedha hizo katika kapu moja ili kutoa huduma bora za afya kwa Watumishi hao pamoja na wategemezi wao. Kabla Mfuko huu haujaanza kutoa huduma hizo Mashirika ya umma yaliingia mikataba na Mifuko ya Bima

binafsi na walikuwa wanapata huduma bora kulingana na tozo za makato yao. Kuna maelekezo ya kutaka Mashirika ya Umma kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wakati Mfuko huo haujajiandaa vya kutosha kutoa huduma hizo za afya kama mahitaji ya wachangiaji mfuko huo na ndani na hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuupa muda Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa kujiaandaa vyema ili uweze kutoa huduma bora kwa wateja wake ili hata Mashirika hayo yakijiunga wasione tofauti ya upatikanaji wa huduma walizokuwa wanapata kabla ya kujiunga katika mifuko mingine ya Bima ya Afya .Kwa kufanya hivyo kutaondoa malalamiko na pia kuwapa uwezo wa kuendana na soko la utoaji wa huduma bora za afya kama mifuko mingine inayotoa huduma ya Bima ya Afya hapa nchini na hata nje ya nchi.

5.18 Ujenzi wa Vituo vya Afya

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina upungufu mkubwa wa vituo vya Afya kwani kwa mujibu wa Takwimu ni kuwa kuna upungufu wa vituo vya Afya kwa asilimia 85 Hali hii inasikitisha kwani asilimian kubwa ya Watanzania wanaishi maeneo ya vijijini ambako wanategemea vituo vya Afya kupata huduma. Kamati inajiliza je ni jukumu la nani kujenga vituo hivi vya Afya?

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kwaujumla wake kuhakikisha vituo vya Afya vinajengwa vya kutosha ili kusaidia kutoa huduma ya afya nchini.

5.19 Utenganishajiwa Majukumu ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

Mheshimiwa Spika, Katika Udhibiti waBidhaa nchini Serikali iliamua kuunda Taasisi kwaajili ya usimamizi wa majukumu haya kwa Mujibu wa Sheria. Katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo, Kamati imebaini kuwa kumekuwa na muingiliano wa majukumu siyo tu baina ya TFDA na TBS lakini pia na Taasisi nyingine kama Bodi ya Maabara Binafsi za Afya

(*Private Health Laboratories*). Muingiliano huu umekuwa ukikiuka utaratibu wa kisheria na kuleta usumbufu katika utekelezaji wa majukumu ya kila Taasisi. Kutokana na hali hii, ***Kamati inashauri Serikali iziangalie Sheria zinazounda Taasisi hizi ambazo pia zimeainisha majukumu yao na pale kwenye tatizo basi marekebisho yafanyike kuepusha muingiliano wa majukumu ya Taasisi moja kufanywa na Taasisi nyingine.***

5.20 Vikwazo katika uingizwaji wa Misaada kutoka kwa Wahisani

Mheshimiwa Spika, Katika uboreshaji wa Sekta ya Afya kumekuwa na Wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wakisaidiana na Serikali hasa katika upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Kamati imebaini kuwa pamoja na nia njema ya wahisani ya kutupatia msaada wa dawa muhimu pamoja na dawa za uzazi wa mpango, kumekuwa na vikwazo mbalimbali katika utekelezaji wa azma hii ikiwemo urasimu na gharama kubwa za kuhakikisha msaada huo unawafikia wananchi. Vikwazo hivyo ni pamoja na tozo za kutupatia msaada ambazo Serikali imekuwa ikimtaka anayetoa msaada kulipa kodi ya kutupatia msaada huo, gharama za kupakua mzigo ufikapo bandarini, gharama ya kutunza msaada huo ufikapo bandarini gharama za kuwalipa Mamlaka ya kukagua msaada huo ambayo ni Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ipo chini ya Wizara ya Afya na inatengewa Bajeti ya kutekeleza majukumu yak echini ya Wizara ya Afya na Serikali inaitengea fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na taratibu za kwamba msaada huo unatakiwa utolewe bandarini ndani ya siku saba (7) baada ya hapo gharama zinaongezeka kila siku, kodi zimekuwa zikiongezeka kwa baadhi ya Misaada kutokana na kuchelewa kutolewa kwa msaada (Mzigo) kutokana na urasimu. Kwa Mfano imewahi kutokea msaada wa sindano zenye thamani ya shilingi **milioni 800** kutakiwa kulipiwa kodi kiasi cha shilingi **Bilioni 1.2** iliyopelekea Wahisani kushindwa kutoa na hatimae msaada huo kuishia hewani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia TFDA ifanye jukumu lake bila kutoza kiasi chochote kwa Wizara kwani hayo ndiyo majukumu yake ambayo amepangiwa Bajeti na haipaswi kulipwa vilevile, Kamati inaona hiki ni kikwazo kikubwa kwa wafadhili na inaweza kuwa ni moja ya sababu ya wao kuanza kupunguza msaada ambao wamekuwa wakiahidi. Pia Serikali itambue kwamba kodi na tozo mbalimbali kunapelekea kuongezeka kwa gharama za matibabu ya afya na anayeumia hapa ni mwananchi ambaye ndiyo mlaji au mtumiaji wa mwisho wa huduma hiyo.

5.21 Magonjwa yatokanayo kwa kukosekana kwa matumizi bora ya vyoo, maji safi na salama

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO 2004) imeonesha kwamba kuboresha kwa **Usafi** wa mazingira kunaweza kupunguza magonjwa ya kuhara kwa asilimia 32 na kuboresha **Afya** ya mazingira kunaweza kupunguza magonjwa ya kuharisha kwa **asilimia 45**. Uboreshaji wa afya ya mazingira ni pamoja na ujengaji wa vyoo bora, upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu matumizi bora ya vyoo.

Mheshimiwa Spika, Utunzaji wa usafi wa mazingira ni jukumu la kila mmoja wetu kuanzia katika ngazi ya familia (ujenzi na utumiaji bora wa vyoo) hata katika shule. Taarifa za utafiti mbalimbali unaonesha kwamba ni **asilimia 11** tu ya shule ya msingi nchini zilikuwa na namba ya vyoo vya kutosha na **asilimia 1** ya sehemu zinazotumika kunawia mikono na sabuni (*School WASH Mapping Report 2011*). Kumekuwa na tabia a wananchi kujisaidia kiholela (*Open defecation*) majumbani, shuleni na hata wakati wa safari ndefu (kuchimba dawa) ambao ni uchafuzi wa mazingira. Matumizi bora ya vyoo kutapelekea kulinda vyanzo vya maji ambayo yanatumika na wananchi wetu hivyo kulinda afya kwa kujikinga na magonjwa yatokanayo na maji kwani imebainika kwamba **asilimia 70** ya wagonjwa kwa siku ni wagonjwa wenye magonjwa yatokanayo na maji (*Waterborne Diseases*).

Mheshimiwa Spika, Hakuna siku ambayo itapita mwanadamu asitumie maji tumekuwa tusikia kila siku kuwa maji ni uhai na maji ni afya. Nchi yetu imekuwa na tatizo kubwa sana la magonjwa yatokanayo na kukosekana kwa maji safi na salama (*Waterborne diseases*) yakiwemo magonjwa ya homa ya tumbo, Kichocho, kipindupindu, magonjwa ya kuhara na kuharisha na hata magonjwa ya ngozi .

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali ihimize ujengaji na matumizi bora ya vyoo na kuhakikisha kupitia Wizara ya Afya inashirikiana na Wizara ya Maji katika kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama ili kuepuka magonjwa hayo.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa muda wa kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu (Mb) pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Hamis Kigwangala(Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa Kamati wakati wote wa shughuli za Kamati hasa Kamati ilipokuwa ikijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Vilevile napenda kuwashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara Idara kuu Afya na Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Maafisa Waandamizi wao wa Wizara na Taasisi zake zote kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wadau wetu wote wa Sekta ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoutoa kwa Serikali yetu katika kuendelea kutoa huduma bora ya Afya kwa wananchi wetu. Naomba kuwataja kwa uchache Wadau hao ni pamoja na Wadau wote wa Kimataifa

wanaoendelea kutoa fedha za Maendeleo ya Afya, Tanzania *Gender Networking Program (TGNP)*, *Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)*, Shirika la Utepe Mweupe (*White Ribbon Association*), *Tanzania Health Promotion (HDT)*, Tanzania Water and Sanitation Network (TaWaSaNet) na Mashirika mengine yasiyo ya kiserikali kwa juhudi zao wanazoendelea kuzifanya katika kusaidia uboreshaji wa Sekta Afya hapa nchini. Kamati inalomba Serikali kuendelea kuwapa ushirikiano mkubwa ili waweze kuendelea kutimiza majukumu yao hasa katika utoaji wa Huduma za Afya kwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Kwa nafasi ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na ufinyu wa muda lakini walikuwa tayari kutekeleza jukumu hili kubwa na hatimaye kukamilisha Uchambuzi wa Bajeti hii kwa weledi mkubwa na kwa wakati. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuatao:

1. Mhe. Peter Joseph Serukamba, Mb, -**Mwenyekiti**
2. Mhe.Mussa Azzan Zungu, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe.Hussein Mohamed Bashe, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb - Mjumbe
5. Mhe.Peter Ambrose Paciece Lijualikali, Mb - Mjumbe
6. Mhe.Joseph Osmund Mbilinyi, Mb - Mjumbe
7. Mhe.Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb Mjumbe
8. Mhe.Kasuku Samson Bilago, Mb - Mjumbe
9. Mhe.Juma A. Juma, Mb - Mjumbe
10. Mhe.Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb - Mjumbe
11. Mhe.Dkt. Jasmine Tiisekwa, Mb - Mjumbe
12. Mhe.Ahmed Ally Salum Mb - Mjumbe
13. Mhe.Susan Anselm Lyimo, Mb - Mjumbe
14. Mhe.Juma Selemani Nkamia, Mb - Mjumbe
15. Mhe.Seleman Said Bungara, Mb - Mjumbe
16. Mhe.Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe, - Mjumbe
17. Mhe.Boniphace Mwita Getere, Mb - Mjumbe

- | | | |
|-----|-------------------------------|----------|
| 18. | Mhe.Bernadeta K. Mushashu,Mb | - Mjumbe |
| 19. | Mh.Hussein Nassor Amar, Mb | - Mjumbe |
| 20. | Sikudhani Yassin Chikambo, Mb | - Mjumbe |
| 21. | Savelina Sylvanus Mwijage, Mb | - Mjumbe |
| 22. | Jaku Hashim Ayoub, Mb | -Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, wakiongozwa na Dkt. Thomas D. Kashillillah, Katibu wa Bunge, Ndugu Athman Brambath Hussein Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge na Ndugu Dickson Bisile Mkurugenzi Msaidizi kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa.Kipekee nawashukuru Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera (Makatibu Kamati) na Ndg.Gaitana Chima msaidizi wao kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika,baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja **Fungu 52** jumla ya shilingi **Trilioni moja, Bilioni sabini na nane, Milioni mia tatu arobaini na nne na Laki mbili na themanini na mbili elfu (1,078,344,282,000/=)** na **Fungu 53** jumla ya shilingi **Bilioni Arobaini, Milioni Mia Moja na Thelethini, Laki Mbili na Kumi na Tano na Mia Saba Themanini na Nne (40,130,215,784/=)**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mh. Peter Joseph Serukamba (Mb),
MWENYEKITI
KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII
3 MEI, 2017

MWENYEKITI: Tunaendelea sasa namuita msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naona Mheshimiwa Ester Bulaya, karibu. *(Makofi)*

MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO): Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda naomba hotuba yote ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iingie kwenye *Hansard* na nina furaha leo kusimama kwenye Bunge lako Tukufu nikiwa upinzani baada ya kuhama CCM na sasa ni Mbunge wa Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mheshimiwa Godwin Mollel, naomba kuwasilisha Maoni Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara husika kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha maoni hayo, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi sote afya njema na kutuwezesha kushiriki mkutano wa Bunge la Bajeti tukiwa salama. Kipekee namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda dhidi ya njama na hila za shetani zenye lengo ovu la kudharirisha jitihada zangu na Kambi nzima ya Upinzani katika kupigania misingi ya haki na demokrasia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa busara na moyo wake wa ujasiri ambao amefanikisha kuiunganisha Kambi ya upinzani Bungeni, licha ya vikwazo na changamoto nyingi zinazozikabiri siasa za upinzani hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri Kivuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Godwin Mollel (Mbunge) na Naibu wake Mheshimiwa Zubeda Sakuru kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sina fadhila kama sitawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Bunda Mjini kwa kuendelea kuniamini na kunipatia ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu. Napenda kuwaahidi utumishi uliotukuka na kamwe sitowaangusha katika kuhakikisha kwamba maendeleo ya Jimbo letu yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, naishukuru sana familia yangu hasa mtoto wangu mpendwa Brighton, kwanza kwa kunitia moyo lakini kwa uvumilivu hasa pale ninapokuwa mbali nao kwa muda mrefu kutokana na majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuzungumzia masuala ya afya naomba kumnukuu nguli wa Kiswahili na mwanafalsafa mashuhuri Hayati Shaabani Robert, alisema hivi: "Msema kweli hukimbiwa na rafiki zake, nikipatwa na ajali kama hiyo sitawaonea wivu wale wanaodumu na marafiki zao siku zote, siweze kuikana kweli kwa kuhofia upweke wa kitambo na kujinyima furaha ya milele inayokaribia kutokea baada ya kushindwa kwa uoga."
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ni muhimu na ya faraja sana kwa wote walioamua kusimama na kupinga unafiki mkubwa dhidi ya hofu, ubinafsi, ubabe, matisho, kujipendekeza, dhuluma na ufedhuli wowote juu ya haki.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kutafakali maneno haya ya Shaabani Robert ni vyema pia wenye mamlaka wakatambua ahadi namba nane ya TANU inayosema; "Nitasema kweli daima, fitina kwangu ni mwiko."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani tafakari hiyo itatusaidia kusema ukweli na kutetea ukweli tunapojadili Bajeti ya Wizara ya Afya, ambayo imebeba maisha ya Watanzania wote. Tafakuri hiyo itatusaidia kuponya afya na nguvu ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Salamu hizo za utangulizi sasa naomba nianze kuzungumzia masuala yaliyomo katika hotuba. Hotuba hii imebeba mambo muhimu yafuatayo; mkanganyiko wa kiutendaji ndani ya Wizara ya Afya, hali ya sekta ya afya nchini, upungufu wa vituo vya kutolea huduma ya afya nchini, ongezeko kubwa la wagonjwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na vitengo vyake, upungufu wa watumishi katika sekta ya afya, huduma ya afya ya mama na mtoto, uhaba wa chanjo nchini, changamoto za kibajeti katika utatuzi wa vifo vitokanavyo na afya ya uzazi, kukabiliwa na tatizo la akili nchini, lishe duni na ongezeko la utapiamlo na udumavu, kansa ya shingo ya uzazi, uhibitaji na upungufu wa dawa nchini, ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukizwa na athari zake, ongezeko kubwa la wagonjwa Hospitali ya Taifa Muhimbili na vitengo vyake, wanawake na usawa wa kijinsia, masuala ya watoto, ukatili dhidi ya watoto, Vyuvo vya Maendeleo ya Jamii na utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na mkanganyiko wa utekelezaji ndani ya Wizara ya Afya; kumekuwepo na mkanganyiko mkubwa juu ya utendaji wa Wizara ya Afya hapa nchini. Wizara hii imekosa uhuru wa kiutendaji na utekelezaji wa shughuli zake kutokana na kuingiliana na Wizara nyingine. Mkanganyiko huu umesababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi na wadau wa afya hususan katika masuala ya kiutawala, masuala ya kutoa huduma na kupokea huduma kwenye hospitali za wilaya mpaka zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mkanganyiko huu, Wizara imeshindwa kutoa majibu mahsusi kwenye changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya afya kwa kigezo kuwa masuala mengine yako chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na mengine chini ya Ofisi ya Rais - Manajimenti ya Utumishi wa Umma. Hivyo Wizara hizi huishia kutupiana mipira pale linapotokea suala la uwajibikaji. Tutambue kuwa ni vigumu sana kwa Waheshimiwa Wabunge kuongelea Wizara

ya Afya, bila kuongelea pale walipo wapiga kura wao au wanapoishi Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya kwa mujibu wa hati idhini pamoja na mambo mengine inasimamia Sera ya Afya na huduma za kinga na tiba, kusimamia na kudhibiti ubora wa dawa, vifaa na vifaa tiba, kusimamia mpango wa afya ya uzazi na mtoto, kuendesha ukaguzi wa huduma za afya katika ngazi mbalimbali, kuongoza na kusimamia taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkawanyiko mkubwa unajitokeza pale ambapo Wizara ya Afya inapokaa pembeni katika kuhakikisha kuwa zahanati, vituo vya afya, na Hospitali za Wilaya zinakuwa chini ya jukumu lake la msingi badala ya kuiachia majukumu mengine Ofisi ya Rais – TAMISEMI na pengine Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha Wizara hii inafanya kazi zake vizuri kwa kuweka mfumo utakaoipa Wizara mamlaka kamili katika utekelezaji wa majukumu yake yote badala ya kutumia muingiliano wa kimajukumu kama kichaka cha kukwepa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa vituo vya kutolea huduma za aya nchini; hali ya vituo vya kutolea huduma ya afya nchini ni mbaya sana. Siku zote Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikilisemea jambo hili, lakini Serikali hajjalichukulia kwa uzito wake. Upatikanaji na utoaji wa huduma za afya umekuwa na changamoto lukuki ukiwemo ufinyi wa bajeti, upungufu wa watoa huduma za afya, ukosefu wa mawasiliano, usafiri na uhaba wa vitendea kazi na zaidi uwepo wa mikakati isiyoendana na mabadiliko ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kwamba mikakati mingi tuliyonayo katika sekta ya afya nchini haiwezi kutatua changamoto za afya, kutokana na kushindwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia. Tafiti

zilizochapishwa na jarida la uchumi na fedha la nchini Canada mwezi Julai, 2016 zilieleza kwa kina kwamba matokeo ya tafiti iliyofanywa nchini Tanzania juu ya changamoto ya upatikanaji wa huduma za afya nchini zinaonesha kuwa takribani asilimia 45 ya wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilometa moja huku asilimia 93 wakilazimika kutembea kwa zaidi ya kilometa 10 kufuata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Shirika la SIKIKA lilibaini takribani asilimia 80 ya Watanzania waishio vijijini hutembea zaidi ya kilometa tano kufuata huduma za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanalazimika kwenda mbali sana kutafuta huduma za afya, hali inayopelekea kuongezeka kwa vifo ambavyo vingeweza kuepukika endapo huduma zingepatikana kwa urahisi katika maeneo ya karibu. Maeneo mengi ya nchi bado hayana zahanati za kutosha, vituo vya afya na hata Hospitali za Wilaya ambapo vituo hivyo vya kutolea huduma vinapaswa kuwa karibu zaidi na wananchi hususani maeneo ya vijijini. Pamoja na hayo yapo maeneo ambayo Hospitali za Wilaya zinabeba majukumu makubwa ya Hospitali za Mikoa na vituo vya afya vinabeba majukumu ya Hospitali za Wilaya na kadhalika. Sisi Waheshimiwa Wabunge tumeyashuhudia hayo katika maeneo yetu

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa muda mrefu sasa, Kituo cha Afya cha Manyamanyama kilichopo Bunda Mjini, kimekuwa kikitumika kama Hospitali ya Wilaya huku mgao na vifaa tiba vikiendelea kutolewa kwa mgao wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa kituo hiki kimekuwa kikitoa huduma kubwa na muhimu kwa wananchi wa Bunda kutokana na umuhimu wake wa kijiografia bado mpaka leo kituo hiki cha afya hakina chumba cha kuhifadha maiti, jambo ambalo limesababisha kituo hiki kushindwa kupandishwa hadhi kwa muda mrefu sana huku majukumu yake yakibeba hadhi ya Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Hospitali ya Mji wa Tarime ambayo inatumika kama Hospitali ya Wilaya inahudumia idadi kubwa sana ya wananchi wanaotoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya Mji wa Tarime. Baada ya Halmashauri kugawanywa Serikali ilishusha hadhi Hospitali hii ya Wilaya kuwa Hospitali ya Mji huku Mganga Mkuu wake akiwa ni TMO. Bado mpaka leo kwenye vitabu hospitali hii inasomeka kama Hospitali ya Wilaya ya Tarime. Hospitali hii imekuwa ikielemea na mzigo mkubwa ya kutoa huduma kuliko uwezo wake kwani watu wanaotoka nje ya Mji wa Tarime hutumia Hospitali hii pia. Tukumbuke kuwa Halmashauri ya Mji wa Tarime haina hata kituo kimoja cha afya, japo Serikali iliahidi kujenga vituo vinne katika mwaka wa fedha 2016/2017. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo makubwa yanayojidhihirisha hapa ni pamoja na Serikali kushindwa kuweka mipango ya ufuatiliaji wa vituo vya kutolea huduma ya afya vinavyoendana na uhitaji wa huduma ya afya. Kugawa majimbo kisiasa bila kuzingatia huduma za msingi za eneo husika, idadi ya watu na rasilimali zilizopo, Serikali kukosa mpango wa uendelezaji na ufuatiliaji wa mipango inayojiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuacha kuwahadaa katika masuala ya kimsingi ya afya za wananchi. Tabia ya Serikali ya kuweka pamba masikioni pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wanaleta kero hizi za msingi zinazohitaji ufumbuzi wa haraka lakini inachukua takribani miaka kumi mpaka ishirini kutatua tatizo dogo inazidi kudhihirisha kuwa hatuwezi kupata suluhisho la matatizo kwa kutegemea uwelewa ule ule uliotengeneza tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa watumishi katika sekta ya afya; hatuwezi kuizungumzia Wizara ya Afya bila kugusia suala la watumishi ndani ya Wizara hii. Uhaba wa wahudumu wa afya ni tatizo sugu linaloonekana kuelemea Serikali. Tatizo hili lipo kwenye ngazi zote kuanzia kwenye zahanati, vituo vya afya, Hospitali za

Wilaya, Mikoa, Hospitali ya Taifa na linalenga taaluma zote za afya ambapo ni madaktari, wauguzi, mafundi sanifu, wataalamu wa miale, wafamasia, watoa dawa na maafisa dawa wasaidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ripoti ya madaktari wenza wa Afrika Kusini, ukuaji wa rasilimali watu kwa ajili ya afya katika Tanzania; Tanzania ina upungufu wa wataalamu wa afya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaktari bingwa ni kwa asilimia 58.1; wauguzi wa sekta ya umma ni kwa asilimia 54.4; wataalamu wa miale ni kwa asilimia 50.8; maafisa kliniki ni kwa asilimia 50; waganga wasaidizi na waganga wasaidizi wa meno ni kwa asilimia 46.2; wafamasia ni kwa asilimia 49.9; mabwana afya ni kwa asilimia 45.7; mafundi sanifu wa maabara ni kwa asilimia 41.5; maafisa kliniki wasaidizi ni kwa asilimia 40.7; madaktari kwa asilimia 37.3; maafisa wauguzi asilimia 33.2 na makatibu wa afya ni kwa asilimi 27.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha pia, kwamba zaidi ya asilimia 74 ya madaktari waliopo nchini, wanafanya kazi maeneo ya mijini, hii ina maana kwamba wafanyakazi walio wengi ambao wanaishi vijijini wanahudumiwa na asilimia 26 tu ya madaktari. Aidha, uwiano kati ya daktari mmoja na wagonjwa anaohudumia ni wa kutisha, daktari mmoja anahudumia wagonjwa 77,880 kwa maeneo ya vijijini kinyume kabisa na maelekezo ya Shirika la Afya Duniani ambapo daktari mmoja anatakiwa kuhudumia wagonjwa elfu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba huu mkubwa wa watumishi katika sekta ya afya umekuwa ni jipu lililoshindikana kutumbuka. Pamoja na uhaba huu mkubwa wa watumishi, Serikali ya Awamu ya Tano iliamua kuweka afya za Watanzania rehani kwa kuruhusu hao hao madaktari wachache ambao ndio tegemeo la Watanzania kwenda nchini Kenya kuwahudumia raia wa Kenya huku raia wake wakipata adha kubwa ya matibabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jambo hilo lililokosa uzalendo, mwezi April mwaka huu wa 2017 Waziri wa Afya alitangaza kuwa Mheshimiwa Rais ameamuru madaktari 258 walioomba kufanya kazi Kenya waajiriwe mara moja. Jambo hili si tu limewashangaza Watanzania bali ulimwengu kwa ujumla. Serikali hii imefanya maamuzi ya ajabu ambayo hayakuwahi kutokea katika historia ya nchi hii tangu uhuru. Kitendo cha Serikali kuwaajiri madaktari walioomba ajira nje ya nchi na kuwatupia kapuni mamia ya madaktari ambao kwa namna moja au nyingine waliionesha uzalendo wa kutamani kuitumikia nchi yao ni kitendo cha kibaguzi na kikatili sana kwa wazalendo wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapata wasiwasi juu ya uwezo wa Serikali katika kuratibu na kupambana na vipaumbele vyake. Serikali imeshindwa kabisa kujua kama Nchi hii ina huduma duni za afya na inakabiliwa na uhaba wa watendaji katika sekta ya afya kuliko Kenya. Katika ripoti ya Benki ya Dunia ya mwezi Mei, 2016 inaonesha kuwa utendaji wa sekta ya afya na maendeleo ya sekta hii katika nchi mbalimbali, ikiwemo Tanzania na Kenya, Serikali hii pengine itueleze na itoe takwimu sahihi juu ya watumishi katika sekta ya afya kwa kuwa hali inaonesha dhahiri takwimu hizo hazikuwepo Wizarani na ndiyo maana Serikali ikawa radhi kupeleka madaktari nje ya nchi ilhali hospitali nyingi majimboni zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa madaktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga wanasema mtu mzima akivuliwa nguo huchutama, hivyo basi Serikali ni lazima ijue kuwa ilipotoka na ijisahihishe katika hili. Hatuwezi kuendelea kuhubiri uzalendo kwa maneno bila vitendo. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali itoe tamko kuhusu maamuzi yake ya kutaka madaktari waende nchini Kenya kutoa huduma kwa wananchi wa Kenya huku ikijua Tanzania tuna uhaba mkubwa wa watoa huduma wa afya. *(Makofi)*

Pili, Serikali ieleza Bungeni mpaka sasa mwaka 2017 Tanzania inakabiliwa na uhaba wa watumishi wa afya kwa asilimia ngapi na huku ikizingatia kuwa kwa muda mrefu ilisitisha zoezi la kutoa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali ituambie imepanga kutoa ajira ngapi katika sekta ya afya kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 zenye uhakika katika utelekezaji? Katika hili Serikali izingatie imewaacha mamia ya madaktari wakikosa ajira nchini kwa sababu ya uzalendo wao wa kutamani kuitumikia nchi zaidi kuliko kwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha madaktari 258 kujitokeza kwenda nchini Kenya kimeonesha kuwa kuna madaktari wengi nchini ambao wanapenda kufanya kazi nje ya nchi kwa sababu mbalimbali. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maslahi ya watumishi katika sekta ya umma yanaboreshwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanapata *call allowance, overtime* na nyumba za watumishi wa afya hususan maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ustawi wa jamii, wanawake na usawa wa kijinsia; usawa wa kijinsia ni nyenzo muhimu katika kufikisha maendeleo endelevu ya Taifa. Changamoto kubwa inayowafanya wanawake washindwe kukabiliana na usawa wa kijinsia ni pamoja na uwepo wa mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke. Hii ni pamoja na changamoto ya Sheria kandamizi ya Ndoa ya mwaka 1971 ambayo inaendelea kukandamiza watoto wa kike na kuchochea ndoa za utotoni; Sheria ya Mirathi ya Kimila, tohara kwa watoto wa kike, watoto wanaopata ujauzito shuleni kukosa fursa ya kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo kubwa la kutisha la ongezeko la ndoa na mimba kwa watoto wenye umri wa kwenda shule na wale walio mashulen nchini. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani iliyotolewa mwezi Januari, 2016 inaonesha kuwa Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa matukio ya mimba na ndoa za utotoni ikiongoza kwa takribani asilimia 28. Hii ina maana kwamba watoto

wengi chini ya umri wa miaka 18 wanajihusisha na vitendo vya ngono visivyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto alithibitisha kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la mimba kwa wasichana wenye umri kuanzia miaka 15 mpaka 20, na ongezeko hili asilimia 28 ni kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 pekee ikilinganishwa na mwaka 2010 ambapo tatizo hilo lilikuwa asilimia 10 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Idadi ya Watu Duniani lilibaini kuwa kila kwenye wasichana kumi wenye umri kati ya miaka 12 mpaka 16 kati yao wanne wamepata mimba. Pamoja na hilo lilibaini kuwa kwa wastani wasichana wawili kati ya watano huolewa kabla ya kufikia umri wa miaka 18 hususani kwa maeneo ya vijijini. Vilevile Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (*UNICEF*) katika ripoti ya mwaka 2012 lilibaini kuwa mikoa ifuatayo inaongoza kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni, Shinyanga ni asilimia 59, Tabora asilimia 58, Mara asilimia 55, Dodoma asilimia 51 na Lindi asilimia 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kitaifa na kimataifa Kambi ya Upinzani imebaini kuwa ongezeko la mimba za utotoni linatokana na kushuka kwa kipato cha familia, kubadilika kwa mfumo wa maisha ambapo wazazi wengi wamekuwa wakitumia muda mwingi katika shughuli za kujipatia kipato na hivyo kuwa na muda kidogo kwa malezi, kukua kwa teknolojia hususan matumizi ya simu ya mkononi kwa mjini ambapo watoto wa kike hulaghaiwa na vijana kwa kuahidiwa simu; kushuka kwa hali ya kujifunza na mfumo wa elimu nchini, ukosefu wa ajira hususani kwa vijana wa kiume, kubadilika kwa mfumo wa maisha ambapo utamaduni uliokuwa umejengeka katika jamii kuwa mtoto wa jamii sasa unabakia na mtoto anaonekana kama ni wa familia pekee na hivyo jamii kujiondoa katika ulinzi wa mtoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la ndoa na mimba za utotoni limekuwa na mtazamo mkubwa kwani jamii imekuwa na maoni tofauti kutokana na makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya watoto; watoto ni rasilimali muhimu ya maendeleo ya Taifa lolote, ili watoto waweze kukua na kuwa raia wema, wanahitaji kupewa haki zao za msingi ambapo ni pamoja na kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kutobaguliwa na kushirikishwa. Haya yote yanaongozwa na Sera ya Mtoto ya mwaka 2008 na kutunga Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Aidha, uanzishwaji wa madawati ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi nchini pamoja na kutoa mafunzo kwa polisi hususan masuala ya madawati hayo hayajaongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili dhidi ya watoto. Vitendo vya kikatili dhidi ya watoto vimekuwa vikishamiri nchini, mifano hai ni kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Juni 27, 2016 katika kitongoji cha Moha, kijiji cha Ilugu, kata ya Nyigogo, tarafa ya Itumbili Wilayani ya Magu Mkoani Mwanza, Julius Leonard aliyekuwa na umri wa miaka saba aliuawa kwa kupigwa fimbo na baba yake wa kambo Leonard Joseph kwa kuchelewa kurudi nyumbani baada ya kutumwa kwenda kuchukua *battery*. Mtoto huyu alipigwa mpaka kifo na mwili wake baada ya kuchunguzwa na madaktari ulionyeshwa kuvilia damu ndani kutokana na fimbo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Fungu 52 ni kuwa taarifa ya utekelezaji wa bajeti inaonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2017 Wizara ilikuwa imetengewa jumla ya shilingi 319,000,000,000 sawa na asilimia 40 ya bajeti ya Wizara ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida pamoja na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuhusu fedha za maendeleo, randama zinaonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2017 ni asilimia 37 tu ya fedha za ndani ndizo

zilizotolewa Hazina, na kwa fedha za nje ni asilimia sita tu ya fedha hizo zilizokuwa zimetengwa na Hazina kwa kipindi hicho. Hii ina maana ya kwamba bajeti ya maendeleo kwa fedha za ndani haijatekelezwa kwa asilimia 63, na kwa fedha za nje haijatekelezwa kwa asilimia 94. Kwa utekelezaji huu duni wa bajeti ya maendeleo katika fungu hili Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba Serikali haiko makini kabisa na afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Fungu 53 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 49.9. Kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida 41,000,000,000 na shilingi 8,848,000,000 zikiwa ni fedha za maendeleo. Hata hivyo, fedha za maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Machi, 2017 ni shilingi 497,000,000 sawa na asilimia 5.62 tu ya shilingi 8,000,000,000 zilizoidhinishwa na Bunge hili. Hii maana yake ni kwamba bajeti ya maendeleo katika fungu hili la maendeleo ya jamii haikutekelezwa takribani asilimia 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu hili ndilo linalohusika na vyo vya maendeleo ya jamii, na kwa maana hiyo utekelezaji duni wa bajeti wa vyo hivyo haviwezi kuwa na uwezo wa kujiendesha na kuzalisha wataalam wa kuzisaidia jamii zetu kujiletea maendeleo kwa kuweza kuibua fursa hizo katika jamii zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; Serikali hii ya Awamu ya Tano imekuwa ikijigamba kuwa afya ni mojawapo ya vipaumbele katika utekelezaji wa majukumu yake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitegemea hayo yaonekane katika utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa angalau kwa kutenga asilimia 80 ili kuudhihirisha uhalisia wa majigambo ya hapa kazi tu. Tofauti na tegemeo hilo, Wizara hii ni miongozi mwa Wizara zinazoongoza kwa utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Wizara hii kusema kwamba mojawapo ya vipaumbele vyake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kusimamia upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee, imewasahau wazee kabisa.

Ikumbukwe kwamba Serikali ya Awamu ya Nne ilishatoa uamuzi wa kuwapatia mafao ya uzeeni wazee wote lakini Serikali hii ya Awamu ya Tano imeweka kapuni azimio hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa Serikali kuacha kufanya mzaha na afya za Watanzania. Serikali iache kuwahadaa wananchi kwa kutenga bajeti kubwa ya kushindwa kuitekeleza. Ni vema Serikali ikapanga mipango inayotekelezeka kuliko kupanga mipango yenye lengo la kukidhi matakwana ya kisiasa na kuwaacha wananchi wakihangaika. Ili kukabiliana na maadui watatu yaani umaskini, ujinga na maradhi ni lazima uwekeze katika afya ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya kwa niaba ya Kambi Rasmi humu Bungeni tunakushukuru sana.

**HOTUBA YA MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI, MHESHIMIWA DR GODWIN OLOYCE MOLLEL (MB),
AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA
UPINZANI BUNGENI KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA AFYA,
MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO KWA
MWAKA WA FEDHA WA 2017/2018 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Yanatolewa chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9),
toleo la mwaka 2016)*

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Godwin Oloyce Mollel (Mb), naomba kuwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelazaji wa bajeti ya Wizara husika kwa mwaka wa fedha 2016/17 na makadirio

ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2017/18.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha maoni hayo, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia sisi sote afya njema, na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu wa Bunge la Bajeti tukiwa salama. Kipekee namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda dhidi ya njama na hila za shetani zenye lengo ovu la kudhoofisha jitihada zangu na jitihada za Kambi nzima ya upinzani katika kupigania misingi ya haki na demokrasia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii, kumpongeza kwa dhati Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe (Mb), kwa busara na moyo wake wa ujasiri, ambapo amefanikiwa kuiunganisha Kambi ya Upinzani Bungeni, licha ya vikwazo na changamoto nyingi zinazokabili siasa za upinzani hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sina fadhila, kama sitawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo Bunda Mjini, kwa kuendelea kuniamini na kunipatia ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Napenda kuwaahidi utumishi uliotukuka na kamwe sitawaangusha katika kuhakikisha kwamba maendeleo ya Jimbo letu yanapatikana. Mwisho lakini si kwa umuhimu, naishukuru sana familia yangu, kwanza kwa kunitia moyo, lakini pili, kwa uvumilivu wao hasa pale ninapokuwa mbali nao kwa muda mrefu, kutokana na majukumu yangu ya kibunge.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuzungumzia masuala ya afya, naomba kumnukuu nguli wa Kiswahili, na mwanafasihi mashuhuri Hayati Shaabani Robert. *Alisema hivi: "Msema kweli hukimbiwa na rafiki zake, nikipatwa na ajali kama hiyo sitawaonea wivu wale wanaodumu na marafiki zao siku zote. Siwezi kuikana kweli kwa kuhofia upweke wa kitambo na kujinyima furaha ya milele inayokaribia kutokea baada ya kushindwa kwa uongo".*

Mheshimiwa Spika, Maneno haya ni muhimu na ya faraja sana kwa wote walioamua kusimama na kuupinga unafiki mkubwa dhidi hofu, ubinafsi, ubabe, matisho, kujipendekeza, dhulma na ufedhuli wowote juu ya haki. Aidha, katika kutafakari maneno hayo ya Shaaba Robert ni vema pia wenye mamlaka, wakakumbuka ahadi namba nane ya TANU inayosema: *“nitasema kweli daima na fitina kwangu mwiko”*. Ninadhani tafakari hiyo itatusaidia kusema ukweli na kuutetea ukweli tunapojadili bajeti ya Wizara ya afya ambayo imebeba maisha ya watanzania wote. Tafuakuri hiyo, itusaidie kuponya afya na nguvu kazi ya taifa hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo za utangulizi, sasa naomba nianze kuzungumzia masuala yanayohusu wizara hii.

2. MKANGANYIKO WA KIUTENDAJI NDANI YA WIZARA YA AFYA

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mkanganyiko mkubwa juu ya utendaji wa Wizara ya afya hapa nchini. Wizara hii imekosa uhuru wa kiutendaji, na utekelezaji wa shughuli zake kutokana na kuingiliana na wizara nyingine. Mkanganyiko huu umesababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi na wadau wa afya hususani katika masuala ya kiutawala, masuala ya kutoa huduma na kupokea huduma kwenye hospitali za wilaya mpaka zahanati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mkanganyiko huu, Wizara imeshindwa kutoa majibu mahususi kwenye changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya afya kwa kigezo kuwa masuala mengine yapo chini Ofisi ya Rais - TAMISEMI na mengine chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hivyo, Wizara hizi huishia kutupiana mpira pale linapotokea suala la uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, tutambue kuwa ni vigumu sana kwa waheshimiwa wabunge kuongelea wizara ya afya bila ya kuongelea pale walipo wapiga kura wao, au wanapoishi watanzania walio wengi. Wizara ya afya kwa mujibu wa hati

Idhini pamoja na mambo mengine, inasimamia sera ya afya na huduma za kinga na tiba, kusimamia na kudhibiti ubora wa dawa, vifaa na vifaa tiba, kusimamia mpango wa afya ya uzazi na mtoto, kuendesha ukaguzi wa huduma za afya katika ngazi mbalimbali, kuongoza na kisimamia taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii n.k

Mheshimiwa Spika, mkanganyiko mkubwa unajitokeza pale ambapo Wizara ya afya inapokuwa pembeni katika kuhakikisha kuwa zahanati, vituo vya afya, na hospitali za wilaya zinakuwa chini ya jukumu lake la msingi badala ya kuiachia majukumu mengine Ofisi ya Rais TAMISEMI na pengine Menejimenti ya Utumishi wa umma. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha Wizara hii inafanya kazi zake vizuri kwa kuweka mfumo utakaoipa Wizara mamlaka kamili katika kutekeleza majukumu yake yote badala ya kutumia mwingiliano wa kimajukumu kama kichaka cha kukwepa utelekezaji wa majukumu ya Wizara hii.

3. HALI YA SEKTA YA AFYA NCHINI

Mheshimiwa Spika, Sote tunatambua suala la afya ni suala la ‘msingi’ katika ustawi wa taifa (primary concern). Ili kuhakikisha taifa linakuwa na watu wenye afya bora, serikali ina jukumu la kuhakikisha hali ya utoaji huduma ya afya mijini na vijijini inaboreshwa ili kupunguza maradhi, vifo na hivyo kuongeza umri wa kuishi (life span).

Mheshimiwa Spika, katika azimio la Alma Ata la mwaka 1978, (Declaration of Alma Ata), liliazimia kuwa nchi zote duniani ni lazima kuwa na huduma za afya ya msingi (Primary health care) mpaka mwaka 2000. Azimio hilo lilikwenda mbali zaidi likizitaka nchi zote kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma za afya haziishii kwenye kupunguza magonjwa tu bali pia kuhakikisha haki za binadamu zinazingatiwa katika utoaji wa huduma za afya na tiba.

Mheshimiwa Spika, Mpaka sasa Serikali hii ya CCM haijaweza kutekeleza azimio hili la Alma Ata ipasavyo, kutokana na kushindwa kutoa huduma za afya za msingi zinapatikana

kwa uhakika hususani maeneo ya vijijini, na pia imeshindwa kutoa huduma hizo kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Tume ya Takwimu nchini (NBS) kufikia mwishoni mwa mwaka 2015, jumla ya hospitali za serikali na zile za binafsi ni 252 sawa na 3.4%, vituo vya afya 718 sawa na 9.5%, na jumla ya zahanati 6549. Hii ikiwa ni jumla ya vituo 7,519 vinavyotoa huduma za afya nchi nzima. Hii ina maana kwamba takribani wananchi milioni 56 kwa mujibu wa tume ya Taifa ya takwimu ya mwezi March 2016, wanategemea idadi hii ndogo ya vituo vya kutoa huduma ya afya nchi nzima ambapo kimsingi idadi hii haikidhi hata nusu ya mahitaji yanayoendana na ongezeko hili la watu nchini.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa idadi ya watu nchini inakuwa kwa kasi sana huku miundo mbinu hii ya afya ikishindwa kuendana na kasi ya ukuaji huo. Kwa mujibu wa Takwimu za Tanzania Demographic and Heath Survey (TDHS) 2015/16, wastani wa kujifungua kwa wanawake wa Tanzania ni kuanzia **watoto 5.2**. Hii ina maana kwamba idadi ya watu nchini itaendelea kuongezeka kwa kuwa mpaka sasa wastani wa kujifungua kwa wanawake waishio vijijini ni kuanzia watoto 6.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili kubwa na la kasi linaonyesha kwamba, nchi ni lazima iwe na mpango wa ukuaji wa sekta ya afya unaoendana na kasi ya ukuaji wa watu na teknolojia. Ikiwa na maana ya kuongeza hospitali za utoaji wa huduma maalum, hospitali za rufaa za Kanda, Mikoa, Wilaya, mpaka zahanati zenye uwezo wa kutoa huduma kwa wagojwa wengi zaidi ili kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na magonjwa ambayo yangeweza kupata tiba (Death due to illness)

Mheshimiwa Spika, Mpaka sasa takribani Kanda tatu hazina hospitali za Rufaa za Kanda kuacha hospitali za Rufaa za Mikoa. Mfano, Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Singida, na Dodoma ambapo ndipo Makao Makuu ya nchi hakuna hospitali ya Rufaa ya Kanda ukiachilia mbali za mikoa na

hospitali ya magonjwa maalum ya Mirembe. Hali kadhalika kwa kanda ya Kusini yenye mikoa ya Lindi na Mtwara na Kanda ya Magharibi mikoa ya Katavi, Tabora na Kigoma. Mikoa yote hii imekuwa ikitegemea hospitali za mikoa pekee ambazo zinazidiwa na wingi wa wagonjwa na haziendani kabisa na ongezeko la idadi ya watu katika mikoa husika.

Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (National Five Year Development Plan 2016/17-2020/21 ukurasa wa 266; serikali ilikusudia kutenga shilingi bilioni 80 kwa mwaka wa fedha 2016/17 na bilioni 80 pia kwa mwaka 2017/18 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za Kanda ya Kusini, Magharibi, Kaskazini na Kanda ya Ziwa ili kupunguza tatizo la uhaba wa hospitali nchini .

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua je, serikali imeanza kujenga hospitali hizo za Rufaa za Kanda kama zinavyoonyeshwa katika Mpango wa Mandeleo wa miaka mitano? Na kama bado, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa hospitali hizo zinajengwa kama ilivyokusudiwa katika mpango huo?

4. UPUNGUFU WA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA NCHINI

Mheshimiwa Spika, hali ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini ni mbaya sana. Siku zote Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikilisema jambo lakini serikali haijalichukulia kwa uzito wake. Upatikanaji na utoaji wa huduma za afya umekuwa na changamoto lukuki zikiwemo ufinyu wa bajeti, upungufu wa watoa huduma za afya, ukosefu wa mawasiliano, usafiri na uhaba wa vitendea kazi na zaidi uwepo wa mikakati isiyoendana na mabadiliko ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana kwamba mikakati mingi tuliyonayo katika sekta ya afya nchini haiwezi kutatua changamoto za afya kutokana na kushindwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi kijamii na kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, Katika tafiti zilizochapishwa na jarida la uchumi na fedha la nchini Canada Mwezi Juni 2016, lilieleza kwa kina matokeo ya tafiti iliyofanywa nchini Tanzania juu ya changamoto za upatikanaji wa huduma za afya nchini (Challenges hindering the accessibility of Tanzania's health services) zinaonyesha kuwa takribani 45% ya wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilometa 1, huku 93% wakilazimika kutembea zaidi ya kilometa 10 kufuata huduma za afya. Vilevile Shirika la Sikika lilibaini takribani 80% ya Watanzania waishio vijijini hutembea zaidi ya kilometa 5 kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalazimika kwenda mbali sana kutafuta huduma za afya hali inayopeleka kuongezeka kwa vifo ambavyo vingeweza kuepukika endapo huduma zingepatikana kwa urahisi katika maeneo ya karibu. Maeneo mengi ya nchi bado hayana zahanati za kutosha, vituo vya afya na hata hospitali za wilaya ambapo vituo hivi vya kutolea huduma vinapaswa kuwa karibu zaidi na wananchi hususani maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, yapo maeneo ambayo hospitali za wilaya zinabeba majukumu makubwa ya hospitali za mikoa na vituo vya afya vikibeba majukumu ya hospitali za wilaya n.k Sisi Waheshimiwa Wabunge tumeyashuhudia hayo katika maeneo yetu. Mfano, kwa muda mrefu sasa, kituo cha afya cha Manyamanya kilichopo Bunda mjini kimekuwa kikitumika kama hospitali ya Wilaya huku mgao wa bajeti na vifaa tiba vikiendelea kutolewa kwa mgao wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuwa kituo hiki kimekuwa kikitoa huduma kubwa na muhimu kwa wananchi wa Bunda kutokana na umuhimu wake kijografia, bado mpaka leo kituo hiki cha afya hakina chumba cha kuhifadhia maiti jambo ambalo limesababisha kituo hiki kushindwa kupandishwa hadhi kwa muda mrefu sana huku majukumu yake yakibeba hadhi ya hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hilo, hospitali ya mji wa Tarime ambayo inatumika kama hospitali ya Wilaya inahudumia idadi kubwa sana ya wananchi wakutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya mji wa Tarime. Baada ya halmashauri kugawanywa serikali iliishusha hadhi hospitali hii ya Wilaya kuwa hospitali ya mji, huku mganga mkuu wake akiwa ni TMO. Bado mpaka leo kwenye vitabu hospitali hii inasomeka kama hospitali ya Wilaya ya Tarime (Tarime District Hospital). Hospitali hii imekuwa ikielemea na mzigo mkubwa wa kutoa huduma kuliko uwezo wake kwani watu wanaotoka nje ya mji wa tarime hutumia hospitali hii pia. Tukumbuke kuwa halmashauri ya mji wa Tarime haina hata kituo kimoja cha afya japo serikali iliahidi kujenga vituo vinne katika mwaka wa fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, matatatizo makubwa yanayojidhihirisha hapa ni pamoja na:

- serikali kushindwa kuweka mipango ya ufuatiliaji wa vituo vya kutolea huduma ya afya vinavyoendana na uhitaji wa huduma ya afya
- Kugawa majimbo kisiasa bila kuzingatia huduma za msingi za eneo husika, idadi ya watu na rasilimali zilizopo
- Serikali kukosa mpango wa uendelezaji na ufuatiliaji wa mipango inayojiweka.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmiya Upinzani Bungeni, inaitaka serikali kuacha hadaa katika masuala ya kimsingi ya afya za wananchi. Tabia ya serikali ya kuweka pamba masikioni pale ambapo waheshimiwa wabunge wanaleta kero hizi za msingi zinazohitaji ufumbuzi wa haraka lakini inachukua takribani miaka kumi mpaka ishirini kutatua tatizo dogo inazidi kudhihirisha kuwa *"hatuwezi kupata suluhisho la matatizo kwa kutegemea uwelewa ule ule uliotengeneza tatizo hilo"*.

5. UPUNGUFU WA WATUMISHI KATIKA SEKTA YA AFYA

Mheshimiwa Spika, uhaba wa wahudumu wa afya ni tatizo sugu linaloonekana kuelemea serikali. Tatizo hili lipo kwenye ngazi zote kuanzia kwenye zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa mpaka hospitali ya Taifa na linalenga taaluma zote za afya ambazo ni madaktari, wauguzi, mafundisanifu, wataalamu wa miali, wafamsia, watoa dawa, na maafisa dawa wasaidizi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya madaktari wenza wa Afrika (Africa Cuamm) '*Ukuaji wa rasilimali watu kwa ajili ya afya katika Tanzania*' ;Tanzania ina upungufu wa wataalamu wa afya kama ifuatavyo:

- Madaktari bingwa (Specialist doctors) kwa 58.1 %
- Wauguzi wa sekta ya umma II (Public health nurses II) kwa 54.4%
- Wataalamu wa miale (Radiographers) kwa 50.8%
- Maafisa kliniki (clinical officers) kwa 50.0%
- Waganga wasaidizi na waganga wasaidizi wa meno(assistant medical officer/assistant dental officer) kwa 46.2%
- Wafamasia(pharmacist) 49.9%
- Mabwana afya (health officers) kwa 45.7%
- Mafundisanifu wa maabara (laboratory technicians) kwa 41.5%
- Maafisa kliniki wasaidizi (assistant clinical officers) 40.7%

- Madaktari (medical doctors) kwa 37.3%
- Maafisa wauguzi (nursing officers) 33.2%
- Makatibu wa afya (health secretaries) kwa 27.1%
- Makatibu wa afya (health secretaries) kwa 21.8%.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha pia kwamba, zaidi ya asilimia 74% ya madaktari waliopo nchini, wanafanya kazi maeneo ya mijini. Hii ina maana kwamba, wananchi walio wengi ambao wanaishi vijijini wanahudumiwa na asilimia 26 tu ya madaktari. Aidha uwiano kati ya daktari mmoja na wagonjwa anaohudumia ni wa kutisha. Daktari mmoja anahudumia wagonjwa 78,880 kwa maeneo ya vijijini kinyume kabisa na maelekezo ya Shirika la afya duniani ambapo daktari mmoja anatakiwa kuhudumia wagonjwa elfu moja. (1:1,000).

Mheshimiwa Spika, uhaba huu mkubwa wa watumishi katika sekta ya afya umekuwa ni jipu lililoshindikana kutumbulika. Pamoja na uhaba huu mkubwa wa watumishi, serikali ya awamu ya tano iliamua kuweka afya ya watanzania rehani kwa kuruhusu hao hao madaktari wachache ambao ndio tegemeo la watanzania kwenda nchini Kenya kuwahudumia raia wa Kenya huku raia wake wakipata adha kubwa ya matibabu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) kupinga uamuzi wa serikali kupeleka madaktari 500 nchini Kenya, bado Serikali ilipuuza maoni ya Chama cha madaktari mpaka pale serikali ya Kenya ilipositisha ombi la uhitaji wa madaktari. Kitendo kilichofanywa na serikali cha kuipigia debe nchi ya Kenya na kujigamba kuwapa madaktari huku ikijua dhahiri Tanzania inakabiliwa na uhaba wa wataalamu hao pengine kuliko nchi ya Kenya ni kitendo kisicho cha kizalendo na

kimedhihirisha nia mbaya ya serikali ya awamu ya tano kwa wananchi wake wanaoteseka kwa kukosa huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jambo hilo lililokosa uzalendo, Mwezi April mwaka huu wa 2017 Waziri wa Afya alitangaza kuwa Mheshimiwa Rais ameamuru madaktari 258 walioomba kufanya kazi Kenya waajiriwe mara moja. Jambo hili sio tu limewashangaza Watanzania bali Ulimwengu kwa ujumla. Serikali hii imefanya maamuzi ya ajabu ambayo hayakuwahi kutokea katika historia ya nchi hii tangu uhuru. Kitendo cha serikali kuwaajiri madaktari walioomba ajira nje ya nchi na kuwatupia kapuni mamia ya madaktari ambao kwa namna moja au nyingine walionyesha uzalendo wa kutamani kuitumia nchi yao ni kitendo cha kibaguzi na kikatili sana kwa wazalendo wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya upinzani, inapata wasiwasi juu ya uwezo wa serikali katika kuratibu na kupambanua vipaumbele vyake (coordination and prioritization). Serikali imeshindwa kabisa kujua kama nchi hii ina huduma duni za afya na inakabiliwa na uhaba wa watendaji katika sekta ya afya kuliko Kenya. Katika ripoti ya Benki ya Dunia ya mwezi Mei, 2016, *“Tanzania Service Delivery Indicators”* inaonyesha kuwa, utendaji wa sekta ya afya na maendeleo ya sekta hii katika nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania na Kenya. Serikali hii pengine itueleze na itoe *takwimu sahihi*, juu ya watumishi katika sekta ya afya kwa kuwa hali inaonyesha dhahiri takwimu hizo hazikuwepo wizarani na ndio maana serikali ikawa radhi kupeleka madaktari nje ya nchi ilhali hospitali nyingi majimboni zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa madaktari.

Mheshimiwa Spika, wahenga wanasema *“mtu mzima akivuliwa nguo huchutama”*. Hivyo basi, serikali ni lazima ijue kuwa ilipotoka na ijisahihishe katika hili. Hatuwezi kuendelea kuhubiri uzalendo kwa maneno bila vitendo. Kuna mithali ya kingereza inasema *“one’s first responsibility is for the needs of one’s own family”* kwa tafsiri isiyo rasmi ikiwa na maana kwamba *‘jukumu binafsi la kwanza ni kwa ajili ya mahitaji ya*

familia yako mwenyewe. Hivyo basi, Kambi rasmi ya upinzani inapendekeza mambo yafuatayo:

i. Serikali itoe tamko kuhusu maamuzi yake ya kutaka madaktari waende nchini Kenya kutoa huduma kwa wananchi wa Kenya huku ikijua Tanzania tuna uhaba mkubwa wa watoa huduma wa afya.

ii. Serikali ilieleza Bunge, mpaka sasa mwaka 2017 Tanzania inakabiliwa na uhaba wa watumishi wa afya kwa asilimia ngapi huku ikizingatia kuwa kwa muda mrefu ilisitisha zoezi la kutoa ajira nchini?

iii. Serikali ituambie imepanga kutoa ajira ngapi katika sekta ya afya kwa mwaka huu wa fedha 2017/18 zenye uhakika katika utelekezaji? Katika hili serikali izingatie imewaacha mamia ya madaktari wakikosa ajira nchini kwa sababu ya uzalendo wao wa kutamani kuitumia nchi zaidi kuliko kwenda nje.

iv. Kitendo cha madaktari 258 kujitokeza kwenda nchini Kenya kimeonyesha kuwa kuna madaktari wengi nchini ambao wanapenda kufanya kazi nje ya nchi kwa sababu mbalimbali. Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maslahi ya watumishi katika sekta ya umma yanaboreshwa ikiwa ni pamoja wa uhakika wa kupata call allowance, overtime, na nyumba za watumishi wa afya hususani maeneo ya vijijini?

6. KANSA YA SHINGO YA KIZAZI

Mheshimiwa Spika, saratani ni miongoni mwa maradhi mengi yanayoisumbua jamii kubwa duniani. Zipo saratani za aina nyingi, lakini saratani ya shingo ya kizazi ndiyo inayoongoza kwa vifo vya akina mama. Takwimu zinaonyesha kwamba saratani ya shingo ya kizazi husababisha vifo 274,000 duniani kote kila mwaka, ambapo kila baada ya dakika mbili, mwanamke mmoja hufariki kutokana na saratani ya shingo ya kizazi. Katika kila

wanawake wawili wanaofariki kwa saratani, mmoja hufariki kwa saratani ya shingo ya kizazi.

Mheshimiwa Spika, asilimia 85 ya vifo vinavyotokana na saratani ya shingo ya kizazi hutokea katika nchi zinazoendelea. Barani Afrika, kwa ukanda wa mashariki asilimia 33.6 ya wanawake wote wanasadikiwa kuwa na virusi vinavyo sababisha ugonjwa huo, navyo vinaitwa human *papilloma virus* (HPV).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Daktari Bingwa wa magonjwa ya Saratani hapa Tanzania Dr. Harrison Chuwa ni kwamba, *wagonjwa wanaokwenda kutibiwa katika Hospitali ya Ocean Road, takriban wagonjwa 22,000 kwa mwaka ni wagonjwa wa Saratani ya Shingo ya Kizazi. Aidha saratani hiyo ndiyo inayoongoza kwa idadi kubwa ya wagonjwa - takriban 40% ya wagonjwa wote wa saratani hapa nchini.* Ugonjwa huu huwaathiri wanawake wengi wa rika zote walio katika umri wa kuzaa, ikiwapata zaidi wanawake wenye umri wa miaka 45 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa huu huchukua zaidi ya miaka 15 mpaka 20 kugundulika lakini kabla ya kujitokeza bayana hutokea mabadiliko kadhaa yanayoweza kugundulika mapema na kufanikiwa kuzuilika katika hatua za mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa hospitali ya Ocean Road imezidiwa na wingi wa wagonjwa wanaokwenda kupata huduma ya mionzi. Wagonjwa hawa hulazimika kutumia fedha nyingi sana kusafiri mpaka jijini Dar es Salaam, malazi na huduma nyingine katika hali hii ngumu ya maisha ili kufuata huduma ya mionzi jambo ambalo linawaongezea msongo wa mawazo na kuugua zaidi.

Mheshimiwa Spika, serikali ni lazima iangalie jambo hili kwa kina, na iwe na huruma kwa wananchi wake. Ni wakati sasa ni kkuona namna bora ya kuboresha huduma kwenye hospitali za mikoa, wapate mashine hizi ili kuokoa maisha ya kina mama wengi na hata kurefusha maisha yao kwa

kuwapunguzia msongo wa mawazo ambao pia unachangiwa na hali ngumu ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ugonjwa huu wa saratani ya shingo ya kizazi unazidi kushamiri hapa nchini; na kwa kuwa ugonjwa huu umekuwa sababu kubwa ya vifo vingi vya kina mama wenye umri uliotajwa; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua Serikali imeweka mkakati gani wa makusudi katika bajeti hii ya 2017/18 kukabiliana na ugonjwa huu ambao umepoteza maisha ya mama zetu?

7. HUDUMA YA AFYA YA MAMA NA MTOTO

Mheshimiwa Spika, katika dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, lengo kuu la dira hiyo ilikuwa ni kuhakikisha maisha bora kwa Watanzania wote (high quality of life for all Tanzanians) na kuhakikisha kuwa sekta ya afya nchini inapewa kipaumbele ili kufikia lengo. Hii ni pamoja na kutoa kipaumbe kwa kina mama wa kitanzania kupata huduma bora ya afya kwa kuwa wao ndio walezi wa kwanza wa Taifa letu. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuboresha afya ya mama na mtoto kwa kutoa huduma bora ya afya ya uzazi.

Mheshimiwa Spika, Bado idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi kwa kina mama ni kubwa. Kwa mujibu wa ripoti ya shirika la tafiti za afya lisilo la kiserikali la Sikika kuhusu *'Tafsiri rahisi ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM 2007-2017'* inaonyesha kuwa akina mama 578 kati ya vizazi hai 100,000 hufariki dunia kutokana na matatizo ya uzazi. Takwimu za serikali zinaonyesha makadirio ya takribani kina mama 42 hufariki kila siku kutokana na changamoto za uzazi. Hii ikiwa na maana kwamba, kina mama 1,255 hufariki kila mwezi na kina mama 15,056 hufariki kila mwaka. Taarifa hiyo inaonyesha pia kwamba, ni asilimia 46 tu ya kina mama ambao wanaojifungua chini ya uangalizi wa wataalamu wa afya.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na hali hiyo, serikali isipochukuwa hatua mahususi tutapoteza kina mama wengi ambao huleta faraja katika hii dunia kwa kutuletea watoto

.Kwa uhalisia ni kwamba ,serikali haitaweza kuyafikia malengo ya kupunguza vifo vya kina mama kutokana na kukosa umakini katika kutelekeza sera za afya kutokana na changamoto za kibajeti, changamoto za miundo mbinu ikiwemo vyumba za kujifungulia,magari ya kubebea wagonjwa na vifaa vya kufanyia upasuaji, elimu ya uzazi wa mpango na uzembe wa baadhi ya watoa huduma ya afya.

7.1 Uhaba wa Chanjo nchini

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 wananchi na wadau wa sekta ya afya walieleza malalamiko yao kuhusu upungufu wa dawa pamoja na chanzo mbalimbali ikiwemo chanjo za watoto wachanga.

Mheshimiwa Spika, chanjo kwa watoto wachanga ni muhimu sana katika kuimarisha afya ya mama na mtoto. Katika hali isiyokuwa ya kawaida chanjo muhimu kwa watoto wachanga wanazopatiwa mara tu baada ya kuzaliwa zilipungua na kusababisha usumbufu mkubwa kwa akina mama mara baada ya kujifungua. Kwa upande wa mijini chanjo nyingi za watoto zilikuwa zinapatikana kwenye hospitali binafsi ambapo bei yake si chini ya laki moja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mapungufu mengi yaliyojitokeza kwenye suala la chanjo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni sababu gani zilizopelekea uhaba wa chanjo nchini na kuleta kadhia kwa wananchi? Serikali imejipanga vipi kukabiliana na changamoto hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018?

Mheshimiwa Spika, ni hivi majuzi tu Shirika la Afya duniani limezindua mradi wa chanjo ya malaria katika nchi za Ghana, Kenya na Malawi kwa ajili ya majaribio. Ikumbukwe kuwa malaria bado ni tatizo kubwa ambalo linawaathiri zaidi watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kufahamu je, serikali imefanya juhudi gani kuhakikisha kuwa nchi yetu inanufaika na chanjo hiyo huko baadae?

7.2 Changamoto za Kibajeti katika Utatuzi wa Vifo Vitokanavyo na Afya ya Uzazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 serikali ilitoa asilimia 25 tu ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya upatikanaji wa huduma ya uzazi wa mama na mtoto. Pamoja na hilo fedha zilizotengwa kwa mwaka huu ni shilingi bilioni 12 tu, tofauti na bajeti iliyopita ya shilingi bilioni 13 kwa mujibu wa mchanganuo wa fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/18 kwa Wizara hii fungu 52. Mara nyingi fedha hizi zimekuwa hazitolewi kama zilivyopangwa na hivyo kushindwa kabisa kumaliza matatizo ya afya kwa mama na mtoto na hivyo kuendelea kuchangia ongezeko la vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, Wizara ilitengeneza mfumo wa tathimini ya vifo vinavyotokana na uzazi (Maternal and Prenatal Death Review). Mfumo huu ilitengenezwa tangu mwaka 2006 ambapo uliwataka wataalamu wa afya kuhakikisha wanafanya kikao maalum cha kuzungumzia, kutathimini na kutoa taarifa juu ya kifo chochote kinachotokana na uzazi (case management). Lengo kuu la Shirika la afya duniani (WHO) katika kuanzisha mpango huo, ni kuhakikisha uwajibikaji wa hali ya juu kwa watoa huduma ya afya. Hata pale ambapo kifo cha mama kimetokea katika mazingira ya nyumbani inahitajika kikao cha kujadili chanzo cha kifo hicho.

Mheshimiwa Spika, Tathimini ya kifo chochote cha uzazi inapaswa kufanyika ndani ya masaa 24 na taarifa ya kifo inapaswa kuhifadhiwa katika jalada la marehemu. Mfumo huu wa MPDR unasaidia kupata taarifa zote zinazopelekea vifo wakati na baada ya kujifungua. Taarifa hizi ni muhimu kwani zinasaidia katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kutatua changamoto za ucheleweshaji wa rufaa na tathimini ya uwepo wa vifaa vinavyohitajika katika masuala yote ya uzazi, pamoja na uwepo wa damu ya akiba kwa kina mama wakati ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona uzembe mkubwa ndani ya wizara hii ambapo fedha nyingi zinatumiwa katika kutengeneza program nyingi lakini utekelezaji wake unakuwa hafifu sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua mpango wa serikali katika utekelezaji wenye tija wa mpango huu ili kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

7. KUKABILIANA NA TATIZO LA AFYA YA AKILI NCHINI

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wenye matatizo ya afya ya akili nchini. Katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilizungumzia ongezeko hili la watu wenye matatizo ya akili. Lakini kutokana na serikali kutokuchukulia tatizo hili kwa uzito wake, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeona ni vyema ikalirudisha jambo hili kwa upana ili serikali hii ya CCM iweze kutambua kuwa hakuna taifa linaloweza kuendelea endapo afya ya akili ya watu wake si salama.

Mheshimiwa Spika, magonjwa mengi ya akili kama vile huzuni kupindukia (bipolar disorder), hali ya wasiwasi (schizophrenia) na magonjwa ya akili (mental disorders) yanachangiwa na mambo mengi kwani huleta mabadiliko katika umbo la ubongo ambapo mabadiliko hayo huathiri hisia na tabia za watu, mazingira ya mtu, uhusiano wake na watu wengine n.k Japo, mapitio mengi ya taarifa yanaonyesha magonjwa ya akili nchini Tanzania hutokana na matatizo ya kurithi (inherited problem)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko kubwa la watu wenye matatizo ya akili ambapo kwa mwaka 2013/2014 takwimu zilionyesha kuna takribani watu 450,000 na wenye matatizo ya akili nchini. Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini kuwa kwa sasa takribani wagonjwa 150 mpaka 200 huudhuria kliniki za watu wenye magonjwa ya akili kwa wiki mkoa wa Dar es Salaam pekee.

Mheshimiwa Spika, ukubwa wa tatizo hili hauendani kabisa na rasilimali zilizopo katika kukabiliana na tatizo. Katika sekta

ya afya Idara ya kuhudumia wagonjwa wa akili ni Idara iliyosahauulika kabisa.Ni moja ya Idara inayopaswa kuangaliwa kwa kina zaidi.

Mheshimiwa Spika, nchi nzima ina takribani madaktari 26 tu wanaoshughulikia matatizo ya afya ya akili nchini. Wengi wa madaktari hawa wanahudumia hospitali za Rufaa pekee .Mfano Kwa Dar es Salaam kuna madaktari takribani 8 tu wanaotoa huduma katika hospitali ya Muhimbili Idara ya afya ya akili, Mwananyama na Temeke, hospitali maalum inayoshughulikia masuala ya afya ya akili Mileembe –Dodoma ina jumla ya madaktari 5 tu,Bugando daktari 1, KCMC kwa sasa haina daktari hata mmoja huku hospitali ya Mawenzi Moshi iliyokuwa inatoa huduma hiyo imebaki na nesi mmoja tu ambae anauzoefu wa muda mrefu wa kutoa huduma hiyo baada ya kufariki kwa daktari bingwa Marehemu Dr. Ringo.

Mheshimiwa Spika, hospitali hizi zinazotoa huduma za afya ya akili zina hali mbaya kwani mpaka sasa hospitali ya Muhimbili ina vyumba viwili tu ambapo kimoja ni cha wagonjwa wa kiume na kingine ni cha wagonjwa wa kike. Pamoja na hayo,kuna chumba kimoja tu cha wagonjwa wenye matatizo makubwa kwani wengi wao hufanya fufanya fujo,kupiga kelele n.k(acute ward)Chumba hiki ni kwa wagonjwa na kiume pekee .Pale inapotokea mgonjwa wa kike wa aina hiyo basi inalazimu mgonjwa huyu achanganywe na wengine jambo ambalo ni hatari sana kwani ilishawahi kutokea mgonjwa wa aina hiyo kumuua mwezake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa vyumba na vitanda inalazimu wagonjwa ambao wamepata unafuu kuruhusiwa haraka hata kama hawajapona vizuri ili kupisha wengine wenye hali mbaya zaidi. Kwa kuwa wagonjwa wengi wamepata tatizo kwa sababu ya kurithi unakuta ni vigumu sana kuweza kumudu matibabu kwani kuna familia hujikuta zikiwa na wagonjwa zaidi ya watatu na hivyo kuathiri hata wale wanaowategemea kuchumi.

Mheshimiwa Spika, dawa za magonjwa ya akili nchini ni chache sana na hazipatikani kwa urahisi. Dawa nyingi hutengeneza usugu kwa wagonjwa kutokana na kwamba wanalazimika kuzitumia kwa muda mrefu. Pale ambapo inalazimu kubadilishiwa inakuwa ni vigumu kwa kuwa dawa zake ni za gharama kubwa, kwani dozi moja inaweza kugharimu zaidi ya shilingi laki mbili jambo ambalo Watanzania wengi hawawezi kuzimudu.

Mheshimiwa Spika, ni wa wakati muafaka sana kwa serikali kuanza kuchukua hatua za dharura. Mpaka sasa chuo cha kutoa mafunzo ya udaktari cha Muhimbili kitengo cha magonjwa ya akili kina wanafunzi wachache sana. Kwa mwaka wa kwanza kuna mwanafunzi mmoja, na kwa mwaka wa tatu kuna mwanafunzi mmoja tu. Mpaka sasa hospitali hii inategema madaktari ambao ni wanafunzi watano na mbobezi (Specialist) mmoja ambae amepewa majukumu mengine ya kufundisha pia. Japokuwa serikali imefungua kitengo kipya cha wanasaikolojia bado wanafunzi ni wachache sana na walimu ni wanne tu ambao ni wahadhiri wasaidizi pekee.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza yafuatayo

1. Serikali ilichukue tatizo hili kwa hali ya upekee kabisa
2. Kwa kuwa tatizo hili ni kubwa, na linapojitokeza katika familia lina madhara makubwa ya kiuchumi na kijamii kwani wengi wao hawawezi tena kumudu maisha yao na pia hawawezi kumudu gharama za matibabu ambazo ni nyingi sana kwani wengi hulazimika kusafiri kutoka mikoani mpaka Dar es Salaam au hospitali za Rufaa ambapo ndipo hupata huduma za matibabu. Hivyo basi serikali iweze kutoa ruzuku katika dawa hizi ili wagonjwa wengi zaidi waweze kunufaika.
3. Serikali ichukue jitihada za makusudi za kuhamasisha watanzania kujiunga na taaluma hii ili kuokoa maisha ya Watanzania wengi.

4. Kwa kuwa tatizo la magonjwa ya afya ya akili huendana na unyanyapaa. Vilevile mara nyingi jamii imekuwa ikihusisha tatizo hili na masuala ya ushirikina Ni vyema sasa serikali ianze kutoa elimu ya kutosha kwa jamii.

5. Serikali iangalie namna bora ya kuboresha huduma katika vituo hivi vya kutolea huduma kwa wagonjwa wa akili na ihakikishe hospitali za Wilaya, Vituo vya afya na zahanati zinaanza kutoa watu watakao jifunza kuhusu masuala ya afya ya akili ili kuanza kutoa huduma kule chini kwa wananchi. Na katika ameneo ambapo wataalamu hawa ni wachache basi wafanye kazi za kitaalamu badala ya kupewa majukumu mengine. Hili litapunguza mrundikano wa wagonjwa katika hospitali za Rufaa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inasikitika sana kuona Wizara hii ikianza na unyanyapaa mkubwa kwa Idara hii kutokana na kutokutenga bajeti ya kusaidia vitengo vya afya ya akili nchini. Mwana falsafa mmoja aliwahi kusema **“unexpressed emotions will never die,they are buried alive and will come forth later in uglier ways”**. Kwa tafsiri isiyo rasmi ikiwa na maana kwamba hisia zilizofichika huwa hazipotei, hutulizwa tu katika uhai wake na siku moja zinaweza kuibuka vibaya zaidi.Ni muhimu sasa serikali ikasikia kilio hiki cha kugugumia cha vitengo na Idara zote zinazohusika na huduma ya afya ya akili ili kuweza kutatua changamoto zilizopo na kuwasaidia wale wote wanaokumbwa na matatizo ya akili nchini.

9. UDHIBITI WA UPUNGUFU WA DAWA NCHINI

Mheshimiwa Spika, upungufu wa dawa na vifaa tiba, umekuwa ni changamoto kubwa katika sekta ya afya duniani. Hata hivyo, kwa nyakati tofauti serikali imetoa kauli zinazokinzana kuhusu tatizo hilo. Kutokana na hali hiyo, Mheshimiwa Upendo Peneza – Mbunge wa Viti Maalum aliandaa hoja binafsi akiliomba bunge liazimie kuitaka serikali kubadili mfumo wa bajeti ya dawa ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa dawa nchini. Hata hivyo, hoja hiyo hoja hiyo haikupata nafasi ya kuingia bungeni kutokana na kukosa

nafasi katika ratiba ya shughuli za bunge katika Mkutano wa Sita wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya hoja yake, alirejea Ripoti ya utafiti uliofadhiliwa na Benki ya Dunia juu ya Mabadiliko ya dawa na vifaa tiba (Pharmaceuticals Reform) ya mwaka 2011, ambayo inaeleza kwamba; licha ya ukweli kwamba dawa ni kiungo muhimu cha ufanisi wa mfumo mzima wa afya, bado kumeendelea kuwa na upungufu wa dawa muhimu katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti huo, kila mwaka watoto zaidi ya milioni 10 hufariki katika nchi zinazoendelea kutokana na magonjwa ambayo yangeweza kuzuliwa au kutibiwa na chanjo au dawa zilizopo. Aidha, inakadiriwa kwamba wanawake 1,000 hufariki kila siku kutokana na matatizo wakati wa ujauzito au wakati wa kujifungua ambao wengi wao wangeweza kuokolewa kwa kupata uangalizi stahiki – ikiwemo kuwapatia dawa shahili.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Shirika la Global Health Tanzania, asilimia ya vifo vinavyosababishwa na magonjwa ambayo yanaweza kutibiwa au kupunguzwa makali yake kwa dawa hapa nchini ni kama ifuatavyo:

- i. UKIMWI – asilimia 17
- ii. Maambukizi ya Mfumo wa chini wa Upumuaji (Lower Respiratory Infections) – asilimia 11
- iii. Malaria – asilimia 7
- iv. Kuhara – asilimia 6
- v. TB – asilimia 5
- vi. Kansa – asilimia 5 nk.

Mheshimiwa Spika, suala la ukosefu wa dawa hapa nchini pia halikuanza juzi wala jana. Utafiti uliofanywa na shirika lisilo la Kiserikali la Sikika mwaka 2011 ulibaini kwamba kati ya wilaya 71 zilizofanyiwa utafiti, asilimia 48 ya wilaya hizo hazikuwa kabisa na pamba (absorbent gauze) inayotumika hospitalini kama kifaa tiba kwa matumizi mbalimbali kama

vile kusafisha vidonda na kwa akina mama wanaojifungua. Katika utafiti huo, ni asilimia 8 tu ya wilaya zilizofanyiwa utafiti zilikuwa na pamba hizo kwa kiwango cha kutosha kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hospitali na vituo vya afya, utafiti ulibaini kwamba, kati ya hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya (health facilities) 30 vilivyofanyiwa utafiti, asilimia 37 ya hospitali au vituo hivyo havikuwa kabisa na pamba hizo. Ni asilimia 10 tu ya hospitali au vituo hivyo vilikuwa na kiasi cha kutosha cha pamba hizo. Aidha, utafiti unaendelea kuonyesha kwamba; miongoni mwa sababu za upungufu ni kutokana na ukweli kwamba ; pamba hizo zilikuwa hazifiki kwa wakati katika hospitali na vituo vya afya. Wakati mwingine hospitali na vituo vya afya vililazimika kusubiri kwa takriban miezi miwili kupokea pamba walizoagiza kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kupitia kwa maafisa afya wa wilaya (DMO's). Utafiti unaonyesha pia kwamba Maafisa afya wa Wilaya pamoja na wakuu wa hospitali na vituo vya afya hawakuagiza pamba hizo kutoka MSD kwa viwango vinavyotosheleza kutokana na ukosefu wa fedha kwenye akaunti zao za MSD.

Mheshimiwa Spika, katika chapisho la "Policy Brief" lililotolewa na Shirika la Sikaka mwaka 2014 juu ya hitaji la Serikali kuongeza bajeti ya dawa muhimu na vifaa tiba ili kukabiliana na upungufu (Stock Outs) linaonyesha kwamba upungufu wa mara kwa mara wa dawa muhimu na vifaa tiba hapa nchini ni tatizao sugu. Jambo hili limesababisha utoaji duni wa huduma za afya na hivyo kuathiri afya za wananchi.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa iliyotolewa katika chapisho hilo inayosababisha upungufu wa dawa muhimu ni bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya dawa muhimu ambayo haikidhi mahitaji. Kwa mfano, ukiangalia bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2013/14; bajeti hiyo iliongezeka kwa asilimia 30.8 kutoka shilingi bilioni 581.7 mwaka 2012/13 hadi kufikia shilingi bilioni 753.9 mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ni kwamba, ongezeko la bajeti ya afya katika mwaka wa fedha 2013/14 halikuwa na tija au maana yoyote katika bajeti ya dawa muhimu na vifaa tiba kwani bajeti ya dawa muhimu na vifaa tiba ilishuka kwa asilimi 20.5 kutoka shilingi bilioni 80.5 mwaka 2012/13 hadi kufikia shilingi bilioni 64 mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Sikika unaonyesha pia kwamba kwa mwaka wa fedha 2014/15 bajeti ya dawa muhimu na vifaa tiba ilishuka tena kwa asilimia 28.4 kutoka shilingi bilioni 64 mwaka 2013/14 hadi kufikia shilingi bilioni 45.8 mwaka 2014/15.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Upatikanaji wa Dawa Nchini iliyowasilishwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii – Oktoba, 2016; bajeti ya dawa kwa mwaka wa fedha 2016/17 imeongezeka karibu mara nane hadi kufikia shilingi bilioni 251.5 ukilinganisha na bajeti ya dawa iliyotengwa mwaka jana 2015/16 ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 29 tu. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa hiyo, fedha ambazo zilikuwa zimeshatolewa hadi kufikia tarehe 30 Septemba (robo ya kwanza ya mzunguko wa bajeti) zilikuwa ni shilingi bilioni 20 tu sawa na asilimia 7.95 tu ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya dawa.

Mheshimiwa Spika, licha ya taarifa hiyo ya Wizara kuonesha kwamba bajeti ya dawa kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni kubwa (shilingi bilioni 251) lakini katika fedha hizo kuna matumizi ya miradi mingine ya maendeleo ambayo hayahusiki na dawa kama vile ugharamiaji wa wa tafiti mbalimbali, ugomboaji wa magari bandarini, ununuzi wa vitanda, gharama za usambazaji wa dawa nk. Kwa sababu hiyo, kiasi halisi kitakachotumika kwenye dawa tu katika hiyo shilingi bilioni 251 hakijulikani.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba kwa mwenendo huu wa ufinyu wa bajeti ya dawa muhimu na vifaa tiba; sambamba na utekelezaji duni wa bajeti hiyo; tatizo la

upungufu wa dawa na vifaa tiba katika hospitali, zahanati na vituo vyetu vya afya litaendelea kuwepo ikiwa Serikali haitachukua hatua za makusudi za kuongeza bajeti ya dawa ili kuondokana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti nyingi zilizofanyika kuhusu ukosefu au upungufu wa dawa muhimu na vifaa tiba, yanaonyesha kwamba, sababu kubwa inayopelekea ukosefu au upungufu huo ni bajeti ndogo inayotengwa na Serikali kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Hata hivyo, miongoni mwa mapendekezo yaliyotolewa na tafiti hizo ni kuongeza bajeti ya afya angalau kufikia asilimia 15 ya Bajeti Kuu ya Serikali ikiwa ni utekelezaji wa Azimio la Abuja ambapo nchi za Afrika zilikubaliana kwa kauli moja kutenga asilimia 15 ya Bajeti za Serikali zao kwenda kwenye huduma za afya. Itakumbukwa kwamba Tanzania iliridhia kwa kutia saini azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tafiti zinaonyesha kwamba, sababu kubwa ya upungufu wa dawa ni utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo ambayo ndiyo inabeba fedha za dawa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na inaunga mkono mapendekezo ya hoja ya Mheshimiwa Upenzo Peneza (Mb) kwamba; Serikali ibadili mfumo wake wa bajeti ili kutenga fedha za dawa katika kifungu maalum kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida (recurrent expenditure) na kuziwekea fedha hizo zuio (ring fence) kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 na kuendelea. Kinachopendekezwa ni kwamba; matumizi ya fedha katika fungu la matumizi ya kawaida kwenye wizara husika (kwa maana ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais – TAMISEMI) yafuate vipaumbele katika mpangilio ufuatao:

1. **Mishahara**
2. **Dawa za Binadamu na vifaa tiba (ring fenced)**
3. **Matumizi Mengineyo (OC)**

Mheshimiwa Spika, msingi wa pendekezo hili unatokana na ukweli kwamba mahitaji ya dawa na vifaa tiba kwa

wananchi wetu ni mahitaji ya kila siku na hayawezi kusubiri kwa muda mrefu kama miradi mingine ya maendeleo kaitika sekta hiyo hiyo ya afya inavyoweza kusubiri. Kwa mfano utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la hospitali unaweza kusubiri kwa muda fulani ukisubiria fedha, na pia utekelezaji huo unaweza kufanywa kwa awamu na hata ukachukua miaka miwili mitatu kukamilika bila kuathiri maisha ya mwananchi. Fedha za mradi wa namna hii kuwekwa kwenye bajeti ya maendeleo ni sahihi kabisa.

Lakini mgonjwa anayehitaji dawa sasa hivi ili aone, hawezi kusubiri, vinginevyo atapoteza maisha. Kutokana na umuhimu wa kulinda afya na maisha ya wananchi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba, fedha za dawa ziwekewe zuio (ring fence) ili zisitumiwe kwa matumizi mengine yoyote isipokuwa tu kwa manunuzi ya dawa na vifaa tiba. Vifaa tiba vinavyozungumziwa hapa ni vile vifaa vidogo vidogo vinavyohitajika kila siku katika '*administration*' ya dawa kama vele pamba, sindano pamoja na vitendanishi (reagents). Vifaa tiba vikubwa kama vile mashine za mionzi (X-ray) MRI, CT Scan nk. viendeele kuwa chini ya fungu la bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kutenga fedha za dawa na vifaa tiba na kuziweka kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida. Afrika ya Kusini wanafanya hivyo, na hata nchi ya Zambia – jirani zetu wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, licha ya faida tutakayoipata ya kupunguza tatizo la ukosefu wa dawa kwa wananchi wetu kwa kuweka bajeti ya dawa kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida; faida nyingine tutakayoipata ni kwamba tutakuwa tumeweza kutoa huduma za afya kwa wananchi wetu kwa kutumia fedha za ndani kwa kuwa bajeti ya matumizi ya kawaida ni ya fedha za ndani. Kwa kufanya hivyo; tutaingia katika rekodi nzuri ya utekelezaji wa bajeti kwa vigezo vya Benki ya dunia . Nchi inayotekeleza bajeti yake vizuri kwa vigezo vya Benki ya dunia ni ile inayotekeleza bajeti yake ya

matumizi ya kawaida katika kuwapatia wananchi wake huduma za kijamii zinazokidhi mahitaji.

10. LISHE DUNI NA ONGEZEKO LA UTAPIAMLO NA UDUMAVU

Mheshimiwa Spika, katika bunge la bajeti lililopita 2016/2017 Kambi Rasmi ya Upinzani ilizungumzia kwa kina tatizo la upungufu wa lishe na madhara ya utapiamlo kwa Taifa. Pamoja na hayo, bado tatizo la utapiamlo linazidi kuongezeka hususani hivi karibuni ambapo nchi imekumbwa na ukame na ukosefu wa chakula katika maeneo mengi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la utapiamlo ni tatizo kubwa sana kwa nchi kwani ni tatizo lenye madhara ya muda mrefu kwa taifa kwani lina athari kubwa katika ukuaji wa ubongo ikiwa ni pamoja na uwezo wa kufikiri na ukuaji wa maungo kwa watoto wadogo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1991 asilimia 49.7 (takriban nusu) ya watoto chini ya umri wa miaka mitano walikuwa na udumavu. Mwaka 2010, asilimia 42.5 ya watoto wote chini ya umri wa miaka mitano walipata udumavu. Ripoti iliyolewa na taasisi ya utafiti ya REPOA ilionyesha mpaka mwaka 2014 takribani watoto milioni 2.7 walikuwa na udumavu na kati yao watoto 100,000 walikuwa na udumavu uliokithiri. Tafiti zilizofanywa mwaka 2015 zilionyesha kiwango hicho kimepungua kwa mijini na kufikia asilimia 35 wakati vijijini bado tatizo likiwa kubwa kwa takribani asilimia 45. Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na gazeti la Mtanzania la tarehe 18 Machi, 2015 mikoa inayoongoza kwa udumavu ni Dodoma 57.1%, Lindi 53.3%, Iringa 52%, Rukwa 51.4% na Mbeya 51.3% huku mikoa yenye udumavu mdogo ikiwa ni Dar es Salaam 19.7% , Kilimanjaro 27.6% na Mara 30 %.

Mheshimiwa Spika, tatizo la udumavu, unyafuzi na utapiamlo ni tatizo linaloweza kuzuilika au kupunguzwa kabisa. Nchi ya Haiti ilikumbwa na tetemeko mwaka 2010 hivyo wananchi wengi walikumbwa na uhaba wa chakula pamoja na

ongezeko kubwa la maradhi. Lakini pamoja na hilo waliona umuhimu mkubwa wa kuanza kukabiliana na tatizo la udumavu wa watoto kuanzia miezi 6 mpaka miezi 59 ili kuepusha jamii yao na matatizo ya uwezo mdogo wa kufikiri na kudumaa kwa viungo siku za mbeleni. Katika tafiti ilizonyesha ndani ya kipindi cha miaka miwili tatizo la udumavu lilipungua kutoka asilimia 29 mpaka 22. Hii ni kutokana na mpango wa serikali kuongeza uzalishaji wa chakula, virutubisho pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa lishe bora kwa urahisi kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, nchi ya India ilianzisha mpango maalum wa kukabiliana na tatizo la udumavu lililokuwa limeikumba nchi hiyo ambapo watoto zaidi ya milioni 60 waliathirika. Katika mji wa Maharashtra ambao ni mji tajiri bado tatizo hilo lilikuwa kubwa. *Hii ni kwa sababu watoto wanaweza kushiba lakini wakakosa lishe bora.* Hivyo serikali ilianzisha program maalum ya "Mother-Child Health and Nutrition Mission" iliyoanzia katika maeneo yaliyoathirika zaidi. Serikali ya India ikaanza usambazaji wa vyakula vyenye virutubisho kwa bei rahisi ambapo kina mama wajawazito na wale wanaohudhuria kliniki baada ya kujifungua waliweza kuimudu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itambue kuwa, hakuna taifa lolote duniani, lililowahi kupata maendeleo huku wananchi wake wakikosa afya bora hasa afya ya akili. Hatuwezi kupata viongozi wa serikali wenye uwezo mkubwa wa kutafuta suluhu ya matatizo yanayolikabili Taifa kama utotoni waliwahi kuugua tatizo la udumavu au hawakupata lishe bora. Hatuwezi kupata usalama wa taifa wenye uwezo wa kuwa tanuru la fikra (think tank) kama utotoni hawakupata lishe bora iliyojenga afya ya akili. Mwalimu Nyerere aliwahi kusema maadui watatu wa taifa hili ni ujinga umaskini na maradhi. Matatizo haya yote yanachangiwa na tatizo kubwa la kukosa lishe bora kwa wananchi wetu. Ili binadamu awe na uwezo mzuri wa kufikiri hasa katika hali ya utupu (in vacuum) ni lazima kuhakikisha anapata lishe yenye kujenga ubongo na kinga imara za mwili.

Mheshimiwa Spika, Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha kuwa tatizo la udumavu, unyafuzi na utapiamlo linapunguzwa. Hii ni kutokana na madhara makubwa yanayoweza kulikumba taifa endapo watoto au vijana watakumbwa na matatizo hayo. Kama taifa tutapoteza kabisa kisima cha fikra cha taifa hili kutokana na ukosefu wa lishe bora unaosababisha udumavu.

11. ONGEZEKO LA MAGONJWA YASIYO YA KUAMBUKIZA NA ATHARI ZAKE

Mheshimiwa Spika, magonjwa yasio ya kuambukiza kama vile saratani za aina zote, magonjwa ya moyo, shinikizo la damu, figo, matatizo ya upumuaji na kisukari yameendelea kuwa visababishi vya ongezeko la vifo nchini. Takwimuzinaonyesha watu wazima 9-11 kati ya 100 wanaugua ugonjwa wa kisukari na kati ya watu wazima 3 mmoja ana tatizo la shinikizo la juu la damu. Aidha, tatizo la Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza linakua kwa kasi katika nchi zinazoendelea, kama Tanzania. Inakisiwa kuwa mwaka 2020 Magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza yatasababisha asilimia 73% ya vifo vyote duniani na asilimia 60% ya ukubwa wa tatizo la magonjwa duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara kwa kushirikiana na Tanzania Diabetes na World Diabetes Association ya mwaka 2013 ni kwamba, gharama ya kukabilliana na Magonjwa yasiyo ya kuambukiza duniani kote ni mabilioni ya dola na hivyo kusababisha upotevu mkubwa wa rasilimali finyu zilizopo. Kwa mwaka 2010 Shirika la Afya Duniani lilikadiria kuwa, jumla ya gharama za huduma za afya zinazohusiana na kisukari zilifikia dola za kimarekani bilioni 378 duniani kote, na kiasi hiki cha fedha kinaweza kufikia dola za kimarekani bilioni 490 ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kuwa magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza yanachangiwa sana namfumo wa maisha ya kila siku ikiwa ni pamoja na ulaji na unywaji usiofaa, matumizi ya sigara na madawa ya kulevya tabia ya kutokufanya mazoezi,shughuli za kimaendeleo zenye athari

kwa miili yetu na matumizi mbalimbali ya vipodozi,msongo wa mawazo n.k.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zimekuwa mstari wa mbele katika kupambana na magonjwa hayo kutokana na athari kubwa zinazosababishwa na magonjwa haya ikiwa ni pamoja **na** serikali kupoteza nguvu kazi ya taifa, familia kupotelewa na wapendwa wao hali inayopelekea ongezeko la yatima na wajane katika jamii, ongezeko la umaskini ndani ya familia kutokana na vifo vya wategemezi wa familia, kuwa na taifa la watu wengi walio wagonjwa n.k

Mheshimiwa Spika, Kutokana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua yafuatayo:

- Je, serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha angalau vifo vinavyotokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza nchini vinapungua?
- Je, ni fedha kisiasi gani ambazo mpaka sasa zimekwisha tumika kupeleka wagonjwa nje ya nchi kupata matibabu kutokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuzuia tatizo (preventive measures). Fedha hizo zitumike katika uratibu wa kuamsha uelewa wa wananchi(awareness campaign) kwa kada zote, kurudisha michezo mashuleni kwa nia ya kujenga afya, kuimarisha michezo katika sekta zote za umma,kuhakikisha serikali inakuja na mpango mahususi ya kurudisha viwanja vya wazi vya umma kwa ajili ya matumizi ya mazoezi na michezo ili kuboresha afya kupunguza kodi katika vifaa vya kufanyia mazoezi,kuzuia kabisa matumizi ya vipodozi vyenye kemikali, kuzuia kabisa biashara ya kuuza dawa kiholela bila cheti cha daktari,kushirikiana na taasisi mbalimbali yakiwemo mashirika,taasisi za dini, wasanii na wanasiasa katika kutoa elimu kwa jamii juu ya tabia hatarishi.

12. ONGEZEKO KUBWA LA WAGONJWA HOSPITALI YA TAIFA MUHIMBILI NA VITENGO VYAKE

Mheshimiwa Spika, Kwa sasa hali ya hospitali ya Taifa ya Muhimbili inakabiliwa na ongezeko kubwa la wagonjwa. Wapo wanaotoka mikoani bila hata ya rufaa yoyote na kulazimika kwenda hospitali hii ya Taifa. Tatizo hili linachangiwa sana na ukosefu wa huduma katika hospitali za mikoa, wilaya na vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, Katika Taasisi ya Mifupa (MOI), hali ya ongezeko la wagonjwa nayo ni ya kutisha sana. Kumekuwa na idadi kubwa ya wagonjwa kuliko uwezo wa taasisi hii. Japokuwa jengo la taasisi hii halijakamilika wala kukabidhiwa limekuwa likitoa huduma kwa wagonjwa wengi wanaozidi uwezo wa jengo. Jambo hilo sio tu ni la hatari kwa wagonjwa na wale wanaowahudumia bali pia linaiweka serikali katika hatari kwani matatizo yoyote yakitokea ndani ya jengo lile hakuna wa kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mrundikano wa wagonjwa kwenye hospitali moja linaweza kuepukika kabisa endapo serikali itajikita kwenye kuhakikisha huduma za afya za msingi zinapewa kipaumbele chini ya utekelezaji na usimamizi wa Wizara hii. Ni lazima Serikali ikatambua kuwa mahitaji ya huduma za afya yanaongezeka kwa kasi kwa kadiri idadi ya watu inavyoongezeka na changamoto za afya zinajitokeza

Mheshimiwa Spika, kusingekuwepo na sababu yoyote ya wagonjwa wanaopata ajali au kuvunjika kukimbizwa hospitali ya Taifa na hususan MOI, endapo serikali ingeboresha huduma za afya katika vitengo mbalimbali kuanzia kwenye zahanati mpaka hospitali za Rufaa.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili kubwa la watumiaji wa huduma ya afya, linazikumba hospitali na zahanati nyingi nchini. Mfano, Mwaka 2013 takribani watu 45,682,479 walipata huduma za afya katika zahanati ikilinganishwa na watu 39,917,117 walipata huduma za afya katika zahanati mwaka 2011. Kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Taifa ya mwaka

2004 ni kwamba; mwaka 2004 Tanzania ilikuwa na idadi ya zahanati 4,400 na zahanati moja ilitoa huduma kwa takribani watu 8,020 ikilinganishwa na ile ya mwaka 2003 ambayo ilieleza kwamba zahanati moja ilitakiwa kutoa huduma kwa takribani watu 5,000. Hii ikionyesha kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja tu kumekuwa na ongezeko la uhitaji kwa takribani 38%. Pamoja na hilo kuanzia mwaka 2012 mpaka mwezi Machi 2017 kipindi cha miaka mitano pekee kumekuwa na ongezeko la idadi ya watu takribani milioni 11.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni jitihada za makusudi za serikali katika kutatua matatizo ya afya kama kipaumbele cha kwanza cha taifa. Serikali hii ya awamu ya tano imeshindwa kabisa kuimarisha uchumi shirikishi kwa raia wake (economic inclusiveness) kwa kupitia huduma za afya za msingi. Serikali imekuwa na tabia ya kuwekeza **zaidi** katika uchumi wa kibaguzi ambao unanufaisha kundi la watu wachache katika huduma kama za usafiri wa ndege na huku ikisahau kabisa kwamba afya ndio uchumi wa kwanza unaoiunganisha jamii. Ni wakati muafaka sasa wa serikali kujitathimini kama bado inahitaji kukuza uchumi wa kwenye makaratasi au uchumi shirikishi kwa maendeleo ya taifa.

USTAWI WA JAMII

13. ONGEZECO LA KUTISHA LA MIMBA KWA WANAFUNZI NCHINI.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa na la kutisha la ongezeko la ndoa na mimba kwa watoto wenye umri wa kwenda shule na wale walio mashuleni nchini. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani iliyotolewa mwezi Januari 2016, ilionyesha kuwa Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa matukio ya mimba na ndoa za utotoni, ikiongoza kwa takribani asilimia 28. Hii ina maana kwamba, watoto wengi chini ya umri wa mika 18 wanajihusisha na vitendo vya ngono zisizo salama.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ,Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto alidhibitisha kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la mimba kwa wasichana wenye umri kuanzia miaka 15 mpaka 20 na ongezeko hili la 28% ni kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 pekee ikilinganishwa na mwaka 2010 ambapo tatizo hilo lilikuwa ni asilimia 10 tu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Idadi ya watu duniani (UNFPA) lilibaini kuwa kila kwenye wasichana kumi wenye umri kati ya miaka 12 mpaka 16 kati yao wanne wamepata mimba. Pamoja na hilo lilibaini kuwa kwa wastani wasichana wawili kati ya watano huolewa kabla ya kufikia umri wa miaka 18 hususani kwa maeneo ya vijijini.Vilevile, Shirika la watoto duniani (UNICEF) katika ripoti yao ya mwaka 2012 lilibaini kuwa mkoa ifuatayo inaongoza kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni: Shinyanga 59%,Tabora 58%,Mara 55%,Dodoma 51% na Lindi 48%.

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kitaifa na kimataifa Kambi ya Upinzani imebaini kuwa ongezeko la mimba za utotoni linatokana na kushuka kwa kipato cha familia, kubadilika kwa mfumo wa maisha ambapo wazazi wengi wamekuwa wakitumia muda mwingi katika shughuli za kujipatia kipato na hivyo kuwa na muda kidogo kwa malezi, kukua kwa teknolojia hususani matumizi ya mitandao ya simu kwa mijini ambapo watoto wa kike hulaghaiwa na vija kwa kuahidiwa simu,kushuka kwa ari ya kujifunza na msukumo wa elimu nchini, ukosefu wa ajira hususani kwa vijana wa kiume, kubadilika kwa mfumo wa maisha ambapo utamaduni uliokuwa umejenga katika jamii kuwa mtoto ni wa jamii sasa unabadilika na mtoto anaonekana kama ni wa familia pekee na hivyo jamii kujiondoa katika ulinzi wa mtoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, jambo hili la ndoa na mimba za utotoni limekuwa na mtanzuko mkubwa kwani jamii imekuwa na maoni tofauti kutoka kwenye makundi mbalimbali ya kidini,tamaduni, wasomi, wanaharakati wa haki za binadamu, wanaharakati wa kutetea haki za watoto wa

kike, wanasiasa n.k Lakini pamoja na hayo ni lazima Serikali itoe tamko ili watoto hawa wasiendee kuumizwa na sheria hii au pengine sheria hii iweze kuwa na manufaa kwao. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua msimamo wa Wizara hii ya maendeleo ya jamii, jinsia ,wazee na watoto katika kusimamia, kulinda na kutetea haki za watoto hususani watoto wa kike ambao ndio walengwa wakubwa wa sheria hii.

14. VYUO VYA MAENDELEO YA JAMII

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kupanua maeneo ya kiutawala nchini, bila kupanua uwezo wa kutoa huduma kwa wananchi. Ushahidi wa hili ni ongezeko la Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji ikiwa ni pamoja na ongezeko la Majimbo ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kuwa ili kujenga uwezo wa jamii kuibua miradi ya maendeleo ni lazima kama nchi kuwa na uwezo wa kuzalisha wataalam wa maendeleo ya jamii ili kuisaidia jamii kuibua miradi na masuala yanayogusa jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa serikali hii, haijaweka kipaumbele katika kuendeleza vyuo vya maendeleo ya jamii. Hii inatokana na uzito au ugumu wa Serikali kutoa fedha za maendeleo katika wizara hii. Nasema hivi kwa kuwa Serikali imetoa asilimia tano tu ya fedha za maendeleo hadi kufikia Machi, 2017 kwa ajili ya vyuo vya maendeleo ya Jamii. Ikumbukwe kuwa fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya maendeleo kwa ajili ya vyuo hivi ilikuwa ni bilioni 8.8 lakini mpaka Machi mwaka fedha zilizotolewa zilikuwa takribani milioni 497 sawa na asilimia 5.6.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kulieleza Bunge lako tukufu sababu za kutoa fedha pungufu kwa ajili ya vyuo hivi huku ikijulikana wazi kuwa vyuo hivi vinakabiliwa na uchakavu wa majengo pamoja na mazingira duni ya kujifunzia.

15. WANAWAKE NA USAWA WA KIJINSIA

Mheshimiwa Spika, usawa wa kijinsia, ni nyenzo muhimu katika kufikia maendeleo endelevu ya Taifa. Changamoto kubwa inayowafanya wanawake washindwe kukabiliana na usawa wa kijinsia ni pamoja na uwepo wa mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke. Hii ni pamoja na changamoto ya Sheria kandamizi ya Ndoa ya mwaka 1971, ambayo inaendelea kukandamiza watoto wa kike na kuchochea ndoa za utotoni, Sheria ya Mirathi ya kimila, tohara kwa watoto wa kike, watoto wanaopata ujauzito shuleni kukosa fursa ya kuendelea na masomo n.k

16. MASUALA YA WATOTO

Mheshimiwa Spika, watoto ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Taifa lolote. Ili watoto waweze kukua na kuwa raia wema, wanahitaji kupewa haki zao za msingi ambazo ni pamoja na: kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kutobaguliwa, na kushirikishwa. Haya yote yanaongozwa na Sera ya Mtoto ya mwaka 2008 na kutunga Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Aidha, uanzishwaji wa Madawati ya Jinsia na Watoto katika Vituo vya Polisi nchini pamoja na kutoa mafunzo kwa Polisi kuhusu kusimamia madawati haya hakujaongeza ufanisi wala kuleta tija katika kusimamia upatikanaji wa haki za watoto na wanawake. Uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Halmashauri haujaweza kutekelezwa nchini na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kudorora kwa utoaji na upatikanaji wa haki za watoto. Mabaraza hayo yanawezesha ushirikishwaji wa watoto katika masuala yanayohusu maendeleo yao. Vilevile, Serikali imeshindwa kuendeleza mipango yake iliyoanisha ikiwemo Mpango wa Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto. Mpango huu ulilenga kuhamasisha wazazi kuwapeleka watoto kupata chanjo ya maradhi mbalimbali ya utotoni, lische bora na upatikanaji wa maji safi na salama.

16.1 Ukatili dhidi ya watoto

Mheshimiwa Spika, vitendo vya kikatili dhidi ya watoto vimeendelea kushamiri nchini, mifano hai ni kama ifuatayo;

i. Juni 27, 2016 katika kitongoji cha moha, kijiji cha Ilungu Kata ya Nyigogo, tarafa ya Itumbili wilaya ya Magu mkoani Mwanza, Julius Leonard aliyekuwa na umri wa miaka 7 aliuawa kwa kupigwa fimbo na baba yake wa kambo Leonard Joseph kwa kuchelewa kurudi nyumbani baada ya kutumwa kwenda kuchukua betri. Mtoto huyu alipigwa mpaka kifo na mwili wake baada ya uchunguzi wa daktari ulionesha kuvuja kwa damu kwa ndani kutokana na fimbo hizo.

ii. Julai 2016, mtoto John Kyando mwenye umri wa miaka miwili (2) aliuawa kikatili na baba yake wa Kambo kwa kushirikiana na mama yake mzazi katika kitongoji cha Mang'oto, kijiji cha Ujuni kata ya Kitulo wilayani Makete kwa kunyongwa mpaka kufa kasha kutupwa mtoni.

iii. Aprili, 2017 mtoto wa mwaka mmoja na miezi sana aliuwawa kikatili kwa kuchomwa moto sehemu za makalio na baba yake wa kambo anayejulikana kwa jina la Petro Bahatu huko kijiji cha Nyalubanga, kata ya Lwezera wilaya na mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Spika, haya ni baadhi tu ya matuko ya ukatili dhidi ya watoto ambayo yameripotiwa. Bado watoto wameendelea kukubwa na ukatili mkubwa na matukio hayo mengi yanapita bila kufanyiwa kazi ipasavyo, ipo haja sasa ya Serikali kupitia wizara hii kuhakikisha kesi za watoto wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia zinapewa uzito na adhabu yake iwe kali ili kufikisha ujumbe kwa jamii.

17. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

a. Fungu 52

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa bajeti inaonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 314,673,230,000.95 sawa na 40% ya bajeti ya Wizara zikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida pamoja na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuhusu fedha za maendeleo, randama zinaonesha kuwa, hadi mwezi Machi, 2017 ni asilimia 37 tu ya fedha za ndani ndizo zilizotolewa na Hazina na kwa fedha za nje ni asilimia 6 tu ya fedha hizo zilikuwa zimetolewa na hazina kwa kipindi hicho. Hii ina maana kwamba bajeti ya maendeleo kwa fedha za ndani haijatekelezwa kwa asilimia 63, na kwa fedha za nje haijatekelezwa kwa asilimia 94. Kwa utekelezaji huu duni wa bajeti ya maendeleo katika fungu hili, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba Serikali haiko makini kabisa na afya za watanzania.

b. Fungu 53

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Bunge liliidhisha jumla ya shilingi bilioni 49.9 kati ya fedha hizo, matumizi ya kawaida shilingi bilioni 41 na shilingi bilioni 8.848 zikiwa ni fedha za maendeleo. Hata hivyo, fedha za maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Machi, 2017 ni shilingi 497,718,250/- sawa na asilimia 5.62 tu ya shilingi bilioni 8.8 zilizoidhinishwa na Bunge. Hii maana yake ni kwamba, Bajeti ya maendeleo katika fungu hili la maendeleo ya jamii haikutekelwa kwa takriban asilimia 95. Fungu hili ndilo linahusika na vyo vya maendeleo ya jamii, na kwa maana hiyo hiyo utekelezaji duni wa bajeti vyo hivyo haviwezi kuwa na uwezo wa kujiendesha na kuzalisha wataalam wa kuzisaidia jamii zetu kujitea maendeleo kwa kuweza kuibua fursa zilizo katika jamii zao.

18. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya awamu ya tano imekuwa ikijigamba kuwa afya ni mojawapo ya vipaumbele katika utekelezaji wa majukumu yake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitegemea hayo yaonekane katika utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo kwa angalau kwa asilimia 80 ili kudhihirisha uhalisia wa majigambo ya “hapa kazi tu”. Tofauti na tegemeo hilo, wizara hii ni miongozi mwa wizara zinazoongoza kwa utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, licha ya wizara hii kusema kwamba mojawapo ya vipaumbele vyake kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni kusimamia upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee, imewasahau wazee kabisa. Ikumbukwe kwamba Serikali ya awamu ya nne ilishatoa uamuzi wa kuwapatia mafao ya uzeeni (universal pension) wazee wote lakini Serikali hii ya awamu ya tano imeweka kapuni azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa rai kwa serikali kuacha kufanya mzaha na afya za watanzania. Serikali iache kuwahadaa wananchi kwa kutenga bajeti kubwa na kushindwa kuitekeleza. Ni vema Serikali ikapanga mipango inayotekelezeka kuliko kupanga mipango yenye lengo la kukidhi mataakwa ya kisiasa na kuwaacha wananchi wakihangaika. *Ili kukabiliana na maadui watatu yaani ujinga, umaskini na maradhi; ni lazima kuwekeza katika “Uchumi wa afya (health economy)”.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Esther Amos Bulaya (Mb)

**K.N.Y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO
YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO.**

3 Mei, 2017

MWENYEKITI: Kabla sijaitoa hoja hii kwenu muanze kujjadili nina tangazo moja lilisahaulika tu, linatoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu - Bunge na linahusu zoezi la upimaji na ushauri wa afya linaloratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Tunaarifiwa kwamba zoezi la upimaji na ushauri wa afya zetu kwa Wabunge, Watumishi na familia zao litaendelea hapa kwa wiki mbili kuanzia jana tarehe 02 hadi 13 Mei, 2017. Huduma zitakazotolewa ni kama ifuatavyo: moja, upimaji wa magonjwa ya moyo, mbili, upimaji wa tezi dume, tatu, uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi, nne, uchunguzi wa saratani ya matiti na tano, uchunguzi wa magonjwa ya kisukari. *(Makofi)*

Zoezi hili litafanyika katika Kituo cha Afya cha Bunge kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kila siku, yaani kuanzia jana mpaka tarehe 13 Mei, zoezi hili linashirikisha Madaktari Bingwa kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunakaribishwa, ni muhimu sana kwa ajili ya afya zetu, hivyo tuna muda kidogo ili tuanze kazi. Waheshimiwa Wabunge wawili wanaweza, sasa nianze na Mheshimiwa Selemani Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo. (*Makofi*)

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema ili na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene niweze kuchangia hoja muhimu sana ya Wizara ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Umyy Mwalimu kwa uwasilishaji mzuri sana na hotuba nzuri sana ambayo imewasilishwa kwa weledi wa hali ya juu, hongera sana Mheshimiwa Umyy. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kabisa kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii asilimia 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene, kwa dhati kabisa ya moyo wangu niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuhakikisha kwamba Jimbo langu la Bukene kwa mara ya kwanza linapata huduma ya upasuaji kwa vituo viwili vya afya. Huduma ambayo imekuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nichukue fursa hii nimpongeze Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ambaye alifunga safari baada ya kufanya ufuatiliaji wa muda mrefu na kuja hadi kituo cha afya cha

Itobo kufanya uzinduzi kwa niaba pia ya kituo cha afya cha Bukene, hongera sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri hiyo uliyoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo hivi vya upasuaji ni azma ya Serikali ya Awamu ya Tano kupunguza vifo visivyo vya lazima vya akina mama na watoto. Kabla ya vituo hivi akina mama walokuwa wakihitaji huduma za upasuaji katika Jimbo la Bukene walikuwa wakilazimika kusafiri zaidi ya kilometa 80 kutoka maeneo mengine hadi hospitali ya Wilaya ili kupata huduma hii. Lakini sasa huduma hii imesogezwa karibu sana na niseme tu kwamba katika muda wa hii miezi miwili ambayo upasuaji umeanza muitikio ni mzuri sana na tumeweza kufanya operesheni za kutosha na kuokoa maisha ya akina mama na watoto wa ndani ya Jimbo la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni moja tu, pamoja na kwamba huduma hii imeanza, lakini kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi. Katika kituo cha afya cha Bukene mganga anayeweza kufanya upasuaji yuko mmoja tu na huyu anaifanya shughuli hiyo kwa muda wa saa 24. Kwa hiyo, inapotokea kwamba anakuwa kwenye majukumu yasiyoweza kuzuilika mgonjwa akifika pale kama anahitaji upasuaji anakosa hiyo huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivyo hivyo kwenye kituo cha afya cha Itobo, mganga anayeweza kufanya upasuaji kwa sasa tunaye mmoja tu na kwa Itobo ni mbaya zaidi kwa sababu mganga huyu bado ana miezi michache tu ili astaafu. Kwa hiyo, kama hakutakuwa na jitihada za ziada ili kupata mganga basi huenda kituo hiki kikashindwa kutoa huduma ya upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Halmashauri ya Nzega tumejaribu kufanya *re-allocation* ya kuwatoa waganga kutoka Hospitali ya Wilaya kuwapeleka kwenye hivi vituo vya afya lakini *re-allocation* hii sasa imefika mwisho kwa sababu hata Hospitali ya Wilaya nao wana upungufu. Hata hao wawili huyu aliyeko Bukene na aliyeko Itobo tumewatoa pale Hospitali ya Wilaya ya Nzega. Kwa hiyo, *re-*

allocation ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imefika mwisho haiwezekani tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe kwa niaba ya wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega Wizara itufikirie kama ombi maalum ili tuweze kupata madaktari wanaoweza kupasua wapangwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na mmoja hususan apelekwe kituo cha afya cha Itobo na mmoja hususan apelekwe kwenye kituo cha afya cha Bukene ili huduma hizi muhimu na nzuri za upasuaji ziendeleo kupatikana ili wananchi wetu, na hasa akina mama na watoto waweze kuepukana na vifo ambavyo kimsingi vinaweza kuzuilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia ni huduma za *x-ray* katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega. Leo hii tunapozungumza hapa ni miezi mitano sasa *x-ray* ya Hospitali ya Wilaya ya Nzega imekufa haifanyi, kazi. Hoja yangu hapa ni kwamba tatizo sio kufa kwa *x-ray*; *x-ray* ni kifaa ambacho kinafanya kazi kwa hiyo kinaweza kufa. Lakini hoja yangu hapa ni uharaka wa namna ambavyo *x-ray* iliyokufa inaweza kushughulikiwa ikapona na ikaendelea kutoa huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *x-ray* ya Hospitali ya Wilaya ya Nzega imekufa tangu tarehe 13 Desemba, 2016 na baada ya kufa tu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega aliandika barua kwa Katibu Mkuu wa Wizara ili Wizara wai-engage kampuni ambayo ina mkataba wa kutengeneza hizi *x-ray* za Phillips ili iweze kuja Nzega na kutengeneza. Lakini *speed* imekuwa ndogo mno, mpaka leo tunaongelea mwezi wa tano ni danadana tu. Hao mafundi walikuja mara moja wakaangalia vifaa, wakatoweka mpaka sasa hawajaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho tutataka tujue utaratibu au mkataba uliopo kati ya Wizara na hawa watoa huduma wa ku-service hizi *x-ray* aina ya Phillips ukoje na umekaa vipi kwasababu kama utaratibu ni mbaya basi tupendekeza kwamba Hospitali za Wilaya zenyewe zitafute mafundi au

service provider wenye uwezo ili waweze kutengeneza *x-ray*. Kwa sababu ni jambo ambalo halikubaliki *x-ray* kukaa miezi mitano imekufa na wagonjwa wanakwenda pale wanakosa huduma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaleta usumbufu mkubwa sana kwa wagonjwa wanaofika Hospitali ya Wilaya ya Nzega na ambao matatizo yao yanahitaji huduma za *x-ray* wanapata taabu sana. Kwa hiyo, niombe kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majumuisho atoe ufumbuzi, kwamba *x-ray* ya Hospitali ya Wilaya ya Nzega ambayo miezi mitano sasa imekufa ni lini itaweza kushughulikiwa ili wananchi waweze kupata huduma hiyo muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie upatikanaji wa dawa katika Bohari Kuu ya Dawa (MSD). Kwanza niipongeze Serikali kwa dhati kabisa kwa kutenga hela nyingi za kutosha kununua dawa. Hili kwa kweli ni jambo la kupongezwa, haijawahi kutokea kiwango cha bajeti kilichokwenda kwenye dawa mwaka huu ukilinganisha na miaka ya nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja hapa ni sasa madawa yapatikane, kwa sababu kupatikana kwa fedha za kununua dawa ni jambo moja lakini kupatikana kwa dawa pia ni jambo lingine. Kwa sababu utaona kwamba fedha za dawa ambazo zinapelekwa kwenye akaunti za vituo vya afya au zahanati kule MSD kwa hiyo, unakuta vituo vya afya au zahanati vikiomba dawa MSD kunakuwa na *out of stock* nyingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Taarifa za tarehe 28 mwezi uliopita, ukijumlisha vituo vya afya na zahanati zote tuliomba dawa za shilingi milioni 126 lakini tukapata dawa za shilingi milioni 24 tu, ambayo ni kama asilimia 20 tu. Kwa hiyo, utakuta kwamba sasa hivi tuna *balance* ya fedha za dawa ambazo ziko MSD, karibu shilingi 503,000,000. Hata hivyo ukiomba dawa sasa upatikanaji wa dawa unakuwa

mdogo. Kwa hiyo upatikanaji wa fedha uendane sambamba na upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia 100 na Wizara ya Afya wanafanya kazi nzuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi niweze kuchangia kwenye hoja ya Wizara hii muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara hiyo, Naibu Waziri wake Dkt. Kigwangalla, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nianzie kwenye hili la madaktari. Mwezi uliopita tulikuwa na sherehe zetu za wazazi pale Kagera, mojawapo ya kazi yetu ni kwenda kutoa huduma katika hospitali. Hospitali ya Mkoa wa Kagera inahitaji Madaktari Bingwa 21, madaktari waliopo ni wawili. Sasa naiomba Wizara hii, nina imani hawa wakubwa niliyowapongeza ni wasikivu sana. Ukitafuta *ratio* ya 21 na mbili pale watu wanapata shida sana. Nawaamini, lakini nichukue nafasi hii kuomba kwamba kazi mnayofanya ni kubwa lakini hao wenzetu hospitali inalemewa na hawana mahali pa kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili tulikuta tatizo lingine pale, kama alivyosema aliyemaliza kuongea sasa hivi. Tuipongeze Serikali kwa mara ya kwanza pesa ya dawa ipo katika Halmashauri. *MSD* inafanya kazi kubwa lakini inawezekana imelemewa sasa. Isaidiwe, iongezewe nguvu ili dawa zipatikane ziweze kwenda kwenye vituo vya afya na hospitali zetu. Kila unayemuuliza hapa kwenye Halmashauri yake, pesa zipi, dawa hatujapata kutoka *MSD*.

Kwa hiyo, nina uhakika Mheshimiwa Ummu na Naibu kwa kazi mnayofanya hebu elekezeni macho yenu kule kwenye MSD, kwa sababu MSD ndiye anafikisha dawa kwa Watanzania waliokuwa wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru hicho wanachokipata lakini kila mtu anakwambia nimeshapeleka hela sijapata dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niende kwenye hiyo hiyo MSD. Tunaomba MSD ule utaratibu mliotengeneza kidogo wa kuweka alama kwenye madawa ya Serikali, kila dawa ya Serikali iwe na alama yake ya nembo inayojulikana ili tuweze kuendelea kutunza dawa hizi zisiende kwenye maduka ya watu binafsi. Katika hilo naipongeza sana Serikali, lakini sasa yale maeneo ambako hamjaanza kuweka zile nembo ni vizuri zile alama ziwepo ili mtu akienda kuuziwa dukani anasema ile ni ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yangu kwa sababu bajeti iliyopita kwenye eneo la dawa ilikuwa kama shilingi bilioni 50 au 65, lakini mwaka huu wameenda zaidi ya shilingi bilioni 200 na mpaka leo Serikali yangu imeshaweza kutoa zaidi ya shilingi bilioni 120, ni kitu cha kupongeza sana kwa maana kwamba Serikali hii inajali afya ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie kwenye maendeleo ya jamii, ndugu zangu haya maendeleo ya jamii mbona wanyonge hivi? Kila Halmashauri utakayokwenda ukamkuta mtu wa maendeleo ya jamii hana hamu na kazi yake. Hapewi gari, hapewi huduma, haonekani kama ni mtumishi, kwa nini ndugu zangu? Hawa ni watumishi na wana haki kama idara zingine! Lakini wao wanakuwa ni watumwa fulani katika ofisi, hakuna mtu utamkuta amechangamka kwenye kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe, Wizara hii ni kubwa dawa zipo, mazuri yapo. Mheshimiwa Ummu hebu hamia hapo kwenye watu wa maendeleo ya jamii. Hawa ni

watu muhimu sana katika taasisi yetu, shughuli zao ni nyeti sana. Lakini unakuta Mkurugenzi akisema lazima "ah wewe subiri" akifanya hivi "wewe ngoja bado kasma haipo." Kwa nini hawa watu wawe wanyonge? Hebu tuwaongezee nguvu basi kama idara zingine zinavyofanya kazi ili na wao wawe na afya katika meza zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niongelee madaktari. Tunaipongeza Serikali, imesema inaajiri madaktari hao 258; mimi nafikiri tumpongeze Rais kwa uamuzi wa haraka. Hotuba ya wenzangu huku wamesema kwa nini watu wanasikia hamu kwenda kufanya kazi nje. Unajua ajira ni nafasi, zamani tulikuwa kila mtu anaweza kuajiriwa kwa nafasi zilikuwa chache, lakini leo lazima ikama iwepo, mshahara uwepo, na taratibu ziwepo ndiyo mtu aajiriwe. Sasa watu wameambiwa wanaenda Kenya na wanajua wanaenda kulipwa dola, kuna mtu atabaki? Habaki mtu ukishatamka dola.

Sasa Rais wetu tumpongeze kwa maamuzi ya haraka kwamba hawa waliokwishajitolea wanataka kwenda nchini nyingine kufanya kazi hebu tuwape ajira moja kwa moja watufanyie uzalengo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri badala ya kulaumu hebu tumpongeze Rais kwenye uamuzi huo. Rais hata kama mtu unatakiwa kupinga akifanya jema basi tumpongeze, na siamini kama kuna Mbunge yeyote wa upinzani atasema madaktari wanaoajiriwa kesho kutwa kwenye Jimbo langu wasije, yupo? Mtawapokea, sasa kwenye kuwapongeza tumpongeze Rais anataka kutuondolea ile kero.

Kwa hiyo mimi nimeona niseme lakini watani wangu wa upande wa pili kwamba hoja Rais akiajiri kote Watanzania tutapata faida ya wale wanaoajiriwa. Sasa msingi wa kubeza unapunguza nguvu ya wale watendaji wetu. Mimi niwaombe sana, mema anayofanya Rais wetu tumpigie makofi, yakiwa mapungufu mna haki ya kusema kwa sababu kazi yenu ni kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naendelea kusema kwamba akifanya mema Rais tumpungeze wala haina tatizo. Hata hivyo ninyi kukosoa ni jukumu lenu ndiyo maana mmekuja humu mkosoe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo mimi hoja zangu zilikuwa zinaishia hapo. Naunga mkono hoja, naendelea kuipongeza Wizara chapeni kazi, mko vizuri, fanyeni muungano, tuko nyuma yenu, Chama cha Mapinduzi kitawaunga mkono. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Bulembo kwa mchango wako mzuri. Wachangiaji wetu wa mchana tutakaoanza nao; tuna orodha ndefu lakini hawa wa kuanza nao tu, Mheshimiwa Innocent Bilakwate, Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Martha Umbulla, sasa mnajua *style* yangu, nitachanganya baadaye.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 06.56 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, niliwataja wachangiaji wetu wa kwanza, kwanza tuanze na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu na kuweza kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kipekee kumpongeza Rais wetu, kwa kazi nzuri anayoifanya, hakika imeonekana mbele ya Watanzania kuwa huyu ni Rais mtetezi wa wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri wetu Mheshimiwa Ummu, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa kweli kazi mnayoifanya ni nzuri, Mheshimiwa Ummu na timu yako ninasema msonge mbele na Mungu atawafanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia bajeti. Kwanza niipongeze Wizara ya Afya kwa kuboresha kituo chetu cha afya cha Nkwenda. Kituo hiki sasa hivi akina mama wanapata huduma nzuri, kituo hiki kimeboreshwa, Mheshimiwa Ummu nakushukuru sana umetupatia *ambulance*, tulikuwa na hali mbaya. Sasa hivi kile kituo kwa kweli ni cha kisasa ingawa bado wananchi wanahitaji huduma zaidi kwa sababu ukilinganisha na jioografia ya jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwa upande wa dawa. Kwa kweli Serikali inajitahidi lakini bado mahitaji ni mengi na dawa bado haziwafikii wananchi wetu. Niombe Serikali iongeze nguvu na tumeona kwenye bajeti imetenga hela nyingi lakini bado. Niombe Serikali, Mheshimiwa Waziri hizi dawa mnazopeleka hebu zisimamiwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine mimi bado ninaamini pesa inayotengwa dawa zinanunuliwa lakini zile dawa zinachakachuliwa zinazwa mitaani. Mimi nitoe mfano kama kule kwangu Kyerwa. Ukimuuliza *DMO* atakwambia dawa zipo, lakini unapooenda kwa wananchi wanakwambia kila tunapoenda kituo cha afya hatupati dawa za uhakika. Kwa hiyo, mimi niombe Mheshimiwa Waziri uweke utaratibu ambao tunaweza kufuatilia hizo dawa tukajua kwa siku ni watu wangapi, ikiwezekana hata majina yale waliotibiwa na kupewa dawa yawe yanabandikwa ili tupate uhakika hizi dawa zinaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuiomba Serikali yangu, bado wananchi wanahitaji sana kwa upande wa vituo vya afya, Serikali inajitahidi kuboresha, lakini bado kuna maboma ambayo wananchi wameanzisha wao wenyewe, mengine yamekaa muda mrefu miaka mitano mpaka kumi. Niiombe sana Serikali, hawa wananchi tusije tukawakatisha tamaa, tujitahidi kumaliza haya maboma ili wananchi wetu waweze kupata huduma. Lakini kuna jambo ambalo mimi nishauri, kwenye ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tunasema kituo cha afya kila kata na zahanati kila kijiji. Hili jambo ni zuri lakini mimi niishauri Serikali, kwa kipindi hiki ambacho bado hatujaweza kufikia hapo hebu tupeleke nguvu yetu kila kituo cha afya kila tarafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mimi nina tarafa nne, katika tarafa nne nilizonazo mimi nina kituo cha afya kimoja ambacho kina uhakika. Tunaposema tunapeleka kwenye kila kata nina uhakika hatutaweza kufikia hayo malengo kwa wakati tulioupanga; lakini tukipeleka kwenye kila tarafa ikapata kituo cha afya mimi ninaamini wananchi wetu tutaweza kuwasogezea huduma kwa ukaribu. Kwa hiyo, huo ni ushauri Mheshimiwa Waziri uuchukue na iwe kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwenye majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la watumishi. Mheshimiwa Waziri bado watumishi ni wachache, wananchi wanakosa huduma kwa sababu ya watumishi. Kwa mfano mimi kwenye kituo changu pale Nkwenda tuna watumishi wachache sana. Nimuombe Mheshimiwa Waziri Ummy, mmetangaza ajira kwa ajili ya madaktari, hebu tuangalie haya majimbo ambayo yako pembezoni kama kwetu Kyerwa, kwa kweli hali ni mbaya sana. Tusiangalie maeneo ya mijini hebu tuangalie na huku pembezoni ili Watanzania wote waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la bima ya afya. Suala la bima ya afya ni zuri sana, niombe sana Serikali tuendeleo kuwahamasisha wananchi ili kila mwananchi aweze kupata bima ya afya. Vilevile tuangalie hawa wazee wetu ambao tumesema wapate matibabu bure, bado

huduma hii ni ngumu, wazee wetu bado hawapati huduma bure. Wanapokwenda kwenye zahanati au hospitali wanahudumiwa na daktari lakini mwisho wanaambiwa waende kununua *pharmacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wazee kama tumesema wapate huduma bure, Mheshimiwa Waziri hebu tuweke utaratibu ili waweze kupata huduma bure ili na wao wafurahie matunda ya taifa lao wakati wanaelekea jioni kuaga dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi michango yangu sehemu kubwa ni hiyo, lakini niombe sana Mheshimiwa Ummy, kwa kweli umekuwa ukitoa ushirikiano pale tunapokuja kwako kuleta matatizo ya wananchi wetu. Nikuombe sana Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Kigwangalla moyo huo uendelee bado wananchi wetu wanayo mahitaji mengi, bado huduma za afya hazijaweza kukidhi viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ninaishukuru sana Serikali yetu kwa kazi zinazofanyika, ahsanteni sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Martha Umbulla.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na neno la shukrani. Nashukuru kwa maana ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, taarifa ya kamati nikiamini vyote vimesheheni mambo ambayo macho yanapenda kuona na masikio kusikia. Nikianza na nukuu kama ambavyo wenzetu wa kamati waliitoa ya Mahatma Gandhi, wao waliitoa kwa kingereza lakini mimi nitaitoa kwa tafsiri ya Kiswahili changu mwenyewe kwa maana ya afya ndio utajiri halisi na si vipande vya dhahabu na fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo nakwenda kuisemea Hospitali yetu ya Manispaa ya Mpanda. Hospitali

ya Manispaa ya Mpanda ilianza mwaka 1957 ikiwa kituo cha afya. Leo hii inafanya kazi kama Hospitali ya Manispaa, na kwa misingi hiyo watu wote ndani ya mkoa wanaitegemea hospitali ile, na ndiyo maana sisiti kuishukuru Serikali yangu kwa sababu najua tuko mbioni kutengeneza hospitali ya mkoa na fedha zimekuwa zikitengwa na hivi karibuni tumetengewa shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini, Serikali itaendelea kutuangualia kwa jicho la huruma nikiamini sisi tuko pembezoni na tukikosa huduma muhimu za afya tunakuwa pembezoni zaidi. Kwa hiyo, hilo nilikuwa napenda kuliweka katika sura hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hospitali yetu hiyo hiyo, mara ya mwisho alikuja Naibu Waziri. Katika kuitembelea hospitali, alipokwenda kwenye chumba cha upasuaji, nasikitika kusema alikifananisha chumba kile na machinjio; yaani kwa maana kwamba vifaa vilivyomo mle havifanani na vifaa vya chumba cha upasuaji, kwa huduma zote, kama vile utoaji hewa na vinginevyo. Kwa hiyo, mahali ambapo tunakusudia tuokoe maisha ya watu ukifananisha na machinjio Mheshimiwa Waziri unaona kabisa kwamba watu wale wanatakiwa kuangualiwa kwa jicho la huruma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua pia kuna changamoto ya upungufu wa dawa. Ni kweli mara ya mwisho alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu akatusaidia tukaanzishiwa duka la *MSD*, hilo nashukuru maana usiposhukuru kwa kidogo hata kwa kikubwa unaweza usishukuru. Hata hivyo pamoja na uwepo wa duka hilo bado tuna tatizo kubwa la uhaba wa madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakumbuka Mheshimiwa Waziri wetu mara ya mwisho aligusia habari ya kuiangualia mikoa ya pembezoni kwa maana ya kupeleka madaktari bingwa. Nilikuwa naomba wazo hilo muhimu, wazo hilo la uokoaji liendeleo kuwa katika kichwa chako Mheshimiwa Waziri. Nafahamu tuna ukosefu wa magari na katika hili uungwana tu kama binadamu naomba niwapongeze wale

wote waliobahatika kupata *ambulance*. Hata hivyo wakati nikiwapongeza hao Mheshimiwa Waziri maana yake na mimi natoa shukrani *in advance* kwa maana najua mgao unafuata na sisi tutafikiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mkoa wangu wa Katavi napata aibu kuhusu suala la mimba za utotoni nikiwa mwakilishi wa wananchi. Tunapozungumzia habari za mimba za utotoni, na kwamba Mpanda ndio wa kwanza katika nchi hii sisi wawakilishi wa wananchi tunayo kazi nzuri kubwa ya kufanya. Nilikuwa naomba hiyo kazi kubwa ya kufanya, kwa maana ya kuwafikia vijana katika kuendelea kutoa elimu katika suala hili na tatizo la mimba za utotoni nahitaji msaada kutoka katika ofisi yako Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshazungumzia habari ya ujenzi wa hospitali ya mkoa ambayo inahitaji msisitizo na msukumo. Tunacho chuo cha afya, miundombinu yote ya kile chuo ambacho kilikuwa cha zamani imeshafufuliwa, kila kitu kipo katika hatua za mwisho. Rai yangu na ombi langu kwako, Serikali ifanye jitihada kuhakikisha chuo kile kinaanza. Najua ni chuo kwa ajili ya matabibu, lakini ningomba tukibahatika pia katika chuo hicho hicho tukawa tunatoa na wauguzi tafsiri yake ni nini? Kwanza habari ya mahitaji ya wataalamu hawa itakuwa ni ndoto katika hospitali yetu, nilikuwa naomba hilo tusaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze, kwenye kitabu chako Mheshimiwa Waziri umeongelea habari ya huduma ya matabibu bingwa. Nafahamu kwa kupitia huduma ya matabibu bingwa kwa Taasisi ya Jakaya Kikwete na kwa MOI, huu ni mwarobaini wa kutusaidia Watanzania kwenda nje ya nchi, mimi hilo nalipongeza sana. Hata hivyo, pamoja na kulipongeza basi maeneo hayo yapewe fedha, na hapa si suala tu la kusema fedha zimetengwa ila ionekane fedha zikipelekwa, nilikuwa naomba kutoa rai hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niendeleee tena kutoa pongezi kwa kupunguza rufaa nje ya nchi. Suala hili ni la msingi, najua ni kwa maana ya kupunguza

rufaa ya nje ya nchi kama vile kwa masuala ya kupandikiza figo. Tumeona pale ukizungumzia nje ya nchi ni shilingi milioni 80 lakini kwa shughuli hiyo kufanywa ndani ya nchi inakuwa ni shilingi milioni 20, huu ni msaada mkubwa kwa wananchi wetu. Naamini nchi ya uchumi wa viwanda bila kuwekeza kwenye afya ya watu, rasilimali watu, nguvu kazi ndoto ya uchumi wa viwanda itakuwa mashakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye ushauri, lakini wakati nikienda kwenye ushauri kuna suala la dharura...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kapufi. Mheshimiwa Martha Umbulla atafuatiwa na Mheshimiwa Faida Bakar na hawa sasa wajiandae dakika tano, tano kila mmoja, Mheshimiwa Suzana Mgonokulima na Mheshimiwa Lucy Owenya. Mheshimiwa Martha Umbulla karibu.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uzima na kunipa afya kuweza kusimama hapa ili kuchangia hoja ya Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kwa kweli kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Naibu wake, na jopo zima la wataalam katika Wizara yao kwa kazi nzuri sana wanayoifanyia nchi yetu na kuitendea haki sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mweyekiti, kipekee pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa dhamira njema sana ya kuhakikisha kwamba sekta ya afya hapa inakwenda kuboresha afya za wananchi walio wengi wa vijijini na hasa wale watu maskini ambao hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamekwishafanyika na Mheshimiwa Rais wetu, kipekee naomba nilenge sekta ya afya, ametenda mengi lakini kubwa ambalo katika sekta hii naweza kulisema ameondoa tatizo sugu la uhaba wa vitanda katika Hospitali ya Muhimbili; ameweza kutoa amri na kurekebisha vitendea kazi ambavyo vilikuwa havifanyi kazi, na zaidi sana dhamira yake njema ya kuboresha sekta ya afya kwa kuinua hadhi hospitali mbalimbali, vituo vya afya na zahanati katika vijiji katika kuboresha afya ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Mkoa wa Manyara hatuna la kusema, tunatoa pongezi na shukrani nyingi sana kwa kuridhia kupandisha hadhi Hospitali yetu ya Haydom ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja akaitembelea, akaiona na akatoa pendekezo kwamba anakubali iwe Hospitali ya Rufaa ya Kanda, lakini vilevile akatoa jopo la wataalamu kuja kuangalia vigezo na ninaamini kwamba vigezo vinakidhi. Kubwa la kushukuru amemtuma Mheshimiwa Waziri wa Afya hivi karibuni, hana hata siku tatu ametoka Manyara kuangalia Hospitali ya Haydom kama inakidhi vigezo vya kuwa Hospitali ya Rufaa. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu, hongera Mheshimiwa Waziri Mkuu, hongera Mheshimiwa Ummu Mwalimu na timu yako nzima katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ametupandishia hadhi kituo chetu cha afya cha Dongobesh kuwa Hospitali ya Wilaya na hilo nalo ni katika harakati za kuboresha afya katika Mkoa wetu wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa shukrani nyingi, kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Lakini sambamba na kupandisha hadhi ya Hospitali ya Haydom kuwa ya Rufaa ninatoa tahadhari na ombi kwa Serikali kwamba mara nyingi

wakipandisha hadhi hospitali, huduma zinazotolewa kwenye hospitali hizo zinakwenda kupanda gharama. Tunaomba kwa dhamira hiyo hiyo ya kuboresha afya katika vijiji tunaomba wasimamie kwamba Hospitali ya Haydom itakapopanda hadhi kuwa ya rufaa, basi na huduma zitakazotolewa ziweze kuwa wananchi wetu wanazimudu kwa maana ya kwamba kutopandisha gharama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na habari njema hizi nilizotaja bado Mkoa wa Manyara una matatizo lukuki. Kubwa sana ni katika Wilaya za Simanjiro na Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Kiteto, mimi nimekuwa Mkuu wa Wilaya katika Wilaya ya Kiteto kwa miaka mitatu. Wilaya haina gari la wagonjwa. Miaka yote niliyokuwa pale, gari ni moja iko *garage* kila wakati, miundombinu ya Wilaya ile ni mibaya sana, bila gari wananchi wanafia barabarani na sasa hivi tunasikia habari njema za kugawa magari kwenda katika Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa moyo wa dhati Hospitali ya Kiteto iweze kupata gari ya kubeba wagonjwa ili iweze kuondokana na tatizo la usafiri kwa wagonjwa wetu. Tukizingatia Wilaya ile ni kubwa sana, miundombinu ni mibaya barabara ni za *rough roads*, tunakuomba Mheshimiwa Ummu Iangalie Kiteto kwa jicho la ziada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika Wilaya ya Simanjiro, hapo ndipo fungakazi. Wilaya ya ile ni ya siku nyingi lakini hakuna Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, leo, walivyosikia jina langu nachangia mchana, Mkurugenzi alinipigia simu. Akasema najua kwamba na Mbunge yupo mama tunaomba utoe kilio chetu kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Menyekiti, hakuna kituo cha afya pale au Wilaya yetu ya Simanjiro haina Hospitali ya Wilaya na hili ni tatizo kubwa sana. Wagonjwa wanatoka Orkesment

kwenda kupata huduma ya afya Seliani – Arusha, kilometa karibu 200. Wanatoka Orkesment kwenda Mererani kilometa karibu 122, wataoka hapa wanakwenda KCMC kwa kilometa nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuomba, najua kwamba Wilaya imeshakuandikia barua toka Disemba, 2016 na ninadhani hapo nitashika shilingi pamoja na mambo mazuri na sifa niliyokupa.

Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Simanjiro iweze kupandisha hadhi Kituo cha Afya cha *Urban* cha Orkesment kuwa Hospitali ya Wilaya ili wananchi wale wapate huduma ya afya kwa urahisi zaidi kuliko ilivyo sasa hivi ambapo hali ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo niendeleo kuchangia kwamba huduma za afya hasa zahanati zetu za vijijini, katika Wilaya hizo nilizotaja ni za duni sana. Hata hivyo tumepata habari njema kwamba, Wizara ya Afya imetenga shilingi bilioni 251, hizo zinakwenda kuboresha huduma za afya. Pamoja na hayo, katika zahanati na vituo vya afya vingi vijijini hakuna madaktari, hakuna wahudumu wataalam wa afya kwa hiyo, hizo fedha zinakwenda kutumika kwa jinsi ambavyo haitaboresha afya za wananchi. Tunaomba sambamba na kutoa fedha kwa ajili ya huduma za afya, Serikali iangalie kupeleka wataalam, madaktari, wauguzi na wahudumu wenye taaluma katika Wizara ya Afya. Kituo kizima kinakuwa na mhudumu ambaye hana hata elimu yoyote na ndiye anayetegemewa kama daktari, kama muuguzi. Haya ninayosema ni ya kweli, tufanye utafiti tusaidie wataalam waende katika wilaya zetu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka nije kwenye sekta ya maendeleo ya jamii na mimi nioneshe masikitiko yangu kidogo katika sekta hii. Najua kwamba umefanya mengi na tumesikiliza jinsi ambavyo umetueleza mengi katika sekta ya afya na hata katika sekta ya maendeleo ya jamii, lakini niseme mengi bado yanaonekana kama nadharia. Tutakwenda kuboresha, tutasimamia, bado hatujapata hasa

hasa ni nini kimefanyika, hatujaona sheria zinazokandamiza wanawake kuletwa hapa ili tuweze kuzirekebisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuoni mikakati madhubuti ya kuondoa ajira haramu ya watoto wetu katika migodi na kadhalika. Hatujaona ni jinsi gani wazee wetu wanaenda kunufaika na hizi shilingi 251,000,000,000 za sekta ya afya. Kwa hiyo, mimi nitoe rai kwamba pengine ni vizuri Wizara ya Afya ni *giant ministry*, sekta ya maendeleo ya jamii ni kama imemezwa, nilikuwa nashauri na kwa kuzingatia kubana matumizi, pengine sekta ya maendeleo ya jamii ingeenda kwenye wizara ambayo si kubwa kama Wizara ya Afya ili iweze kutendewa haki na yenyewe iweze kuhudumia wananchi zaidi kwa jinsi ambavyo sasa hivi inahudumia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni ombi ambalo niliona nilitoe na ni mawazo yangu, lakini ninazingatia suala la kubana matumizi. Ninaomba kwamba Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atueleze sasa sisi wananchi wa Mkoa wa Manyara, kwanza pamoja na shukrani tulizompa, na asituone kwamba hatuna shukrani, lakini atutendee haki katika Wilaya zetu nyingine, hasa hizi za wafugaji za Simanjiro na Kiteto. Waheshimiwa Wabunge wa Wilaya nilizotaja, mimi ni Mbunge wa Viti Maalum, tunajenga nyumba moja, tusaidiane wala mtu asinieleme vibaya, lakini mimi pia nimepata kura zangu kutoka kwa wananchi Wilaya hizo, naomba tusaidiane kuhakikisha kwamba na Wilaya hizi zinapata huduma ambazo wananchi wengine wanapata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ni gari la kubeba wagonjwa. Wilaya zetu hizi zina kilometa nyingi sana, hususan Wilaya ya Simanjiro ina *square kilometer* zaidi ya 20,000; unaweza kuangalia kutoka kituo cha afya hadi makazi ya wananchi ni zaidi ya kilometa 20, 30 hadi 50, nadhani utaona umuhimu wa kupeleka gari katika maeneo haya. Tunakuomba Mheshimiwa Ummy na tunakuamini, wewe unatosha na unatosha kabisa na chenji inabaki, naomba upeleke gari katika Hospitali za Kiteto na Simanjiro ili tuweze

kuhudumia wananchi wetu na wenyewe wanufaike na huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, hongera CCM, hongera Serikali yangu ya CCM kwa kufanya haya, hasa Serikali ya Awamu ya Tano, wamefanya kazi kubwa na tunampongeza Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana Mheshimiwa Umbulla, naelewa kwa nini umesema hivyo. Tunaendelea, Mheshimiwa Faida Bakar, atafuatiwa na Mheshimiwa Suzana Mgonokulima na Mheshimiwa Lucy Owenya wajiandae. Hawa ni dakika tano-tano tu.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. *(Makofi)*

Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia pumzi hadi kufikia siku ya leo na tunawaomba *maghufira* ambao wametangulia mbele ya haki, *Inshallah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi sana kwa Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na chama changu kitukufu Chama cha Mapinduzi. Na pia, napenda kuipongeza Serikali yangu ya Mapinduzi Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Shein, na vilevile kumpongeza Rais wangu Magufuli kwa jitihada kubwa ambazo anazichukua katika nchi hii, na kwamba ametujali sisi wanawake kwa kumteuwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza jembe! Huyu ni jembe kabisa! Huyu ni Mheshimiwa dada yangu

Ummy, napenda kumpongeza kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kushirikiana na Naibu wake Dkt. Kigwangalla. Hawa ni viongozi bora sana na wanaiweza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuongelea Benki ya Wanawake. Hii Benki ya Wanawake kila ninaposimama ninaitetea. Kwanza naipongeza kwa sababu imefanya kazi kubwa sana. Mheshimiwa Waziri ameongea kwamba shilingi 12,000,000,000 zimetolewa kwa wajasiriamali mbalimbali 9,650 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma, Ruvuma, Pwani na Mwanza, lakini kila nikisimama najuliza, napata wivu sana mimi nasema kwa nini hii Benki ya Wanawake na Zanzibar isiwepo? Hii Benki ni ya Wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii benki si ya Dar es Salaam wala si ya Mwanza wala si ya Songea wala si ya sehemu moja tu, hii ni Benki ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba Mheshimiwa Ummy uniambie leo, kila nikikuuliza unaniambai sijui hazijatolewa pesa milioni ngapi, kwani hii kazi ya kutoa hii pesa ni ya nani? Si iko katika bajeti ya Wizara yako? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba mshirikiane na Serikali na Wizara ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kule, mshirikiane Mheshimiwa Ummy, mimi sitapenda kusimama hapa tena kuongelea Benki hii ya Wanawake wa Zanzibar.

Zanzibar kuna wanawake kama sehemu nyingine yoyote, Zanzibar kuna wanawake ambao ni wafanyabiashara kama sehemu nyingine yoyote, Zanzibar ni wapiga kura wakubwa wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo iwe mwisho, Mheshimiwa Ummy, naomba leo iwe mwisho wewe ni mwanamke mwenzangu naomba unisikie. Nasema mwisho iwe leo, la kama mimi sitajibiwa leo hapa kama Benki ya Wanawake itaanza shughuli zake Zanzibar, mimi na wewe tutakuwa hatuelewani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili dhidi ya watoto wa kike na wa kiume. Wote hapa ni mashahidi juu ya mambo yanayotokea katika dunia yetu hii, si hapa tu dunia nzima wanawake, na watoto wanadhalilishwa, wengi wa watoto wanadhalilika; wengi wa watoto jamani ni mashahidi kwenye *whatsApp* siku hizi mengi. Utaona mtoto kakatwa mkono, sijui kakatwa mguu, kakatwa kichwa; wanadhalilika watoto; kwa nini watoto wanadhalilika Mheshimiwa Ummu Ally Mwalimu kwa nini watoto wadhalilike? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kama Wizara yako inajitahidi katika kuwatetea watoto wa kike na wa kiume, lakini bado. Tunaomba watoto wa nchi wasidhalilishwe kwa sababu watoto ndio Taifa letu la kesho. Mheshimiwa Ummu Ally nakuomba sana maafisa wako wafuatilie sana habari kama hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo linajitokeza jamani, mimi naomba kusema tu ukweli, unanua sipendi kufichaficha. Watoto wanadhalilishwa kijinsia jamani ninyi hamjui wenzangu ninyi? Watoto wanadhalilishwa kijinsia, mimi nimekwenda kufanya ziara Mkoa wa Kusini Pemba, kila ninapokwenda wananiambia Mheshimiwa Mbunge tunalalamika watoto wetu washaharibika, watoto wameshaharibiwa, kwa nini baba mtu mzima uende kumharibu mtoto mchanga? Mtoto mdogo anayesoma shule, wa kike na wa kiume, kwa nini jamani? Nililia watoto wanadhalilishwa, wanaharibiwa maumbile yao jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudi kwa Mwenyezi Mungu binadamu, akina baba nawaomba hii si nzuri. Mheshimiwa nasema kwa uchungu kwa sababu mimi ni mzazi Mheshimiwa Ummu, watoto wanabakwa na wanadhalilishwa. Sitaki niseme mengi leo, nikisema nitalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Kusini Pemba walinililia wakasema watoto wetu wanadhalilishwa

mpaka shule kule, na kuna baadhi ya walimu wanawadhalilisha watoto. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Sitaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani inakuwa hivi? Watoto wetu tunawazaa wenyewe watoto, mtu babu eti anakwenda kumfanyia ushenzi mjukuu wake! Eeh! Baba aliyemzaa mtoto anamgeuka, kwa nini? Turudi kwa Mwenyezi Mungu sisi binadamu, si nzuri, inatisha. Tanzania hii inatakiwa iwe ya amani na utulivu na upendo, kwa nini tunabadilika? Tumeacha dini sasa hivi tunahururika na dunia tunafanya mambo ya ajabu binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimba za utotoni. Baba mtu mzima anakwenda kumjaza mimba mtoto; Sheria ya Ndoa irekebishwe, iletwe Bungeni turekebishe sheria hii, haikubaliki, watoto wanadhalilika wanapigwa mimba na watu wazima walio na madevu yao mengi tu, wanawadhalilisha watoto. Hii haikubaliki katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wengine wanawaozesha watoto umri mdogo kwa sababu ya visenti, kwa sababu ya ng'ombe. Kwa nini tunafanya hivi binadamu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto tuwajali na tuwatunze. Watoto ndio watakaokuja kutusaidia sisi, tusijione vijana kesho kutwa sisi tutakapozeeka na tutakapokuwa hatujiwezi wao watatusaidia; kwa nini tunafanya hivi?

Mheshimiwa Waziri nakuomba ulisimamie, na anayepatikana na hatia hii achukuliwe hatua kali, naona bado hatua hazijachukuliwa kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wetu, mzee wa mwenzako ni mzee wako, leo wewe mzee wa mwenzako unamdhalilisha. Kuna makabila mbalimbali wanawanyanyasa wazee kwa sababu ya kuona kwamba ni washirikina, wazee wakiwa na macho mekundu wanawaua; nashukuru Serikali siku hizi inajitahidi sana katika hili; na kuwaua

ma-*albino*; nashukuru sana sasahivi Serikali imejitahidi, lakini tusichoke na tuone kwamba wadhallishaji wa wazee wamo. Tuwalinde wazee, wapewe vituo vyao, nyumba zao ziwe safi, wapewe lishe kwenye vyakula vyao na vile vile walindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzee wa mwenzako ni mzee wako tusijione leo vijana, sisi wenyewe tutakuwa wazee na tutataka kuhudumiwa. Ukiwaona saa nyingine unalia wazee nyumba wanazolala zile. Vituo vile Mheshimiwa Ummy jitahidi, vituo hata kama... *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea!

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Suzana Mgonokulima, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae kwa dakika tano na mwenzake.

MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia jioni ya leo kwenye Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze na kundi la walemavu. Ninarudia tena kusema Mheshimiwa Ummy - Waziri wa Afya, matatizo wanayoyapata wanawake wenye ulemavu wakati wa kujifungua bado yako pale pale. Niliiongea mwaka wa jana katika Bunge hili lakini wakati nikiwa *field* huko kwenye majimbo nimekuta wauguzi wengi wanawanyanyapaa sana wanawake wenye ulemavu wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kwa dhamana ya nafasi yako, hili ulichukue na ulifanyie kazi, wale watakaobainika wanaendeleza vitendo vya kuwanyanyapaa wanawake wenye ulemavu wakati wa kujifungua wachukuliwe hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 mpaka mwaka 2012 Hospitali ya Mkoa wa Iringa ilipata hadhi ya kuwa Hospitali ya Rufaa. Tatizo ambalo linaikumba hospitali ile ni ukosefu wa madaktari bingwa. Hitaji la madaktari ni 24, hadi sasa hivi hospitali yetu ile ya rufaa ina madaktari watano, hivyo kusababisha kazi ya kiutendaji ya kuokoa maisha ya wananchi wa Mkoa wa Iringa kuwa ngumu sana. Mheshimiwa Waziri, naomba hili ulichukue kwenye mgawo wako wa madaktari hao wanaopata ajira, basi Madaktari Bingwa uwapeleke kwenye Mkoa wetu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja kwenye Mfuko wa Bima. Afya kwa wazee wetu wa Taifa hili imekuwa ni tatizo. Serikali imejikita kuwasaidia wazee hawa huduma ya magonjwa ya homa, tumbo, lakini si pale wanapopata magonjwa yale ya moyo, ini, figo, vipimo hivi lazima walipie. Sasa kama Serikali inataka kusaidia kundi la wazee; hivi vipimo nilivyovisema gharama yake ni kubwa; na Serikali haitaki kuwekeza mkono wake, hii huduma ambayo tunasema tunataka kuwasaidia wazee naona sio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi Wizara ichukue jukumu hili kuhakikisha hawa wazee ambao Serikali imesema itawatibia bure, iwe bure ya magonjwa yote hata hayo niliyoyaaanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Hospitali ya Mkoa wa Iringa kupata hadhi ya kuwa Hospitali ya Rufaa, Manispaa ya Iringa tulijenga Hospitali ya Wilaya ambayo iko maeneo ya Frelimo na inaitwa Hospitali ya Frelimo. Hospitali hii ina wauguzi wakutosha, madaktari wakutosha, kinachokuja kuleta shida ni upungufu wa vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi ninapozungumza sasa hivi hospitali hiyo yenye wauguzi wa kutosha na madaktari wa kutosha haina vifaa vya uuguzi ambapo tumekosa kupata vipimo vya *full blood picture, x-ray, ultra sound* ambapo ingekuwa vipimo hivi viko pale, hospitali hii ingepokea msongamano wa wagonjwa ambao wanatakiwa kutibiwa pale ili wasiende kutibiwa kwenye hospitali ya rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ningependa nijikite kwenye unyanyasaji wa watoo wadogo wa kike. Sipo sambamba na wachangiaji waliosema, mtoto wa miaka chini ya miaka 18 kuoreshwa na kuwa mama wa nyumba ni makosa makubwa sana kiefya. Kwanza nyonga zake zenyewe hazijakomaa kuweza kuendeleza mambo ya mipango mingine ya kiutu uzima na hivyo tunawafanyia hayo matendo kiunyama kwa sababu tendo la ndoa kwa mtoto wa miaka chini ya 18 hana hisia nalo kwenye akili yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Wizara hii kama sheria inakingana, kuwa haiwezekani kutungwa sheria hiyo, basi tutalazimisha Wizara ya Elimu iweke kiwango cha elimu ya mtoto wa kike ni Kidato cha 12, ili kama itaonekana kuna mzazi yeyote yule ana binti yake ameolewa chini ya miaka 18 aweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tutakuwa tumewakwamua kundi la watoto wa kike ambao kwa tamaa za wazazi wao... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SUZANA C. MGOONOKULIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani kwa maana hii ndio inayo... *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lucy Owenya, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka na Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika ajiandae.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa saratani kwa sasa hivi katika dunia ni ugonjwa hatari sana pamoja na saratani ya shingo ya kizazi imekuwa ni tishio. Zaidi ya wanawake 274,000 duniani wanafariki kwa ugonjwa huu na Tanzania ikiwa ni mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru hospitali ya *Ocean Road* imekuwa ikitoa huduma ya mionzi na kusaidia wagonjwa wa saratani lakini hospitali ile wote tunashuhudia imezidiwa na wagonjwa ni wengi. Nashukuru hospitali ya rufaa *KCMC* ilipata wafadhili na wakafadhili jengo kwa ajili ya *unit* ya kansa, walijenga kwa shilingi bilioni 1.2 na wafadhili kwa sasa hivi wako tayari kununua vifaa kwa ajili ya mionzi, kutoa vifaa zaidi ya shilingi bilioni sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwenye kitabu cha maendeleo umetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya *KCMC*, jengo ambalo ni *special* kwa kitaalam linaitwa *banker* linahitajika kwa ajili ya kuweka vile vifaa vya mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *KCMC* tunachoomba, Serikali itusaidie wanahitaji shilingi bilioni saba. Tunamwomba Waziri wa Fedha na Kamati yako ya Bajeti mkae chini muangalie ni kwa jinsi gani mnaweza mkaipatia *KCMC* hizi shilingi bilioni saba ili waweze kujenga lile jengo. Kwa sababu, Kanda ya Kaskazini itapunguza msongamano katika Hospitali ya *Ocean Road*, inaweza ika-save zaidi watu milioni 15 na kwa kiasi kikubwa tunaweza tukapunguza ugonjwa wa saratani ya kizazi kwa wanawake na kutoa huduma ya mionzi pale *KCMC*.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie

kidogo magonjwa yasiyoambukiza (*non-communicable disease*). Nimekuwa nikiongea mara nyingi hapa, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri amesema wameanzisha watu kwenda mazoezi na kadhalika, nafikiri ni vizuri sasa Wizara hizi zikashirikiana Wizara ya Miundombinu na Michezo ili muweze kujenga *pavement* kwa ajili ya watu kutembea kwa miguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pale Dar es Salaam kwa mfano, zile njia ya majitaka (*sewage system*) mnaweza mkazifunika na watu wakaweza kupita kwa miguu. Nchi zilizoendelea kwa sasa hivi wanahimiza watu waende kazini kwa kutumia baiskeli, kwa sehemu kama Dar es Salaam mtu atatembeaje na baiskeli? Kutembea tu kwa miguu unagongwa na bodaboda. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali mkashirikiana kwa pamoja mkatengeneza *pavement* kwa ajili ya watu wa kutembea kwa miguu na kwa kiasi kikubwa sana tutapunguza magonja ya kisukari ambayo inasemekana Tanzania watu zaidi ya asilimia tisa wana ugonjwa wa kisukari mpaka watoto wadogo wana wanapata kisukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea wameacha kabisa *ku-serve* hivi vyakula vya *junk food*, lakini sasa hivi ndiyo vimeanza kuletwa Tanzania kama *Kentucky, Fried Chicken* na kadhalika. Ni vizuri mkazidi kutupa elimu ili watu waachane na hivyo vyakula ambavyo vinaongeza magonjwa ya shinikizo la damu ya kupanda na kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nizungumzie mimba za utotoni. Mimba za utotoni imekuwa ni hatari kwa kweli. Pamoja na kusema watoto wadogo wanaweza kuolewa chini ya miaka 18 mimi napinga jambo hili, kwa sababu kwanza tunawakosesha watoto wale elimu, pili mtoto wa kike akijifungua kabla ya umri wake anaweza akapata magonjwa kama ya fistula, tatu anaweza kushindwa kujifungua inabidi atumie *scissor* na wengine baada ya hapo wanakuwa ni *single parent*, unakuta wazazi wenyewe wakati mwingine wana wanyanyapaa wanawaambia hukusoma, kwa hiyo watoto wale wanaishia kuwa watoto wa mtaani, wanashindwa kuendelea na masomo, wanaweza kwenda

kuwa machangudoa na hii ni kumrudisha mtoto wa kike nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna moja au nyingine naomba Wabunge tukubaliane na hili, tuliona wenyewe juzi tulivyoongelea suala hili, Sheria ile ya Ndoa ya mwaka 1971 ibadilishwe wengine walikuwa wanapinga kutokana na imani zao za dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Upinzani naomba muichukue na mulfanyie kazi kwa sababu ina ushauri wa kutokasha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Mgeni Kadika.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nichangie Wizara hii ya Afya.

Awali ya yote nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu wa Wizara hii kwa haki walioyonitendea katika kipindi hiki. Mwaka jana nilisimama hapa nikalalamika sana, nikalia sana, kwamba hospitali yangu ile ya Wilaya ya Liwale haina wafanyakazi kwa maana ya madaktari lakini nashukuru *Alhamdulillah* Mheshimiwa Waziri ameisikia kilio changu amenipa madaktari wawili namshukuru sana nasema ahsante sana. (Makofi)

Pamoja na hilo bado nitaendelea kukuomba kwamba katika zahanati 31 za Wilaya ya Liwale zinaongozwa na *enrolled nursing*, kwa maana ya kwamba hatuna *clinical officers*. Wilaya mzima ile ina *clinical officer* wanne tu. Kwa hiyo, bado tunaendelea kulia pengine kama utapata nafasi hiyo utuongozee hao *clinical officers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hospitali ile ya Wilaya ya Liwale ina *x-ray* haina mtaalamu wa hiyo *x-ray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwenye taasisi moja muhimu sana ambayo ni taasisi ya Mirembe. Taasisi ya Mirembe kama ilivyo umuhimu wake, nimefanya utafiti huu kwa muda wa miezi sita, taasisi ya Mirembe inakabiliwa na matatizo lukuki. Kwanza kabisa ni lkama ya wafanyakazi, posho ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongea posho ya mazingira magumu Hospitali ya Mirembe inafahamika. Pia madai ya watumishi mbalimbali waliopandishwa madaraja pamoja likizo. Kikubwa zaidi katika taasisi ile ya hospitali ya Mirembe sasa hivi imegubikwa na tatizo kubwa la rushwa. Kwa utafiti niliufanya, tatizo hili na matatizo mengine yote lukuki niliyoyaorodhesha hapa, tatizo kubwa liko kwenye uongozi wa Hospitali ya Mirembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiongea na wafanyakazi wa Hospitali ya Mirembe morali ya kufanyakazi imeshuka. Hawana ushirikiano kutoka ngazi ya juu mpaka kwa mtu wa chini. Naomba Mheshimiwa Waziri ufanye utafiti, nenda Hospitali ya Mirembe, Mkurugenzi wa Hospitali Mirembe siyo rafiki kwa wafanyakazi wa Mirembe, na hii inashusha hadhi na morali ya wafanyakazi ya Hospitali ya Mirembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna wafanyakazi ambao wameshushwa madaraja na wanashushwa na mshahara, hivi mfanyakazi aliyeshushwa daraja, mkashusha na mshahara halafu unamuacha kituo hicho hicho, huo ufanisi wa kazi atautoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Liwale. Hospitali ya Wilaya ya Liwale aina hadhi ya kuitwa Hospitali ya Wilaya, kama ambavyo Katibu wa Wizara ya TAMISEMI anayeshughulikia mambo ya afya alivyosema. Halmashauri pamoja na kwamba tumeambiwa sisi wenyewe ndiyo tuanzishe vipaumbe, kweli sasa hivi tumeshatafuta kiwanja tumeshapata kiwanja, na *Inshaallah* bajeti inayokuja tunaweza tukaanza ujenzi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri *support* yako tujengee Hospitali ya Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama nilivyosema awali Wilaya ya Liwale ina zahanati 31, ina kata 20 lakini tuna kituo kimoja tu cha afya. Hapa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa TAMISEMI ameweza kutusaidia pesa kidogo kwa ajili ya kuboresha kile kituo chetu kidogo cha afya, naye nasema *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa bado naendelea kusisitiza takwimu za ...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hotuba ya upinzani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mgeni Kadika, atafutiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema na leo hii kuweza kusimama kwa ajili ya kuchangia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipatia nafasi hii. Nampongeza Katibu Mkuu wa Chama changu CUF Maalim Seif Sharif Hamad, pamoja na uongozi wa Taifa kwa kazi kubwa aliyonayo kupambana na wanafiki walioko ndani ya chama chetu, kututaka kutugawa na kusambaratisha chama chetu. Nasema chama chetu kiko imara Maalim Seif chapa kazi tuko pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu uzazi salama. Takwimu za hivi karibuni zinaonesha wanawake 30 wanafariki kila siku kwa kujifungua. Hii ni idadi tu ya wale wanawake wanaofika kwenye vituo vya afya na wanaofika

hospitali kwani wengi wanajifungulia majumbani, idadi ni kubwa na hii hali inatisha. Wanawake wengi tunapoteza maisha kwa uzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto nyingi zinazo msababisha mwanamke kufariki. Kwanza ni kukosa vifaa tiba na dawa; pilli, lishe bora na umaskini unachangia pamoja vituo vya afya kujengwa mbali na wananchi, hivyo, inapelekea kupata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishauri Serikali bajeti ya Wizara ya Afya iongezwe na wale watu wanaofanyakazi kwenye sekta ya afya waboreshewe pia maslahi yao ili wapate kufanyakazi kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa kudhibiti na kupambana na madawa ya kulevya katika nchi hii vijijini na mijini. Waathirika wengi wanaopoteza nguvukazi ni vijana walio chini ya umri wa miaka 18. Watoto hawa wanatoroka shule na baadaye wanajiingiza katika vitendo vya kutumia dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa za kulevya zinachangia kiasi kikubwa maambukizi ya UKIMWI na magonjwa ya akili, naishauri Serikali kupitia *sober house* ni lazima akiingia mle walipie ada, wengi wao hawana uwezo, wazazi wao tayari wameshawatelekeza, kwa hiyo Serikali iwatibu bure kupitia Wizara ya Afya kwa sababu hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu ukatili wa kijinsia. Wanawake wengi katika nchi hii wananyanyasika, wananyanyaswa na waume zao, kupigwa hata kuuawa, kwa sababu ya mapenzi tu. Wengine ni waume zao, wengine ni wapenzi tu, hilo jambo lipo, mashuleni, vyuo vikuu watoto wanajiingiza kwenye mapenzi na baadaye wanauawa. Hili jambo ni la kutiliwa nguvu sana kwa sababu linapoteza vijana wetu wengi kwa ukatili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Devotha Minja ajiandae.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye hoja muhimu sana ya afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri tu kwamba na mimi ni Mjumbe wa Kamati hii, kwa hiyo mambo mengi yanayozungumzwa kwa kweli yananifurahisha na niseme tu kwamba Wizara inajitahidi, lakini Serikali inashindwa kupeleka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kwa Taifa kubwa kama Tanzania, lenye watu zaidi ya milioni 50, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hii ndiyo ambayo imeshika jamii nzima nazungumzia hasa Fungu namba 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kwa mwaka unaoisha Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii nikiondoa Fungu lile la Afya wametengewa fedha za maendeleo mpaka sasa hivi zilizoenda ni asilimia 2.3. Hii ni aibu kubwa mno, hivi tuaacha kuwaona watoto wa mitaani, tuaacha kuwaona watoto wadogo wenye mimba changa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara inayoshughulikia wazee, niseme tu labda ndiyo sababu mvua hazinyeshi na zikinyesha zinanyesha za mafuriko, kwa sababu nchi hii ni kwamba tumelaaniwa na wazee. *(Makofi)*

Nimepita hapo nje kuna bango la Wizara ya Afya linasema "Mzee Kwanza," na linasema "Mzee alikuwa kama wewe na wewe utakuwa kama huyo mzee." Ajabu ukiangalia hotuba nzima ya Waziri ameongelea kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi hapa nina hotuba ya Waziri ya mwaka jana alizungumza na alisema mwaka huu wa wataleta Sheria ya Wazee. Mwaka huu

hakuna chochote kinachozungumzwa kuhusu Sheria ya Wazee. Wakati Sera ya Wazee inapita toka mwaka 2003 leo ni mwaka wa 14, hakuna Sheria ya Wazee na ndiyo sababu leo wazee wanauawa kwa sababu hakuna sheria inayowasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa kuwa Mheshimiwa Waziri mwaka jana alisema na siyo mara moja, amekuwa akijibu maswali hapa kwamba sheria italetwa, leo kwenye kitabu chake chote hakuna jambo lolote linalozungumzia kuhusu sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wazee wa Taifa hili wamelitumikia Taifa hili wametusaida kuleta uhuru, lakini wazee hawa wametelekezwa. Makazi yao hayaeleweki, chakula wanachokula ni taabu, kubwa zaidi naomba Serikali sasa ituambie ni lini inaleta Sheria ya Wazee, ili wazee wa nchi hii waweze kujua haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Wizara ya Afya. Wizara ya Afya, afya ndiyo jambo la msingi, afya ndiyo utajiri kama ambavyo Mahatma Gandhi amesema. Utajiri namba moja ni afya zetu wananchi. Unapokuwa na afya njema ndiyo unaweze kujenga Taifa. Afya za Watanzania ziko mashakani na ninasema hivi kwa sababu fedha hazijaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali kama ya Muhimbili ni hospitali ya Taifa, ilikuwa inaomba shilingi bilioni tano kwa ajili ya vifaa tiba hawajapewa hata senti tano. Hospitali ya KCMC imeomba shilingi bilioni nne hawajapewa hata senti tano. Hospitali ya Bugando kwa ajili ya mashine ya Kansa haijapewa fedha, tunategemea nini? Kubwa zaidi Hospitali ya Jakaya Kikwete ambayo inafanya kazi kubwa sana ya kutibu wagonjwa wa moyo, ambayo inasaidia sana kupunguza gharama za kwenda nje, lakini taasisi ile haijapewa fedha. Pamoja na kwamba Mawaziri inawezekana wanajitahidi sana, lakini fedha hakuna. Tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kama mwaka jana tulitoa shilingi trilioni 28 zimeshindwa kwenda japo asilimia 50 za fedha za maendeleo, leo tunaongeza tunasema shilingi trilioni 33 hizo hela zinatoka wapi. Kwa hiyo, jambo ambalo linashangaza hata zile fedha zetu za ndani bado haziendi tatizo liko wapi? Au mnatudanganya kwamba mnakusanya sana lakini fedha hazipo. Hili jambo kwa kweli linatutia wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo ninapenda kuzungumza ni suala la madaktari walioajiriwa juzi. Hapa nina barua mbili kutoka TAMISEMI kwa ajili ya hawa madaktari. *In fact*, walikuwa waje Dodoma Chuo cha Mipango kwa ajili ya semina elekezi na wafike kabla ya tarehe nane, baadaye kuna barua nyingine inasema waende moja kwa moja. Hii imetoka juzi tarehe Mosi, waende moja kwa moja kwenye vituo, jana tena Dkt. Chaula ameandika barua nyingine waende moja kwa moja kwenye Halmashauri, huko kwenye Halmashauri watafutiwe sehemu za makazi na fedha. Hivi najuliza hizo Halmashauri tayari zimetengewa hizo fedha au mnataka hawa madaktari waende huko kama ambavyo walimu wanateseka, wanafika wanaolewa na Wenyeviti wa Mitaa au viongozi wa kata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana tunahitaji kweli madaktari, kama ambavyo Kambi ya Upinzani imesema, sielewi inawezekanaje Rais tu ndiyo aseme baada ya hao madaktari kushindwa kupokelewa kule Kenya, leo anatoa kibali kwa hawa madaktari 258. Je, hawa 3,000 walioko mitaani wanakwenda wapi? Ndiyo sababu Kambi ya Upinzani inasema je, huu siyo ubaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawa wasingekuwa wamejiandikisha kwenda Kenya ina maana leo wasingejiriwa, kwa hiyo kuna haja ya Serikali kuwa na mipango thabiti ya ajira ya watu wake na siyo kusubiri watu waende mahali fulani, wanatakiwa kwenda nchi fulani wakikosa ndiyo Serikali inawapa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba

hawa madaktari wamesomesywa kwa gharama kubwa sana, kwa maana hiyo, ni lazima kama wanapelekwa mahali kwenda kufanya kazi maandalizi ya kina yawe yamefanyika ili wasiye kuwa *frustrated*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie nadhani hiyo ni bado dakika tano. Pamoja na kwamba nia njema haikuwepo ya kupeleka madaktari hawa, kwa sababu wote tunajua Kenya ina madaktari wengi kuliko Tanzania, *World Health Organization* inasema kwamba daktari mmoja Kenya anahudumia wagonjwa 16,000 wakati Tanzania daktari mmoja anahudumu watu 20,000. Kwa hiyo, hainiingii akilini ni sawa na mgonjwa yuko *ICU* halafu na mwingine ana nafuu unasema daktari ampe dawa yule mwenye nafuu amwache yule ambaye amezidiwa. Kwa hiyo, hili jambo halikubaliki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niongelee suala la ndoa za utotoni. Pamoja na kwamba sheria yetu inakinzana lakini hatuwezi kuvumilia watoto wa kike wakiendelea kupata mimba za utotoni, maana yake ni kwamba Serikali inaruhusu mimba za utotoni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunajua kuna watoto wengi wako mitaani, rai yangu ni kwamba lazima tulete sheria hiyo, tuiptishe na nina hakika Mheshimiwa Umy ulikuwa mstari wa mbele katika hili naomba usirudi nyuma. Suala la imani kweli lipo, lakini tuangalie madhara makubwa ambayo wanayapata watoto wa kike na yameshazungumzwa mengi na wewe unayafahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa kweli Serikali kupitia Wizara hii na Wizara ya Sheria na Katiba walete sheria hiyo ili tuibadilishe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni kuhusu Benki ya Wanawake. Ukiangalia katika randama benki hii ilikuwa inatakiwa kila mwaka ipewe shilingi bilioni moja, bado Serikali imetoa kwa mwaka huu shilingi milioni 69.

Jamani hivi kweli tunataka kuwawezesha wanawake mdogo wangu Mheshimiwa Ummu? Kama hii benki kwanza moja ipo Dar es Salaam na sehemu chache sana, tunataka benki hii iende maeneo yote. Wanawake ni wengi sana nchi hii na wanaume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani pamoja na Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, Mheshimiwa Devatha Minja ajiandae na Mheshimiwa Halima Ali Mohammed atafuatia.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niweze kumshukuru Mwenyenzu Mungu aliyenijalia afya na pia niwashukuru sana wote waliochangia kuhusu Wizara hii ya Afya kwa sababu bila afya hatuna hiyo Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza kwa huzuni sana kwa sababu bajeti ya Wizara hii kwa kipindi hiki ambacho tumebakiza muda mfupi sana hajiatekelezeka kwa asilimia 60; japokuwa tuna Mawaziri ambao kwa kweli wanajitajidi kufanya kazi, lakini hawapati fedha za kutosheleza bajeti yao, na tunaona afya za Watanzania zinazidi kudorora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinga ni bora kuliko tiba, nilikuwa natengemea Mheshimiwa Waziri pia aje na jinsi ambavyo tutazungumzia jinsi ya kuwakinga Watanzania kutokupata maradhi mbalimbali, ukija ukaangalia katika maendeleo ya jamii ambako ndiko wako vijana wetu wafanyakazi ambao wanaweza wakaenda na wakawasaida Watanzania, bajeti yao ni ndogo na huko tunakotoka kwenye Halmashauri hawajaliwi, wako kama wanyonge ukiwakuta kule utawaonea huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri vijana wetu kule wananyanyasika hawako vizuri kabisa katika hii *sector*, ninaona kwa mfano, kuna masuala ya afya ya mazingira ambayo unaweza ukashirikiana na Wizara ya Mazingira, mkaanza kuona ni jinsi gani mnaweza kupunguza masuala ya maabukizi mbalimbali. Kwa mfano, Dar es Salaam asilimia 90 ni vyoo vya shimo, asilimia tisa tu ndiyo ina vyoo vya kuvuta, hizi ni takwimu ambazo zimetolewa na mashirika mbalimbali waliopita na kufanya tafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaona kipindi cha masika jinsi ambavyo mtiririko wa maji taka unavyosambaa katika Jiji lile. Hii inakwenda kuleta maambukizo mbalimbali. Tunaambiwa kwamba Watanzania asilimia kubwa tuna kawaida ya kutonawa baada ya kwenda sehemu za kujisaidia na sehemu mbalimbali na hizi zinasababisha maradhi mbalimbali ambayo tunayapata na magonjwa mbalimbali. Kwa mfano, *UTI* ambao inafikia mahali sasa umekuwa ni ugonjwa wa kawaida lakini pia unaua. Mheshimiwa Waziri uweze kulitizama hilo na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika makubaliano ya Abuja (*Abuja Declaration*) makubaliano yalikuwa asilimia 15 ya bajeti mzima inaweza kutatua changamoto za afya, lakini asilimia hii imekuwa haitolewi kwa muda wote wa bajeti. Ukianzia mwaka 2015/2016 zilitengwa shilingi trilioni nne zikaidhinishwa shilingi trilioni 1.5 tu. Ambayo ilikuwa ni asilimia saba hatukuweza kufikia hata hapo. Kwa hiyo, hii inaonesha jinsi ambavyo hatuwezi kutekeleza baadhi ya mipango ambayo tumeipanga ili iweze kutekelezeka kwa Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala hili la kutokupeleka fedha vizuri ambalo linaanzia ngazi ya sera tunavyotunga sera katika Wizara ya Afya tunakwenda katika mikoa, halmashauri mpaka vijijini, jinsi ambavyo mtiririko mzima unavyochanganya. Huu mchanganyiko wa kiutendaji katika Wizara hii unatuletea shida katika utekelezaji na ufuatiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati tumependekeza mara zote kwamba ingewezekana Wizara ya Afya kama ilivyo Wizara ya Elimu, kuwe na mtiririko kutoka sera mpaka utendaji wake. Unakuta katika Halmashauri baadhi ya masuala hayatekelezeki tunaambiwa hii iko TAMISEMI, hii iko Wizara ya Afya, basi unakuta ni mchanganyiko na fedha zinakuwa hazifuatiliwi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri aweze kumshauri Rais jinsi juu ya Wizara hii nyeti ambayo itatengeneza Watanzania ambao wenye akili timamu na nzuri, wenye afya bora wa kuweza kuendeleza na kuleta maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Menyekiti, nizungumzie kule kwangu japokuwa kuna baadhi ya mambo ambayo yalitakiwa yazungumzwe kwa TAMISEMI, kwa sababu sikupata nafasi lakini pia kwa sera yakwenda. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa waliomba shilingi milioni 150 waliidhinishiwa shilingi milioni 35 na hawakupata hata shilingi moja, unategemea hawa watafanyaje kazi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia OC ilikuwa ni shilingi milioni 25 badala yake wamepelekewa shilingi milioni sita tu. Ukija katika Halmashauri ya Kilolo kwanza Halmashauri ile ina upungufu wa watumishi asilimia 51, waliopo ni asilimia 49 na hao tumepata wenye vyeti *fake* 13 bado kuna upungufu wa watumishi katika Halmashauri hiyo ya Kilolo. Kwa hiyo, katika mgawanyo wenu wa watumishi wa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ndiyo hivyo muda umeisha, ahsante sana.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Devotha Minja,

atafuatia Mheshimiwa Halima pacha wako simuoni wa dakika tano, mimi naendelea.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii muhimu kwa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia sana hotuba zote tatu ikiwemo ya Waziri, hotuba ya Kamati na hotuba ya Kambi ya Upinzani. Katika hotuba zote hizi, kila hotuba iligusa kuwapongeza madaktari kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa Watanzania. Tunafahamu kazi yao ni ngumu kazi ya kutetea uhai wa wanadamu siyo kazi rahisi. Kazi ya kuahirisha kifo siyo kazi rahisi ni kazi ambayo kwa kweli inatoka moyoni katika kuhudumia watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia madaktari wakifanyakazi katika mazingira magumu, tumeshuhudia wengine hata waki- *risk* kwenye kazi zao magonjwa, kupata maambukizi, lakini madaktari hawa hawakati tamaa wanaendelea kuwahudumia Watanzania. Kwa kweli, niwapongeze sana madaktari kwa kazi ngumu wanayoifanya. *(Makofi)*

Pamoja na kazi hii sasa wanayoifanya lakini kuna mambo ambayo tukiyaangalia yanakatisha tamaa. Daktari anafanya afanyavyo kuhudumia wagonjwa walio wengi, lakini inatokea viongozi kama *DC, RC* anamtumbua hadharani Daktari - *DMO* akishasikiliza malalamiko ya wananchi kwenye mkutano wa hadhara, anasema kuwanzia leo hana kazi. Nafikiri ifike mahali tuwape moyo watu hawa ambao wanajitoa kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madaktari wana madai yao ya msingi, kwa zaidi ya mwaka mmoja hivi sasa Daktari Bigwa kwenye zile *call allowance* kwa maana mgonjwa kazidiwa saa nane saa tisa ya usiku analipwa shilingi 25,000 na dakitari wa kawaida analipwa shilingi 15,000. Madaktari hawa kwa zaidi ya mwaka hospitali nyingi hawajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwa Mkoa wa Morogoro. Hospitali ya Mkoa wa Morogoro inahudumia wagonjwa 500 kwa siku na hii ni baada ya hospitali ile kuwa ya rufaa kwa maana inahudumia wagonjwa wanaoshindikana katika Wilaya zake zote. Hospitali hii pamoja na ukubwa kuhudumia wagonjwa 500 ni sawa na wagonjwa 15,000 kwa mwezi, lakini hospitali hii haina *x-ray machine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *x-ray machine* iliyopo ni ambayo imenunuliwa tangu vita ya pili ya dunia, kwa sababu hospitali ile ilikuwa ya Jeshi. *X-ray* inagharimu siyo zaidi ya shilingi milioni 100, hospitali hii haina. Wagonjwa wanatoka na *drip* wanakwenda Mazimbu, wanakwenda hospitali ya Jeshi kwenda kufanya *x-ray*. Hilo nimelishuhudia mwenyewe na tumefuatilia na tumewahi hata kusema hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *mortuary*, hivi leo ndugu yako akipoteza maisha katika Mkoa wa Morogoro utalazimika kumsitiri pasipo hata kusubiri ndugu, kwa sababu *mortuary* hazifanyi kazi. Kweli kwa hospitali hii ambayo ina hadhi ya kuwa ya rufaa inashindwa kutengeneza tu *mortuary* kwa ajili ya kuwaifadhi wapendwa wetu ili basi walau waweze kuagwa kwa heshima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia suala lingine la Madaktari Bingwa. Tumekuwa na ajali nyingi sana Mkoa wa Morogoro, Daktari Bingwa wa mifupa hakuna, *theatre* kwa ajili mifupa hakuna, *theatre* iliyopo ni moja na inategemewa kwa maana ya magonjwa yote, akina mama wanaojifungua ndiyo hiyo hiyo. Watu wenye vidonda ndiyo hiyo watu wa ajali ndiyo hiyo. Nafiki Waziri alitizame kwa namna nyingine suala hili ili kuipa hadhi hospitali ya Mkoa wa Morogoro iweze kuwa na *theatre room*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la sakata la madaktari. Serikali ya Awamu ya Nne, kipindi cha nyuma ilikuwa ikihamasisha kwa maana ya ule mpango wa *brain bridge* kutoka nje, madaktari wetu ambao wamesomeshwa na kwa fedha za Tanzania watoke nje,

waje nchini, tena nakumbuka Rais wa Awamu ya Nne, ndiyo ulikuwa mkakati wake wa kuwaomba Watanzania walioko nje warudi hapa nchini watoe huduma kwa Watanzania wenzao. Nakumbuka walikwenda Cuba, Botswana Uingereza na kwingineko na baadhi ya madaktari nafikiri waliitika wito wa Rais wa Awamu ya Nne wakarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii cha kushangaza Tanzania ambayo ina upungufu wa madaktari, inawachukua madaktari kwenda kutoa huduma kwa Wakenya. Tumeushangaza ulimwengu kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia daktari mmoja kwa takwimu nimepitia hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa vijijini daktari mmoja anahudumia watu zaidi ya 78,000 na nane, kwa mjini anahudumia watu 25,000. Wenzetu Kenya daktari mmoja anahudumia watu 15,000. Leo hii sisi ndiyo wa kupeleka Madaktari Bingwa, madaktari wetu, watoto wetu, waende wakahudumie kuwaponyesha Wakenya wakati wamesomeshwa na kodi za Watanzania! Kuna mahali ambapo tunabidi kukubali kwamba tumefanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu, najaribu kuwatizama wale ambao hawakujitokeza kwa maana walikuwa na nia pengine ya kutoa matibatu kwa Watanzania, kuwaajiri madaktari 258 kati ya wale ambao walitahiniwa na kuwaacha wale wazalendo ambao walikuwa na nia ya uzalendo siyo sawa. Nafikiri *priority* ingekuwa kwa wale ambao walisema wana nia ya kuwatumikia Watanzania zaidi, kubaki nchini na kusaidia Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Serikali inasema ni kuhakikisha kila kata inakuwa na kituo cha afya, hivi sasa tuna kata zaidi ya 3,900, hospitali ambazo zinamejengwa katika kata hizi ni hospitali 448 ambayo ni sawa na asilimia 11 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu unatekelezeka

kwa namna hii? Yako mengi ambayo tunataka kuyajua, *flyover* ndiyo ni maendeleo, *flyover* moja ambayo ni shilingi bilioni 100 ni sawa na kujenga hospitali ngapi za Kata? Ni zaidi ya hospitali 250. *Priority* kwa Watanzania walio wengi ni *flyover* au ni kupata hospitali ili wapate huduma za afya? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie kuhusu suala la upungufu wa vifaa. Ukienda kwenye hospitali kifaa cha kupima wingi wa damu baadhi ya hospitali za *private* unapata, siyo hospitali za *government*. Ukienda kupima hospitali za *government* itakuchukua siku tatu kufahamu wingi wa damu, *private* ndani ya saa kadhaa unapata jibu, kwa sababu hospitali za *government* zinazidiwa na wagonjwa, ni kwa nini vifaa hivi muhimu visiwepo kwenye hospitali za *government* zikaweza kuwasaidia wagonjwa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa naliangalia sana suala la....

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Halima Ali Mohammed dakika tano na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali dakika tano.

MHE. HALIMA ALI MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyenzi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kutujalia afya njema. Ninakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mada iliyoko mbele yetu. Namwomba Mwenyenzi Mungu

amjalie maisha marefu Katibu Mkuu wa Chama cha CUF Maalim Seif Sharif Hamad ili aweze kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia kuhusu hoja ya haki za watoto. Tanzania tumekuwa tukiridhia mikataba mbalimballi inayohusiana na haki za watoto, kama Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1989, vilevile kuna Mkataba wa Haki za Mtoto wa Afrika ambao umeridhiwa mwaka 1979, lakini Tanzania tuna sheria inayomlenga mtoto wa Tanzania sheria hii imepitishwa katika mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekusudia Kuna watoto wengi wa Kitanzania watoto hawa aidha baba ama mama wamehukumiwa jela kifungo cha muda mrefu ama wazazi hawa wako rumande kwa muda mrefu. Sasa watoto hawa wanakosa haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia sheria, sheria hii imekaa kimya kuhusiana na mtoto ambaye mzazi wake mmoja ma wote wawili wako gerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wetu wanasoma, watoto wetu tunawatibia vizuri, watoto wetu wanacheza wanafurahi lakini watoto wa Watanzania hawa wanakosa haki zao za msingi. Sasa nilikuwa naiuliza Serikali je, imefanya utafiti kwa kiasi gani kuhakikisha kwamba watoto hawa wa Kitanzania nao wanapatiwa haki zao za msingi kwa mujibu wa Katiba? *(Makofi)*

Je, kwa sasa Serikali watakubaliana na mimi ili watoto hawa waweze kupatiwa haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria za nchi hii? Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nizungumzie suala la uzazi salama. Uzazi salama umeshazungumziwa hapa kwa Wabunge waliotangulia na mimi nazungumzia, nawaomba na Wabunge wengine walizungumzie suala la

uzazi salama. Takwimu zinaonyesha wanawake wengi wanapoteza maisha wakati wakitimiza jukumu lao la kuleta watoto duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za hivi karibu ni kwamba wazazi 30 wanapoteza maisha kila siku. Sasa idadi hii ni idadi kubwa na inawezekana kwamba idadi hii ni wale ambao wanajifungulia sehemu husika ambao ni zahanati, vituo vya afya na hospitali. Lakini kuna idadi kubwa ambayo wanajifungulia vijiji, huko ambako wanakosa huduma halisia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napendekeza kwa Serikali yenye kusikia kwamba bajeti basi ya Wizara ya Afya iweze kuongezwa kwa maksudi ili kuokoa vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali dakika tano.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa fursa na mimi kama ada nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi, aliyetujalia uhai, uzima na afya na akatuwezesha kuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze hapo alipomalizia Mheshimiwa Halima kwa kuzungumzia suala la kunusuru akina mama na vifo wakati wa ujauzito. Mimi nimeogopa kweli labda kwanza nianze kusema naipongeza Kamati ya Bunge husika kwenye Wizara hii kwa ripoti yao hii na naunga mkono hoja hii ya wao walichosema na pia ripoti ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 33 Kamati inasema bajeti hii inayoitwa *Support to Maternal Mortality Reduction* imepungua kutoka shilingi bilioni 13 mpaka shilingi bilioni nane. Mheshimiwa mdogo wangu Ummy ana lile tangazo lake anatoka sana kwenye televisheni "Kama

Halmashauri zinataka kuona kipaumbele cha kunusuru wakina mama watatenga pesa." Wizara yenyewe inapunguza bajeti, Halmashauri itatenga pesa za kutosha kutosha kutoka wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani tuishi yale tunayoyasema, kama kweli tunataka kunusuru akina mama hawa wanaotimiza jukumu la msingi, kweli tuwatengenezee mazingira ya kuwanusuru na tusiwanusuru kwa maneno tu. Hii inauma na haikubaliki, mdogo wangu Mheshimiwa Ummu nakuelewa, nakufahamu na ninakuamini katika utendaji kazi wako, hili lirekebishe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linaloendana na Halmashauri kubebeshwa mzigo ambao hawauwezi ni haya masuala ya kuhakikisha huduma za msingi kama afya zinatolewa ipasavyo. Ajira zinatangazwa Serikali Kuu, watu wanaomba halafu wanapangiwa kwenye Halmashauri, kisha watu hao wanatakiwa washughulikiwe na Halmashauri. Halmashauri hizi hazina uwezo, mbaya zaidi hii tofauti ya uwezo wa Halmashauri inajenga matabaka ya watendaji wa kada moja katika sehemu mbalimbali za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani *midwife professional* ataenda kukaa Mafia ambako Halmashauri yenyewe hohehahe aache kukaa Kinondoni kwenye mabilioni huku? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali Kuu ishughulikie wafanyakazi wa kada hizi nchi nzima. *Nurse* wa Mafia, *nurse* wa Kinondoni na *nurse* wa Ilolangulu huko wote wapate hadhi sawa, kwa maana ya mishahara na stahiki nyingine. Vinginevyo yale maeneo ya pembezoni yataendelea kuwa ya pembezoni na watumishi watatukimbia kila siku. Hili lirekebishwe watu wapate stahiki zinazostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia *in particular* jamani ni kisiwa, tena kisiwa kile kilichosahauliwa. Hatuna usafiri wa kuaminika ambao watu wengi wangeweza kutumia wa meli, Hospitali ya Wilaya *x-ray* hatuielewi na vipimo vingine

sijui vitendanishi na vitu gani, mpaka kumpima mama mjamzito kuangalia tu mkojo wake, ile kama sijui kuna vidude gani vingine visivyotakiwa, sukari na vitu vingine hakuna vitu vya kuwezesha kufanya hivyo. Sasa watu hawa wakipata dharura tunawapeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafia huko hospitali hiyo haijiwezi, majeruhi chungu mzima wanaovunjika, tunawafanya nini? Hata tukimudu kuwatia kwenye ndege, ndege zetu zinazokwenda ni hivi vidogo vya *private companies* vya *eight seaters* sijui *13 seaters*; kumingiza mgonjwa mle aliyevunjika mguu au aliyevunjika ni mtihani, angalau maeneo kama haya yangepewa kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Serikali inayofanya mambo kwa jumla bila kuangalia *specific case* kama hizi kwenye masuala kama haya ya afya na mengineyo naona siyo sahihi lazima Serikali ibadilike katika kuweka mipango yake na kutuambia wananchi kwamba kweli wanataka kutupa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwenye kikao kilichopita tubadilike kwenye *budgeting process* yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Riziki. Tunaendelea kwa dakika kumi sasa, Mheshimiwa Azza Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa Kemilembe Lwota na Mheshimiwa Juliana Shonza ajjandae.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na hatimae niko ndani ya ukumbi huu wa Bunge nikiwa na afya ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono bajeti ya Wizara ya Afya kwa asilimia mia moja. Kwa nini

naunga mkono bajeti ya Wizara ya Afya? Nitumie fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu na Baraza lote la Mawaziri bila kuwasahau Mheshimiwa Ummy na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. Mmefanya kazi kubwa ambayo inaonekana kwa muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mfupi mmeweza kugawa *ambulance* 67 katika baadhi ya Halmashauri zetu. Kwa muda mfupi mmeweza kutoa vitanda 20 vya kulalia wagonjwa, vitanda vitano vya kujifungulia, magodoro yake na mashuka 50 kwa kila Halmashauri zetu. Kwa hilo, nawapongeza sana na nawatia moyo pigeni kazi tupo pamoja na ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nirudi katika Mkoa wangu wa Shinyanga, niwasemee wanawake wa Mkoa wa Shinyanga walionileta ndani ya ukumbi huu. Najua Wizara ya Afya hamjengi miundombinu katika hospitali zetu, lakini ndugu yangu Mheshimiwa Ummy wewe ni ndugu yangu sana, kwa hili naomba unisamehe. Pamoja na yote unayoyafanya na pamoja na jitihada zote za *ambulance*, sijui vitanda na nini kama hamtokaa sawa na TAMISEMI hakuna ambacho kitawezekana. Hivyo vitanda vitakuwa havina pahala pa kuviweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hilo kwa sababu gani? Miaka mitano iliyopita kila nikisimama ndani ya bajeti hii huwa nasema ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na suala hili halijawahi kuchukuliwa hata siku moja. Najua siyo la Wizara ya Afya lakini kwa sababu Mheshimiwa Simbachawene yupo hapa na sikupata nafasi kusema TAMISEMI naomba niliseme. Hamtutendei haki Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, tumeanzisha ujenzi kwa nguvu zetu wenyewe, lakini hakuna fedha ambayo tunapewa kutoka Serikalini. Tukipewa fedha tunapewa fedha kidogo, tutamaliza lini ujenzi wa hospitali hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga, toka tumeanza kila mwaka tunapewa shilingi bilioni moja, ujenzi huu utakamilika lini? Ndiyo maana ninasema Mheshimiwa Umy na Mheshimiwa Kigwangalla pamoja na jitihada zote bila kukaa sawasawa na TAMISEMI yote mnayoyafanya hayatakuwa na maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba pamoja na kwamba ni Wizara ya Afya nitaomba TAMISEMI watujibu ni kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kila mwaka hatupewi pesa kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga inahudumia wagonjwa wengi zaidi kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Manispaa ya Shinyanga hatuna Hospitali za Wilaya. Kwa hiyo, inabeba mzigo mkubwa ambao haikustahili kuubeba. Hospitali hii ya Mkoa wa Shinyanga pamoja na kuhudumia wagonjwa wote hao *x-ray machine* ni mbovu, hazifanyi kazi, kila zikitengenezwa zinaharibika. Kuna kampuni inaitwa Phillips wala hawaonekani kwenda kutengeneza mashine hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata taabu kidogo, kwa sababu nikienda Hospitali ya Kahama hawana *x-ray machine*, Hospitali ya Wilaya ya Kishapu hawana *x-ray machine* na nikienda Mkoani *x-ray machine* ni mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake hawa na wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanga wanakwenda kupata wapi huduma za *x-ray*? Namuomba Mheshimiwa Waziri wa Afya akija atuambie wanaiangaliaje Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga kwa kuiletea *x-ray machine* mpya kwa sababu hii ni ya muda mrefu na imekwishachoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Mkoa wa Shinyanga haina vifaa vya upasuaji, ninaiomba Wizara ya Afya, kwa sababu hospitali hii inabeba Mkoa mzima na uzito

mnauona, tunaomba Wizara ya Afya mtuletee vifaa vya upasuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Mkoa wa Shinyanga inaitwa Hospitali ya Rufaa, inapaswa kuwa na Madaktari Bingwa 21, mpaka hivi ninavyoongea ina Madaktari Bingwa watatu tu. Sasa madaktari hawa wanafanya kazi kwa kiasi gani? Ninakuomba sana Waziri utakaposimama utuambie, ni lini mtatuongezea Madaktari Bingwa katika hospitali ya Mkoa wa Shinyanga, kwa sababu hawa waliopo hawatoshelezi hata kidogo. Kinachonisikitisha zaidi katika hawa watatu hakuna hata Daktari Bingwa wa Wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu vya vituo vya afya, Mkoa wa Shinyanga tuna vituo vya afya 21, katika vituo hivi ni vituo vitano tu ambavyo vinatoa huduma ya upasuaji. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 76 nimeona amesema kwa mwaka huu wa fedha wataboresha vituo 150 vya afya kwa kuwa na majengo ya upasuaji. Nikupongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wako wote kwa jambo hili kubwa ambalo mnakwenda kulifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kubwa sasa ni lini utekelezaji huu utaanza? Tunaposema tunakwenda kupunguza vifo vya mama na mtoto ni kupeleka huduma ya upasuaji kwenye vituo vyetu vya afya. Bila kuwa na huduma ya upasuaji kwenye vituo vyetu vya afya vifo vya mama na mtoto vitazidi kuongezeka. Ninakuomba Waziri utuambie hivi vituo 150 ambavyo umevisema kwenye hotuba yako ni lini utekelezaji wake utaanza? Niwashukuru sana lakini niwaombe Serikali ijangalie kila mwaka ijaribu kuboresha vituo vyetu vya afya tulivyonavyo ili viweze kutoa huduma zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgawanyo wa watumishi. Nasikitika kusema kwamba mgawanyo wa watumishi hauko sawasawa. Ukienda maeneo ya mijini watumishi unawakuta wako wengi, unakuta labda hospitali

inahitaji watumishi labda 30 lakini wapo 50, kwa nini? Hamtutendei haki tunaishi maeneo ya vijijini. Ninaomba Wizara na wanaohusika mtuangelie hata tunaotoka maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini watumishi wengi wanakwenda maeneo ya mjini na maeneo ya vijijini tunakosa watumishi. Naomba hili mliangalie kwa makini ili na sisi wananchi wetu waweze kupata huduma zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongelee kuhusu maendeleo ya jamii. Katika Mkoa wa Shinyanga kuna vituo vya wazee viwili, kituo cha Kolandoto na Usaanda. Bajeti iliyokwisha nakumbuka kuna fedha zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya wazee ingawa hazikuainishwa zinakwenda kujengwa wapi, naomba Waziri akija aniambie, kile Kituo cha Kolandoto ambacho hali yake ni mbaya sana, majengo karibu yanadondoka, Wizara inafikiria nini kuboresha majengo haya ya wazee ambao kwa kweli yanasikitisha na yanatia huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mtuambie maendeleo ya jamii vituo hivi vya wazee mnafikiria lini na fedha zake zipo wapi kwa ajili ya kuwaweka wazee wetu katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema haya yote nirudi kwenye Mfuko wa Wanawake katika Halmashauri zetu. Fedha zinazotoka maendeleo ya jamii kwenda katika Halmashauri zetu sielewi kidogo ni kwa nini usimamizi wake unakuwa mgumu na mbaya. Kuna fedha zinazotoka Wizarani na kuna fedha zinazotoka Halmashauri, ninawaomba Wizara Halmashauri isipotoa fedha zake za asilimia kumi ya mapato ya ndani msiwape fedha za Wizarani. Kwa sababu mnapokuwa mnawapa fedha kutoka Wizarani ndipo wanapokuwa na jeuri ya kutokutoa ile asilimia kumi ya mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga

mkono hoja, Waheshimiwa Mawaziri pigeni kazi, Mwenyezi Mungu atawabariki. *(Makofi)*

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa kabisa anayoifanya na Watanzania wote wanaona, ninampongeza Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanazofanya na niwatie moyo ninawaambia wakaze buti, wapige kazi, hapa kazi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza pia Mawaziri Dada yangu Mheshimiwa Ummu na Naibu wake Mheshimiwa Kigwangalla kwa kazi kubwa wanazofanya, wametuletea *ambulance* kwenye Mkoa wetu wa Mwanza, wametupatia fedha za dawa, lakini hizi fedha za dawa mlizotupatia ni fedha ndogo hazitoshi, bado kuna baadhi ya vituo vyetu vya afya vina upungufu wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuzungumzia ni suala la vifo vya akina mama na watoto. Hili ni janga na naomba kama Serikali tulichukulie kwa umuhimu wake na tulipe kipaumbele. Kila siku ya Mungu akina mama kati ya 24 mpaka 30 wanapoteza maisha yao kutokana na uzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watoto kati ya 170 mpaka 180 kila siku ya Mungu wanapoteza maisha kwa sababu ya vifo vitokanavyo na uzazi. Ninashukuru katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza na amesema tukimpitishia bajeti hii itakuwa ni muarobaini wa haya masuala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu, mwaka 2000 kwa kila vizazi hai 100,000 vizazi 529 vilikuwa vinapotea, mwaka 2005 kwa kila vizazi 100,000 vizazi 578 vilikuwa vinapotea, mwaka 2010 vikapungua vikafika 454

na sasa kwa bahati mbaya mwaka 2015/2016 vizazi hivi vimeongezeka kwa kila vizazi 100,000 tunapoteza watu 556, hili ni janga na ninaomba sana Mheshimiwa dada yangu Umy tulifanyie kazi hili ili tuweze kuepusha vifo hivi, akina mama hawa wakiwa wanatimiza wajibu wao wa msingi kabisa wa kupata watoto, kwa bahati mbaya vifo hivi vinatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vingi vya akina mama hawa vinatokana na mambo makuu manne, jambo la kwanza ni upungufu wa damu, damu salama ya kuongeza akina mama hawa inakosekana akina mama hawa wanapoteza maisha. *(Makofi)*

Jambo la pili ni uzazi pingamizi, akina mama hawa wanapotakiwa kwenda kufanyiwa upasuaji zahanati wakati mwingine ziko mbali, zilizopo karibu hazitoi huduma ya kupasua akina mama hawa wanapoteza maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kifafa cha mimba, Mheshimiwa Umy ameongelea na tiba ni sindano za *magnesium sulphate*. Ninaomba sana katika vituo vyetu vya afya mambo haya yawepo ili tuweze kuokoa vifo vya akina mama. Mimba za utotoni na kuharibika kwa mimba, akina mama hawa mimba zinaharibika wanaenda kwenye zahanati zetu hatuna vifaa vya kusafisha hizi mimba na hii inasababisha vifo kwa akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la upungufu wa wataalam kwenye sekta ya afya, Mheshimiwa Waziri amesema kuna ajira mpya kwenye sekta ya afya lakini ni janga kubwa kweli, hatuna wafanyakazi wa afya wa kutosha. Naomba hili suala tuliangalie na tuajiri wafanyakazi wa afya ili tuweze kuokoa maisha ya Watanzania hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilisimama hapa na nikaongelea suala la vifaatiba. Hospitali yetu ya Sekou Toure kubwa kabisa ya Mkoa wa Mwanza hatuna C7

Scan, tumeomba hapa Mheshimiwa Waziri akaahidi akasema *CT Scan* hii inakuja lakini mpaka sasa ninavyosimama na kuongea hapa *CT Scan* haipo. Hii inapelekea Watanzania wa Mkoa wa Mwanza waende kufanya vipimo hivi kwenye *private clinics*. *Private clinics* vipimo hivi ni kati ya shilingi 300,000 mpaka 400,000, ni aghali na Watanzania wengi hawawezi kumudu fedha hizi kuzilipa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba unapokuja hapa kuhitimisha utuambie ni lini vifaatiba hivi vitaenda kwenye Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la watoto njiti sijalionga kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Watoto wanaozaliwa njiti ni wengi katika wodi yao, nimetembelea wodi yao Mkoa wa Mwanza, wodi haina vifaa. Watoto njiti hawa wanahitaji *suction machines*, wanahitaji *blood pressure monitors*, wanahitaji *incubators* ili waweze kuwekwa na kuhifadhiwa ili waweze kufika siku zao za kuweza kuruhusiwa na kwenda nyumbani, lakini inabidi watoto hawa waruhusiwe kwa sababu wodi ya watoto hawa haina vifaa. Mheshimiwa Waziri tunaomba sana uweze kutupatia vifaa hivi, wananchi na akina mama hawa wanahangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *D by D, concept* yake ni nzuri kabisa haina tatizo, lakini inatokea mkanganyiko kati ya Wizara ya Afya na TAMISEMI. Naomba ifike mahali sasa Wizara ya Afya isimame kama Wizara ya Afya. Tunapokuwa kwenye Halmashauri zetu huko tunauliza hili suala la afya mbona halifanyiki, mbona haliendi, tunaambiwa hili suala lipo TAMISEMI, ukienda TAMISEMI unauliza unaambiwa hili suala lipo Wizara ya Afya, sasa tufike mahali tuone *ownership* iko wapi na tujue Wizara ya Afya isimame kama Wizara ya Afya na tu-*deal* na Wizara ya Afya, peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba hii tumeona fedha zilizotengwa za dawa ni zaidi ya shilingi bilioni 230, kiuhalisia fedha za dawa zilizoenda ni shilingi bilioni 88 tu, nyingine zinaenda kwenye kusafirisha dawa, kwenye kujenga

majengo, kwenye vifungashio, tungejua kabisa *specific* hela za dawa zimetumika... *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea, Mheshimiwa Juliana Shonza, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Raphael Mbogo na Mheshimiwa Silafu Maufi ajjandae.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuweza kuchangia Wizara hii ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. *(Makofi)*

Awali ya yote nichukue nafasi hii kuweza kumpongeza Waziri wa Wizara hii, kwa kweli anafanya kazi nzuri na kazi yake siyo ya kubeza hata kidogo anastahili pongezi pamoja na Naibu Waziri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijikite sasa katika kuelezea Idara ya Maendeleo ya Jamii. Naomba nielezee kwanza historia, Idara hii ya Maendeleo ya Jamii ni zao la kihistoria la mapinduzi ya viwanda yaliyofanyika katika karne ya 19 katika Bara la Ulaya. Walipojenga viwanda yalijitokeza matatizo mengi ya kijamii hivyo wakaanzisha masomo ambayo yatazalisha wataalam ambao watashughulika na masuala ya mabadiliko katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu nchi za Afrika ikiwemo Tanzania haikufanya makosa kuchukua funzo hili na hatimae kujenga na kuanzisha Vyuo Vikuu vya Maendeleo ya Jamii, pamoja na vyuo vya kati ambavyo moja kwa moja vita-*deal* na mabadiliko ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana hata ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 87 ameelezea kabisa kwamba vyuo hivyo vitaendelea na udahili wa

wanafunzi watakoajishughulisha na masuala ya maendeleo ya jamii, ni vema tukaangalia kwamba tunapoendelea kudahili wanafunzi katika vyuo vya maendeleo ya jamii tuangalie na wale ambao kwa sasa hivi wapo maofisini, hawa Maafisa wa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, ni wazi kwamba kwa sasa hivi ambapo nchi yetu inapiga hatua kuelekea kwenye uchumi wa viwanda hakuna namna yoyote ambayo tunaweza tukaiacha nyuma Idara hii ya Maendeleo ya Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha sana idara hii kwa kifupi imesahaulika. Mwaka jana wakati nachangia Wizara ya Afya, nilizungumzia Idara ya Maendeleo ya Jamii, lakini ni wazi kwamba sijaona mabadiliko yoyote ambayo yamefanyika. Leo hii ukitembea katika Halmashauri zetu nyingi, siyo katika Mkoa wa Songwe tu nchi nzima Idara hizi za Maendeleo ya Jamii ziko hoi. Watumishi wa idara hii ya maendeleo ya jamii hawapelekewi fedha za *oc*, wala hakuna vitendeakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Halmashauri nyingine unakuta idara ya maendeleo imewekwa nyuma ya Halmashauri, nyingine ziko nje kabisa ya Halmashauri kuonesha kwamba siyo *part* ya Halmashauri zetu. Suala hili linasikitisha sana. Hali hiyo imepelekea sasa hata fedha ambazo zinapelekwa fedha za miradi, miradi mingi katika Halmashauri zetu inakufa haizai matunda, haioneshi mafanikio kwa sababu tumeiacha nyuma idara ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mbozi, kuna miradi mizuri sana ambayo imeanzishwa na Serikali, lakini kwa sababu wananchi hawajashirikishwa, watu wa idara ya maendeleo ya jamii hawajashirikishwa, inapelekea wananchi sasa hawana ile *sense of ownership*, wanaona kwamba ile miradi siyo ya kwao, wanaona miradi ile ni ya Serikali, kumbe tatizo hawajaelimishwa kuona kwamba ile miradi ina faida hivyo

wanapaswa kuitunza, hii yote ni sababu Idara ya Maendeleo ya Jamii imesahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi utaratibu uliowekwa na Serikali wa kutenga asilimia tano ya vijana pamoja na asilimia tano ya wanawake, lengo lilikuwa ni zuri lakini ukiangalia katika Halmashauri idara inayohusika moja kwa moja kufuatilia pesa hizi ni idara ya maendeleo ya jamii lakini hawashirikishwi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda leo hii katika Halmashauri zetu hususan Halmashauri ambazo zipo katika Mkoa wangu wa Songwe, wanawake hawana kabisa uelewa wa asilimia tano ambayo inatengwa na Halmashauri. Ukienda kwenye makaratasi unaona kabisa kwamba fedha zinatengwa lakini *impact* kwenye jamii haionekani, swali ukijiuliza ni kwa sababu Idara hii ya Maendeleo ya Jamii ambayo ndiyo inategemewa kwenda kutoa mafunzo kwa vijana pamoja na wanawake wajue namna gani ya kuweza kuzitumia hizo fedha za Halmashauri, wajue namna gani ya kuweza kuzifuatilia fedha hizo ili ziweze kutumika kama ilivyopangwa. Kwa sababu idara hii haishirikishwi, unaona kabisa kwamba fedha hizo hazijulikani zinaenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, Wabunge wa Viti Maalum siyo Wajumbe wa Kamati ya Fedha, kwa hiyo unaweza ukaona ni namna gani ambavyo hizi asilimia tano za wanawake na asilimia tano za vijana zinapotea katika mazingira ambayo ni ya kutatanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la bima ya afya. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba bado mwamko ni mdogo sana wananchi kuweza kujiunga na hii mifuko ya hifadhi ya hifadhi ya jamii, mifuko ambayo ingeweza kuwasaidia pia wanawake ambao wako vijijini, ambao kimsingi wao ndiyo wana matatizo makubwa sana ya kiafya, wanapata matatizo makubwa sana wanapoenda kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaojiunga na hii mifuko

ukiangalia idadi ni ndogo kwa sababu wanachi bado hawajaelimishwa, elimu bado haijawafikia kwa hiyo hawaelewi umuhimu wa kujiunga na hii mifuko ya bima ya afya. Hii yote ni kwa sababu tumepuuza Idara hii ya Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia hata katika jamii zetu, masuala ya unyanyasaji wa kijinsia ya wanawake na watoto yamekua kwa kasi kubwa sana. Dada yangu hapa ameongea kwa uchungu, ni masuala ambayo hata katika Mkoa wangu wa Songwe yapo kwa kiasi kikubwa, watoto wadogo wanaozeshwa, hivi ninavyosema nina mtoto ambaye namsomesha sekondari kwa sababu tu mzazi wake alikwishakupokea ng'ombe 60 ili amuozeshe huyo mtoto. Masuala kama haya tunapaswa kama Taifa kuyapinga... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nashukuru sana. Mheshimiwa Raphael Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Silafu Maufi na Mheshimiwa Ester Mahawe ajiandae.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nirekebishe jina siitwi Raphael Mbogo naitwa Taska Restituta Mbogo.

MWENYEKITI: Ahsante Restituta Mbogo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru kwanza wewe kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja hii ya Wizara ya Afya ambayo ni Wizara muhimu kwa sisi akina mama na ni Wizara muhimu kwa nchi yetu.

Napenda kwanza kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kasi yake ya hapa kazi. Ninasema hivi kwa sababu katika Mkoa wetu wa Katavi tulikuwa hatuna duka la dawa tangu labda niseme tangu Wilaya ile ianzishwe mwaka 1945.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata Mkoa hapa juzi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea kule akatuahidi duka la dawa na ndani ya miezi sita duka la dawa la *MSD* lilikuwa limejengwa na tukaenda kulizindua, naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummu na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa kazi nzuri, kwa sababu baada ya uzinduzi tuliweza kupata pia vitanda, hivyo naishukuru sana Serikali hii kwa kasi yake ya ufanyaji kazi maana yake ndani ya miezi sita duka la dawa lilijengwa. Hongera Serikali yote, hongera kwa Mawaziri wote na hongera sana kwa Mheshimiwa Rais wetu na tunakupongeza sana endelea na kazi na hekima zako unazozitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niende moja kwa moja kwenye hoja ya Wizara ya Afya. Ninampongeza Mheshimiwa Ummu na Naibu wake, naomba nitoe ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sihoji uwezo wao wa Watendaji wanafanya kazi vizuri sana akiwepo mwenyewe Mheshimiwa Ummu na Naibu wake, lakini naona Wizara hii ni kubwa, naona kama vile upande wa maendeleo ya jamii, wazee, unasahaulika. Naomba kutoa ushauri kwa Serikali iweze kuigawa Wizara hii, Wizara ya Afya ibaki peke yake, Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Wazee itenganishwe na hii Wizara, huu ni ushauri tu nautoa maana Wizara ya Afya ina mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye dawa hospitalini Waziri na Naibu wake washughulikie, zahanati,

vituo vya afya, hela za mgao kwenda kwenye Mikoa yote mpaka Wilaya, vifaatiba kuangalia japokuwa ndiyo tunasema viko TAMISEMI, lakini Waziri pia anatupia jicho, yote hayo yanamkabili Waziri wa Afya na Naibu wake, naona kama vile kazi inakuwa kubwa mno. Ntoa ushauri tu kuomba Wizara ya Afya ingeachwa peke yake ili iweze kutoa huduma vizuri kwa sababu kila Mtanzania bila kuwa na afya njema sidhani kama kuna kitu ambacho mtu anaweza akafanya. Hata hapa tunakaa kwa sababu tuna afya, ukiwa na afya iliyotetereka sidhani kama utaingia humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niongelee sakata la vyeti *fake*. Ninavyoongea hapa kule Mkoani kwangu Katavi kuna Halmashauri Tano, ndani ya hizo Halmashauri tano wafanyakazi 60 wa Wizara ya Afya walikuwa na vyeti ambavyo vinasemekana kwamba havijakaa vizuri au ni vyeti *fake*. Sasa tuna uhaba wa wafanyakazi 60 ghafla kwenye Mkoa wetu wa Katavi, tunaomba *replacement*. Uajiri wafanyakazi kama wafanyakazi wapya madaktari pamoja na wauguzi, hili limewakumba madaktari pamoja na wauguzi. Mkoa mzima kupoteza wafanyakazi wa sekta ya afya 60 ni wengi mno, utaangalia mwenyewe jinsi gani vituo vya afya, zahanati na hospitali zetu zitakavyokosa huduma na jinsi gani wananchi wa Mkoa wa Katavi watakavyokosa huduma. Naomba ajira iharakishwe ya hawa madaktari, Serikali jinsi ambavyo imezungumzia suala la vyeti *fake* basi wakamilishe huo utaratibu na ajira mpya za wale madaktari pamoja na wauguzi wenye vyeti ambavyo ni *genuine* iweze kutangazwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la Kituo cha Afya cha Mkoani Katavi. Mheshimiwa Waziri kile kituo cha afya ambacho mwaka jana tulisimama hapa tukaomba kirekebishwe na kifanyiwe ukarabati, napenda kushukuru Serikali kituo cha afya kimefanyiwa ukarabati kimekwisha, tatizo hakijafunguliwa. Namuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho yake atuambie kile kituo cha afya cha Mkoa wa Katavi ambacho kimekwisha kitafunguliwa lini?

Naomba pia kile chuo cha afya kiweze pia ku-*train* wauguzi wasaidizi ili tuweze kuwa na ma-*nurse* wengi na hawa *Medical Assistants* wengi ambao watakuwa wamekuwa *trained* Mkoani Katavi, kwa sababu ukiangalia jioografia kule kwetu ni Mikoa ambayo iko pembezoni lakini kama mtu atakuja atasoma kule ile miaka miwili atazoea mazingira kiasi kwamba hata kama atapangiwa kufanya kazi katika Mkoa wa Katavi atakaa. Ukimtoa mtu Mikoa ya mbali ukamleta kule anaweza akaona jioografia ni mbaya na hiyo kazi yenyewe asiipende kwa hiyo naomba kile chuo pia kiweze kuwa-*train* wauguzi wasaidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la ndoa za utotoni. Sheria zetu tulizojipangia wenyewe katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unaweza ukasema kwa upande mwingine zinachangia ndoa za utotoni. Tunazo sheria ambazo zinakinzana, tunayo Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo ibara ya kwanza inasema kwamba mtu yeyote ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18 ni mtoto. Ibara ya kwanza hiyo ambayo ni ya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inasomeka hivyo. Ukienda kwenye Sheria za Kimataifa ambazo tumeziridhia tunayo Sheria ya Kimataifa ya Mwanamke ambayo inatoa tafsiri ya umri wa mtoto na tunayo mikataba ambayo imeonesha umri wa mtoto ni miaka mingapi. Ukichukua zile sheria ambazo tumezisaini na tuliziridhia ambazo tunatakiwa tuzifuate zinakuja zinakinzana na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1970 ambayo inamruhusu mtoto wa kiume kuoakiwa na miaka 18 na mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa unakuta kwamba kunakuwa na *discrimination*, ukishaweka ile tofauti ya *age*, moja kwa moja umeweka utofauti wa mtu mmoja kuwa *supreme* na mwingine kuwa chini yake kwa ajili ya jinsia. Kama unataka kuwaweka watoto wote kuwa sawa, unatakiwa ule umri usiweke ile tofauti kati ya mtoto wa kike na mtoto wa kiume. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Taska Mbogo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Haya tunaendelea na Mheshimiwa Silafu Maufi atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Mahawe na Mheshimiwa Neema Mgaya ajiandae.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipatia afya nami kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa ni mnyimi wa fadhila kama nisipomshukuru Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli. Kwa kweli amefanyakazi kubwa na kazi nzuri na tarajio jema kwa wananchi wa Tanzania kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, wamefanya kazi nzuri ambayo sikutarajia kabisa katika kipindi hiki kifupi kuweza kuifanya kazi kubwa hii ndani ya afya katika nchi yetu. Wakati akisoma mdogo wangu Mheshimiwa Ummu taarifa yake ya Wizara, kwa kweli ameni-*impress* na kujua ya kwamba kumbe yeye ni *bush doctor* lakini kwa kweli ni daktari kamili, kwa jinsi anavyoifanya kazi yake kwa kuipenda na kuifahamu Wizara ya Afya na kweli ameishika na kuhakikisha kwamba anaifanyia kazi njema katika kipindi chake hiki cha uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia suala la maendeleo ya jamii. Kitengo cha Maendeleo ya Jamii kimesahaulika hivi sasa ndani ya utekelezaji wake wa kazi. Maendeleo ya jamii ilikuwa kila mwaka wanaketi Maafisa Maendeleo ya Jamii kukaa pamoja, kushauriana, kuelekezana na hatimaye kupeana ubunifu wa kuweza kuitekeleza Wizara yao, tatizo vikao hivi sasa hivi havifanyiki

ikidaiwa kwamba bajeti ni finyu. Ninaomba vikao hivi virejee ili maendeleo ya jamii iweze kufufuka tena upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya jamii ni kitengo ambacho kinatoa elimu kwa akina Mama katika kuhamasisha ujasiriamali, kuwahamasisha akina mama kiuchumi, kuelekeza akina mama umuhimu wa kujiunga na tiba, umuhimu wa kujiunga na bima, umuhimu wa mikopo na namna ya utekelezaji wa mikopo hiyo ya vyombo vya fedha na SACCOS na kadhalika. Tatizo ni kwamba hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii hawana vitendea kazi, hawana usafiri na hata alivyozungumza Mheshimiwa Waziri ya kwamba wasitumie magari ya miradi ya UKIMWI na kadhalika, ajue wazi ya kwamba maendeleo ya jamii hawana usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa hatuna usafiri, Wilaya zote hazina usafiri na hata ngazi ya Kata hawana usafiri hata wa pikipiki. Mimi ninavyoelelwa ni kwamba, Maafisa Maendeleo ya Jamii siyo *desk officers*, hawa ni *field officers*, wanahitaji kwenda kwenye maeneo, wanahitaji kupatiwa usafiri, vinginevyo watatumia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri wana mambo mengi, wanawapa usafiri kwa kubahatisha, lakini wakiwa na usafiri wao watu wa maendeleo ya jamii watafanya kazi nzuri kwa wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninapenda kuishukuru Serikali yangu kwa kutoa ajira takribani kwa wananchi 52,000; ninaomba katika hawa 52,000 hebu tuangalie ajira ya Maafisa Maendeleo ya Jamii. Hatuna Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Rukwa ndani ya kata 97 ukiacha zile zilizoongezeka tunao Maafisa 51 tu, tuna upungufu mkuwa wa Maafisa Maendeleo ngazi ya Kata, tuna upungufu mkubwa wa Maafisa Maendeleo ngazi ya vijiji na tunao upungufu mkubwa wa Maafisa Maendeleo wa Wilaya ya Nkasi na Wilaya ya Kalambo bado wana kaimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hawa Maafisa Maendeleo wa Jamii wa Wilaya ya Nkasi na Kalambo wapatiwe uthibitisho kamili wa Maafisa Maendeleo wa Wilaya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu suala la afya. Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Katavi tuko mbali na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ambayo iko Mbeya. Tumekubaliana Mikoa hii miwili tuweze kujenga hospitali ya rufaa kati ya Rukwa na Katavi na tumeweza kupata eneo la hekari 97 kujenga hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa awamu ya awali imetupatia shilingi bilioni moja kwa maana ya kulipa fidia ya wananchi wetu waliokuwa katika lile eneo, ninashukuru sana kwa ngazi hiyo mliyoifikia. Kutokana na Halmashauri zetu kutokuwa na pato la kutosha, tunaomba Serikali Kuu iweze kuongeza hatua inayofuata ya uchoraji wa ramani na ujenzi wa hospitali ile iweze kuanzishwa katika Mkoa wetu wa Katavi na Mkoa wa Rukwa haraka iwezekanavyo ndani ya kipindi hiki tuweze kuifungua hiyo Hospitali ya Kanda ambayo ni hospitali ya Rufaa kwa Mikoa hii miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika upande wa afya ni upungufu wa madaktari. Katika Hospitali ya Mkoa tunao madaktari 20, kati ya madaktari 20 tunaowahitaji tunao madaktari 12 tu ambao hawakidhi mahitaji. Upande wa Madaktari Bingwa, tunao madaktari watano lakini tuna uhitaji wa Madaktari Bingwa 15 waweze kukidhi pale. *(Makofi)*

Jambo lingine katika upande wa afya ni kuhusu vituo vya afya na zahanati. Tunazo zahanati na vituo takribani 54 ambavyo vimejengwa lakini bado havijakamilika. Tunaomba Serikali iweze kuhakikisha ya kwamba haya majengo ambayo hayajakamilishwa 54, zahanati zikiwa 48 na sita ikiwa ni vituo vya afya viweze kukamilishwa ili viweze kutoa huduma kamili na hatimaye kuondoa msongamano katika hospitali ya

Mkoa ambayo hivi sasa ndiyo inaifanya hiyo kazi ili akina mama na watoto vifo viwe vichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa vifo vya akina mama na watoto kwa kweli vimekithiri na tuna kila sababu ya kuweza kuhakikisha vinapungua kama siyo kuisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia suala la *10 percent* za Halmshauri; wakati TAMISEMI ikizungumza, ilisema kwamba itatoa waraka kupeleka kwenye Halmshauri kuhakikisha ya kwamba wanafungua mifuko na hizo fedha za asilimia 10 zinapatikana na zinagawiwa katika vikundi vinavyohitaji vya akina mama na vijana. Tunaomba waraka huo kutoka TAMISEMI utoke ili Halmshauri ziwe na uhakika wa kutoa hizi asilimia 10 na Wabunge wa Viti Maalum tupate hizo nakala za waraka huo ili tuweze kufuatilia hizi fedha kama zinatoka na kuwafikia walengwa wanaohitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalopenda kulizungumzia ni kuhusu ziara ya Mheshimiwa Waziri. Waziri alikuja Mkoa wa Rukwa bahati mbaya jioni yake akapata dharura ikabidi arudi Dar es Salaam na ziara yake ikafutika, hivyo tunamuomba Mheshimiwa Waziri urejee tena katika ziara yako ya Mkoa wa Rukwa ili uweze kufahamu changamoto za afya katika Mkoa wa Rukwa, kwa sababu Mkoa wa Rukwa hatuna hata Wilaya moja yenye Hospitali ya Wilaya, tuna Hospitali Teule tu, tunahitaji kuwa na Hospitali ya Wilaya.

Katika kuhangaika kutafuta hospitali ya Wilaya, tuliweza kuomba majengo ambayo yako chini ya *TANROADS* yaliyokuwa kambi ya kujengea barabara bahati mbaya inasemekana kwamba majengo yale ni madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na juhudi uliyonayo Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Kigwangalla, nina imani kwamba mtasimamia kuhakikisha Mkoa wetu wa Rukwa tunapata hospitali za Wilaya katika Wilaya zake zote nne ambazo kwa sasa hatuna hizo hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonekana ya kwamba Mkoa wa Rukwa tuko mwisho, tuko pembezoni, bila ya kuwa na afya bora itakuwa ni hatari, sisi ndiyo wazalishaji tunaowalisha katika nchi hii ya Tanzania. Hivyo tunawaomba kabisa kwamba tujaribu kuangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika upande wa afya ni huduma ya damu salama, akina mama na watoto ndiyo wanaohitaji kuhakikisha kwamba wanapata huduma salama na huduma salama ni damu, damu kwetu kuna tatizo la chupa za damu, sasa katika hizi chupa 250,000 sijui Mkoa wa Rukwa una kiasi gani cha hizo chupa, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la pili ni kwamba, vituo vyetu vya afya havina majokofu ya kuhifadhi hiyo damu salama na wale wataalam wa kukusanya damu salama wengi wao hawajapata mafunzo, hivyo ni kwamba hawapo ambao wanaweza kukusanya damu salama na kuhakikisha kwamba wagonjwa wetu wanapata damu salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunawaomba mtoe mafunzo kwa wale wataalam wanaoshughulika na damu salama...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na *big up*. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ester Mahawe, Mheshimiwa Neema Mgaya na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ajiandae.

MHE. ESTER A. MAHAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mawazo yangu katika Bunge lako Tukufu.

Kwanza kabisa naomba nitoe shukrani zangu za dhati na pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Umyy pamoja na Mheshimiwa Kigwangalla. Amezungumza mwenzangu Mheshimiwa Mama Martha Umbulla muda si mrefu ya kwamba juzi tu tuna kama siku mbili, tatu alitoka katika Mkoa wetu wa Manyara kwa sababu ya Hospitali ya Haydom, kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Umyy lakini kubwa zaidi nimshukuru pia na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye alisema atamtuma Waziri wake kwenda kuangalia jinsi gani Hospitali ya Haydom inaweza ikawa Hospitali ya Rufaa ya Kikanda kwa sababu hospitali hii inahudumia watu wengi sana, inahudumia Mikoa siyo chini ya mitano, ina Wabunge wanaoweza kuisema humu ndani siyo chini ya 20, kwa hiyo hili siyo jambo dogo. (*Makofi*)

Nimuombe sana sada yangu Mheshimiwa Umyy kwamba ikiwezekana kwa vile ile hospitali iko kijijini, kuna umbali wa zaidi ya kilometa 900 kutoka Haydom mpaka Muhimbili, kuna umbali wa zaidi ya kilometa 400 kutoka Haydom mpaka *KCMC*, kuna umbali wa zaidi ya kilometa 200 kutoka Haydom mpaka Hospitali ya Mkoa wa Manyara, tunakuomba sana Mheshimiwa Umyy kwa hili acha *legacy*. Watu wa Haydom, watu wa Mkoa wa Manyara, Arusha kupitia Wilaya yake ya Karatu, Meatu, Simiyu upande mkubwa sana wa Simiyu hawatakusahau, Singida ndiyo usiseme hata Dodoma.

Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri Umyy hospitali hii iweze sasa kufikiriwa kuwa Hospitali ya Kikanda ili kwa ukanda huu tuwe tumepata hospitali ya rufaa ya kuweza kumaliza matatizo ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Baada ya pongezi hiso naomba sasa nijielekeze katika pongezi hizo, nisisahau kumshukuru Rais wangu ametoa vitanda kwa kila Halmashauri. Kwa kweli Mheshimiwa Rais Mungu ambariki sana jamani kazi inafanyika, tunaona kwa macho ya nyama, Mungu ambariki sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu ya Babati

tuna changamoto mbalimbali, ninaomba tu niongelee kwa uchache hospitali yetu ya Mkoa wa Babati haina *theatre* inayooleweka, haina *x-ray* inayooleweka, haina haya *ultrasound* inayooleweka, haina wataalam wa *radiology*, tunaomba sana Mheshimiwa Ummu, tunajua kazi inafanyika, tunajua mnajitahidi sana, lakini penye changamoto lazima tuseme, tunaomba muikumbuke hospitali hii ya Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna Hospitali ya Mrara ambayo inatoa huduma kama Hospitali ya Wilaya pale, tunakuomba sana Mheshimiwa Ummu changamoto nilizotaja zilizoko katika Hospitali ya Mkoa zipo na kwenye hospitali ya Mrara, tunaomba uikumbuke hospitali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, pia nisisahau kuishukuru Wizara yako Mheshimiwa Ummu umepeleka vifaa vya kutosha na wataalam wa kutosha katika Kituo cha Afya cha Magugu hili lazima tukupongeze sana. Kwa kweli, tunakushukuru sana, tumeona juhudi zenu na pale kwa kweli sasa neno upungufu hakuna, ahsanteni sana kwa hili mlilolifanya pale Magugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaishukuru Serikali kwa sababu sasa inafanya sana kazi nzuri kupitia PPP, tayari imepeleka ruzuku katika Hospitali ya Dareda, hii ni Hospitali ya *Mission* ambayo inahudumia wananchi wengi sana wa Wilaya ya Babati Mji na Babati Vijijini Halmashauri zote hizi zinasaidiwa sana na hospitali hii ya Dareda, kwa kweli naishukuru Serikali imepeleka ruzuku pale ya kutosha lakini pia inasaidia kulipa watumishi wa kada hii ya afya wa hospitali ile. Kwa kweli kwa ujumla wake, niombe Serikali iendelee kutoa ushirikiano kwa hospitali hizi za makanisa ambazo kwa kweli ni hospitali teule katika maeneo yetu, zinafanya kazi nzuri sana kutoa huduma kwa wananchi. Hivyo, niipongeze Serikali kwa kukubali kufanya kazi kupitia PPP na hizi hospitali za makanisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Wilaya yetu ya Babati tuna mapungufu, tuna vituo saba na mahitaji yetu ni

vituo 25, tuna zahanati 32 mahitaji ni zahanati 102; tunaomba sana haya mapungufu yatazamwe kwa jicho la kipekee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwamba badala ya kuhangaika kuja kuweka labda Hospitali ya Wilaya pale Babati, ningeshauri zile fedha ambazo zilipaswa kuelekezwa kwenye ujenzi wa hospitali, vituo hivi vikiboreshwa vinaweza vikachukua nafasi kubwa sana ya kumaliza tatizo kiasi kwamba hata umuhimu wa kuwa na hospitali ya Wilaya pale unaweza usiwe wa lazima sana. Hivyo, naomba Kituo cha Bashnet, Hospitali ya Dareda pamoja na Kituo cha Mrara hospitali hizi zikiboreshwa ukweli ni kwamba taabu itakuwa imekwisha maana wananchi hawa watakapokuwa wanahitaji huduma yoyote ya rufaa wataelekea Haydom ambako siyo mbali. Naomba tuboreshe kwanza huku chini ili tuweze kusaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa pia la hospitali zetu katika Mkoa mzima wa Manyara hatuna *ambulance*. Kwa mfano, Wilaya ya Simanjiro imesemwa tayari kwamba tuna *ambulance* moja ambayo ni mbovu kila wakati ipo *garage*. Tunaomba jiografia ya Mkoa wa Manyara imekaa kidogo ni tatizo. Kwa mfano, Wilaya ya Simanjiro kutoka kata moja kwenda kata nyingine unakuta siyo chini ya kilometa 50 mpaka 80, kwa hiyo tunapokuwa na *ambulance* ambayo kwa kweli haipo vizuri tunapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisahau pia kuishukuru Serikali, tayari pale Simanjiro tunapanua wodi sasa, huduma ya mama na mtoto inakwenda kupatikana vizuri sana pale Orkesment, ninaishukuru sana Serikali kwa kuliona hili. Pia nisisahau kuishukuru hospitali ya Orkesment ya KKKT, hospitali teule iliyoko pale Simanjiro inaendelea kutoa huduma nzuri kwa wananchi wetu. Niiombe tu Serikali kama nilivyosema kwa sababu gharama kwa kiwango fulani ni kubwa katika hospitali hizi ambazo zina muundo wa hospitali binafsi, ninaomba ile *Urban Orkesment* itakapokuwa imeboreshwa vizuri na kuwekwa vifaa vyote vinavyotakikana, kwa kweli wananchi wetu watapata huduma bora ya afya pasipokuwa na tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze suala sasa la afya ya mama na mtoto - uzazi salama. Uzazi salama ni kitu muhimu sana, kama takwimu zinavyoonesha kwamba akina mama wasiopungua 30 wanakufa kila iitwapo leo. Hii idadi siyo ndogo, tunaomba katika vituo hivi vya afya huduma hii iboreshwe, katika zahanati zetu huduma hizi ziboreshwe. Kwa mfano, katika Wilaya ya Simanjiro, kata ya Ngorika pana umbali wa kilometa 60 kutoka Ngorika mpaka Orkesment. Nilikuwa naomba ikiwezekana ile zahanati iliyoko pale iweze kupandishwa hadhi kidogo, iweze kukaa vizuri ili wale wananchi wa Ngorika waweze kupata huduma pale Ngorika maana kutoka Ngorika mpaka Orkesment mtu anatembea kilometa 60 kwa kweli huu umbali ni mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema jiografia ya Simanjiro ni zaidi ya *square kilometer* 17,000 hiyo Wilaya ni kubwa sana na sehemu kubwa ni pori, kwa hiyo tunaomba msaada wenu sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nizungumzie suala la ndoa za utotoni; vifo vingi vimekuwa vikitokea kupitia ndoa hizi za utotoni. Ninaomba sana ikiwezekana Mheshimiwa Waziri sasa alete marekebisho ya sheria hii huku ndani. Ninawaomba wakina baba mlioko humu ndani, ninawaomba sana akina mama watoto wetu wanateketea. Hii biashara ya kusema kwamba kigezo cha mtoto wa kike kuolewa ni baada ya kuvunja ungo hii siyo sahihi. Siku hizi watoto kwa ajili ya hizi *chips, corie* na kadhalika wanavunja ungo wana miaka 10, wana miaka 11, wana miaka tisa, hivi kweli mtoto huyo ame-*qualify* kuwa mke wa mtu?

Jamani akina baba tunaomba mtusaide, hawa ni watoto wenu kama siyo wa kwako ni wa mjomba wako, kama siyo wa mjomba wako ni wa kaka yako, kama siyo wa kaka yako ni wa shangazi yako. Ninaomba katika hili tuungane jamani, tuweke itikadi zetu pambeni, tunafahamu mambo mengine ya kidini yapo humu na imani za watu tunaziheshimu, lakini ili kuokoa nafsi hizi za watoto wa kike tunaomba basi tushirikiane kwa pamoja ili kwamba watoto wetu waweze kupona. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba niunge hoja kwa asilimia mia moja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na kama muda utakuwepo kwa dakika tano Mheshimiwa Bashe.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Afya. Nianze kwa kumpongeza Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa jitihada kubwa ya kuimarisha upatikanaji wa dawa.

Ukiangalia kwenye bajeti ya mwaka 2015/2016 pesa zilizopelekwa kwenye huduma ya upatikanaji wa dawa ilikuwa shilingi bilioni 24, hivi sasa ndani ya miezi tisa chini ya Dkt. John Pombe Magufuli, pesa zilizopelekwa za dawa ni shilingi bilioni 112. Kwa Mkoa wa Njombe mpaka dakika hii hospitali, zahanati, vituo vya afya tumeshapokea karibia asilimia 80 mpaka 90 ya pesa za dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mawaziri kwa usimamizi mzuri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa kweli wanasimamia vizuri zoezi hili, pongezi sana kwao. Ombi langu moja kwa Serikali, Mheshimiwa Ummy ile hospitali yetu pale ya Makambako ni Hospitali ambayo ipo katikati inahudumia Mikoa ya karibu kama Iringa, wengine wanatoka Mbeya maeneo yale ya Mbarali kuja kupata huduma za matibabu pale Makambako. Hivyo basi, zile pesa mnazotupangia zinakuwa chache mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru tumepata pesa karibu asilimia 90 za dawa lakini mnazo tupangia ni ndogo tunaomba muongeze bajeti katika pesa za dawa katika Hospitali ile ya Makambako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo pia kuwapongeza tena Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa kusimamia kikamilifu huduma ya matibabu ya kibingwa. Kwa kweli katika hili mmefanya vizuri, tumeona katika hotuba yenu rufaa sasa hivi zimepungua za kwenda nje, hivyo naamini zile pesa ambazo zingetumika kwa ajili ya rufaa za wagonjwa kwenda nje zitatumika katika masuala mengine ya maendeleo kama maji, umeme, barabara na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitochoka kuendelea kupongeza, nawapongeza pia Mheshimiwa Rais, Waziri Ummy, Naibu Waziri Kigwangalla kwa kuweza kufanikisha upatikanaji wa vifaa vya hospitali kama magodoro, vitanda, mashuka, tumeona kwamba Wilaya zote ndani ya nchi yetu ya Tanzania tumeweza kupata vifaa hivyo. Hongera sana kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la vifo vya mama wajawazito, kila mwanamke aliyesimama hapa amezungumzia tatizo hili la vifo vya akina mama wajawazito. Takwimu zinaonesha na kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameonesha kabisa kwamba vifo vya akina mama wajawazito vimeongezeka kutoka 430 mpaka 556 katika vizazi hai 100,000, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ummy wewe ndiye Waziri mwenye dhamana katika Wizara hii ya Afya, wewe ni mwanamke, wewe ni mzazi, wewe ni mama wa watoto. Mheshimiwa Ummy unatusaidiaje wanawake wenzio katika tatizo hili? Hakikisha unapambania tatizo hili kutusaidia wanawake wenzio ili uweze kuacha alama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Ummy katika Wizara hii unaye kaka yetu Naibu Waziri Dkt. Kigwangalla yeye ni daktari kwa taaluma na Balozi wa Wanawake, shirikianeni katika kuhakikisha kwamba tatizo hili la vifo vya wanawake linakwisha nchini kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala pia la huduma za afya kwa watoto wachanga. Nataka nijue ni lini Serikali itaweke utaratibu mzuri wa kuweza kusimamia afya ya mtoto mchanga kwa maana ya siku 30 mpaka siku moja. Nimesoma vijarida mbalimbali vya wataalam vinaonyesha kwamba tukiweza kudhibiti vifo vya watoto kuanzia siku 30 mpaka siku moja kwa maana ya kuboresha afya za watoto wao, tutaweza kupunguza vifo vya watoto wadogo chini ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ulaya wenzetu watoto ambao wanazaliwa kwa gramu 500 mpaka gramu 600 wanaishi tofauti na hapa kwetu. Naiomba Serikali sasa ione umuhimu wa kuweza kuanzisha huduma ya afya za watoto hawa wachanga wa siku 30 mpaka siku moja, waanzishe wodi kwenye kila Wilaya ndani ya Tanzania kama ilivyopeleka vifaa vile kila Wilaya na hizi wodi za watoto wachanga zifunguliwe kila Wilaya ili kina mama wa Wilaya ya Wanging'ombe waweze kupata huduma hiyo, Ludewa, Makete, Njombe na Wilaya zingine ndani ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya matibabu ya saratani, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba sasa hivi wanakwenda kununua mitambo ya kutoa huduma ya tiba kwa ajili ya saratani. Mheshimiwa Waziri na dada yangu Ummy, kwa nini Serikali msiwekeze zaidi kwenye kinga, ukizingatia kwamba saratani ambayo inaua Watanzania wengi ni saratani ya shingo ya uzazi. Wanawake wengi wanakufa, hebu wekezeni zaidi kwenye kinga, kwenye Wilaya zetu kule tunakotoka ili mwanamke wa Ludewa kule aweze kupata huduma hiyo na kugundua hilo tatizo mapema. Kwa sababu inaonekana kwamba wagonjwa wa saratani wanakuja kugundulika wana matatizo hayo wakati imeshafika *stage* ya hali mbaya, matokeo yake Serikali inatumia gharama kubwa kuwatibia, kuwafanyia huduma na matibabu ya mionzi, *chemotherapy* wakati tungezigundua mapema tungeweza kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina *experience* Mama

yangu amekufa kwa *pancreatic cancer*, na tumekuja kugundua muda umeshapita, kama kungekuwa na huduma hizi mapema hata akina mama wanapokwenda tu hospitali anaweza aka-*check*, akagundua mapema, mtu anaweza akakaa kwa muda mrefu zaidi ya miaka 15 mpaka 20, lakini wagonjwa wengi wa kansa wanagundulika wakati hali imeshakuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ijikite zaidi kwenye kinga na kushusha kule kwenye Wilaya zetu ili kila Wilaya tuweze kupata huduma hii ya kinga ili tuweze kuokoa wanawake wengi, Kwa sababu kansa ya shingo ya uzazi ndiyo ambayo inaua wanawake wengi. Wengi wanaokufa na kansa ni wanawake ukiangalia katika takwimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la uwezeshwaji wa wanawake kiuchumi. Mheshimiwa Waziri, Dada Umy kwenye hotuba yako umejinasibu kwamba kule Dar es Salaam mmefungua Benki ya Wanawake, Pwani wamefaidika, Dar es Salaam wamefaidika na mikopo wamepatiwa viwanja. Mimi naomba kwenye majumuisho yako ukija kujumuisha hapa uniambie ni lini Benki ya Wanawake itafunguliwa Mkoa wa Njombe ili sisi wa kina mama wa Njombe tuweze kufaidika na sisi na mikopo hiyo, lakini vilevile tuweze kufaidika tupate viwanja kama walivyopata akina mama wa Dar es Salaam, kama walivyopata akina mama wa Pwani. Hivyo, katika majumuisho yako nitapenda unijibu kwamba ni lini benki hiyo itafunguliwa ndani ya Mkoa wa Njombe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kuzungumza suala la haki za watoto hasa watoto wa kike. Akina mama wenzangu Mheshimiwa Faida Bakar mpaka ametoa machozi hapa kuhusiana na suala la watoto, nakubali kabisa sisi kama walezi, wazazi tunajitahidi sana kuwasaidia watoto wetu wasiingie kwenye ndoa za utotoni, lakini Sheria ya Ndoa ni kichocheo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kabisa kuwa suala hili ni la Katiba na Sheria, lakini Mheshimiwa Waziri wa Afya,

Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dada Ummy wewe ndiye unayesimamia haki ya mtoto wa kike. Nakuomba sasa kushirikiana na Waziri wa Katiba na Sheria, mlilite suala hili mapema ndani ya Bunge ili tuweze kulifanyia maboresho na tusibaki tu tunalalamika hapa.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara muhimu kabisa Wizara ya Afya.

Kwanza nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya Taifa letu hasa katika suala la maendeleo kwa ujumla. Wote tunaona kazi inayofanyika ndani ya nchi yetu kwa kipindi kifupi cha mwaka mmoja na tunaona mambo makubwa yanafanyika kwa namna ya kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu kwa kutupatia gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Katoro. Napenda kutoa salamu hizi kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Busanda hasa Katoro, salamu hizi kwa kweli wamekushukuru na wamekupongeza wamefurahia sana na wanasema hakika vifo vya akinamama vitakwisha sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri Kigwangalla, kupitia wataalam wa taasisi ya *AMREF* walikuja kuzindua mradi mkubwa sana wa kuweza kuboresha huduma za afya katika Kituo cha Afya Chikobe, Zahanati ya Nyamalimbe, Zahanati

ya Rwamgwasa pamoja na Kituo cha Afya cha Kashishi. Kwa hiyo, kipekee nitumie fursa hii kushukuru sana *AMREF* kwa kazi kubwa kuweza kuungana pamoja na Serikali katika kuboresha huduma hizi kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kuwashukuru *GGM* kwa kuweza kujenga mochwari pale katika Kituo cha Afya Katoro. Hakika ushirikiano huu pamoja na Serikali yetu inaonesha jinsi ambayo tutaweza kutatua changamoto mbalimbali za afya katika sehemu mbalimbali katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, napenda kuzungumzia suala la watumishi. Katika sekta ya afya kweli kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi, nikiangalia katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Geita kuna upungufu mkubwa sana, mahitaji ni watumishi 824, waliopo ni watumishi 345, kwa hiyo upungufu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa kuwa Serikali inakusudia kutoa ajira iangalie upungufu huu katika Halmashauri ya Wilaya yangu ya Geita, ndiyo maana kunatokea hata hivi vifo, vilevile kunatokea changamoto mbalimbali kwa sababu kuna upungufu mkubwa sana wa wataalam wa afya hasa katika sehemu za vijijini ambapo kunakuwa na upungufu mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimesoma hii bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha, kipekee sijaweza kuona ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita. Ninaomba katika majumuisho Mheshimiwa Waziri uweze kutueleza wananchi wa Geita kwamba kuna mpango gani sasa wa kuanzisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa katika Mkoa wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu hospitali ambayo sasa hivi imepewa hadhi kuwa ya rufaa ni Hospitali ya Wilaya ya Geita na sababu hiyo hatuna kabisa hospitali ya Wilaya kwa sasa. Tunaomba Serikali ione umuhimu sasa wa kuanzisha hospitali ya Mkoa ili kurahisisha

huduma kwa wananchi wa Mkoa wa Geita. Kumbuka Mkoa wa Geita tuna watu wengi sana zaidi ya milioni moja, kwa sababu hiyo tunahitaji huduma. Nichukue fursa hii kumuomba Mheshimiwa Waziri muangalie uwezekano wa kipaumbele katika kuhakikisha kwamba tunapata Hospitali ya Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika suala la mama na mtoto, nilikuwa nikiangalia bajeti, ninapenda kuunga mkono hoja ya Kamati ya Bunge ambayo imezungumzia katika ukurasa wa 33, kutokana na kwamba bajeti imepunguzwa hasa katika kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi kwa asilimia 33.8. Mimi naungana na Kamati, kuona kwamba Serikali iangalie umuhimu wa kuweza kuongeza bajeti hii kwani akina mama wengi wanakufa kutokana na suala la kujifungua. Kwa vile tunapunguza bajeti maana yake ni kwamba tatizo hili litashindwa kutatulika kwa sababu bajeti imepunguzwa.

Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie uwezekano mkubwa wa kuendelea kuongeza bajeti hasa katika suala hili, ili kuwezesha kupunguza vifo vya kina mama hasa wakati wa kujifungua na katika uzazi baada ya kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya ni suala muhimu sana. Serikali kupitia Sera ya Taifa inasema kwamba kila kijiji tuwe na zahanati, kila kata tuwe na kituo cha afya. Suala hili ukiangalia kiuhalisia hasa katika sehemu mbalimbali Tanzania na hasa nikiangalia kwenye Jimbo langu tuna upungufu mkubwa kabisa. Mimi ninazo kata 22, lakini katika kata hizo ninavyo vituo vya afya vinne tu, hivyo bado tatizo ni kubwa. Naiomba Serikali iwekeze zaidi katika kuhakikisha kwamba iweze kutekeleza sera yake ambayo ni kuwa na kituo cha afya kwenye kila kata na kila kijiji tuwe na zahanati ili kuweza kuboresha huduma hasa kwa akina mama wajawazito pamoja na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala la watoto wetu wa kike waliopo hasa katika sekondari. Wakati wa hedhi, tunaomba Serikali iwaangalie watoto

hawa tuweze kutoa hivi vifaa vya kujihifadhi, kutokana na kwamba wengine wanashindwa hata kuendelea na masomo kwa sababu hiyo.

Kwa hiyo, niombe katika bajeti hii iangalie uwezekano kwenye shule zetu za sekondari watoto wapewe huduma hii, wapewe vifaa vya kujihifadhi, wengine wanashindwa kuendelea na masomo hasa kipindi hicho wanashindwa ku-*concentrate* katika masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuiomba Serikali kama bajeti haijapangwa basi waangalie namna ya kuipanga ili kuweza kunusuru watoto wetu ili waweze kuendelea mbele zaidi hasa watoto wa kike ambao wapo shuleni. Sambamba na hilo nilikuwa naomba pia Serikali ipunguze kodi, iondoe kodi kabisa zile *pad* ziwe zinaingia *free* zisiwe na kodi zozote. Hii itawezesha pia akina mama pamoja na wasichana kuweza kupata vifaa hivi kwa bei nafuu ili waweze kujihifadhi. Kwa sababu hali ya hedhi ni hali ya kawaida tu ambayo Mwenyezi Mungu ameiweka kwa wanawake, ni *nature*, kwa hiyo Serikali inatakiwa ituangalie wanawake, iangalie namna yakutusaidia na kutu-*support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la maendeleo ya jamii, ninapenda kuungana na wenzangu, kusema kwamba Halmashauri nyingi kwa kweli hazitilii mkazo suala la maendeleo ya jamii. Haiwezekani kama tutaweza kushindwa kusimamia sekta ya maendeleo ya jamii, hatutaweza kufikia maendeleo ambayo tumekusudia katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema nchi yetu tunaelekea kwenye viwanda, tutafikaje kwenye viwanda bila kuimarisha sekta ya maendeleo ya jamii? Hivyo nitumie fursa hii kuiomba Wizara iweke mkazo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bukwimba kwa mchango wako. Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nianze kabisa kwa kuunga mkono hoja.

Mimi nina mambo machache, jambo la kwanza alilisema Mheshimiwa Selemani Zedi, tarehe 19 Januari, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega alimuandikia Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya kuitaka kampuni inayoitwa *Mokasi Medical Systems and Electronics* iliyopewa mkataba wa ku-*service x-ray* waje waifanyie marekebisho *x-ray* ya Hospitali ya Wilaya ya Nzega. Mpaka leo ni miezi mitano, ninataka nimuombe Mheshimiwa Waziri anapokuja ku-*wind up* atuambie kwa nini, kwa sababu nimemsikia hata ndugu yangu wa Mafia amelalamika sana kuhusu hili suala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hii kampuni kama ina mkataba na Serikali usivunjwe huu mkataba? Jambo la kwanza. Jambo la pili kwa nini hatua za kisheria zisichukuliwe? Hili ni jambo ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na Halmashauri ya Mji wa Nzega wanapata shida, *x-ray* ipo, hairuhusiwi kuguswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe taarifa kwenye Bunge na nimpongeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, ninaamini kaka yangu Simbachawene hatamchukulia hatua kwa maamuzi aliyoyafanya huyu Mkurugenzi. Mkurugenzi ameamua kuwasialiana na Hospitali ya Rufaa kwa ajili ya kumpata *Biomedical Engineer* anaitwa Emmanuel Nkusi kutoka Bugando ili aje aweze kwa sababu ni mtaalamu kushughulikia suala la *x-ray* ya Hospitali ya Wilaya ya Nzega. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwamba kwa

kuwa mkataba ni Philips huyu mtu amefanya maamuzi kwa kuangalia maslaha mapana ya nchi, nataka niseme kwamba maamuzi haya yamefanyika na mtaalamu amefika na ameshalipwa na amechukua kifaa kuondoka nacho. (Makofi)

Hoja yangu, Mheshimiwa Waziri anapokuja *why* huyu *Mokasi* asifukuzwe kufanya hizi kazi, hili ni jambo moja. Jambo la pili mimi ni mpongeze sana Mheshimiwa Rais, mimi ni mjumbe wa Kamati, *support* aliyotoa Mheshimiwa Rais kwenye suala la hospitali ya *Ocean Road* na tunafahamu matatizo ya *cancer*, na mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Umyy kwa sababu tupo kwenye Kamati yeye na Mheshimiwa Kigwangalla tunaona tatizo la *resource* lililopo na namna anavyoweka *priority*, nataka niombe kwa ushauri, mwaka huu tunamaliza ile *Phase II* pale *Ocean Road* na tutakuwa kwenye nafasi nzuri sana kwenye *Ocean Road*. Niombe jitihada ziongezwe kwenye Hospitali ya Kikwete ya Moyo na Hospitali ya *MOI* ili ziweze kuongeza utoaji wa huduma katika maeneo hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nataka niishauri Serikali, Ilani yetu ya uchaguzi *it is very clear*, kwamba kila kijiji - zahanati na kila kata - kituo cha afya, hii ndiyo *commentment* yetu kwa Watanzania. Ningeomba kuwepo na *proper plan* na kuwe kuna *strategic unit* kati ya Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Afya ni namna gani tunajenga kila mwaka vituo vya afya. Kama kila Halmashauri ikiwekewa *condition* kwamba kila mwaka wa fedha angalau vijengwe vituo viwili, vitatu vya afya tuna uwezo wa kupata kwa mwaka angalau vituo 200 vya afya. Hii itatusaidia sana kupunguza matatizo katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niwapongeze sana Wizara ya Afya na TAMISEMI, kuwepo kwa Dkt. Chaula pale anayeshughulika na masuala ya afya, angalau anatupunguzia.

Nataka niwaombe Mheshimiwa Simbachawene na Waziri wa Afya, hebu ondoeni haka ka-*condition* kwa tofauli

za nchi sita. Kule kwenye Halmashauri wananchi tumewahamasisha, mfano kwangu sasa hivi tunavyoongea tuna zahanati 15 tunajenga sisi wananchi, zimefika kwenye *level* ya madirisha, lakini kuna kale ile *condition* ya kusema kwamba ili ujenge zahanati lazima iwe tofali ya nchi sita. Tofali ya nchi sita kwa kule kwetu Nzega ni 1200, mwaka huu mimi nimegawa matofali 47,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua hiyo *twenty percent* ya *incremental cost* ni milioni tisa na laki nne, gharama *additional cost*. Hivyo, tuwe na *flexibility* kwenye haya mambo ili angalau kama tulivyojenga madarasa katika kuanzishwa kwa shule za kata, wananchi walijitahidi sana kwa sababu tuliondoa zile *condition* za *ki-engineer*. Niombe sana Serikali iangalie namna gani Serikali inaweza kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwapongeza kwa jitihada mnazofanya lakini Mheshimiwa Waziri usipokuja na hoja ya huyu *Mokasi Medical Systems.....*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HUSSEIN M. BASHE:nitashika shilingi. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo. Ninawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa hoja hii, tutaendelea nayo kesho ambapo ndiyo itahitimishwa. Kwa hiyo, sina matangazo niliyoletewa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Alhamisi saa tatu asubuhi.

(Saa 1.43 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 4 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)